**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 3 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mhe. Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania kwa Mwaka 2004/2005 *[The Annual Report and Accounts of the Tanzania Bureau of Standards for the year* 2004/2005]

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI – MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 345

**Mambo Yanayochochea Ugonjwa wa Kipindupindu**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa kipindupindu umekuwa ni tatizo hapa nchini:-

Je, nini msimamo wa Serikali kuhusu kuwepo kwa masoko na shule za msingi ambavyo havina vyoo au vyoo vibovu kiasi cha kuhatarisha afya za wananchi kwa kuchochea magonjwa hayo ya kuambukiza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kipindupindu huambikizwa kwa kunywa maji au kula chakula kilichofuliwa na kinyesi au matapishi yenye vimelea vya kipindupindu. Aidha, maeneo ambayo kipindupindu kimeonekana kushamiri zaidi ni yale yasiyokuwa na maji ya kutosha, yasiyo safi na salama kwa ajili ya kunywa na matumizi mengine ya nyumbani. Katika maeneo mengi ya mijini mabomba ya maji yamebomoka, hivyo ni rahisi kuingiza uchafu unaoweza kuwa na vimelea vya kipindupindu. Pia hali hii huathiri watu wasiokuwa na desturi ya kuchemsha maji au kuweka dawa ya kuua vijidudu katika maji ya kunywa au kutotumia vyoo pamoja na utayarishaji wa chakula katika mazingirra duni.

Mheshimiwa Spika, shule zote za msingi nchini zina vyoo isipokuwa tatizo lililopo ni la upungufu wa matundu ya vyoo kwa shule mpya pamoja na uchakavu wa vyoo kwa shule za zamani kwa baadhi ya shule. Kwa sasa, Halmashauri zinafanya jitihada za kukabiliana na hali hiyo kwa kuongeza matundu ya vyoo na kuvifanyia ukarabati vyoo vyote ambavyo vimeharibika ili viweze kukidhi mahitaji kulingana na idadi ya wanafunzi kwa mujibu wa Kanuni za Elimu *(The education provision for the structure,Hygiene sanitation, and health inspection of schools Regulation)* za mwaka 2002, iliyotungwa chini ya Sheria ya Elimu namba 25(60)(a)(b) ya mwaka 1978

pamoja na Sheria za Afya *(Public Health Drainage and Sewarage*) namba 70 ya mwaka 1955. Kwa bahati nzuri pamoja na kipindupindu kuwa sugu katika baadhi ya Mikoa, haijawahi kuripotiwa kujitokeza kwa wananfunzi waliombukizwa kipindupindu katika shule yoyote kwani usafi wa Mazingira na Kanuni za Afya huzingatiwa sana shuleni.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu uliopo sasa Halmashauri nyingi zimebinafsisha huduma za vyoo vya masoko kwa wadau mbalimbali. Aidha, Halmashauri zimeboresha utaratibu wa uratibu na usimamizi wa huduma za usafi kwa kuhakikisha kwamba ushuru unaotozwa kwenye vyoo unatumika katika shughuli za usafi wa vyoo na kufanya ukarabati ili kuhakikisha kwamba hakuna hali yoyote ya kuhatarisha afya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Serikali ni kutafuta na kuratibu rasilimali kwa ajili ya ujenzi wa vyoo bora vya masoko na shule nchini pamoja na kuhimiza Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba majengo yote nchini yanakuwa na vyoo bora vinavyokubalika kisheria na pia vinakidhi mahitaji kulingana na idadi ya wanafunzi na wafanyabiashara waliopo katika maeneo husika. Aidha, kuhimiza Halmashauri kushiriki kikamilifu kukabili mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu pamoja na magonjwa mengine ya milipuko kwa kushirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna shule yoyote inayokubaliwa kufunguliwa bila kuwa na vyoo (matundu 8 kwa wasichana na 6 kwa wavulana). Ndiyo maana wakaguzi wanakagua shule kabla ya kufunguliwa. Kadhalika, kwa upande wa vyoo kwenye masoko, Bwana Afya hufunga soko iwapo halina choo au choo kikiwa kibovu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza, kwa kuwa ugonjwa wa kipindupindu ni ugonjwa wa kujitakia kama alivyosema Naibu Waziri. Kwa kuwa, pale Muhimbili kuna kitengo cha elimu ya Afya kwa Umma, yaani *Health Education Unity,* na wanafundisha *Health Educators* kwa ajili ya kuelimisha wananchi vijiji. Je, Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuimarisha kile kitengo kwa Elimu kwa Umma na kuwapatia vitendea kazi ili elimu iendelee kutolewa katika hospitali zetu juu ya afya na zahanati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nakubaliana na Meshimiwa Mbunge iko haja ya kuimarisha elimu kwa umma kuhusu kujihadhari na ugonjwa wa kipindupindu. Na hivyo ndivyo ilivyofanyika kwa Wizara ya Afya kutoa elimu mbalimbali kuhusu kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu. Kama atakumbuka Mheshimiwa mbunge ni kwamba kila hospitali inatoa elimu kwa hii kwa kina mama na wagonjwa kuhusu kujihadhari na ugonjwa wa kipindupindu, sio tu wakati wa mlipuko bali wakati wote katika shughuli za kila siku.

Mheshimiwa Spika, pia nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni wakati muafaka kwa sasa kuimarisha kitengo hicho, naomba nikubaliane naye tuchukue wazo lake ili twende tukalifanyie kazi ili liweze likatumika kwa wananchi wetu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana pamoja na majibu mazuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu unatokea kila mwaka hasa wakati wa mvua Dar es Salaam, hasa Kata za Buruguni, Vingunguti, Kipawa na sababu kubwa ni kwamba zinaponyesha mvua watu wasio na uwezo hufungulia vyoo vya kutoboa maji yaweze kutiririsha maji machafu viweze kupungua. Je, Serikali kwa mwaka huu iko tayari kabla mvua hazijaanza kuweka mkakati kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Ilala ili iweze kupambana na kupiga dawa kwenye hivyo vyoo au kusaidia kuvivuta ili visiwe vimejaa ili wananchi wasifungulie kwa mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni sehemu nyingi ambazo *squator* kwa Dar es Salaam, mara nyingi ndizo zinazopata matatizo ya kipindupindu, kama alivyosikia kwenye vyombo vya habari na muda mfupi uliopita kama miezi miwili mitatu Jiji la Dar es Salaam, limejitahidi sana katika kupunguza adha ya ugonjwa wa kipindupindu kwa kuelimisha wananchi. Pia kuwasaidia wananchi kuhakikisha kwamba vyoo vyao vinajengwa kwa *standard* inayotakiwa. Na hivi sasa ina mpango wa kutengeneza sehemu zote ambazo ni *squator* kwa kusaidiwa na *UN Habitat* ili kuhakikisha kwamba sehemu hizo zinapitika, sehemu hizo zinajengwa kama zinavyotakiwa.

Kwa hiyo Serikali imeliona na limelifanyia kazi ndio maana kuna mradi mkubwa, katika Jiji la Dar es Salaam, Manispaa zote tatu, katika kukabiliana na ujenzi holela pamoja na kuimarisha miundombinu mbalimmbali ikiwemo vyoo, vibarabara vidogo pia njia za kupita katika sehemu hizo za *squator*.

Na. 346

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Katoro na Bukoli**

**MHE. FAUSTINE KABUZI RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi ya watu inazidi kuongezeka kwa kasi katika miji ya Katoro na Bukoli kufikia zaidi ya 100,000; na kwa kuwa umbali kutoka Katoro hadi Geita au Butundwe ni mbali na kutoka Bukoli hadi Kashishi au Geita ni mbali; na kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo hupata shida ya tiba:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya viwili katika maeneo ya Katoro na Bukoli?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naiba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za afya kwa maisha ya Binadamu, si kwa miji midogo ya Katoro na Bukoli pekee bali kwa nchi nzima. Kwa kutambua umhimu huo, Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha huduma za Afya nchini kwa kuendeleza ukarabati wa vituo vya Afya na zahanati kupitia mpango wa ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya chini ya ofisi yangu na kujenga zahanati pale ambapo huduma hiyo haipatikani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ukiwemo mpango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukuaji wa kasi wa miji midogo ya Katoro na Bukoli na ongezeko kubwa la idadi ya watu kwa wstani wa asilimia 3.4 kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2002, Serikali katika mwaka 2004/2005 ilipandisha hadhi zahanati za Katoro na Bukoli kuwa vituo vya afya, ingawa zina upungufu wa idadi ya majengo yanayohitajika kuwa na hadhi iliyopewa. Kwa kutambua upungufu huo, Halmashauri ya Wilaya ya Geita katika Bajeti ya Mwaka 2007/2008 imetenga kiasi cha shilingi 70,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa wodi 2 kati ya wodi tatu zinazohitajika katika kituo cha afya cha Bukoli. Aidha, kituo cha afya cha Katoro kimetengewa kiasi cha shilingi 316,796,320/22. Fedha hizi za ujenzi wa kituo cha Afya cha Katoro zitapatikana kutokana na michango ya wadau kama ifuatavyo; *TASAF* shilingi 214.558,220/22, Halmashauri shilingi 53,198,000/=

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa michoro ya ujenzi wa vituo hivi imekamilika na imegharamiwa na Halmashauri kwa kiasi cha shilingi 7,000,000/=na kukusanya fedha taslimu shilingi 16,000,000/= kutoka michango ya wananchi ili kuweza kufanikisha mpango wa ujenzi wa kituo wa afya katika mji wa Katoro. Serikali kupitia Halmasharui ya Wilaya ya Geita itaendelea na ujenzi wa vituo hivi kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha kwenye Bajeti yake.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA**: Mheshimiwa Spika, ahsante kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na sahihi ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili na ya nyongeza. Kwa kuwa, mji wa Katoro sasa una watu wengi sana na wilaya ya Geita ina watu wengi na ina hospitali moja ambayo kwa ajili ya huduma kwa wilaya ya Geita haitoshelezi. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kukifanya kituo cha Katoro kiwe hospitali kamili, kwa sababu kuwa kituo cha afya bado kitakuwa hakitoshelezi?

Wilaya ya Geita pamoja na watu wake walivyo wengi haina gari kwa ajili ya wagonjwa, na ina vituo vya afya saba inasemaje Serikali kuisaidia Halmashauri kulingana na ukubwa wa wilaya hiyo na kazi nyingi kuipatia gari kwa ajili ya kituo cha Katoro.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kulingana na *population* ya

Wilaya ya Geita ambayo ni watu 800,000 zaidi inastahili kuwa na hospitali kama tatu kulingana na *population* yake. Na kwa mipango ya baadaye ya Geita ni kwamba kupandisha hadhi baadhi ya vituo vya afya kuwa hospitali na katika mipango yao wenyewe wanataka kupandisha hadhi vituo vya afya vya Kalumwa pamoja na kituo cha afya cha Katoro kuwa hospitali. Lakini vigezo vilivyowekwa havijafikiwa, baadaye vigezo vikifikiwa Serikali iko tayari kuwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kwamba tuna upungufu wa magari katika vituo vya Afya, na katika vituo vya Afya vyote Tanzania ambayo ni 344 kila kituo cha afya kinahitaji gari. Kwa upande wa Geita kwa upande kwa mwaka 2007/2008 wametenga fedha kwa ajili ya kununua *ambulance* kubebea wagonjwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie na Serikali pia inafanya kila mbinu kuhakikisha kwamba magari hayo yananunuliwa. Lakini pia naomba nizishauri Halmashauri waige mfano wa Geita kutenga angalau gari moja kwa mwaka kwa ajili ya vituo vyake vya Afya.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuwa katika vituo vilivyotajwa vinane, kimoja ni cha Tasamwa na kingine cha Nzela, na vituo hivi havina waganga pamoja na madawa ni machache. Je, Serikali inasemaje kupeleka waganga katika vituo hivi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyotolewa katika Bajeti ya Wizara ya Afya kwamba tuna upungufu wa watumishi wa Afya katika nchi yetu. Kwa hiyo, hao waganga watapelekwa kulingana na idadi ya wahitimu katika vyuo vyetu.

Naomba tuwe wavumilivu tatizo la waganga liko katika sehemu mbalimbali sio kituo Afya cha Nzela peke yake ni vituo vya Afya vyote. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira na waganga watagawanywa kulingana na wahitimu ambao wanahitimu katika vyuo vyetu Tanzania.

Na. 347

**Vyuo Vikuu Nchini.**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, shule nyingi za Sekondari na *High Schools,* zimeongezeka sana nchini tofuati na ongezeko la Vyuo Vikuu hapa nchini:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kupitia Wizara ya Sayasi, Teknolojia na Elimu ya Juu wa kujenga au kuanzisha ujenzi wa vyuo vikuu katika kila mkoa?

(b) Je, kwa nini Serikali haijaweka mkazo kwa masomo ya Sayansi hasa kwa kusaidia wanafunzi wa Elimu ya Juu wanaochukua masomo hayo kutoa, motisha ili wengi wajiendeleze katika masomo ya Sayansi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyami (Nkasi) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa sasa haina uwezo wa kujenga au kuanzisha vyuo vikuu katika kila mkoa. Hata hivyo ieleweke kwamba Vyuo Vikuu vilivyojengwa na Serikali ni vya kitaifa na kwamba yeyote mwenye sifa kutoka hapa nchini au nje ya nchi anaweza kujiunga na vyuo hivi. Vyuo Vikuu binafsi navyo hadahili wanafunzi kutoka mahali popote hapa nchini na nje ya nchi ili mradi mwombaji awe na sifa husika.

Aidha, ieleweke ya kwamba kutokana na Serikali kutokuwa na uwezo, Serikali ilikaribisha Mashirika yasiyokuwa ya Serikali, Mashirika ya Dini, watu binafsi kuwekeza katika elimu ya juu kuanzia mwaka 1992. Pale inapotokea kuna mwekezaji wa kujenga chuo kikuu kipya, Serikali itashauri mahali pa kujengwa chuo hicho. Hadi sasa kuna vyuo kikuu vinane (8) na vyuo vikuu vikishiriki vinne (4) vya Umma na vyuo vikuu 11 na vyuo vikuu vishiriki 9 vya binafsi.

Pamoja na jitihada hizo, Serikali imeweza kufikisha Elimu ya Chuo Kikuu kwa kuanzisha matawi ya Chuo Kikuu huria katika kila mkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali haijaweka umuhimu katika masomo ya sayansi. Maana Serikali imefanikiwa kuhamasisha wanafunzi kuchukua masomo ya Sayansi kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosomea fani zote za Sayansi na Ualimu.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa kike ambao hawakufaulu kiwango cha kudahiliwa katika vyuo vyetu vikuu hupata upendeleo wa kupewa mafunzo ya wiki 6 *(pre-entry programme for female science students*) katika masomo ya sayansi, hufanya mitihani wakifaulu hudahiliwa. Kwa hali hiyo, hii ni motisha kwa wanafunzi hawa wa kike kujiunga na masomo ya Sayansi.

Aidha, Wizara katika mwaka 2006/2007 imetoa jumla ya tuzo 119 kwa wanafunzi wa kike kutoka shule 20 zilizofanya vizuri katika masomo ya sayansi na hisabati katika mitihani ya kumaliza kidato cha nne mwaka 2006 (18); kidato cha sita mwaka 2006 na 2007 (25); vyuo vikuu, taasisi za Serikali na binafsi za elimu ya juu na ufundi (43) na wakuu wa shule za sekondari waliowezesha wanafunzi hao kufanya vizuri katika masomo hayo (33) pia Wizara iliwapatia tuzo.

Aidha Wizara ina kipindi cha redio kinachohamasisha wanafunzi kujiunga na masomo ya sayansi na kuhamasisha juu ya matumizi ya sayansi na teknolojia. Kipindi hiki hurushwa hewani kila siku ya Ijumaa saa 2.45 usiku na Redio Tanzania Dar es Salaam yaani *(RTD).*

Aidha, Mpango wa Maendeleo wa elimu ya juu na ufundi (MMEJU) unaoandaliwa utabainisha mahitaji halisi ya wahitimu wa elimu ya juu na ufundi. Wizara katika mwaka wa fedha 2007/2008 imeweka mpango wa kufanya tathimini ya mahitaji ya wahitimu wa elimu ya juu na ufundi ili kuwa na mpango thabiti wa mafunzo ikiwemo na mafunzo ya wanasayansi.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri na mipango mizuri ya Serikali, na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa elimu ya Chuo Kikuu ni ya muhimu na ya lazima kwa Watanzania, na kwa kuwa taifa halina pesa kwa wakati huu na uwezo wa kujenga Vyuo Vikuu vya kila mkoa.

Je, Serikali inaweza ikatueleza ina mipango gani ya kuandaa maeneo ya kujenga vyuo vikuu vya Serikali kwa kila mkoa kwa hapo baadaye badala ya kuendelea kutokuwa na maeneo kwa kila mkoa kwa fikra za kujenga chuo kikuu, hapo baadaye kila Serikali inapopata pesa, ina mipango gani?

La pili kwa kuwa masomo ya sayansi ni muhimu duniani na kwa kuwa wanafunzi wengi wanakwepa masomo hayo kutokana na vifaa kuwa vichache ikiwa ni pamoja na ukosefu wa umeme katika mashule mengi vijijini.

Je, Serikali isingeweka umuhimu wa kusaidia vifaa hivyo, ikiwa ni pamoja hatuwezi tukawa na *sponsorship* ya wazi kabisa kwa wanafunzi wa chuo kikuu wanaochukua masomo ya Sayansi ikiwa ni pamoja na kuwapeleka nje kusomea masomo ya sayansi ya fani mbalimbali? Huo ni mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, je, hilo halifai?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, masuala ya kuandaa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vikuu ni suala ambalo linakuja kwa wakati ule ambao tunahitaji kujenga hicho chuo. Na tunajua kabisa kwamba kila mkoa utakuwa na nafasi watakubali kutoa maeneo iwapo Wizara itakuwa imekuwa tayari kujenga chuo kikuu katika eneo hilo.

Kwa hiyo hilo sio tatizo, taratibu zote za ujenzi wa chuo kikuu ikiwepo pamoja na utafutaji wa maeneo utafuatwa kwa wakati muafaka. Kwa hiyo nafikiri Mheshimiwa hilo sio tatizo, tatizo letu tumesema ni pesa, lakini maeneo ya ujenzi sio tatizo. Swali la pili kwa masomo ya Sayansi kama nilivyosema hatua zote nilizotaja Wizara imefanya kwa makusudi kabisa kwa ajili ya kuendeleza somo la sayansi. Kwa wavulana na kwa wasichana, na kwa wasichana nimetaja mikakati, na kwa kweli tunatoa *sponsorship* kwa wanafunzi wote wanaochukua masomo haya ya sayansi. Sasa labda Mheshimiwa alikuwa anazungumzia *granty* ambapo hatuna pesa ya kutosha kutoa kwa wanafunzi wote *granty*, lakini *granty* tunatoa kwa wanafunzi wanachukua udaktari, tukijua kwamba tunahitaji madaktari mengi, tunatoa kwa wale wanaochukua masomo ya udaktari katika vyuo vyetu vya umma, chuo cha Muhimbili.

Kwa hiyo Serikali imeshajitahidi na nafikiri akisoma jibu langu ataona hii mikakati nilivyoitaja na inatosheleza sasa kama tutakuwa na pesa basi tutaendelea kutoa *granty* kwa ajili ya wanasayansi wetu na hasa madaktari. Pia sisi Wizara ya Elimu ya Juu tuna taasisi ya *TEHA,* Mamlaka ya Elimu Tanzania, Mamlaka ya Elimu Tanzania ina *sponsor* na inatoa vifaa vya maabara kwa shule zetu za sekondari, na vifaa vya maabara maana yake vikasaidie kujifunza masomo ya sayansi. Kwa hiyo Serikali ina mikakati hiyo na tunaomba muendelee kuchangia mamlaka haya au mfuko huu wa elimu ili usaidie katika kutoa vifaa hivi vya sayansi kwa ajili ya shule zetu na hivyo kuweza kupata wana sayansi bora.

Na. 348

**Elimu ya Watu Wazima**

**MHE. AZZAN M. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, takwimu zinaonyesha kwamba, elimu ya watu wazima imeshuka sana ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo watu wengi walijitokeza kujiunga na elimu hyo, lakini sasa elimu hiyo ni sawa na kwamba imekufa kutokana na wafadhili kujitoa katika kugharamia elimu hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujifufua elimu hiyo ili Watanzania wengi zaidi waelimike.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua suala la kushuka kwa elimu watu wazima nchini. Hivi sasa Wizara inaandaa mpango mkakati wa kuimarisha na kuendeleza elimu ya Watu Wazima kwa kushirikiana na wataalam kutoka Cuba ambao tayari wamekwisha anza kazi hiyo.

Aidha, Serikali itaendelea na jitihada za kuimarisha programu za MUKEJA na MEMKWA kwa kuboresha mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa katika utoaji wa elimu ya watu wazima. Lengo ni kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanapata elimu hiyo ili kufuta ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu. *(Makofi)*

**MHE. AZZAN M. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sababu nyingine kubwa sana iliyojitokeza kwa elimu ya watu wazima kushuka ni malipo au posho ndogo wanayolipwa walimu hao.

Je, Serikali sasa ina mikakati ipi ya kuhakikisha kuwa angalau inaongezea malipo kwa walimu hao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Azzan Zungu kama ifuatavyo. Ni kweli posho inayotolewa kwa walimu hao wanaofundisha elimu ya watu wazima ni kidogo, wameshalalamika mara nyingi kuhusu suala hili lakini kama mnavyoelewa shughuli hii ya elimu ya watu wazima imekuwa ni kazi ya kujitolea na ndio maana hatuna ajira ya kudumu kwa watu hao wanaofundisha elimu ya watu wazima. Tunatoa tu posho ya kuwakimu tu ili wanapokuwa katika eneo lile la ufundishaji wapate walau kiasi kidogo cha kuweza kuwasaidia, hii ajira ni makubaliano ili waweze kusaidia kuondoa ujinga katika nchi yetu ya Tanzania ndio maana tunaingilia. Lakini kama suala hilo la posho linalozungumzwa ni suala la kujadiliana pale Serikali itakapokuwa na uwezo Serikali itaweza kuongeza lakini kwa sasa tunasema tunatoa hiyo kama posho kwa wale wanaojitolea kufanya kazi hiyo ya kufundisha elimu ya watu wazima.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya mimi kuongezea katika majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu swali la nyongeza la Azzan Zungu kutoka Ilala. Mimi ningetaka kusema kwamba elimu ya watu wazima hapa katikati imetetereka kiasi fulani kutokana na kutegemea misaada kutoka nje, kwa hiyo mimi ningeshauri kwamba halmashauri hazikatazwi kutoa posho zaidi katika maeneo yao ili hao walimu waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu tunaogopa sisi kama Wizara ya Elimu kuendelea kuongeza fedha wakati hasa katika sehemu kubwa itegemee misaada. Kwa hiyo halmashauri mpo huru kuongezea chochote kwa kile wanachokipata walimu ili waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu elimu ya watu wazima kwa kweli ina umuhimu wake.

Na. 349

**Vyuo vya Kufundisha Maafisa wa Afya**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa waganga (*Clinical Officers)* hapa nchini; na kwa kuwa zipo zahanati ambazo zinaendeshwa na Wauguzi Wasaidizi (*Nursing Auxiliaries*) zikiwemo zahanati za Wilaya ya Mpwapwa; na kwa kuwa vipo Vyuo vya Afya ambavyo vilikuwa vinafundisha Maafisa wa Afya Wasaidizi (*Health Assistants*) na mafunzo hayo yalisitishwa:-

Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuvitumia Vyuo hivyo vya afya vya Ngudu, Kagemu, Mpanda, Iringa na kadhalika, kufundisha waganga hao (*Clinical Officers*) na *Up Grading* ya *Health Assistants* kuwa *Health Officers* ili kupunguza tatizo la wataalam/Waganga nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Kwa hivi sasa kuna jumla ya vyuo 14 vinavyotoa mafunzo ya utabibu (*Clinical Medicine*) hapa nchini. Vyuo hivyo ni Bumbuli, Kigoma, Kilosa, Kibaha, Lindi, Lugalo *JWTZ*, Mafinga, Masasi, Maswa, Mtwara, Musoma, Sengerema, Songea, na Sumbawanga. Takriban wataalam 600 huhitimu toka kwenye Vyuo hivyo kila mwaka.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa sasa haikusudii kuongeza idadi ya vyuo bali kupanua uwezo wa vyuo vilivyopo ili viweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi na kutoa taaluma iliyo bora zaidi kwa kuongeza nafasi za madarasa, mabweni, maktaba na kuvipatia vyuo hivyo walimu wa kutosha na wenye sifa zinazohitajika..

Kwa kuwa idadi ya Maafisa Afya hapa nchini nayo ni ndogo sana kulingana na mahitaji, Wizara yangu haina mpango wa kuvitumia Vyuo vya Ngudu na Kagemu kufundishia Maafisa Tabibu (*Clinical Officers*) bali vitaendelea kufundisha Maafisa Afya kama vile Vyuo vya Mpwapwa, Muhimbili na Tanga.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu nina maswali ya nyongeza. Kwa

kuwa Vyuo vya Afya vya Kagera Kagemu, Ngudu, Mpanda na Iringa walikuwa wanafundisha maafisa wa afya wasaidizi na kada hii ilikuwa muhimu sana kwa ajili ya kutoa elimu ya afya vijijini na kwa kuwa mafunzo hayo yasitishwa. Je, ni sababu zipi za msingi zilizofanya kada hii ya *Health Assistants* kusitishwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa waganga katika zahanati, vituo vya afya na hospitali zetu na kufuatana na idadi ambayo ameitaja Mheshimiwa Naibu Waziri sasa mimi naomba nifahamu. Je, maadili ya uganga au *Medical Ethics* zinaruhusu *Nursing Auxiliary* ku-*prescribe* dawa kwa kuwa hospitali ni zahanati nyingi zina hawa *Nursing Auxiliaries*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) :** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo.

(a) Kufutwa kwa *course* ya *Health Assistants* ni kuendana na wakati kwa sababu kada hii ilikuwa na taaluma ndogo sana hivyo basi kuwa kozi ya *Health Officer* ni kwa maana tunataka kupeleka huduma zilizo bora kwa wananchi vijijini.

(b) Kwa wauguzu ku-*prescribe* dawa au kuandika dawa si kazi yao lakini pale ambapo kuna matatizo kwa sababu nia njema kabisa ni kuokoa wale wagonjwa basi wanaweza wakasaidia kwa sababu pale pasipo daktari hata mganga wa kienyeji husaidia wananchi.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, kwa kuwa tatizo la upungufu wa waganga siyo *clerk officers* nchini linatugusa sana Wilaya yetu ya Namtumbo tuna upungufu mkubwa sana na kwa kuwa Serikali ili-*allocate* waganga wauguzi wasaidizi 56 Wilayani kwetu na walioripoti ni sita tu.

Je, Serikali inaweza kuruhusu wale waliokuwa na sifa na waliokosa fursa ya kuomba kupitia Wizarani wakaomba kule kule Halmashauri na maofisa wa Wizara ya Afya wakaja kuwasahili na kuasisi sifa zao na kutoa kibari cha ajira?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Spika, ajira za Serikali zinatolewa kwa nafasi zile zilizopo kwa kupeleka taarifa Wizara ya Utumishi ambayo ndio hao hutoa kibali cha ajira kwa maana ya kwamba kwa sasa Serikali imeshaweka wazi kwamba madaktari, wauguzi na waganga wasaidizi wataajiriwa moja kwa moja kufuatana na taaluma yao. Hivyo basi ni wajibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kupeleka taarifa ya nafasi zilizo wazi utumishi ili waweze kuruhusiwa kuajiri.

Na. 350

**Mpango wa Bima ya Afya**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilianzisha mpango wa Bima ya Afya kwa watumishi ili uwasaidie kupata tiba bila usumbufu, na kwa kuwa, wanachama wa mfuko wa bima hupewa vitambulisho vya kuwawezesha kupata tiba:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa, kuna watumishi wanaolipa Bima ya Afya na hawapati tiba kutokana na Bima ya Afya kwa sababu hawajapewa vitambulisho (kadi);

(b) Je, Serikali iko tayari kuwarudishia watumishi pesa waliyokwisha katwa bila kupata huduma ili waanze upya baada ya kupewa vitambulisho.

(c) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge sababu zinazosababisha watumishi kukosa vitambulisho huku wakiendelea kukatwa pesa za mishahara yao.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa ya kuwa kuna watumishi ambao ni wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambao hawapati matibabu kutokana na kutokuwa na vitambulisho, isipokuwa kuna taarifa ya baadhi ya watumishi ambao hawajawasiliasha fomu na ambao fomu zao zinakosa taarifa muhimu za kuwawezesha kutengenezewa vitambulisho.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uchangiaji katika mfuko huu hauruhusu Mfuko kurudisha fedha kwa mwanachama asiyepata huduma. Hii ni kwa sababu fedha inayochangwa na kila mwanachama na huingizwa katika kapu moja ili atakayeugua atibiwe kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo lake na sio kiasi alichochangia. Hii ndipo sababu hata wale wasiougua hawaruhusiwi kisheria kudai pesa yao. Kwa msingi wa maelezo hayo na kwa kuzingatia sheria iliyounda mfuko wa bima ya afya, Serikali haiwezi kurejesha fedha kwa watumishi waliokatwa bila kupata huduma.

(c) Mheshimiwa Spika, sababu zinazosababisha wanachama kutopatiwa vitambulisho vya matibabu kwa wakati ni kama zifuatazo:-

1.Watumishi husika kuendelea kukaidi kujaza fomu za uandikishaji kwa kisingizio cha kutokuwa na picha zao za wategemezi wao. Hadi tarehe 30 Aprili 2007, asiliamia 16% ya watumishi wachangiaji walikuwa bado hawajajaza fomu hizo.

2. Watumishi kutoa taarifa zisizo kamili au zenye mapungufu na wakati mwingine kukosea kujaza fomu za uanachama na hivyo kusababisha kuchelewa kwa maandalizi ya vitambulisho husika.

3.Waajiri yaani Idara za Serikali, Wizara na Halmashauri kutowasilisha mapema fomu za watumishi wao ili vitambulisho viandaliwe kwa wakati.

4.Waajiri kushindwa kusambaza vitambulisho vya matibabu vya watumishi na wategemezi wao kwa wakati na hivyo kuendelea kukaa navyo kwa muda mrefu.

5.Waajiri kushindwa kutunza vitambulisho husika mara wavipokeapo na wenginge hata kuvipoteza bila kuwa na kumbukumbu sahihi na hivyo kupeleka malalamiko kutoka kwa wanachama na wategemezi wao.

6.Watumishi kutojaza fomu kwa sababu kisingizio cha kutougua mara kwa mara hivyo kutokuona umuhimu wa kuharakisha kujaza fomu.

7.Watumishi wa Sekta ya Afya na wenye ngazi za juu Serikalini hupata matibabu bila kuonyesha vitambulisho. Hata hivyo jambo hili tumekwisha litolea miongozo kwa vituo vya Serikali kuwa wasitoe matibabu bila mtu kuonyesha kitambulisho au kibali cha muda kwa sababu kwa kufanya hivyo wanavinyima vituo vyao mapato.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mtu hunatoa pesa kwa ajili ya kupata matibabu na huo unakuwa ni mkataba baina ya Wizara ya Afya na Mtumishi mhusika, sasa anapokuwa amechanga michango yake na asipate matibabu na anapokuwa ameruhusiwa asirudishiwe pesa ambazo alizokatwa Serikali haioni kwamba huko ni kumwibia mtumishi? Je, Serikali inafahamu kwamba hata wale ambao wameruhusiwa wanavyo vibali kwa kuwa mara nyingi hospitali huwa hazina hela zinategemea kutumia pesa za michango kununua madawa jambo linalosababisha kwamba hata wale walio na vibali kuna madawa mengine wanayoambiwa waende wakanunue kutoka mahali pengine. Je, Serikali inajua hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Phares Kabuye, kama ifuatavyo. Kwanza kabisa ieleweke kwamba maana ya mpango wa Bima ya Taifa ya Afya imejengeka katika utaratibu wa kuchangiana huduma za afya katika vipindi vya dharura kwa maana inakuwa ni *social solidarity and risk pulling* na chini ya utaratibu huu hakuna suala la *account* ya mtu mmoja mmoja na hivyo basi fedha zinaziokusanywa huwekwa katika kapu moja yaani *baskets.*

Mheshimiwa Spika, pili, kwamba pesa hizo zikichangwa zinatumika kwa ajili ya vile vituo ambavyo vinakuwa vimeishiwa zile pesa na hivyo hata wale watu ambao walistahili kupata hizo dawa hawapati, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba pesa hii imewekwa ili watu wachangie ili katika nyakati hizo za dharura pesa hiyo itumike. Kwa hiyo haijali ile pesa anayotumie ni ile aliyochangia au yule

mwananchi wa kawaida ambaye anapata chini ya utaratibu wa kutoa huduma za Serikali. *(Makofi)*

Na. 351

**Suala la Kuundwa kwa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeunda Mabaraza ya Ardhi toka ngazi za Kijiji hadi Wilaya kwa lengo la kushughulikia migogoro ya ardhi kwa wananchi; na kwa kuwa, Baraza la Ardhi la Wilaya kwa mkoa wa Kigoma liko mjini Kigoma tu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunda Mabaraza ya Ardhi kila Wilaya kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Kibondo ambao kwa jiografia ya Wilaya hiyo wanashindwa kufika Makao Makuu ya Mkoa ili kufuatilia haki zao za msingi pale Mabaraza ya chini yanaposhindwa kuwatendea haki.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, zilitungwa sheria mpya za Ardhi Na. 4 na 5 za mwaka 1999, Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Sheria hizi zimeweka mfumo mpya wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba ambao unaanzia ngazi ya kijiji hadi Mahakama ya Rufaa.

Aidha, Sheria Na.2 ya mwaka 2002 imetungwa ili kuunda na kutoa majukumu na mamlaka ya Mahakama mbalimbali za kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba. Mahakama hizo kwa mujibu wa sheria mpya za Ardhi ni Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi na Mahakama ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, mwenye mamlaka ya kuunda Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Mabaraza ya Kata na kusimamia utendaji wa mabaraza hayo ni Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, Waziri wa Ardhi anao uwezo wa kuunda Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na analo jukumu la kusimamia Mabaraza hayo. Sheria Na.2 ya mwaka 2002 imezingatia uwezo mdogo wa Serikali. Kwa hiyo, inamruhusu Waziri wa Ardhi kuunda Mabaraza haya katika ngazi ya Wilaya, Mkoa au Kanda.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma Waziri ameunda Baraza katika ngazi ya Mkoa ambalo liko Kigoma Mjini. Baraza hilo tangu liundwe mwezi Novemba, 2005 hadi Aprili, 2007 lilikukwa na mashauri 119 kati ya hayo mashauri 15 yanatoka Wilaya ya Kibondo. Inawezekana idadi ndogo ya mashauri yaliyofunguliwa katika Baraza kutoka Wilaya hiyo inatokana na umbali mrefu kutoka Kibondo kwenda Kigoma Mjini. Kwa hiyo, kwa kuwa gharama za kuunda na kuendesha Mabaraza ni kubwa na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kibondo wanagharamia umbali mrefu kufuatilia haki zao, Wizara itawasiliana na Uongozi wa Wilaya ya Kibondo ili kupata ofisi ambayo itakuwa inapokea mashauri mapya katika Wilaya ya Kibondo na hatimaye Mwenyekiti wa Baraza atakwenda huko kusikiliza mashauri na kuyatolea maamuzi huko huko.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali madogo mawili kama ifuatavyo. Napenda kukiri kwamba Naibu Waziri ameona kwamba Baraza la Mkoa wa Kigoma lina kesi 119 mpaka alipofikisha hesabu yake hapa. Lakini napenda kumweleza kwamba utendaji wa kazi wa Baraza la Mkoa wa Kigoma linafanya kazi kwa kusua sua sana kutokana na wazee wa Baraza kushindwa kuhudhuria vikao kutokana na kutolipwa posho zao.

Je, Serikali ina msimamo gani kuhusu hilo?

Mheshimiwa Spika, pili, ni lini hawa wazee watalipwa posho zao kusudi kazi ya Baraza iendelee na ni lini mtandao wa Baraza hilo utaenezwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma ili kuondoa adha inayoendelea na umbali uliopo kwa wilaya zote tatu za Mkoa wa Kigoma. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kijiko kama ifuatavyo: Nasikitika kusikia kwamba Baraza la Mkoa ambalo liko Mkoani Kigoma linasuasua kutokana na ulipaji wa posho, tutalizingatia hilo tutakaporudi ofisini tutalifuatilia kwa makini au kutizama kwa nini hawajapewa posho yao mpaka sasa hivi kwa sababu kutokana na sheria Na. 2 ya ulipaji wa fedha ya mwaka 1982 lazima Baraza hilo wajumbe walipwe posho kwa wakati unaopaswa.

Mheshimiwa Spika, la pili kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali haina fedha ya kuanzisha Mabaraza Wilaya zote na nimetoa wito katika *Budget Speech* yetu kwamba tunaomba wilaya ambazo zina majengo watuambie na kutusaidia kutoka kwa Mkuu wa Wilaya au Halmashauri ili tuweze kupata majengo ya kuanzisha Mabaraza hayo. Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kabisa kuchagua wenyeviti pamoja na wajumbe ili Mabaraza yaweze kuanzishwa mara moja. Lakini kwa sasa bado tutajitahidi kutumia yale ya mkoa na pale ambapo kuna matatizo ya ziada kama ya Wilaya ya Kibondo tutafuata huko na Mwenyekiti atakuwa anakuja katika maeneo yenu.

Na. 352

**Mrundikano wa Wafungwa na Mahabusu Magereza**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza mrundikano huo?

(b) Je, endapo hali hiyo itaendelea na kutokea maafa nani atakayepaswa kuwajibika?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah, lenye sehemu (a), (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza mrundikano wa mahabusu Magerezani Serikali inachukua hatua mbalimbali zifuatazo:-

(a) Kuongeza idadi za Majaji na Mahakimu katika ngazi mbalimbali. Mathalan hivi karibuni majaji ishirini na moja wa Mahakama Kuu na wawili wa Mahakama ya Rufaa waliteuliwa;

(b) Kuanzisha Kamati za kusukuma kesi za Mikoa na Wilaya. Kamati hizi hujadili kesi zote zenye matatizo na kuziwekea mikakati ya kuzimaliza;

(c) Kutembelea Magereza kunakofanywa na Majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali kwa lengo la kusikiliza malalamiko ya mahabusu;

(d) Kupitia kesi kwa lengo la kupata uchambuzi wa kisheria na kufuta kesi zote zisizo na ushahidi;

(e) Kuongeza idadi ya vikao vya kusikiliza mashauri ya mauaji; na

(f) Kuharakisha ushughulikiaji wa majalada yote yanayopelekwa kwa uchambuzi wa kisheria kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa mahabusu Magerezani ni matokeo ya tuhuma dhidi yao na pia katika kuhakikisha kuwa sheria inafuata mkondo wa kulinda na kutetea haki za wanaofanyiwa makosa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kuhakikisha kuwa hali za mahabusu na mazingira wanamoishi yanaboreshwa ili kuepusha aina yoyote ya maafa inayoweza kutokea. *(Makofi)*

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Unaonaje Mheshimiwa Waziri iwapo sheria ya *parole* ikatumika vizuri. Je, isingepunguza mlundikano na huu mfuriko wa Magerezani?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vuai Abdallah kama ifutavyo.

Ni kweli sheria ya *parole* pamoja na ile sheria ya *Community Service* zinasaidia sana kupunguza mlundikano katika Magereza lakini zaidi ya yote pia Serikali inajitahidi kuongeza mabweni ya mahabusu kwa mfano tumefanya hivyo kule Kahama, Bangwe, Njombe, Morogoro, Iringa na Arusha na sasa hivi *actual capacity* ya kuwashikilia hawa mahabusu na wafungwa imeongezeka kutoka wafungwa na mahabusu 22,669 mpaka 27,653 hii ni jitihada zote tunazozifanya katika kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa.

Lakini nakubaliana naye kwamba kweli sheria ya *parole* tutazidi kuitekeleza pamoja ile sheria ya *Community Service.*

Na. 353

**Magari Yanayoegeshwa Kando ya Barabara Kabla ya Mizani ya Kibaha**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na mtindo wa kuegesha magari makubwa kando kando ya barabara kabla ya Kituo cha Mizani ya Kibaha, hali inayosababisha usumbufu na usalama wa barabara hiyo kuu:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu hali hiyo kabla athari mbaya haijatokea?

**NAIBU WAZIRI WA USALAM WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magari ya mizigo yanayoegeshwa barabarani kuelekea kwenye kituo cha Mizani cha Kibaha, hufanya hivyo ili kusubiri kupima uzito kwa mujibu wa sheria kwa lengo la kuzuia uharibifu wa barabara zetu ambazo zimejengwa kwa gaharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafanyabiashara wengi hupenda kusafirisha mizigo yao nyakati za jioni, kutokana na sababu mbalimbali, magari hayo hujikuta yamefika kwa wakati mmoja eneo hilo na kuegeshwa kusubiri ukaguzi kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi litaendelea kuhakikisha kuwa madereva wa mgari mengine yasiyohusika hawaegeshi magari yao ovyo kwenye eneo hilo la mizani ili kuimarisha usalama na kuondoa usumbufu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Je, atakubaliana na mimi kwamba kwa sababu kimeanzishwa kituo kingine cha ukaguzi wa magari kilometa chache kabla ya kufika Kibaha ukitokea Dar es Salaam na kwamba hakijaangaliwa na kinasababisha msululu.

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja kwa kweli kwa eneo hilo sasa litizamwe liwekwe rasmi kama ni kituo cha ukaguzi na kiandaliwe ili kuzuia misululu ya magari?

**NAIBU WAZIRI WA USALAM WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa William Shellukindo kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kumhakikishia kwamba ushauri wake ni mzuri tutaenda kufanya kazi ili tuone kama hali hiyo itasaidia. Aidha hivi sasa Wizara ya Miundombinu ina mpango wa kuimarisha miundombinu katika eneo lile kwa ajili ya kuondosha usumbufu huo kwa kipindi kirefu.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumwuliza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa mwanzo wa awamu hii Mheshimiwa Rais wetu alionyeshwa kukerwa sana na mtindo huu wa kuyarundika magari katika vituo hivi vya kupima uzito na kwa kuwa bado hili suala linaendelea na kimsingi ni kuwa hakuna haraka katika jambo hilo, mara utaona watu wanaitwa ndani mara wanarudi garini.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni wakati umefika sasa wa polisi kusimamia jambo hili liende haraka ili usumbufu usitokee?

**NAIBU WAZIRI WA USALAM WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimwia Khalifa Suleiman Khalifa, kama ifuatavyo.

Ni kweli anachokisema kwamba kwa askari kuhakikisha kwamba inasaidia usumbufu usitokee ni jambo zuri na ushauri huo tutauchukua na tutaufanyia kazi. Hatupendi kuona wananchi wetu wanasumbuka. Kwa hiyo, hilo ni jambo la busara kufanya hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda sasa umefika wa kusitisha shughuli za maswali lakini naona tunaweza kumaliza hili moja kwa sababu tunafidia ule muda wa awali ambapo tulikuwa tunapokea matangazo mbalimbali na taarifa.

Kwa hiyo, swali la mwisho ni la Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi na linaelekezwa Wizara hiyo hiyo ya Usalama wa Raia.

Na. 354

**Matumizi ya Baiskeli Vijijini**

**MHE. VEDASTUSI MATHAYO MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo mengi ya Mji na Vijiji hayafiki kwa urahisi kutokana na ubovu wa barabara, na kwa kuwa, badala ya magari watu wengi hutumia pikipiki na baiskeli lakini kulingana na Sheria za Usalama barabarani watu hawaruhusiwi kubebwa kwa baiskeli:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya mabadiliko ya Sheria hiyo ili baiskeli ziweze kubeba abiria?

(b) Je, Serikali haioni kutoruhusu abiria kutumia baiskeli kunazuia Maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria zinazotumika kuratibu na kuongoza matumizi ya Vyombo vya Usafiri yakiwemo Magari, Pikipiki, Baiskeli na kadhalika haziruhusu Pikipiki na Baiskeli kutumika kibiashara kusafirisha abiria. Sheria hizo ni Sheria Na.30 ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973, Sheria ya Bima za Magari ya mwaka 2002 na Sheria Na.10 ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973 pamoja na kanuni zake, kwani vyombo hivyo siyo vyombo vya kubeba abiria kibiashara.

Hata hivyo, kutokana na maombi mengi ya wananchi kupitia Wabunge wao, Serikali iliahidi kuifanyia marekebisho sheria hiyo na kuleta marekebisho hayo hapa Bungeni katika mkutano wa Tisa wa Bunge utakaofanyika Oktoba/Novemba, mwaka huu 2007.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia na kuheshimu Sheria iliyopo sasa inayotawala matumizi ya Baiskeli na Pikipiki siyo kuzuia Maendeleo ya wananchi wetu kwani wananchi wana ruhusa ya kutumia vyombo hivyo kuwarahisishia usafiri katika shughuli zao za kila siku za kujiletea Maendeleo. Kinachokatazwa na sheria ya sasa ni kutumia vyombo hivyo kufanyia biashara ya kubeba abiria ili kulinda usalama wa abiria na mwenye chombo, kwani vyombo hivyo havina bima na leseni ya biashara.

Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira wakati Serikali inaendelea na mchakato wa kutafakari suala hili, ili kuona masuala muhimu yatakuwaje, kama vile bima endapo itatokea ajali, leseni ya biashara, maeneo yatakayoruhusiwa kufanya biashara hiyo na kadhalika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUSI MATHAYO MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo amewapa wananchi wa Musoma na Watanzania kwa ujumla matumaini makubwa. Swali langu dogo ni kwamba ninapenda kujua pamoja na utaratibu huu ambao Serikali inauandaa wa mafunzo pamoja na leseni na mambo mengine. Ninapenda kujua Serikali itakuwa tayari kwenda kujifunza katika maeneo mengine kama China na India namna ya utumiaji wa vyombo hivyo ili ufanisi mzuri uweze kuwepo?

**SPIKA:** Na kwenye ziara hiyo bila shaka unaomba na wewe uende siyo? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia napenda kumjibu Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo;

Ushauri wake ni mzuri tuko tayari kujifunza kwa sababu nia yetu ni kutengeneza Sheria iliyo nzuri na itakayokidhi haja ya wananchi wetu na wananchi wetu wasipate usumbufu na matatizo ya aina yoyote.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwishapita.

Matangazo kuhusu wageni ni haya, lakini nitaanza wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kazi ambaye ndiye mtoa hoja wa leo Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, anao pale kwenye *gallery* wageni kama ifuatavyo:-

Katika *Speakers Gallery* yupo Mke wa Waziri Mwali Grena Chiligati, karibu sana naomba usimame tafadhali.

Sielewi hii jitihada ya Wabunge kusema hawajamwona na kurudia kumwona. (*Kicheko*)

Yupo pia na Dada yake nadhani ni Dada yake Mheshimiwa Waziri huyu ni Mrs. Mwatujobe, karibu sana. Karibuni sana.

Kutoka Wizarani ni wengi na ningeomba licha ya Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba yupo pia Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi Bibi Edna Mangesho, karibu sana. Naona Wizara hii imezingatia jinsia kuna mchanganyiko hapo.

Halafu kuna Mwenyekiti wa Kamisheni ya Usuluhishi na Upatanishi Ndugu Adam Simbeye, huyu Bwana nadhani ni yule tunayemwona kwenye TVT akihojihoji mambo. (*Makofi*)

Yupo Bwana Cosmas Msigwa Mkurugenzi wa Kamisheni ya Usuluhishi na Upatanishi, Bwana Nestor Ngula ambaye ni Katibu Mkuu wa Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania, Bwana Ally Kiwenge, Katibu Mkuu wa TUGHE, Bwana Nicolous Mbwanji, Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania, Bwana Samuel Mtali, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la *TIJA (NIP),* Bwana Ferdinand Kasenge Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la *TIJA (NIP),* Dr. Ramadhan Dau Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF*.

Niseme tu Dr. Ramadhan Dau ni mmoja wa watu waliosimamia vizuri sana Taasisi yake kuweza kuchangia ujenzi wa Ukumbi huu. (*Makofi*)

Yupo Bibi Blandina Nyoni ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *NSSF* ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Bwana Kassim Kitumbo Mtendaji Mkuu wa *OSHA,* sijui *OSHA* ni kitu gani lakini tutaendelea kufahamu Waziri atakapotoa

hotuba. Bi. Deborah Nyakirang'anyi Mwakilishi wa *International Labour Organisation* yaani *ILO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati hakusahau Jimbo lake wapo wapiga kura wake kutoka Jimboni wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Manyoni Mjini, Ndugu Khamis Masabuni, karibu sana. Amevaa rasmi kabisa huyu. Hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko/Makofi*)

Naibu Waziri wa Kazi Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari ana wageni wake kama ifuatavyo:-

Kwanza ni mkewe Miriam Solomon Sumari, karibu sana. Lakini pia ana wageni wengine itabidi niwataje kwa ujumla wao tu.Kutoka Jimbo la Arumeru Mashariki, wapo Makatibu Kata wote nao ni Leguruki, Mbuguni, Mkwarua. Naomba Makatibu Kata wote wa Jimbo la Arumeru Mashariki wasimame pale walipo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia Makatibu Wenezi kutoka Jimbo hilo hilo wako kumi na nne (14) naomba wasimame, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, Naibu Waziri mwingine katika Wizara hiyo hiyo anao wageni wake kama ifuatavyo:-

Kwanza ni mke wake Jane Kijazi Nchimbi, karibu sana.

**MJUMBE FULANI:** Asimame tena! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ilistahili Naibu Waziri aseme kwamba pamoja na mtoto wao mchanga, hongera sana Mama Nchimbi kwa kutuletea Mtanzania mwingine tena. *(Makofi)*

Yupo pia Baba Mzazi wa Naibu Waziri ni rafiki yangu sana huyu naye ni Ndugu John Nchimbi, nafurahi sana kukuona. Amefanya kazi nyingi akiwa Kamanda wa Polisi na pia katika Chama cha Mapinduzi wengine mtakumbuka aliwahi kuwa Katibu wa CCM wa Mikoa kadhaa. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia yupo Mama Mzazi wa Naibu Waziri naye ni Bibi Selva Nchimbi, ahsante sana Mama na karibu sana. Nadhani Dr. Emmanuel John Nchimbi ameongeza sasa upeo wa mambo kwa sababu siyo tu Mawaziri walikuwa wanaleta wake zao na Watoto lakini sasa wanakuja na wazazi. Yote ni baraka, ni baraka kuona jinsi uzao wenu unavyofanya kazi katika kuwahudumia Watanzania. Yupo pia Shemeji yake Dr. Emmanuel John Nchimbi Bi. Monica Kijazi, karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunaye Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Tanzania Ndugu Amina Mabruk, karibu sana. Ahsante sana Mheshimiwa Amina na vazi lako linapendeza sana. (*Kicheko/Makofi*)

Tunaye pia Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana Ndugu Amos Makala, karibu sana. Tunaye pia Mwenyekiti wa CCM Taifa Ndugu Lydia Richard Mabenga, karibu sana. Pia

wapo Wenyeviti kadhaa wa Umoja wa Vijana wa CCM wa Mikoa ya Tanzania, karibuni sana. Wale mnaogombea *NEC* katika Chama Cha Mapinduzi basi kazi kwenu hapo tena. (*Makofi*)

Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William M. Ngeleja anao wageni wawili nao ni Ndugu Paul Malimbo kutoka Dar es Salaam na Ndugu Constantino Kanyasu ambaye ametambulishwa kama ni Mwenyekiti wa Vijana nadhani ni kutoka mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi wa Muleba Kusini anao wageni nao ni Bwana Mathiam Mugata ambaye ni Mwenyekiti wa Vijana nadhani Mkoa wa Kagera, Bwana Mpokwa Abdallah Mpokwa ambaye ni Katibu wa Vijana, Ndugu Aristide Murio ambaye ni Mjumbe Baraza Kuu na Ndugu Hamimu Mahamudu ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Vijana Mkoa. Karibuni sana. *(Makofi*)

Mheshimiwa Monica N. Mbega Mbunge wa Iringa Mjini na Mkuu Mkoa wa Mkoa wa Ruvuma anao Walimu wanane kutoka Manispaa ya Iringa wakiongozwa na Afisa Elimu Manispaa Bi. Mary Haule na Ndugu Flora Mwalyambi, Mkaguzi Mkuu Elimu Wilaya, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila ana wageni wawili, wa kwanza ni Mzee Alex Sakila ambaye ni Baba yake mzazi, Mzee Alex Sakila karibu sana Mzee wetu. (*Makofi*)

Pia Mwalimu Deusdedit Manegese ambaye ndiye aliyemwandikisha shule Darasa la Kwanza Mheshimiwa Bujiku P. Sakila yaani ni Mwalimu wake wa Darasa la Kwanza Mheshimiwa Bujiku P. Sakila. Ahsante sana kwani ni faraja kubwa sana kuwaenzi watu muhimu kama hao. Karibuni sana.

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Mbunge wa Kyela Dr. Harrison George Mwakyembe, ambao wanaongozwa na Mjumbe wa *NEC* Taifa Bwana Nape Nauye, pamoja na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi yaani TUGHE. *(Makofi*)

Wanafunzi 40 kutoka shule ya Sekondari ya Dodoma yaani *Dodoma Secondary School* na walimu wao pia, karibuni sana. (*Makofi*)

Nimeona imebadilishwa hii ilikuwa inaitwa *UCLAS* sasa ni Chuo Kikuu cha Ardhi, wanafunzi 16 kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, karibuni sana Wataalamu wetu . (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi kutoka *Jubilee High School Dodoma* nadhani wamekosa nafasi leo *Gallery* zimejaa kabisa na wanafunzi 30 kutoka Shule ya Sekondari ya

Kikuyu, naona wamekosa nafasi kama mnavyoona *Gallery* zimejaa kabisa, lakini Karibuni sana.

Wageni wetu wengine ni wale wa Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujebga Taifa, ambaye ni Bwana Juma Abdallah Kipesa, ambaye anatoka Jimbo la Kiembesamaki, Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga Naibu Waziri wa Wizara ya Miundombinu ni Khalid Hussein Kingi Katibu Kata, Kata ya Tabata, Bwana Mohamed Michuzi, Msaidizi wa Mbunge, ahsante sana. Msaidizi wa Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga anaitwa Michuzi. Nadhani kwa kule maeneo ya Tabata, Liwiti na kadhalika inasaidia sana hiyo. Yupo pia mdogo wake wa Mheshimiwa Naibu Waziri anaitwa Paschal Ezekiel, karibu sana. *(Kicheko/ Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sasa ni taarifa za Vikao na ni kama ifuatavyo:- Mheshimiwa John Momose Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, ameniomba niwatangazie kuwa leo tarehe 03/08/2008 Saa tano Asubuhi kwenye chumba Namba 231 kutakuwa na Mkutano wa Kamati ya Hesabu za Serikali, ni mkutano muhimu Ndugu Wajumbe msikose saa tano asubuhi ukumbi 231.

Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi ameniomba niwatangazie Wajumbe wote kwamba saa 5:30 kutakukwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii , Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kwa kikao kifupi sana saa 7.00 mchana jengo la utawala ghorofa ya pili wataonana hapo na watapeana taarifa waingie wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga ameniomba nitangaze kwamba leo saa 7.00 mchana jengo la utawala ghorofa ya pili watakuwa na kikao kifupi sana kwa sababu leo ni siku ya swala kwa hiyo nadhani itachukua dakika chache tu. Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wabunge kuhusu Mfuko wa Uwezeshaji Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama amenimba nitangaze kwamba saa 7.00 mchana Wabunge wote wanachama Wajumbe wa Bodi watakutana saa 7.00 mchana katika Chumba kilichomo ndani ya Ukumbi wa Pius Msekwa nadhani ni kile kilicho pembeni.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumatatu tatehe 6 Agosti kutakuwa na Semina itakayoendeshwa na Ubalozi wa Uingereza, Mheshimiwa Balozi Philip Paham na Bwana David Stanton wa *DFID* wataongoza semina hiyo saa 7.00 kwenye Ukumbi wa Pius wa Msekwa. Semina hiyo itahusu *General Budget Support* yaani tuelewe jinsi mataifa mbalimbali yanayotusaidia yanavyoleta misaada na yanavyohitaji misaada hiyo isimamiwe vizuri ili kuwanufaisha wananchi. Kwa hiyo, wataonyesha misaada yote kwa miradi yao yote na jinsi ambavyo inapaswa kusimamiwa, ni semina muhimu sana naomba Wabunge wote tuwepo. Kutakuwa na chakula cha mchana na viburudisho kabla ya kuanza semina.

Waheshimiwa Wabunge, kesho saa 10.00 pale *Jamhuri Stadium* kutakuwa na mechi kali sana baina ya timu ya Bunge na timu ya *NSSF,* kulingana na taarifa nilizozipata za jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyojifua kwa kweli *NSSF* wategemee kipigo na mimi kama mgeni rasmi nina hakika ya kukabidhi kombe linaloshindaniwa kwa Kapteni wa timu ya Bunge. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wote wanaotuunga mkono tuhudhurie kwa wingi, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi muhimize wananchi ili tuweze kuwepo pale kushangilia timu ya Bunge katika shindano hili. Naelewa kuna baadhi ya Wabunge wako kwenye Bodi ya *NSSF* sasa hawa tutawaangalia kwa makini sana. (*Kicheko*/*Makofi*)

Kesho jioni baada ya mechi kuhitimisha mambo upo utaratibu wetu uleule wa burudani katika eneo la Ukumbi wetu pale jengo la utawala na ni saa 2:30 usiku, mambo yatakayokuwepo ni kama ifuatavyo;

Kwa wale wanaopenda taarabu Afua Suleiman atakuwepo, kwa wale Wabunge vijana kama Mheshimiwa William M. Ngeleja na wenzake Wale watu wazima wa kati kutakuwa na *Msondo Music Band* na kwa wale wanaopenda kuangalia maonyesho tu kutakuwa na kikundi kinachoitwa *THT Dances* ambao wataonyesha fani mbalimbali za uchezaji. Ni burudani tosha tunaomba wote tuwepo pale ili tuweze kushughudia mambo yale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina mkutano na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wananisubiri kwa hiyo sasa nitamwomba Naibu Spika aweze kuja ili kuendeleza shughuli za Bunge kwa leo.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikali Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Naona sasa hivi Bunge letu kuna mtu ameandika kwamba ni kama vile tunaita watalii wa ndani, nilipokuwa India siku moja kulikuwa na watalii wengi sana wa ndani. Kwa hiyo, nadhani hii nayo ni nzuri kwa Dodoma. Karibuni wageni wote. *(Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayohusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Bunge lako tukufu sasa likubali kujadili mpango wa kazi na kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mbunge wa Peramiho iliyojadili na kukubali makadirio ya matumizi ya Wizara yangu tarehe 1 Juni, 2007.

Hotuba hii imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati ambao tunaamini utaiwezesha Wizara yangu kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha. Namshukuru pia Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii kwa ushirikiano wake wa karibu.

Vilevile namshukuru Waziri aliyenitangulia Mheshimiwa Prof. Jumanne, Abdallah Maghembe - Waziri wa Maliasili na Utalii sasa kwa kuniachia msingi mzuri wa kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba mkubwa uliotokea wa kufiwa na aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti na pia Maafisa wa Serikali John Bendera, Nathaniel Katinila na Theresia Nyantori waliofariki dunia kutokana na ajali ya ndege. Vile vile, kwa msiba wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, (Vijana) Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kilichotokea hivi karibuni. Mungu aziweke Roho za Marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi huu ni heshima kubwa kwa Tanzania, Aidha napenda pia kumpongeza Mbunge wa Tunduru Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa kwake katika uchaguzi mdogo wa jimbo hilo, na pia Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa viti maalumu.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2006/2007 na malengo ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilianza kutekeleza Sheria mpya za kazi yaani Sheria namba 6 ya Ajira na mahusiano kazini na Sheria namba 7 ya Taasisi za Kazi. Madhumuni ya Sheria hizo mbili ni kutoa haki na wajibu kwa wafanyakazi na waajiri ili kuongeza tija, ufanisi na uhusiano mwema kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zinazofanywa na Wizara yangu katika kipindi hiki ni maandalizi ya Sera, program na mikakati ya kukuza ajira nchini. katika kuandaa mipango hii ambayo ndiyo itakuwa dira ya kuongoza mapambazo dhidi ya tatizo la ukosefu wa ajira na hasa miongoni mwa vijana,Wizara ilishirikisha wadau mbalimbali zikiwemo Wizara zote, Serikali za Mitaa, Viongozi wa Sekta Binafsi, Vyama vya Wafanyakazi, chama cha waajiri, *NGOs* na pia Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kutoa maoni yao katika semina maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sura kamili ya kazi zinazofanywa na Wizara yangu katika kipindi cha mwaka ni kama zifuatazo;

Mheshimiwa Spika, Maendeleo Ya Kazi. Wizara yangu kupitia Idara ya Kazi katika mwaka 2006/2007 iliendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za kazi kwa Wafanyakazi na Waajiri. Matokeo yake katika kipindi hiki pamekuwa na mahusiano mazuri katika maeneo mengi ya kazi na hivyo kuleta amani na utulivu kazini, ambayo ni moja ya vivutio muhimu kwa wawekezaji. Katika kipindi hiki palitokea migogoro michache ambayo ilipatiwa ufumbuzi, ukiwemo mgogoro wa kiwanda cha Sukari cha *TPC* Moshi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji na malengo 2006/2007. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(a) Imeundwa Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 4 Mei, 2007, na tayari imeanza kufanya kazi ya kusuluhisha migogoro ya kikazi.

(b) Zimeundwa Bodi za Mishahara za Kisekta katika Sekta nane (8) ambazo ni Sekta ya Kilimo; Huduma za majumbani *(Domestic Services*); Viwanda na Biashara, Madini, Mawasiliano na Uchukuzi, Afya, Uvuvi na Usafiri Baharini na Huduma za Ulinzi Binafsi (*Private Security Services*). Bodi hizi zilizinduliwa rasmi tarehe 18 Aprili, 2007, na zimekwishaanza kazi ya kufanya utafiti katika sekta husika na zinatarajiwa kukamilisha shughuli zake mapema iwezekanavyo na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi katika sekta binafsi.

(c) Mazingira ya kazi kwa Maafisa wa Kazi Mikoani na Wilayani yameendelea kuimarishwa kwa kuwapatia vitendea kazi kama vile Kompyuta pamoja na printa. Jumla ya ofisi 9 zimepatiwa vitendea kazi hivi.

(d) Mafunzo yametolewa kwa Maafisa Kazi 25 juu ya ukaguzi wa kazi na Sheria mpya za kazi.

(e) Migogoro 268 ilipokelewa na kati ya hiyo migogoro 199 ilipatiwa ufumbuzi. Aidha jumla ya migogoro 1,902 ilipokelewa kwa utaratibu wa Sheria mpya za kazi na ilianza kushughulikiwa na Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi.

(f) Kwa kushirikiana na Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi semina ziliendeshwa juu ya uundaji na uimarishaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi na kusimamia chaguzi za mabaraza hayo katika Taasisi 38. Aidha semina 30 zilifanywa za kuwajengea uwezo wajumbe wa mabaraza haya katika dhana nzima ya kuelezea wajibu wa matawi ya vyama vya wafanyakazi sehemu za kazi, umuhimu wa ushirikishwaji wa wafanyakazi na Sheria mpya za kazi.

(g) Wizara imeendelea kutekeleza mikataba na makubaliano mbalimbali ya Mashirika ya Kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano yake. Mikutano

iliyohudhuriwa ni pamoja na *EAC, SADC, ECA, AU, UN* na mkutano mkuu wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* huko Geneva, Uswizi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Malengo ya kazi zitakazofanywa na Wizara mwaka 2007/2008 kupitia Idara ya kazi ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuendelea kutoa elimu juu ya Sheria Mpya za Kazi kwa vyama vya wafanyakazi na waajiri.

(b) Kufanya kaguzi 2,000 katika sehemu za kazi ili kuangalia kiwango cha utekelezaji wa Sheria za kazi.

(c) Kuratibu na kusimamia Sera na Sheria zinazopambana na Ajira mbaya ya Mtoto.

(d) Kusimamia majadiliano baina ya wafanyakazi na waajiri.

(e) Kuwezesha idadi kubwa ya Watanzania kufikiwa na huduma za Hifadhi ya Jamii.

(f) Kujenga uelewa juu ya viwango bora vya kazi (*Labour Standards)* miongoni mwa Jamii, na kusimamia utekelezaji wa mpango wa *decent work.*

(g) Kuratibu shughuli za Bodi za Mishahara za kisekta ili kima cha chini cha mishahara katika sekta husika kiweze kutangazwa katika robo ya kwanza ya mwaka huu (2007/2008).

(h) Kuendelea kupokea na kushughulikia madai ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara wakiwa kazini.

(i) Kukamilisha rufaa zilizowasilishwa mbele ya Mheshimiwa Waziri na Kamishna wa Kazi.

(j) Kukamilisha mashauri ya zamani yaliyopo katika Mabaraza ya Usuluhishi mikoani na wilayani.

(k) Kuratibu na kusimamia ukamilishaji wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii na Sheria ya Fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukuzaji wa Ajira Nchini. Katika mwaka wa 2006/2007 Wizara yangu imeendelea kuratibu shughuli za ukuzaji wa ajira mpya, hususan utekelezaji wa azma ya Serikali ya kusimamia upatikanaji wa ajira mpya milioni moja kati ya mwaka 2005 hadi 2010.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2007 jumla ya ajira mpya 201,390 za mwaka 2006 zilikuwa zimeripotiwa. Kulingana na takwimu hizi Sekta binafsi ndiyo inayoongoza katika uzalishaji wa ajira mpya.

Hivyo changamoto iliyopo kwa kila moja wetu ni kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za kukuza uchumi na ajira. Serikali kwa upande wake imeendelea na jukumu lake la kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji na pia kuwawezesha wananchi ili washiriki katika ukuzaji wa uchumi na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa malengo 2006/2007, Wizara yangu kupitia Idara ya Ajira ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 1997 imefanyiwa mapitio na kuboreshwa ili ikidhi mahitaji ya sasa.

(b) Imeandaliwa Programu na Mkakati wa Taifa wa kukuza ajira ambao unalenga kuhakikisha kwamba lengo la ajira milioni moja linafikiwa na hata kuvukwa ifikapo mwaka 2010.

(c) Mradi wa Mfuko wa Dhamana wa Mikopo (*Revolving Loan Fund*) kwa ajili ya wanawake wajasiriamali wadogowadogo umeendelea kuratibiwa ili kuwawezesha wajiajiri. Mikopo iliyotolewa kupitia Mfuko huu ni shilingi 222,455,342/= ambazo ilizinufaisha *SACCOS* za Tukuyu, Tanga, Muheza, Kinondoni, Temeke na Ilala**.**

(d) Mafunzo yalitolewa ya kuwawezesha wananchi kujiajiri na kuboresha miradi yao (*Demand-driven skills programme*). Jumla ya Halmashauri 16 zilihusika, na wajasiriamali zaidi ya 320 walipatiwa mafunzo mbalimbali katika fani za kilimo na ufugaji, ufundi seremala, ushonaji nguo, kutengeneza batiki, ujenzi na kadhalika.

(e) Kuandaa na kusimamia maonyesho ya Nane ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 3 -13 Desemba 2006. Jumla ya wajasiriamali 600 kutoka Kenya, Uganda, Rwanda na Tanzania walishiriki. Maonyesho haya yanatoa fursa kwa wajasiriamali wadogo wadogo katika sekta isiyo rasmi kutangaza bidhaa zao na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Maonyesho haya hufanyika kila mwaka kwa mzunguko kwenye nchi wanachama.

(f) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)* ulifanywa utafiti wa Nguvu Kazi **(***Integrated Labour Force Survey***)** ambao hufanywa kila baada ya miaka mitano. Utafiti huu huangalia hali ya ajira nchini kisekta kwa kuzingatia umri, jinsia na vigezo vingine muhimu. Utafiti huu umebaini kuna jumla watu 20,570,433 wenye uwezo wa kufanya kazi, kati yao walio na ajira ni 18,306,715**.** Hivyo idadi ya watu wasio na ajira ni 2,263,718 sawa na asilimia 11. Idadi hii inaonyesha kuna unafuu wa asilimia 1.9

katika tatizo la ukosefu wa ajira nchini ikilinganishwa na mwaka 2001 ambapo wasio na ajira walikuwa asimilia 12.9

(g) Kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Wizara iliratibu mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira; wa shilingi bilioni 21, sawa na wastani wa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa. Wadau wengine walioshiriki katika mpango huu ni Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Benki Kuu, na Tume ya Uwezeshaji.

(h) Jumla ya shilingi bilioni 10.5 zilitolewa kama dhamana kwa Benki za *CRDB* na *NMB* ili kwa pamoja ziweze kutoa mikopo kwa wajasiriamali yenye jumla ya shilingi bilioni 31.5, sawa na mara tatu ya kiasi kilichotolewa na Serikali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2007 Benki ya *CRDB,* ambayo inatoa mikopo kupitia *SACCOS,* ilikuwa imekwisha toa mikopo ya shilingi 10,413,075,500/= kwa *SACCOS 84* na kuwanufaisha Wajasiriamali 11,384. Aidha, Benki ya *NMB* ilikuwa imetoa mikopo ya shilingi 15,328,188,854/= kwa jumla ya wajasiriamali binafsi 15,960, *SACCOS 11* na vikundi 4. Kwa hiyo, jumla ya mikopo yote iliyotolewa na Benki hizi mbili toka ilipoanza kutolewa mwezi Januari 2007 hadi kufikia tarehe 30/6/2007 kwa mikoa yote ya Tanzania Bara ni shilingi 25,741,264,354/= na jumla ya wajasiriamali waliokopeshwa *ni* 27,344. Kiasi kilichotolewa kwa kila Wilaya na idadi ya wajasiriamali walionufaika kimeoneshwa kwenye .

(i) Vituo vya Ajira viliendelea kuwahudumia wananchi wanaotafuta kazi. Kwa mfano Kituo cha Ajira cha Dar es Salaam hadi Juni 2007, kiliandikisha jumla ya watafuta kazi 879 kati yao Wanawake 283 na Wanaume 596. Watafuta kazi 134 walipatiwa ushauri nasaha, mbinu za namna ya kujiajiri, na namna ya kuhudhuria usaili. Kituo kiliwasiliana na waajiri mbalimbali nchini na kufanikiwa kupata nafasi za kazi 173; pia watafuta kazi 510 wenye ujuzi mbalimbali waliunganishwa kwa waajiri mbalimbali.

(j) Ili kusambaza huduma za ajira kwa Watanzania wengi zaidi, kilianzishwa Kituo kingine cha Ajira kwa kanda ya Ziwa mnamo mwezi Mei 2007 Jijini Mwanza. Kituo hiki kitahudumia mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga na Mara.

(k) Wizara ilieendelea kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kwa wageni. Jumla ya maombi ya vibali 3,762 yalipokelewa, kati ya hayo 2,239 ni maombi mapya na 1,523 ni maombi ya kuongezewa muda. Maombi yaliyokubaliwa ni 2,472. Maombi yaliyokataliwa ni 586. Maombi yaliyohitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi ni 186.

(l) Katika kuwasaidia Watanzania wanaotafuta kazi nje ya nchi, na Watanzania walioko nje kurudi hapa nchini kufanya kazi au kuwekeza, Wizara imeanzisha kitengo cha *Cross Border Placement Services* ambacho majukumu yake ni:-

Kuwasaidia watanzania kupata ajira nje ya nchi kwa kuwaunganisha na Waajiri nje ya nchi wanaotafuta wafanyakazi.

Kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Ajira, kuandaa mazingira mazuri nchini ili kuweza kuwashawishi na hatimaye kuwavutia Watanzania wenye ujuzi waliopo nje ya nchi, kurudi kufanya kazi nchini.

Kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali kuandaa utaratibu mzuri wenye vivutio vya kuwezesha Watanzania walio na mikataba ya kazi na wafanyabiashara nje ya nchi, kurejesha sehemu ya mapato yao nchini *(remittances).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya mwaka 2007/2008. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo ili kuratibu ukuzaji wa fursa za ajira nchini:-

(a) Kuanza kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira 2007 na Mkakati wa Kukuza Ajira.

(b) Kutekeleza Programu ya Taifa za Kukuza Ajira pamoja na kuweka mfumo wa kitaasisi wa kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa kukuza ajira kuanzia ngazi ya chini hadi ya Taifa.

(c) Kuendelea kutekeleza mpango wa kutoa mafunzo ya kuwawezesha wananchi kujiajiri, kupanua miradi yao na kuongeza tija katika Halmashari ambazo hazijafikiwa.

(d) Kufanya kaguzi katika sehemu za kazi hususan kwenye Viwanda na Makampuni binafsi kwa lengo la kufuatilia kama waajiri wanafuata sheria na taratibu za nchi kuhusu ajira.

(e) Kukamilisha na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Huduma za Ajira. Sheria hii itatoa mwelekeo wa kisheria wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2007.

(f) Kuendelea kuratibu fedha za Mfuko wa Dhamana (*Revolving Loan Fund*) wa kuwawezesha wanawake wajasiriamali wadogo wadogo kujiajiri na kuboresha miradi yao.

(g) Kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na wadau wengine kuendelea kuratibu mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi wa Shilingi bilioni moja kwa kila mkoa, ambapo utaratibu wa pili wa kutoa mikopo kupitia Asasi ndogondogo za huduma za fedha utaanza kutumika, hususan katika maeneo ambayo hayakufikiwa chini ya mfumo wa kwanza wa kutumia Benki ya *CRDB* na *NMB,* hasa maeneo ya vijijini na katika Wilaya ambazo hazina Matawi ya Benki hizi.

(h) Kuratibu ushiriki wa Wajasiriamali wadogo wadogo katika maonesho ya Tisa ya Nguvu Kazi/Juakali yatakayofanyika Jijini Nairobi nchini Kenya mwezi Oktoba mwaka 2007.

(i) Kuendelea kutekeleza awamu ya pili ya Marekebisho ya Sheria za Kazi na Ajira *(Labour Laws Reform Programme Phase II*) ambazo zitahusu masuala ya Hifadhi ya Jamii, Fidia ya Wafanyakazi wanaoumia kazini, na Usalama na Afya za Wafanyakazi sehemu za kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Vijana. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kupitia Idara ya Vijana na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuratibu shughuli za vijana nchini, hususan kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana, maandalizi ya mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana, na pia Wizara imewashirikisha vijana katika matukio na mikutano mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2006/2007**.** Mwaka 2006/2007, Wizara yangu kupitia Idara ya Vijana imetekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 1997 yamekamilishwa na kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

(b) Katika mpango wa kuwajengea vijana uwezo wa kukua kiuchumi na hasa kujiajiri katika sekta isiyo rasmi, Wizara yangu iliendelea na utaratibu wa kuwakopesha vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kufuatilia urejeshaji wa mikopo hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya Shs. 45,116,434/= zilikopeshwa kwa vijana wa Jiji la Arusha, Jiji la Mwanza, Halmashauri za Wilaya za Iringa na Sengerema. Kiasi hiki ni kidogo sana kwa vile utaratibu unaotumika ni kupitishia mikopo hiyo kwenye Halmashauri zile tu ambazo zimerejesha mikopo.

Aidha kwa Halmashauri ambazo hazijarejesha mikopo, Wizara yangu imeendelea kuzifuatilia ili waongeze kasi ya marejesho. Katika kipindi hiki ni Halmashauri saba tu, ndizo zilizorejesha mikopo ya jumla ya shilingi 30,762,486/=.

(c) Mpango wa mafunzo kwa vijana uliendelea kutekelezwa. Aidha miongozo ya kufundishia (mitaala) imeandaliwa katika masomo ya Uongozi, Ujasiriamali**,** Utunzaji wa hesabu za fedha na stoo pamoja na Uanzishaji na Uendeshaji wa miradi ya uzalishaji mali. Aidha mafunzo yalitolewa kwa vijana 80 kutoka mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Singida, Tanga na Mbeya chini ya uratibu wa kituo cha vijana Ilonga. Vijana hao waliopatiwa mafunzo wanatarajiwa kupeleka ujuzi walioupata kwenye vikundi vyao vya shughuli za maendeleo.

Vile vile Mafunzo mengine yaliyotolewa ni ya stadi za maisha, dawa za kulevya**,** Afya ya uzazi, VVU/UKIMWI ambapo washiriki 205 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na Arusha walihusishwa.

(d) Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana. Kwa mwaka 2006 sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge zilifanyika mkoani Ruvuma tarehe 14/10/2006 ambapo jumla ya miradi 1,679 yenye

thamani ya shilingi 73,929,512,030/= ilizinduliwa, kufunguliwa na kuwekewa mawe ya msingi pote nchini (*Kiambatisho VI).* Ujumbe wa Mwenge wa mwaka (2006) ulikuwa unahusu Vyama vya akiba na mikopo *(SACCOS),* Dawa za kulevya na Ugonjwa wa UKIMWI. Aidha shughuli za Wiki ya Vijana zilifanywa kuanzia tarehe 08/10/2006 hadi 14/10/2006 mkoani Ruvuma, ambapo vijana walishiriki katika maonyesho na kutangaza shughuli zao za uzalishaji mali na za kijamii.

(e) Uhamasishaji wa upimaji wa hiari wa *VVU/HIV* umefanywa wakati wa Wiki ya Vijana Mjini Songea, vijana 400 walijitokeza kupima *VVU/HIV.* Aidha ilifanyika Semina ya vijana kuhusu UKIMWI Jijini Tanga mada kuu ilikuwa upimaji wa *VVU/HIV* kwa hiari miongoni mwa vijana. *(Makofi)*

(f) Mwaka huu (2007) Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizinduliwa rasmi tarehe 30/05/2007 Mkoa wa Mjini Magharibi- Zanzibar na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar, na kilele cha Mbio hizo kitakuwa Mkoani Arusha tarehe 14 Oktoba, 2007. Ujumbe wa Mwenge mwaka huu umejielekeza katika Vita dhidi ya Rushwa na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa kuhamasisha upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari.

(g) Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kambi za kazi za vijana (*Youth Camps*) nne zilifanyika Sasanda Wilayani Mbozi, Madale – Manispaa ya Kinondoni, Ilonga Wilayani Kilosa na Marangu-Moshi vijijini. Kambi hizi ziliwahusisha vijana zaidi ya 150 na wananchi wa maeneo husika. Aidha sherehe za siku ya kujitolea Duniani ziliadhimishwa Wilayani Mwanga-Kilimanjaro. Vijana kutoka nje na ndani ya nchi walio katika mtandao wa kujitolea Duniani walishiriki katika kazi za ujenzi wa Taifa kwa wiki moja.

(h) Vijiwe vya vijana 169 viliainishwa na kuorodheshwa vyenye washiriki 1,945 katika baadhi ya mitaa ya jiji la Mwanza kama hatua mojawapo ya kuvitambua na ya kuvibadilisha kuwa vikundi vya kuzalisha mali.

(i) Aidha kuhusu kupata takwimu na taarifa sahihi juu ya shughuli za maendeleo ya vijana nchini (*Youth Mapping*), zimekusanywa takwimu na taarifa za vijana kutoka Wilaya 27 kati ya 46 zilizosalia. (*Kiambatisho VII*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu inatarajia kutekeleza yafuatayo kuhusu maendeleo ya vijana:-

(a) Kuchapisha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 na kuisambaza kwa vijana na wadau mbalimbali nchini, ili kurahisisha utekelezaji.

(b) Kuandaa Mpango na Mkakati mpya wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana.

(c) Kuratibu uanzishaji wa Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA).

(d) Kusambaza Mpango wa Maendeleo ya Vijana Afrika (*African Youth Charter*) kwa vijana na wadau wa vijana na kuanzisha mchakato wa kuridhia mpango huo.

(e) Kuendelea kuimarisha vikundi vya vijana vya uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo ya Ujasiriamali, Uongozi, Utunzaji wa hesabu za fedha na stoo na uanzishaji na uendeshaji wa miradi kwa vijana wajasiriamali kupitia Vituo vya Vijana.

(f) Kuendelea kuboresha vituo vya vijana vya Ilonga, Sasanda na Marangu kwa kuvipatia vifaa mbalimbali vinavyohitajika.

(g) Kwa kushirikiana na wadau wengine kuendelea kutekeleza mpango wa malezi kwa vijana katika maeneo ya Stadi za Maisha, Afya ya Uzazi, Dawa za kulevya, VVU/UKIMWI na uongozi.

(h) Kuboresha utaratibu wa mikopo ya vijana kupitia Mfuko wa Vijana kwa kutoa mafunzo kwa vijana, na kuimarisha ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo. Aidha kuanzia mwaka huu wa fedha mfuko huu utabadilisha utaratibu wa ukopeshaji, mikopo sasa itatolewa kupitia Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* vya vijana peke yake, ili kuleta nidhamu ya matumizi ya mikopo na urejeshaji wa mikopo hii.

(i) Kuendelea kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana kitaifa. Mwaka huu sherehe za Kilele cha mbio za Mwenge zitafanyika Jijini Arusha tarehe 14 Oktoba, 2007. Aidha Mwakani Mbio za Mwenge wa Uhuru zitazinduliwa Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani na Kilele chake kitakuwa Jijini Tanga.

(j) Kuendelea kuwahamasisha na kuratibu ushiriki wa vijana katika shughuli za kujitolea na kambi za kazi za Vijana, na kwenye mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2006/2007. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 ofisi ya Msajili wa Vyama ilisajili Vyama viwili vya wafanyakazi ambavyo ni *Tanzania Agro Forestry Workers Union (TAWU)* na chama cha Wafanyakazi marubani (*Tanzania Pilots Union (TPU*)) na hivyo kufanya jumla ya Vyama vya Wafanyakazi vilivyosajiliwa kufikia 21. Shughuli zingine zilizofanyika ni:-

(a) Imepokea ombi la usajili kutoka chama kipya cha Waajiri; uchambuzi wa ombi hili unaendelea. Chama hicho kinajiita *Tanzania Association of Agriculture Commerce Industry and Mining Employers (TAACIME).*

(b) Ilifanyika semina iliyohusisha vyama vyote vilivyosajiliwa kuhusu matumizi ya Sheria Na. 6/2004 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria Na.7/2004 ya Taasisi za Kazi..

(c) Zilifanyika kaguzi 19 za kumbukumbu za wanachama pamoja na vitabu vya mapato na matumizi katika Mikoa ya Kagera, Mbeya, Rukwa, Tanga na Kigoma na kubaini kwamba vyama vingi vinatunza kumbukumbu zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya mwaka 2007/2008. Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kushughulikia masuala yote ya usajili wa Vyama vya Waajiri na Wafanyakazi;

(b) Kuendelea kuwaelimisha viongozi wa Vyama vya Waajiri na Wafanyakazi juu ya Sheria mpya za kazi;

(c) Kufanya kaguzi za wanachama, mapato na matumizi ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na utunzaji mzuri wa kumbukumbu na matumizi mazuri ya fedha za wanachama; na

(d) Kusimamia Sheria za Ajira na Mahusiano Kazini zinazohusu usajili na uhai wa vyama vya wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Watumishi. Utekelezaji wa Malengo ya 2006/2007. Kwa mwaka 2006/2007 Wizara ilitekeleza majukumu yafuatayo yahusuyo maendeleo na maslahi ya watumishi:-

(a) Ilishirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi, kama vile Ulinzi, huduma za usafi na matengenezo madogo madogo ya vifaa vya ofisi.

(b) Idadi ya watumishi imeongezwa kwa kuajiri watumishi wapya na kuboresha mazingira ya kazi. Jumla ya watumishi wapya 54 wameajiriwa, watumishi 20 wamepandishwa vyeo na wengine 5 wamethibitishwa kazini.

(c) Imeanzisha Kamati ya Maadili, Nidhamu na Kudhibiti Rushwa katika Utumishi wa Umma, ambayo imetoa mafunzo kwa watumishi 52 wa Wizara katika Mikoa ya Tabora, Singida, Rukwa, Mbeya, Iringa, Shinyanga, Kagera, Mwanza na Dodoma.

(d) Katika kuhakikisha kuwa Wizara inatoa huduma zinazokidhi mahitaji ya wananchi, Mkataba wa Huduma kwa Wateja *(Clients Service Charter)* ulizinduliwa rasmi tarehe 23 Juni 2007 siku ya kilele cha Wiki ya Utumishi wa Umma.

(e) Kwa kuzingatia umuhimu wa michezo sehemu za kazi, Wizara ilishiriki katika michezo ya Mawizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) iliyofanyika Jijini Tanga na kwenye Sherehe za Mei Mosi 2007 Jijini Mwanza.

(f) Katika kuendeleza watumishi kielimu, watumishi 20 walipatiwa fursa ya mafunzo ya muda mrefu na watumishi 155 ya muda mfupi.

(g) Katika vita dhidi ya UKIMWI mafunzo yalitolewa kwa watumishi wa Wizara waliopo makao makuu, mikoani pamoja na familia zao. Idadi ya Washiriki ilikuwa 322. Aidha mafunzo ya ushauri nasaha na maongozi yalitolewa kwa washiriki 25 ambao ni Maafisa Vijana wa Wizara na watendaji wa asasi zisizo za kiserikali zinazohudumia vijana.

(h) Ili kuboresha hali ya ofisi na vituo vya Mikoani, Wizara ilifanya ukarabati wa kituo cha Ajira (*Labour Exchange Centre*) Mwanza na Ofisi ya Kazi Arusha. Aidha, ukarabati wa Ofisi ya Kazi Dar es Salaam umeanza. Taratibu zimekamilika kwa ajili ya ukarabati wa ofisi ya kazi Mwanza, Morogoro, Songea, Kigoma, Shinyanga, Same na Tanga, na vituo vya maendeleo ya vijana vya Ilonga, Sasanda na Marangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo kwa mwaka 2007/2008. Wizara yangu itatekeleza malengo yafuatayo yanayohusu maendeleo na ustawi wa watumishi kwa mwaka 2007/2008.

(a) Kuendelea kutoa mafunzo ya Maadili, Vita dhidi ya Rushwa na Utawala Bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI.

(b) Kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa Huduma kwa Umma.

(c) Kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za michezo kwa wafanyakazi wa Wizara.

(d) Ili kuondoa tatizo la ufinyu wa Ofisi, mipango inafanywa kwa Wizara kuhamia katika jengo la *NSSF* lililopo mtaa wa Bibi Titi kama hatua ya muda. Aidha ili kuondoa kabisa tatizo hilo, Wizara inaangalia uwezekano wa kujenga Ofisi Dodoma chini ya mpango wa Wizara za Serikali kuhamia Dodoma na tumeishapata tayari kiwanja cha eka nne.

(e) Kukamilisha kazi ya ukarabati wa ofisi za kazi za Mikoa na Wilaya kwa vituo vya Mwanza, Morogoro, Tanga, Same, Kigoma, Shinyanga**,** na Songea na vituo vya maendeleo ya vijana vya Ilonga, Sasanda na Marangu. Aidha kufanya maandalizi ya kukarabati ofisi za Singida,

Kilosa, Kilombero, Musoma, Bukoba, Mbeya, Rukwa, Iringa, Mtwara, Lindi na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Usalama na Afya Mahali pa kazi. Utekelezaji wa Malengo ya 2006/2007. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Wizara kupitia Wakala wa Afya na Usalama sehemu za kazi *(OSHA)* ilitekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Jumla ya kaguzi 9,512 za kawaida (*general workplace inspections*) zilifanyika na ushauri na maonyo yalitolewa;

(b) Mitambo ya kuzalishia mvuke ipatayo 243 ilifanyiwa ukaguzi wa kisheria wa kila mwaka kwa mujibu wa sheria;

(c) Vyombo vya kutunzia upepo *(Air Receivers)* vipatavyo 417 vilifanyiwa ukaguzi;

(d) Ukaguzi wa usalama wa umeme katika sehemu za kazi zipatazo 1,518 zilifanyika nchini kote;

(e) Vipimo vya mazingira ya sehemu za kazi zipatazo 54 vimefanyika;

(f) Wafanyakazi wapatao 15,418 walichunguzwa afya zao katika sehemu mbalimbali za kazi nchini kote;
Kaguzi hizo zimebaini kuwa, bado kuna matatizo ya kiusalama na kiafya mahali pa kazi. Hilo linatokana na ukweli kuwa, kumekuwa na hali ya kuhatarisha usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi, hali iliyopelekea baadhi ya waajiri kupewa onyo na wengine 10 walifikishwa mahakamani.

(g) Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yaliandaliwa maadhimisho ya kitaifa ya siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani tarehe 28 Aprili 2007 Jijini Mwanza, ikiwa ni kampeni maalumu ya kimataifa ya kuwataka wadau wote kuboresha Afya na Usalama wa Wafanyakazi. Kauli mbiu ilikuwa *"Usalama na Afya sehemu ya kazi hufanya hadhi ya kazi kuwa kweli"*.

(h) Mafunzo ya namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Usalama na Afya Mahali pa Kazi yameendelea kutolewa;

(i) Ukarabati wa jengo la ofisi ya Makao Makuu ya *OSHA* uliendelea ambapo sehemu ya ofisi na chumba cha maktaba na maabara vilikamilika;

(j) Wakaguzi 10 wameajiriwa ili kuboresha utoaji wa huduma ya afya na usalama mahali pa kazi.

(k) Maafisa 32 wa Usalama na Afya sehemu za kazi kutoka sehemu mbalimbali wamepata mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2007/2008. Kwa mwaka 2007/2008 Wizara itatekeleza malengo yafuatayo yanayohusu masuala ya Usalama na Afya sehemu za kazi.

(a) Kufanya kaguzi 3,200 za kawaida za Usalama na Afya sehemu za kazi;

(b) Kufanya kaguzi 2,840 maalumu na za kisheria za Usalama na Afya Mahali pa Kazi;

(c) Kuandaa mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi;

(d) Kuimarisha ofisi za kanda ya Kaskazini (Arusha), Pwani (Dar es Salaam) na Ziwa (Mwanza) kati ya kanda sita zinazohusiana na Usalama na Afya Mahali pa Kazi;

(e) Kuendelea kutoa mafunzo ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo redio, televisheni, magazeti na vipeperushi ili kuwafikia walengwa kwa wingi zaidi;

(f) Kuendeleza mchakato wa kuanzisha mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi;

(g) Kuhamasisha wafanyabiashara wadogowadogo na wale wa kati ili waweze kuboresha mazingira ya kazi;

(h) Kuajiri wakaguzi wapatao 40 ili kuimarisha kanda zote nchini;

(i) Kuendelea kutoa mafunzo kwa ajili ya Maafisa wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kutoka katika Makampuni mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. Wizara yangu kupitia Shirika la *NSSF* imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003. Shirika hili, lenye jumla ya wanachama 404,664 katika mwaka 2006/07 limeendelea kutoa mafao kwa wanachama wake. Hivi sasa Shirika hili linatoa jumla ya mafao saba kwa wanachama wake kama ifuatavyo:-

Pensheni ya Uzeeni;
Pensheni ya Urithi;
Pensheni ya Ulemavu;
Msaada wa Mazishi;
Malipo ya likizo ya uzazi (*Maternity benefits*);

Fidia ya kuumia kazini (*Workmen's Compensation*);

Malipo ya gharama za matibabu; na

Aidha kwa sasa *NSSF* ni Shirika pekee Kusini mwa Jangwa la Sahara linalotoa mafao mengi zaidi katika sekta ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba utendaji kazi wa *NSSF* katika kipindi hiki umekuwa ni bora na ni mfano wa kuigwa kiasi kwamba nchi nyingi Barani Afrika wanakuja Tanzania kujifunza kutoka *NSSF* namna nzuri ya kuendesha shughuli za Hifadhi ya Jamii. Baadhi ya nchi hizo ni Kenya, Uganda, Gambia, Sierra Leone, na Ghana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2006/2007. Katika kipindi cha mwaka wa 2006/2007 Shirika la *NSSF* limetekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Liliwalipa pensheni na mafao mengine jumla ya wanachama wake 72,636 yenye thamani ya shilingi 44,946,870,000/=.

(b) Lilikusanya mapato kutoka katika vitega uchumi mbalimbali jumla ya shilingi bilioni 26.8 ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi bilioni 21.4 kwa mwaka 2005/06. Hili ni ongezeko la asilimia 25.

(c) Limejenga vituo vya kuweka kumbukumbu katika mikoa ya Iringa na Mwanza. Aidha, mipango inafanywa ya kujenga vituo kama hivyo katika mikoa ya Mara na Mbeya**.**

(d) Limeendelea na Ujenzi wa majengo ya vitega uchumi katika Jiji la Mwanza na Mkoa wa Kagera.

(e) Limekamilisha ujenzi wa jengo la Benjamin William Mkapa Pension Tower (*Ex-Mafuta House*).

(f) Limekamilisha ujenzi wa nyumba za Serikali katika eneo la Kijitonyama Dar es Salaam zenye uwezo wa kuishi familia 200. Mradi huu uligharimu shilingi bilioni 13.8.

(g) Limekamilisha maandalizi ya mapendekezo ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigamboni na kuwasilisha Serikalini.

(h) Limeendelea na zoezi la kuweka Kompyuta katika Ofisi zake za mikoa na wilaya na kuziunganisha katika mtandao wa Shirika *(Internet Communication*).

(i) Limeendelea kutoa elimu kwa wanachama wake, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa fedha 2007/08, *NSSF* inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kulipa mafao kwa wanachama wake; jumla ya shilingi bilioni 44.6 zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa wanachama 68,000;

(b) Kuendelea kuweka Kompyuta katika ofisi zake za Mikoa na Wilaya na kuziunganisha katika mtandao wa Shirika (*Internet Communication*);

(c) Kuendelea kuboresha uwekaji wa kumbukumbu mbalimbali za wanachama na kujenga vituo vitatu vya kuweka kumbukumbu hizo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Singida;

(d) Kuendelea kufanya ujenzi wa majengo ya Ofisi na vitega uchumi katika Jiji la Mwanza, Mkoa wa Kagera, Arusha na ujenzi wa ofisi Wilaya za Mbozi, Kahama, Kidatu na Njombe; na

(e) Kushiriki katika ujenzi wa Daraja la Kigamboni kwa kuzingatia maamuzi ya Serikali.

(f) Kuanza kutekeleza miradi mipya ya ujenzi kama ifuatavyo:-

(i) Jengo la Ubalozi wa Tanzania huko Nairobi, (Shilingi bilioni 15.0);

(ii) Ujenzi wa Nyumba za Jeshi la Wananchi (Sh. bilioni 21.544);

(iii) Ujenzi wa Nyumba za Jeshi la Polisi (Shilingi bilioni 10.0);

(iv) Ujenzi wa Nyumba za Jeshi la Magereza (Shilingi bilioni 34.0);

(vi) Ujenzi wa Majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki – Chang'ombe; (Shilingi bilioni 25.0)

(vii) Ujenzi wa *Hostel* za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Shilingi bilioni 16.0);

(viii) Ujenzi wa Nyumba za TAKURU (Shilingi bilioni 3.84);

(ix) Ujenzi wa Jengo la Biashara za Wamachinga kule Dar es Salaam (Shilingi bilioni 10.0); na

(x) Ujenzi wa Nyumba za bei nafuu – Kigamboni (Sh. bilioni 10.8).

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Tija lina majukumu ya kuboresha tija na ufanisi kazini katika Taasisi za Umma, Mashirika yasiyo ya kiserikali na makampuni binafsi kwa kutoa huduma za mafunzo, ushauri, uelekezi na utafiti. Hili ni Shirika muhimu sana katika kukuza uchumi kwa kuongeza tija. Katika mwaka uliopita

Shirika hili liliendelea kutekeleza majukumu yake vizuri licha ya kukabiliwa na tatizo la ufinyu wa bajeti kwa kuwa halipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2006/2007. Katika kipindi cha mwaka wa 2006/2007 Shirika la *NIP* lilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Liliendesha mafunzo 90 ikilinganishwa na mafunzo 80 yaliyopangwa ambapo washiriki 1,224 kutoka katika sekta mbalimbali walipata mafunzo yanayolenga kuwapa mbinu za kisasa za kuongeza tija na kuboresha utendaji kazi katika sehemu zao za kazi.

(b) Limetoa huduma ya uelekezi kwa wateja 28 kutoka taasisi za umma na binafsi. Hii ni sawa na asilimia 93.33 ya lengo lililopangwa.

(c) Lilifanya tafiti 6 kati ya 8 zilizopangwa. Hii ni sawa asilimia 75 ya lengo lililopangwa. Aidha shirika lilifanya utafiti wa mishahara kwa taaluma ya Uhandisi (*Tanzania Remuneration Survey for Engineers 2007*).

(d) Liliendelea na matayarisho ya Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Tija (*National Productivity and Competitiveness Programme*) ambapo rasimu yake bado inajadiliwa na wadau kwa ajili ya uchambuzi na kutafuta fedha za kugharimia mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Malengo ya mwaka 2007/2008. Kwa mwaka 2007/2008 Shirika litatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kutoa huduma ya uelekezi kwa wateja 28 kutoka taasisi za umma na binafsi.

(b) Kufanya tafiti kubwa 6 kuhusu uboreshaji wa tija sehemu za kazi ili kuongeza uzalishaji.

(c) Kufanya matayarisho ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Usimamizi wa Tija (*National Productivity and Competitiveness Programme*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA).* Kamisheni hii ni moja kati ya Taasisi zilizoundwa katika kipindi hiki katika kutekeleza sheria mpya za kazi. Jukumu kubwa la Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi *(Commission for Mediation and Arbitration)* ni kusuluhisha migogoro ya sehemu za kazi. Upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Kamisheni, unaweza kupeleka shauri hilo katika Mahakama ya Kazi ambayo kwa sheria za sasa imekuwa ni kitengo katika Mahakama Kuu. Kamisheni hii ilizinduliwa mwezi Mei 2007 na imeanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2006/2007 Kamisheni ya Usuluhishi na Uamuzi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Baada ya kuzinduliwa ulifanyika uteuzi wa Mkurugenzi, Wasuluhishi na Waamuzi.

(b) Kanuni mbalimbali chini ya Sheria mpya za kazi zimeandaliwa.

(c) Iliandaa na kuendesha warsha kwa ajili ya Makamishna, Wasuluhishi na Waamuzi kuhusiana na taratibu na miiko ya utendaji kazi katika utekelezaji wa kazi za usuluhishi na uamuzi.

(d) Katika kipindi kifupi Kamisheni imefanikiwa kusuluhisha migogoro ya kikazi 925 kwa njia ya Usuluhishi kati ya migogoro 1,977 Iliyowasilishwa kwa Kamisheni kati ya Mei 2007 hadi Julai 2007. Kwa Dar es Salaam pekee migogoro 685 kati ya 1,062 imeshughulikiwa na kumalizika katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya mwaka 2007/2008. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Kamisheni itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kushughulikia kwa njia ya Usuluhishi na Uamuzi migogoro ya kikazi iliyokwisha kupokelewa katika mwaka wa fedha uliomalizika.

(b) Kupokea na kushughulikia migogoro itakayopokelewa katika mwaka huu wa fedha.

(c) Kuandaa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya Watendaji wa Kamisheni ili kuboresha utendaji wao.

(d) Kuajiri Watendaji wengine ili kuimarisha utoaji wa huduma ya usuluhishi na uamuzi.

(e) Kuhakikisha upatikanaji wa Ofisi za kudumu na vitendea kazi vya kutosha kwa ajili ya Kamisheni.

(f) Kutoa ushauri pamoja na kuendesha mafunzo kuhusu uzuiaji wa migogoro ya kikazi sehemu za kazi.

(g) Kufanya tafiti katika sehemu za ajira kwa lengo la kubaini malalamiko kuhusu ukiukaji wa Sheria na kuweka mkakati wa kuzuia kutokea migogoro ya kikazi mahali pa kazi.

(h) Kukusanya takwimu, kuweka kumbukumbu na kutayarisha ripoti za kazi kadri sheria inavyoelekeza, kwa manufaa ya Wabia Jamii na Wadau wa sekta ya kazi na ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto za Wizara 2007/2008. Katika mwaka wa 2007/2008 Wizara yangu inajindaa kukabiliana na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha mpango wa mikopo ya wajasiriamali. Kwa kuwa mpango wa wajasiriamali wadogowadogo kupatiwa mikopo yenye masharti nafuu ni silaha muhimu katika kukuza uchumi, kuongeza ajira, na kupiga vita umaskini, katika mwaka huu changamoto kwa wizara yangu itahusu yafuatayo:-

(i) Kuratibu uanzishaji wa mpango wa pili wa kushirikisha Taasisi ndogondogo za fedha ili zianze kutoa mikopo hasa katika maeneo ambayo Benki za *NMB* na *CRDB* hazijawafikia walengwa, hususan maeneo ya Vijijini na kwenye Wilaya ambazo hazina huduma za Benki hizo.

(ii) Kuratibu uwekaji wa utaratibu utakaowawezesha wananchi wasio na mradi wowote lakini wana nia ya kuanzisha miradi nao wapate mikopo kupitia katika vikundi vyao. Taasisi ndogo ndogo za fedha zinaweza kuwafikia wananchi wa aina hii.

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wananchi walengwa kuhusu taratibu za mikopo hii na mafunzo ya ujasiriamali.

(iv) Kuhamasisha urejeshaji wa mikopo ya uwezeshaji ili na wengine wakope. Hadi sasa urejeshaji wa mikopo unatia moyo kwani marejesho yamefikia wastani wa asilimia 91 kwa *NMB* na asilimia 100 kwa *CRDB*. Jitihada hizi zitaimarishwa.

(v) Kuweka utaratibu ili upatikanaji wa mikopo hii usiishie ngazi ya mkoa na wilaya, bali ufike hadi katika kila Kata, ili kuepuka hatari ya mikopo kuishia katika Kata chache na zingine zikakosa kabisa. Hali hii itawezekana kwa kutumia utaratibu wa pili wa kushirikisha Taasisi ndogo ndogo za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuweka utaratibu wa kukusanya takwimu za Ajira. Katika kutekeleza jukumu la kuratibu upatikanaji wa ajira ipo changamoto ya upatikanaji wa takwimu sahihi za ajira mpya zinazozalishwa kote nchini, hasa katika sekta binafsi. Wizara katika kuikabili changamoto hii inatazamia kufanya yafuatayo:-

(i) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kumwezesha Afisa aliyeteuliwa kuwa *Focal Point* wa Ajira ili awasiliane na watendaji wa Kata na wa Vijiji/Mitaa ili kukusanya takwimu za kila ajira mpya inayozalishwa katika maeneo hayo, hii ni pamoja na watu wanaojiajiri wenyewe kupitia mikopo ya uwezeshaji.

(ii) Kutoa mafunzo kwa Kamati za kusimamia mikopo hii katika ngazi ya Vijiji/Mtaa, Kata, Wilaya na Mkoa ili kuleta ufanisi wa ufuatiliaji wa matumizi ya mikopo, urejeshaji wa mikopo na kufanya tathimini ya matokeo ya mikopo katika kukuza

uchumi na kuongeza ajira huko vijijini na mitaani. Aidha mafunzo haya yatalenga kuboresha mawasiliano baina ya Kamati za ngazi mbalimbali.

(iii) Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kufanya "*Survey*" ya kubaini ajira mpya kila mwaka, hususan katika sekta binafsi.

(iv) Kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kupata takwimu za ajira mpya katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa mara kwa mara.

(v) Kuwaomba wananchi watoe ushirikiano kwa kutoa taarifa kwa serikali za mitaa/vijiji kuhusu ajira mpya zinazozalishwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapambano dhidi ya UKIMWI sehemu za kazi. Wizara yangu itaendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI sehemu za kazi ili nguvukazi ya Taifa isiendelee kupotea kutokana na janga la UKIMWI kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuhamasisha wafanyakazi kupima afya zao kwa hiari ili wale ambao wameathirika na ugonjwa huu wapewe msaada wa ushauri nasaha, madawa, lishe na kupangiwa kazi nyepesi.

(ii) Kusimamia sheria inayozuia ubaguzi sehemu za kazi, pamoja na kutowanyanyapaa walioathirika na UKIMWI sehemu za kazi.

(iii) Kuratibu masuala ya elimu ya mapambano dhidi ya Ukimwi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Mapambano dhidi ya Rushwa. Changamoto nyingine iliyo mbele yetu katika mwaka 2007/08 ni kusimamia utoaji wa huduma kwa wananchi kwa misingi ya haki, usawa, uwazi na bila ya bugudha yoyote. Aidha hatua zitachukuliwa kudhibiti vitendo vyote vya rushwa kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutangaza na kusambaza Mkataba wa Wateja *(Clients Service Charter)* kwa wananchi ili waelewe utaratibu wa kuhudumiwa wanapohitaji huduma toka Wizara yangu na kwamba huduma hizo ni bure.

(ii) Kuendelea kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu madhara ya tabia ya kutoa au kupokea rushwa katika jamii, na kwa wao wenyewe pindi wakibainika.

(iii) Kuimarisha na kuhamasisha Kamati ya Wizara ya Maadili na Utawala Bora ili ifanye kazi yake kwa ufanisi ili kuziba mianya ya rushwa.

(iv) Kupokea maoni ya wateja na kufuatilia nyendo na dalili zozote za rushwa Wizarani kwa lengo la kuzuia na kubaini wafanyakazi wanaojihusisha na rushwa wizarani ili wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Matumizi ya Wizara. Changamoto nyingine ni kuhusu kudhibiti matumizi ya Wizara. Kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi wa Serikali *(CAG),* mwaka 2005/2006 Wizara yangu ilipata hati ya Mashaka kutokana na dosari katika matumizi. Changamoto ya mwaka huu ni kusimamia matumizi vizuri ili Wizara isipate ama Hati Chafu au Hati yenye Mashaka. Katika kutimiza azma hiyo hatua zifuatazo zitachukuliwa.

(a) Kuunda Kamati ya Wizara ya Udhibiti wa Matumizi ya Fedha; jukumu la Kamati hii itakuwa kufuatilia kila mwezi mwenendo wa matumizi ya fedha Wizarani ili kubaini dosari na kuzirekebisha.

(b) Kuimarisha kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa kukiongezea wataalamu na vitendea kazi.

(c) Kuelimisha wafanyakazi wa ngazi zote kuhusu nidhamu ya matumizi ya fedha, sheria ya manunuzi ya vifaa vya Serikali, na umuhimu wa kurejesha masurufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani zangu za awali nazielekeza kwa Naibu Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Jeremia Solomon Sumari Mbunge wa Arumeru Mashariki, anayesimamia masuala ya Kazi na Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi Mbunge wa Songea Mjini, anayesimamia masuala ya Ajira na Vijana kwa msaada mkubwa wanaonipa na ushauri wao wa karibu. Aidha napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu Dr. Ladislaus Komba**,** na Naibu Katibu Mkuu Bibi Edine Mangesho**,** pia Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu.

Aidha nawashukuru watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara yaani *NSSF, NIP, OSHA, CMA* na Bodi mbalimbali ambao wameshirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote ambao kwa namna mbalimbali wemetuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu. Na kwa njia ya pekee naomba niwashukuru wajumbe wa Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi Uchumi wa Jamii *(Labour, Economic and Social Council (LESCO)*, Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)* kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yengu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mwisho katika mtiririko wa shukrani zangu lakini sio mwisho kwa umuhimu naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Manyoni Mashariki kwa ushirikiano wanaonipa na uchapakazi wao, ambapo katika kipindi kifupi sana wamejenga shule za sekondari ishirini. Aidha nawashukuru kwa kunivumilia

kwani muda mwingi hawanioni ninapokuwa natekeleza majukumu ya Kitaifa. Napenda kuwahakikishia kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Kwa uchache naomba shukrani za dhati ziende kwa Serikali ya nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, *World Bank, ILO, UNDP, UNICEF, UNFPA, CYP.* Naishukuru pia *TACAIDS* kwa misaada mbalimbali kwa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** Makadirio ya Bajeti ya Wizara. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2007/2008, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 10,924,037,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo Shilingi 6,801,047,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi 1,485,483,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 5,315,564,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (*Other Charges*).

Aidha kiasi cha Shilingi 4,122,990,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo Shilingi 2,396,000,000/= ni fedha za hapa nchini na Shilingi 1,726,990,000/= zikiwa ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge letu, kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa ufanisi na kwa viwango vinavyostahiki. Vilevile ninawashukuru Manaibu Waziri wangu Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi kwa jinsi wanavyonisaidia kwa vizuri kabisa kutekelezaji majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 81(1)(4) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana yaani Fungu 65 kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia aliyefariki dunia tarehe 26 Juni, 2007.

Kifo cha Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia kilipokelewa kwa masikitiko makubwa na watanzania kila pembe ya nchi yetu kutokana na umahiri mkubwa aliouonyesha katika uhai wa maisha yake.

Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, ametutoka katika kipindi ambacho uwakilishi wake katika Kamati ulikuwa ndio kwanza unaanza kujitokeza na nyota yake ya kisiasa ndio ilianza kuangaza. Wajumbe wa Kamati yetu tutamkumbuka Marehemu Amina kwa michango yake muhimu aliyokuwa anatoa wakati wa vikao vya Kamati, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake Mahali Pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 1 Juni, 2007, Mjini, Dar- Es Salaam, Kamati ilifanya Kikao na Wizara ya Kazi na kupata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Kapt. John Chiligati, Mbunge, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mbunge, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, Mbunge, Naibu Waziri na Dr. Ladislaus Komba, Katibu Mkuu wa Wizara hii. Katika kikao hicho timu hiyo wataalam na viongozi wa Wizara ilielezea kwa undani kuhusu:-

Dira na Muundo wa Wizara;

Utekelezaji wa Maoni, Mapendekezo na Maagizo ya Kamati kwa Mwaka wa 2006/2007;

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2006/2007, mafanikio na changamoto; na

Aidha Kamati ilipata maelezo ya kina ya Maombi ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati kwa mwaka 2006/2007. Katika mwaka wa Fedha uliopita Kamati hii ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu:-

(i) Ufuatiliaji Urejeshaji wa Mikopo katika Mfuko wa Vijana.

(ii) Mikakati ya Uanzishwaji wa *SACCOS* Nchini kupitia mbio za mwenge,

(iii) Ukamilishaji wa Muswada wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi**.**

(iv) Kuongezwa kwa Fungu la Fedha katika shirika la *OSHA,*

(v) Uendelezaji kuimarisha Kituo cha Ajira Nchini na Mikakati ya Ahadi ya Rais ya Ajira Milioni Moja Ifikapo mwaka 2010,

(vi) Vibali vya wafanyakazi kwa Wageni hapa nchini kutolewa kwa Uangalifu,

(vii) Mgogoro katika Kiwanja cha Shirika la Tija la Taifa,

(viii) Ujenzi wa Daraja la Kigamboni,

(ix) Ucheleweshwaji wa hati za dhamana ya kusimamia mikopo katika *NSSF* toka kwa msajili wa Serikali na,

(x) Mikakati ya kushughulikia migogoro mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi baadhi ya maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2006/2007. Katika mwaka wa Fedha 2006/2007 Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 11.457. Hadi kufikia tarehe 21 Mei, 2007 jumla ya shilingi bilioni 7.4 zilikuwa zimetumika na kiasi cha shilingi bilioni 2 kilipunguzwa kutoka kwenye bajeti ya Wizara hiyo (*budget cut*). Hata hivyo, Waziri alituelezea kwamba Wizara inatarajia kutumia fedha zote zilizokuwa zimebaki ifikapo tarehe 30 Juni, 2007.

Aidha katika mwaka 2006/2007 Wizara ilitegemea kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 2.8 b, hadi kufikia mwezi Mei, 2007 kiasi cha shilingi bilioni 6.1 kilikuwa kimekusanywa. Hivyo Kamati iliipongeza sana Wizara kwa makusanyo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 Waziri alielezea mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Kamati ilijadili kwa kina maeneo ya mafanikio yaliyoelezwa na Waziri. Maeneo hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Katika Idara ya Kazi kumeanzishwa Bodi za Mishahara za Kisekta zimeundwa katika sekta 8 na zimezinduliwa Aprili, 2007.

(ii) Migogoro ya kikazi 268 ilipokelewa na kushughulikiwa,

(iii) Jumla ya rufaa 1016 kutoka kwa wafanyakazi na waajiri katika sekta binafsi zimetolewa uamuzi.

(iv) Malalamiko ya madai ya kiinua mgongo, mishahara na likizo yalipokelewa na kushughulikiwa.

(v) Muswada wa sheria ya kusimamia sekta ya Hifadhi ya Jamii kufuatia mapendekezo ya wadau yamefanyika na Waraka wa Muswada huu umekwishajadiliwa katika ngazi ya Kamati ya Makatibu Wakuu- *IMTC,*

(vi) Marekebisho ya Sheria ya Fidia sehemu za kazi yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ajira iliripoti mafanikio yafuatayo:-

(i) Kupitia Kituo cha Ajira imeandikisha watafuta kazi na kuunganishwa na waajiri na kufungua kituo cha ajira jijini Mwanza na maandalizi ya awali ya uanzishwaji wa kitengo cha *cross boarder placement* yamefanyika.

(ii) Hadi kufikia Aprili, 2007 maombi 2,851 ya vibali vya kuajiri wataalamu wa kigeni yalipokelewa na maombi 2113 yaliyokubaliwa na 586 yaliyokataliwa na Serikali imeunda Kamati ya kutoa vibali vya ajira kwa wageni.

(iii) Imeratibu utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira kwa kushirikiana na wataalamu ambapo kila mkoa imetengewa shilingi bilioni moja.

(iv) Wizara imekamilisha kuandaa Mkakati wa Taifa wa kukuza ajira pamoja na Programu ya Kukuza Ajira yenye kubainisha maeneo mbalimbali ya kimkakati katika kufikia lengo la ajira milioni moja ifikapo 2010.

(v) Imekamilisha utafiti kuhusu nguvu kazi nchini na taarifa zitatolewa mapema iwezekanavyo

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana imefanikisha mambo yafuatayo:-

(i) Maandalizi ya mkakati wa Taifa wa kukuza ajira nchini hasa Mkakati kwa vijana kuanzisha *SACCOS* kote nchini kupitia mbio za mwenge yalifanyika.

(ii) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana imepitishwa na Baraza la Mawaziri, imepelekwa BAKITA kutafsiriwa.

(iii) Maandalizi ya mchakato wa kisheria yanafanyika ili kuanzisha BAVITA baada ya Sera ya Taifa ya Vijana kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

(iv) Wizara imeendelea kuratibu Mfuko wa Vijana kwa kutenga fedha za mfuko kwa mwaka 2006/2007, Wizara ilitenga shilingi milioni 500.

(v) Wizara inaendelea kukusanya takwimu na taarifa za vijana zinazoelezea waliko na shughuli wanazofanya (*youth mapping)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliridhika kabisa na utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2006/2007 na pale palipohitaji ushauri, Kamati imetoa ushauri ipasavyo. Ni maoni ya Kamati kwamba Wizara itazingatia maoni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeomba jumla ya shilingi 11,924,037,000 ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika mwaka 2007/2008, kati ya fedha hizo shilingi 6,801,047,000 zikiwa Matumizi ya Kawaida na shilingi 4, 122,990,000 Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kamati kujadili kwa kina bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007/2008 na kuipitisha, Serikali ilifanya maamuzi ya kupunguza bajeti ya kila Wizara kwa asilimia 17 kwa ajili ya kufidia pengo katika Wizara ya Miundombinu. Wizara hii imepunguziwa kiasi cha shilingi 1,048,000,000/=. Zoezi hili la kupunguza bajeti kwa asilimia 17 kila Wizara limeleta athari kubwa sana na hasa pale ambapo wizara haikupewa muda wa kufikiria na kuainisha ni maeneo gani yapunguzwe. Hali hii imesababisha kupunguza maeneo ambayo ni nyeti sana. Mfano gharama za mafuta, mafunzo na vitendea kazi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati ilichambua kwa kina malengo na mipango ya bajeti kwa mwaka 2007/2008. Fedha hizo za mwaka 2007/2008 zimepangwa kutumika katika mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja:

(i) Kuratibu na kusimamia Sera na Sheria zinazopambana na ajira mbaya ya mtoto.

(ii) Kuwezesha idadi kubwa ya watanzania kufikiwa na hifadhi ya jamii.

(iii) Kujenga uelewa juu ya viwango bora vya kazi miongoni mwa jamii na kuboresha mazingira ya kazi.

(iv) Kuratibu na kusimamia Bodi za mishahara ili kima cha chini cha mishahara katika sekta husika kiweze kutangazwa.

(v) Kukamilisha rufaa zilizo kwa Waziri na Kamishna wa Kazi.

(vi) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Ajira ya mwaka 2007, kuendelea kutoa huduma za ajira kupitia vituo vya ajira, kuanzisha na kuimarisha kitengo cha kuratibu huduma za ajira nje ya nchi.

(vii) Kuendelea kukusanya mawazo na mbinu za kukuza ajira katika sekta mbalimbali.

(viii) Kuwawezesha wananchi kupata mitaji na mafunzo ili waweze kujiajiri na kuondoa umaskini.

(ix) Kuratibu utoaji wa huduma za ajira ndani na nje ya nchi kwa kutumia kitengo cha *cross border placement*.

(x) Kukamilisha na kupeleka Bungeni Muswada wa Sheria ya Huduma za Ajira. Sheria hii itatoa mwelekeo wa kisheria wa kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira**.**

(xi) Kuendelea kutekeleza hatua ya pili ya Marekebisho ya Sheria za Kazi na Ajira ambazo ni Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia kazini, Sheria ya kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini, Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi na Sheria ya Huduma na Kukuza Ajira.

(xii) Kuchapisha na kusambaza Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana kote nchini na kuanza mchakato wa kisheria wa kuanzisha Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) kwa kuwashirikisha vijana na wataalamu wa Sheria**.**

(xiii**)** Kuratibu shughuli za Mfuko wa Vijana, kufanya tathmini na kufuatilia marejesho ya fedha za mfuko na kuhamasisha uanzishaji wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali nchini**.**

**(**ix**)** Kuendeleza mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya UKIMWI.

(x) Kuratibu uandaaji na Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, Sera ya Taifa ya Ajira, Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii na Sera ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

(xi) Kufanya tafiti inayohusiana na kuboresha tija katika viwanda vidogovidogo na kati na kufanya tafiti inayolenga kuboresha tija katika kilimo na sekta zingine mbalimbali.

(xii) Kuendelea kusimamia kazi zilizofanywa na taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara kama vile Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) na Shirika la Taifa la Tija (*NIP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Mipango iliyopangwa katika mwaka 2007/2008 yanatia moyo. Kamati inaiomba Wizara kutekeleza malengo na mipango hiyo kwa ufanisi mkubwa ili fedha zilizotengwa ziweze kufanya kazi yake kwa malengo yaliyokusudiwa ili yaweze kuzaa matunda kwa manufaa ya wananchi na kuleta maisha bora kwa kila mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili kwa kina utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2006/2007 na Malengo na Mipango ya mwaka 2007/2008, Kamati iliishauri Wizara katika kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilifanya Kikao na Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), mwezi Februari, 2006, Mjini Dodoma kwa lengo la kupata maelezo ya kina kuhusiana na Ujenzi wa Daraja la

Kigamboni. Baada ya kikao hicho Kamati yangu ilifanya tena Kikao, mwezi Aprili, 2006, Mjini Dodoma kwa kushirikisha Kamati ya Miundombinu, na Mawaziri wote wawili kujadili tena utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuhusiana na Ujenzi wa daraja hilo. Kwa pamoja Kamati zote mbili zilitoa maagizo ya kiutekelezaji kwa watendaji wa Wizara na kukubaliana kuwepo kwa kikao kingine cha kuonyesha mwelekeo wa kiutekelezaji wa ujenzi wa daraja hilo. Kikao kilipangwa kifanyike mwezi Oktoba, 2006.

Aidha mwezi Oktoba 2006, Kamati hizi mbili zilikutana tena Dar- es Salaam kwa lengo la kupata taarifa kutoka katika Wizara hizi mbili husika yaani Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na pia Kamati zote mbili zilitembelea eneo linalokusudiwa kufanyika ujenzi wa daraja hilo. Hata hivyo, mpaka sasa Kamati inasikitika kuona hakuna taarifa halisi za kuonyesha mwendelezo wa mradi huo ukizingatia kwamba *NSSF* imekwishafanya kazi ya kutosha ya maandalizi ya mradi huo.

Katika muda huo wote Kamati inaamini kuwa Serikali imefikia hatua maalumu ya kuruhusu sasa ujenzi huo uingizwe katika mpango maalumu wa kuanza kwa mradi. Hivyo basi Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iongeze kasi na ione umuhimu wa kujengwa kwa Daraja la Kigamboni ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka, 2005.

(b) Kwa kuwa *NSSF* wamehusika kwa muda mrefu na kutumia fedha nyingi katika upembuzi yakinifu wa kazi hiyo ya ujenzi wa daraja la Kigamboni, hivyo Msimamizi Mkuu wa ujenzi huo iwe ni *NSSF*.

(c) Kamati hairidhishwi kabisa na utekelezaji wa Serikali kuhusiana na ujenzi wa daraja la Kigamboni. Kamati itahakikisha kuwa inafuatilia kwa karibu kabisa ujenzi wa daraja hili.

(d) Wanaojitokeza kutaka kujenga daraja la Kigamboni waendelee na miradi mingine ya ujenzi wa madaraja, lakini mradi huu uliobuniwa na *NSSF* uendelee kama ulivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shirika la Tija la Taifa lilikuwa linamiliki kiwanja Na. 906/H Mbezi *Beach*, ambacho kilitolewa kwa Shirika toka mwaka 1980 na kupimwa kwa gharama za Shirika na kupewa barua ya toleo (*offer*) mwaka 1989 na kupewa hati mwaka 1990; na kwa kuwa Shirika la Tija la Taifa lilikiendeleza kiwanja hicho kwa kujenga uzio na nyumba moja kwa jumla ya shilingi milioni 49; pamoja na maendeleo hayo, Wizara ya Ardhi ilitoa barua ya kusudio la kubadilisha miliki ya kiwanja hicho mwaka 1995, na Shirika lilipinga barua ya kusudio hilo. Mawasiliano yaliendelea kati ya Kamishna wa Ardhi na Uongozi wa Shirika bila mafanikio, hadi mwaka 2002 wakati kiwanja hicho kilipomilikishwa Chuo cha *IMTU* cha India. Pamoja na Shirika kudai kulipwa fidia ya kiwanja kiasi cha shilingi 190,000,000, *IMTU* ya India ililipa shilingi 15,200,000/= tu. Hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Serikali ipitie upya utaratibu uliotumika wa kumilikisha kiwanja Na. 906/H kwa chuo cha *IMTU*, kwani imeonekana wazi kwamba haki haikutendeka.

(b) Aidha, Kamati inalipongeza Shirika la Taifa la Tija kwa kazi nzuri na itaendelea kushirikiana na Shirika kwa mambo mbalimbali. Pia Kamati inaishauri Serikali kuliimarisha Shirika la Tija la Taifa ili liweze kuwafikia walengwa wengi zaidi na kuchangia vyema zaidi juhudi za kujenga uchumi wa taifa letu.

(c) Ili Shirika liweze kufanya kazi kwa ufanisi, Kamati inaishauri Serikali iharakishe kuandaa Sera ya Shirika la Taifa la Tija ili iwe sahihi kwa Shirika kupata ruzuku angalau kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Serikali iweke mikakati ya kutumia utalaamu kutoka katika Shirika la Taifa la Tija hasa katika kutoa mafunzo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ni muhimu sana katika kusimamia taratibu bora za fedha za Serikali, Kamati inaishauri Wizara kutenga fedha za kutosha katika kuimarisha kitengo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa migogoro mahali pa kazi inarudisha nyuma maendeleo kwa namna yoyote ile; na kwa kuwa mgogoro wa Kiwanda cha Sukari cha *TPC* Mkoani Kilimanjaro unazidi kuendelea na kuleta madhara makubwa na kwa kuwa Mgogoro wa *TPC* ni miongoni mwa migogoro ya wafanyakazi kuhusiana na chama kipi wajiunge nacho kati ya *TPAWU* na *TUICO* ambapo mgogoro huo sasa upo mahakamani; na kwa kuwa baada ya mwajiri kuona migomo akawafukuza wafanyakazi 100 na sasa mashamba yanachomwa moto ovyo:

(a) Kamati inaishauri Serikali kuushughulikia mgogoro huo mapema iwezekanavyo kabla haujaleta madhara makubwa na kurudisha nyuma azima ya Serikali ya kuweka mazingira bora kwa wawekezaji hapa nchini.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kushughulikia migogoro hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa kuwa ufuatiliaji wa urejeshaji wa mikopo ya mfuko wa Vijana katika Halmashauri zetu unaendelea vizuri hasa baada ya kuongezwa mkopo kwa halmashauri zilizorejesha; na kwa kuwa Wilaya ambazo hazitakuwa zimerejesha mikopo ya Mfuko wa Vijana katika mwaka 2002/2003 zilikatwa kutoka katika mgao wa *OC* zao HAZINA, hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Serikali kuangalia upya utaratibu wa kukata fedha za *OC* za halmashauri kwa sababu ni kuwanyima haki wananchi walio wengi.

(b) Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa fedha za mikopo kwa vijana kupitishia katika *SACCOS* kwani ufuatiliaji wa mikopo utakuwa na mafanikio makubwa zaidi kuliko utaratibu ulivyo hivi sasa.

(c) Kamati inaishauri Serikali kwamba ufumbuzi wa tatizo la Halmashauri kutofuatilia mikopo ya Vijana ni kuwaadhibisha watendaji wabovu na sio kukata fedha za *OC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa wafanyakazi wa Wizara hii, Dar-es Salaam wanakaa katika majengo matatu tofauti kutokana na jengo lililopo kutokidhi mahitaji ya kuwawezesha wafanyakazi wote kukaa pamoja; na kwa kuwa Wizara imepata kiwanja Dodoma na imekuwa na mikakati ya kujenga ofisi yake Mjini Dodoma, Kamati inaunga mkono hoja hiyo na kuitaka Serikali kutenga fedha za ujenzi wa ofisi katika mwaka wa fedha 2008/2009 mara Serikali itakapotoa maamuzi ya kujenga ofisi hiyo Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali iko katika mikakati ya kujenga jengo la Wamachinga jijini Dar- Es Salaam kwa kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii- *NSSF*; na kwa kuwa ujenzi huo utakuwa ufumbuzi wa tatizo la Wamachinga kukosa mahali pa kufanyia biashara ndogondogo jijini Dar-es-Salaam, hivyo basi Kamati inashauri:-

(a) Serikali kuendesha mafunzo kwa Wamachinga kuhusiana na uendeshaji wa biashara kabla ya kuanza kwa biashara inayokusudiwa kufanyika katika jengo hilo.

(b) Serikali ifanye zoezi la kuainisha idadi ya wamachinga ili waweze kupatiwa nafasi katika jengo hilo kama ilivyokusudiwa.

(c) *NSSF* iangalie uwezekano wa kujenga majengo mengine yanayofanana na jengo linalokusudiwa kujengwa Dar- es Salaam, kuyajenga mahali pengine hapa nchini hasa Mwanza na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miaka ya hivi karibuni ari ya vijana kufanya kazi imeshuka sana hapa nchini; na kwa kuwa kuna vijana wengi ambao wanakaa vijiweni wengi wao hawasomi wala hawana biashara au shughuli yoyote ya kufanya; na kwa kuwa kila mwaka Serikali huwa inasema inayo mipango endelevu kwa vijana lakini vijana wengi wanaongezeka kukaa vijiweni, hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Serikali iandae mikakati ya kuinua ari ya vijana kufanya kazi na kuwawezesha kwa vitendo ili waweze kushiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na ujenzi wa Taifa letu.

(b) Zoezi la kutambua vijana walipo liendelee na mikakati ya kutafuta ufumbuzi uende sambamba na zoezi hili.

(c) Serikali ianzishe ofisi katika kila wilaya ili ziweze kuwaunganisha kimafunzo, kimaadili na kimikakati vijana wetu ili kuleta ari ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana imepitishwa na Baraza la Mawaziri na kupelekwa BAKITA kutafisiriwa; na kwa kuwa

maandalizi ya mchakato wa kisheria yanafanyika ili kuanzisha BAVITA, hivyo basi Kamati inashauri:

(a) Wizara kuleta mikakati hiyo katika Kamati ili iweze kutoa mchango wake kabla ya kuwasilishwa rasmi katika Bunge.

(b) Maandalizi ya mchakato wa kisheria wa kuanzisha BAVITA uharakishwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeunda Kamati ya kutoa vibali kwa wageni kufanya kazi nchini na Wajumbe wa Kamati ni kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, *TUCTA* na *TIC* na wamekubaliana kutoa majibu ya vibali au kukataa ndani ya siku 14, hivyo basi Kamati inashauri kuwa Serikali iweke mikakati utoaji wa Vibali na kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu utoaji wa vibali holela na ucheleweshwaji wa kutoa vibali hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha za mfuko wa uwezeshaji hapa nchini bado ni mpya na haujaeleweka kwa wananchi na wadau wengine na hivyo kuonekana kuwa na upungufu mbalimbali, kwa mfano kutokuwa na mafunzo kwa wajasiriamali kabla ya kuanzisha miradi; na kwa kuwa mgawanyo wa riba katika mikopo ya *CRDB* ya asilimia 2 kwa *SACCOS*, na asilimia 10 kwa *CRDB* una upungufu mkubwa, hivyo basi:

(a) Serikali ione uwezekano wa fedha za mfuko wa uwezeshaji kwenda moja kwa moja katika *SACCOS* kwani zinazo uwezo wa kuwakopesha wananchi wengi zaidi na ufuatiliaji wa mikopo ni rahisi zaidi.

(b) Serikali iweke mikakati ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kabla ya kutoa mikopo ili wananchi wawe na uelewa zaidi katika uendeshaji wa miradi yao.

(c) Kama Benki ya *CRDB* itaendelea kukopesha *SACCOS* basi mgawanyo wa riba uwe asilimia 6 kwa Benki na asilimia 6 kwa *SACCOS.* Kwa mfano, *NMB* inakopesha kwa asilima kubwa na hivyo wakopaji wanaopitia kwenye *CRDB* wanakopa kwa asilimia 12 ambayo ni juu kuliko wanaokopa kupitia *CRDB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ilipata hati ya mashaka katika mwaka wa fedha 2005/2006, Kamati inaishauri Wizara kuweka mikakati ili wasipate tena hati ya mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maoni hayo napenda sasa kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ambao ndio waliochambua Bajeti hii, nao ni: Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Fatma Othman Ally, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Zulekha Y. Haji, Mheshimiwa Issa K. Issa, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Elietha N. Switi, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa

Florence Essa Kyendesya, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Salimu Abdallah Khalifan na Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman,

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, napenda kumshukuru Mheshimiwa Capt John Chiligati, Mb, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Mb, na Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, Mb, Katibu Mkuu, Dr. C. Komba na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), Dr. Ramadhani Dau na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tija la Taifa, Ndugu Ferdnand. L. Kasenge, kwa kazi zao nzuri na makini katika kuendesha mashirika yao kwa ufanisi mkubwa. Kamati inawatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizowezesha kuiongoza Kamati hii. Michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Lawrence Robert Makigi, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati.

Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya Taarifa hii. Vilevile nitoe shukrani za dhati kabisa kwa wananchi wa jimbo la Msalala ambao walinichagua na kunipa imani ya kuniwezesha kufika mahali hapa kusoma taarifa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wangu. Nawaomba waendelee kuniamini na kuniunga mkono na daima nitasema na kuwatetea kama ambavyo nilikuwa nimewaahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa jinsi mnavyoendesha vikao na nashukuru sana na naunga mkono hoja hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Upinzani, naomba niwaarifu watakaoanza kuzungumza kusudi wawe tayari. Tutaanza na Mheshimiwa Magdalena Sakaya si mnafahamu tena, yeye alikuwa hayupo na hajachangia na tunampongeza sana kwa kazi kubwa aliyotufanyia kutuletea vijana wengine.

Halafu atafuata Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dorah Mushi na Eng. Laus O.Mhina. Tuanze na hao kwanza halafu tutaendelea. Kwa hiyo, nategemea taarifa aliyosoma Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati imesambazwa. Mimi ninayo,

inaelekea kuna wengine hawana.  Sasa namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani Bungeni au Mwakilishi wake.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALIFAN – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake ya uzima kwetu sote. Naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni juu ya Hotuba ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya  43(5) (b) (c) na 81(1), Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Tumbe kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa hoja nyingi za kuleta mbele ya Bunge hili Tukufu na naushukuru uongozi mzima wa Chama cha Wananchi (CUF), kwa kuniwezesha kuwa hapa na kuendelea kuniunga mkono ili niwatumikie Watanzania vizuri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako, napenda kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika pamoja nawe, kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri na hekima kubwa inayofanya shughuli za bunge kwenda kwa utulivu na maelewano. Aidha, niwapongeze wenyeviti wetu kwa kufuata vyema nyayo zenu katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe rambirambi kwa familia ya marehemu Mheshimiwa, mwanakamati mwenzetu Amina Chifupa Mpakanjia. Mungu awape roho ya subira ndugu, jamaa na marafiki katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na mwenzetu na Mungu ailaze roho yake pahala pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Capt. Chilligati na Manaibu wake wawili na watendajai wote wakuu wa Wizara kwa ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na mfumo wa Sheria ya Kazi na Usuluhishi wa Migogoro ya Kazi ni sehemu muhimu sana ya soko la ajira, ulinzi wa haki za wafanyakazi na kuongeza tija. Baada ya kuona kuwa sheria za kazi za zamani hazikidhi mahitaji ya soko la ajira kwa sasa, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria mpya za kazi, Namba 6 na 7 za mwaka 2004. Kutungwa kwa sheria mpya kulitarajiwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuweka uwiano mzuri baina ya wafanyakazi na waajiri. Mojawapo ya sababu zilizochelewesha utekelezaji wa sheria hizi ni kusubiri kanuni na miongozo yake.

Hatua za kutengeneza miongozo (*Regulations*) zitakazopelekea kuanza kutumika kwa sheria hiyo imefikia pazuri na sasa tunazo Kanuni za Mahakama ya Kazi ambazo zimechapishwa tarehe 18/5/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa sasa ni kuwa na wataalamu wa kutosha kuendesha shughuli za mahakama hii kwa ufanisi na kwa haraka. Tunajua

kuwa wale tuliowapa mafunzo ya awali wengi wameondoka baada ya Serikali kushindwa kuwapatia ahadi ya uhakika ya kuanza kazi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga fedha kwa minajili ya kuwapa mafunzo watendaji na kuweka mtaala wa utatuzi wa migogoro katika vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya sheria ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuuzwa kwa mgodi wa chumvi wa Uvinza kwa *Great Lakes Mining Corporation limited*, tarehe 11.2.1999, Serikali kupitia Tangazo la Gazeti la Serikali la Januari 11, 1995, lililotolewa na *PSRC* ilitangaza kuuza asilimia 81.33 za hisa za serikali katika mgodi wa Nyanza *Salt Mines (T).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangazo husika liliweka wazi masharti kadhaa ya kuzingatia katika uuzaji huo. Katika sharti (f) (iv) - Serikali ilisema yafuatayo, nanukuu: "*Undertaking to safeguard the interests of existing employees or in the event of unavoidable redundancy, to pay statutory terminal benefits and 'golden handshake' to the affected employees".*

Kwa tafsiri, maana halisi ya kipengele husika ni kwamba Serikali itachukua hatua zote kuhakikisha kwamba inalinda maslahi ya wafanyakazi waliopo na ikitokea ulazima wa kupunguzwa kazi itahakikisha wanapata maslahi yao kama sheria inavyoagiza, pamoja na mkono wa kwaheri!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ilitegemewa, jumla ya wafanyakazi 383 walipunguzwa kazi na tangu mwaka 1999 ni miaka 8 sasa wamekuwa wakipeleka malalamiko yao katika ngazi mbalimbali za Serikali, bila mafanikio. Ikumbukwe kuwa wafanyakazi hawa walilipwa mafao kidogo mno. Kwa mfano, kwa mujibu wa barua za kupunguzwa kazi (*redundancy),* Abdala Almas aliyefanya kazi kwa miaka 28, alilipwa jumla ya sh.722,121.90, Mzomwe Mzomwe aliyetumikia miaka 37 alilipwa mafao ya sh. 914,064. Malipo hayo ambayo kwa mujibu wa barua hizo ndio mafao, ni malipo ya mshahara wa mwezi mmoja, nauli ya mfanyakazi na familia, gharama za kusafirisha mizigo na malipo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu haki ya mfanyakazi aliyepunguzwa kazi ni zaidi ya kiasi kilichoainishwa hapo juu. Katika kipindi chote hicho *PSRC* wamekuwa wakiwazungusha hawa wafanyakazi pasipo mafanikio huku wakijua fika kwamba kinachodaiwa na wafanyakazi hawa ni haki yao, na ushahidi wa kutosha upo kuthibitisha hilo, na unaweza kutolewa kama ikilazimika kufanya hivyo. Vitendo kama hivi ni ukiukwaji mkubwa wa dhana nzima ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kwa nini haijatekeleza ahadi yake ya kuwalipa mkono wa kwaheri jumla ya wafanyakazi 383 waliopunguzwa kazi katika mgodi huu mpaka sasa, na pia inaitaka Serikali ichukue hatua zilizo sahihi katika kufuatilia haki za wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano mema baina ya wadau wakuu wa ajira, yaani Serikali, Waajiri na Waajiriwa (kupitia Vyama vyao) ni mahitaji muhimu katika

kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Uzalishaji makini na tija hutegemea sana uhusiano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhuru halisi wa Vyama vya wafanyakazi ni nguzo muhimu siyo tu ya utawala bora, ila pia ni mhimili wa demokrasia iliyo ya kweli. Kauli na sauti ya wafanyakazi huwa ni kauli ya wazalishaji, ambayo pia ni kauli na sauti ya walipakodi. Vyama vya wafanyakazi vilivyo huru na makini ni sehemu ya jamii huru ya kiraia au *"Civil Society"*. Watendaji Serikalini ni lazima waijue kwa kina dhana nzima ya Vyama vya wafanyakazi *(trade unionism*), ndani ya ukweli na mazingira ya soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hiki ni kitengo muhimu sana, hasa linapokuja suala la mustakabali wa afya za wafanyakazi kazini. Pamoja na kuanzishwa kwa Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi (*OSHA*) bado hajawa na meno na nguvu ya kusimamia kwa ukamilifu sheria ya Bunge iliyoanzisha *OSHA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya umuhimu wa kitengo hiki, kimekuwa kama hakipo, Kambi ya Upinzani ingependa kupewa taarifa kuhusiana na:-

(i) Utendaji kazi wa Kitengo husika na mipango yake katika kuhakikisha kwamba usalama na afya sehemu za kazi unazingatiwa.

(ii) Mikakati ya Wizara kuhakikisha kwamba fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali wakiwa sehemu za kazi zinaongezwa ikizingatiwa kwamba zilizokuwepo sasa ni ndogo mno na zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inazidi kusisitiza kwamba wakala hawa wa Usalama na afya mahala pa kazi *(OSHA)* wawezeshwe zaidi na Serikali, ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi mkubwa na ili pia waweze kufikia maeneo tofauti ya nchi. Bunge la Tanzania ni lazima lijielekeze katika kutunga sheria zinazotambua haki za msingi za wavuja jasho, walalahoi na wapinda mgongo wa nchi yetu. Mfanyakazi akiumia au hata kupoteza kiungo au viungo akiwa kazini, ni lazima fidia anayoipata imhakikishie maisha ya uhakika yeye na familia yake mpaka mwisho wa maisha yake. Sheria zote zinazohusika na masuala ya ajira ni muhimu ziwe na lengo la kulinda haki za kimsingi za mfanyakazi, lakini bila ya kuzikandamiza haki za waajiri na hata Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Tija a Taifa *(NIP)* ni muhimu kwa taifa letu kutokana na shughuli zake zinazolenga kuongeza tija katika utendaji na ufanisi wa mashirika na makampuni mengi nchini japokuwa lina rasilimali-watu ndogo sana. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa shirika hilo linaidai Serikali shilingi milioni 213 kwa mujibu wa tathmini. Katika fedha hizo shilingi milioni 49 walizitumia kuendeleza kiwanja Na. 906/H *Mbezi Beach* ambacho baadaye walinyanganywa na serikali katika mazingira ya kutatanisha kwa madai kuwa shirika limeshindwa kutimiza masharti ya kukamilisha ujenzi kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba serikali ilitoa fedha za kujenga nyumba moja katika mwaka wa fedha wa 1994/1995, na serikali ilikuwa iendelee kutoa fedha nyingine lakini miradi ya maendeleo ilisimama kutokana na hali ngumu ya fedha katika mwaka huo.Hata hivyo, wakati ujenzi unaendelea hatua ya kutaka kufuta miliki ya kiwanja hiki ilianzishwa na Wizara.

Hatua za kufuta milki ya *NIP* zilianza kuchukuliwa na Wizara mwaka 1995 wakati serikali ilipokuwa inatoa fedha za kukamilisha ujenzi wa nyumba moja. Serikali iliamua shirika lipewe shilingi milioni 26 kama fidia tofauti na madai ya shirika, na cha kusikitisha zaidi shirika limelipwa shilingi milioni 15 tu. Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke wazi nini kimetokea mpaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikakigawa kwa watu wengine kiwanja hicho ambacho tayari shirika lilikwishatumia kiasi cha shilingi milioni 49 katika kukiendeleza. Ni lini Serikali italirejeshea Shirika fedha zake hizo kama linavyodai sawasawa na gharama walizotumia kukiendeleza kiwanja hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya serikali kuwanyang'anya *NIP* kiwanja hicho na kuwapa *IMTU* ilikuwa ni kuwa shirika limeshindwa kukiendeleza, lakini hadi sasa hakuna hatua zozote za kukiendeleza ambazo zimechukuliwa na *IMTU*. Kambi ya Upinzani inataka kujua kama kweli kushindwa kukiendeleza kiwanja hicho kwa miaka mitatu ndio ilikuwa sababu ya kuinyang'anya *NIP* kiwanja chake au kulikuwa na ajenda nyingine ya siri? Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kulirudishia shirika kiwanja chake baada ya *IMTU* kushindwa kukiendeleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni muhimu sana kwa maslahi ya wastaafu. Ili kuwa na ufanisi mifuko hii inapaswa kutunza vizuri fedha za wafanyakazi na ili kuongeza thamani inategemewa kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Tunalo tatizo na mifuko yetu ya hifadhi za jamii.

Kesi za wastaafu kucheleweshewa malipo na wengine taarifa zao kutokuonekana katika kumbukumbu za wastaafu. Tunatoa rai kwa mifuko kuwa makini kuwahudumia wastaafu vizuri na kupunguza kero na gharama za ufuatiliaji. Kuhusu uwekezaji, tunatoa pongezi kwa mifuko ya hifadhi za jamii kwa kuanza kuwekeza katika miradi ya maendeleo na yenye msaada kwa watu wengi kama, uwekezaji katika nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili kuhakikisha kuwa uwekezaji huu unakuwa wa manufaa na kuwa hakuna rushwa na ufujaji wa fedha, tuwe na mkakati wa kuwa na uwazi wakati wa kuamua aina ya uwekezaji na vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* majukumu yake makubwa ni kukusanya michango, uwekezaji wa michango na kulipa mafao kwa wanachama. Kambi ya Upinzani inapenda kuipongeza *NSSF* kwa juhudi hizo za kutimiza wajibu wao.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kuwa michango imekua kwa zaidi ya asilimia 30. Mapato kutokana na vitega uchumi vyake yameongezeka kwa takriban asilimia 25. Aidha, kwa utaratibu uliotajwa katika Sheria Namba 28 ya mwaka 1997, *NSSF* inajitahidi kukamilisha utoaji wa mafao yote 7 kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *NSSF*, bado yapo maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa haraka. Moja ya maeneo hayo ni ujenzi wa daraja la Kigamboni. Hadithi ya ujenzi wa daraja hilo imekuwa ya muda mrefu sasa. Wakati anafanya majumuisho ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu hapa Bungeni tarehe 3 Julai, 2006, aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Basil Mramba, aliliahidi Bunge lako kuwa mradi wa daraja la Kigamboni utatekelezwa kwa mujibu wa mapendekezo yaliyowasilishwa Serikalini na *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kujua kwa nini mradi huu ambao ni muhimu kwa uchumi wa Dar es Salaam na kwa Taifa kwa ujumla haupewi uzito ambao ni stahiki yake? Kwa kumbukumbu zilizopo ni kuwa mwaka jana Kamati mbili za Bunge lako Tukufu ziliarifiwa na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kuwa ujenzi wa daraja hili utaanza haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na hoja mbili zinazoleta utata kwa wananchi, ile ya kununua kivuko na ya ujenzi wa daraja. Kama kumbukumbu zetu ziko sawa Mheshimiwa Kaboyonga alikwishatoa takwimu na ufafanuzi ni kiagi gani mpaka sasa *NSSF* imekwishawekeza na mbia waliyekwishampata amekwishaihakikishia Serikali ni kiasi gani kitawekezwa katika mradi huo wa daraja la Kigamboni. Wote tunaelewa kuwa *NSSF* ni mali ya nani na inafanya kazi kwa niaba ya nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa kuwanyima kazi *NSSF* na kuwapa wawekezaji kutoka nje au kununua kivuko kutoka nje kwa matakwa binafsi ya baadhi ya viongozi ndio uzalendo ambao tunaambiwa? Kambi ya Upinzani inatamka kuwa huu si Uzalendo, kwa namna hii serikali itakuwa ikilifilisi taifa letu. Kambi ya Upinzani ingependa kuuliza, je, Serikali inangoja mpaka vivuko vya Kigamboni vizame kama ilivyokuwa *M.V*. Bukoba ndipo ujenzi wa daraja uanze? Wananchi wa Kigamboni wanaoteseka sana watatoa hukumu katika hili, na watanzania walioahidiwa maisha bora na Tanzania yenye neema kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya pia watatoa hukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaridhishwa na jitihada zinazofanywa na *NSSF* katika uwekezaji kwenye miradi kama vile ujenzi wa jengo la wamachinga na ujenzi wa nyumba za Polisi ila wasisahau kuwa Zanzibar na Pemba vilevile kuna askari wanaohitaji nyumba za kuishi. Pia tunaipongeza kwa dhamira yao ya kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa *NSSF* wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu, Kambi ya Upinzani inashauri ujenzi wa nyumba hizo uwe wa teknolojia ya *Pre-fabricated* kama ambavyo tulishauri katika hotuba yetu ya Kiongozi wa Upinzani wakati akiwasilisha bajeti mbadala. Aidha, *NSSF* katika kuwasaidia wanachama wake izingatie

maombi ya wale wanaohitaji kujengewa nyumba za bei nafuu na ambao tayari wana viwanja vyao binafsi. *NSSF* inaweza kuangalia ni kwa jinsi gani au mhusika achangie ziada ya kiasi gani katika gharama hizo na zingine, na kwa kuwa ni mwanachama aendelee kulipa kidogo kidogo. Kwa njia hii *NSSF* itapata mtazamo mpya toka kwa wananchi ambao wanadhani inatumiwa na kuwanufaisha matajiri tu si kwa wanachama wake. Sambamba na hili uanzishwaji wa benki kwa ushirikiano na taasisi nyingine za hifadhi ya jamii uharakishwe kulingana na mipango iliyopo kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inaishauri Serikali iihamasishe *NSSF* na mifuko mingine ya hifadhi za jamii kujenga hosteli za wanafunzi hasa wasichana ili kukabiliana na tatizo la malazi kwa wasichana katika shule mbalimbali za sekondari na vyuo vya elimu. Shirika lifanye jitihada za makusudi ili kuendeleza mradi huu mzuri katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani inayohitaji huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira ni suala la msingi sana kwa maendeleo ya taifa lolote. Duniani kote serikali zinahangaika kuwapatia watu wake ajira ili kukuza uchumi, kuimarisha huduma na kuboresha kiwango cha maisha. Kila kukicha mikakati inaundwa ya namna ya kutengeneza fursa za ajira. Serikali iliahidi kutengeneza fursa za ajira milioni moja kwa kipindi chake cha miaka mitano. Hii ni ahadi nzito ambayo watanzania walipewa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutimiza ahadi ya lengo dogo la ajira milioni moja kwa watanzania. Kambi ya upinzani inasisitiza kuwa ni lazima kuwe na mkakati maalumu, sera na sheria itakayoharakisha kukua kwa uchumi na upatikanaji wa ajira nchini kinyume na hali halisi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya leo ya ushindani wa soko na utandawazi yanahitaji watu waliojiandaa vizuri na kuwa na vigezo vya ajira. Uwezo ni kigezo muhimu sana ili watu waweze kuajiriwa. Katika soko watanzania wanashindana na watu wengine ambao wamejiandaa vizuri. Ni lazima tuwaandae watu wetu.

Ushirikiano wa kikanda kama Jumuiya ya Afrika Mashariki unatutaka tuwaandae watanzania vizuri kuajiriwa. Hakuna mikakati ya kutosha inayolenga kuwasaidia watu wetu kuajiriwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iliambie Bunge hili ina mkakati gani wa kuwaandaa watanzania kukabiliana na ushindani huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahitaji ya kigezo cha zoefu katika Ajira, Kambi ya Upinzani inalileta tena suala la mahitaji ya uzoefu katika ajira kwa ajili ya mjadala. Tujiulize na kujadili tukikumbuka matangazo mbalimbali ya ajira. Ni asilimia ngapi ya matangazo hayo hayana kigezo cha uzoefu? Tena mengine yanataja miaka mingi, mpaka pengine ingeitwa 'uzeefu' badala ya 'uzoefu'.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua na kuthamini mchango wa uzoefu katika utumishi na kazi. Hivyo, haina tatizo la uzoefu kuendelea kuwa kigezo

muhimu katika kuajiri. Lakini Kambi ya Upinzani haioni maana ya uzoefu kutumika kama kigezo cha lazima.

Utaratibu wa sasa wa asasi nyingi za serikali na sekta binafsi kutumia uzoefu kama kigezo cha lazima unawazuia vijana wahitimu ambao hawajafanya kazi bado, hata kupata nafasi ya kusailiwa na kupimwa uelewa na vipaji vyao kuhusiana na kazi husika. Kwani kuna mtu anazaliwa na uzoefu? Watapata lini uzoefu bila kupata fursa ya kupata uzoefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweke utaratibu wa kuishawishi sekta ya umma na binafsi kupenyeza mabadiliko katika utaratibu wao kuhusiana na suala hili la uzoefu kwa kutoa motisha ya vyeti vya punguzo kidogo la kodi kwa makampuni yatakayochukua wanafunzi toka vyuoni moja kwa moja *(graduate tax relief certificate).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara yetu ya kazi haifanyi kazi yake ipasavyo ya kuwaunganisha waajiri na wanaotafuta kazi. Ili kurahisisha kazi ya kupata ajira na kuwa na mikakati ya kuwasaidia wazalendo ni muhimu mambo yafuatayo yafanyike:

(i) Tuwe na upendeleo wa makusudi kwa wazawa katika kutoa fursa za biashara na uwekezaji nchini. Hii iambatane na kuwapunguzia ugumu wowote unaoweza kujitokeza wakati wa utoaji wa fursa hizo za biashara na uwekezaji.

(ii) Tuwe na vigezo tofauti vya kutoa mikopo na vivutio vya biashara ili tuwasaidie wazawa kutengeneza fursa nyingi za kazi na kuajiri watu wengi zaidi.

(iii) Tuwe wakali katika kutoa vibali vya kazi kwa wageni ili kuwashawishi wawekezaji kuwaajiri watanzania hususan kwa kazi ambazo tuna watanzania wenye uwezo wa kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira za Kujiajiri, kuanzia miaka ya themanini, kutokana na mageuzi ya kiuchumi imekuwa ngumu kwa wananchi hususan vijana kupata ajira. Kabla ya mageuzi hayo sekta ya umma ndio ilikuwa mwajiri mkuu. Baada ya mageuzi hayo sekta binafsi ikachukua nafasi, bahati mbaya kutokana na mipango tenge sekta binafsi katika nchi yetu haijaweza kukua na kuziba pengo ambalo limeachwa kwa kujitoa kwa serikali. Kwa ujumla Serikali imeshindwa kuwapokea vijana wapya wanaoingia kwa wingi katika soko la ajira. Badala ya kuongezeka, sekta rasmi ya ajira inazidi kusinyaa. Mathalani kwa kila mwaka takribani watu 700,000 wanaingia katika soko la ajira. Lakini sekta rasmi ina uwezo wa kuchukua watu elfu 40 wapya tu kwa mwaka. Hivyo watu laki 660,000 wanajiunga na jeshi la wasio na ajira rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ndio '*walala-patupu'* ambao bado wanapaswa kulipa kodi wanayotozwa kupitia *VAT* wanayolipa wanaponunua bidhaa wanazozihitaji ili waishi. Ndio maana wengine wanapoteza kujiheshimu, wengine wanakufa mapema kwa matatizo ya kisaikolojia, wengine wanaathirika kwa msongo wa mawazo na wengine wanajiingiza katika vitendo vya uvunjaji wa sheria. Hivyo suala hili linahitaji si tu kasi

mpya kama sera ya C.C.M inavyosema linahitaji pia uharaka. *We need a sense of urgency as this is a national emergency*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi kadhaa zimekwishatolewa kuhusu upatikanaji wa mikopo ukiwemo mpango wa kutoa shilingi milioni 500 kila Mkoa kwa ajili ya wajasiriamali wanaochipukia. Huu ni uamuzi ambao kwa ujumla unastahili kupongezwa.

Lakini tukipima mahitaji kiasi hiki cha pesa ni kidogo ukilinganisha na watanzania wanaohitaji mitaji. Kwa vyovyote vile ama. Kwa vyovyote vile ama tutatoa mitaji ya kutosha kwa watu wachache na wengi kuambulia patupu ama tutatoa mitaji kiduchu kwa watu wengi na kuwa na biashara nyingi ndogo ndogo na butu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tathmini ya nguvu kazi ya mwaka 2002 inajulisha kuwa kati ya nguvu kazi ya taifa ya watu milioni 17.9, asilimia kubwa ni vijana wa kati ya miaka 15 na 35. Na ukosefu wa ajira katika nchi nzima kwa wastani ni 12.9 % wakati kwa mijini ni asilimia 25.5, huku Dar es Salaam ikiwa na ukosefu wa ajira asilimia 46.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia suala hili la kutaka kumridhisha kila mtu wakati ukweli ni kuwa kila mtu hapati msaada huo.

Huku ni kujidanganya, suala la muhimu lilikuwa ni Serikali kubuni miradi itakayozalisha kwa haraka na kurudisha fedha hizo na kuweza kuingia katika mzunguko wa uzalishaji. Kwa namna hii ajira za kumwaga na *constructive* zingepatikana tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize, hivi kinachokuja kwanza ni nini, "Wazo la biashara ama Mkopo?" Hili sio fumbo la kuku na yai. Mtazamo wa Serikali hii ni kutanguliza mbele mikopo tena midogo midogo.

Kwa misingi hii, hoja ni kwamba vijana wanao utamaduni na nidhamu ya biashara. Hili swali lisipojibiwa vizuri katika utekelezaji wa mikakati yetu, hii mikopo midogo midogo inaweza kuwa chanzo cha umaskini kutokana na kushindwa kwa biashara kutakakozalisha madeni kwa walalahoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweka mkazo katika kujiajiri hususan kwa kukuza sekta isiyo rasmi. Sekta hii bado inakabaliwa na changamoto mbalimbali. Tafiti zinaonyesha kuwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya biashara ndogo ndogo zilizoanzishwa na watu waliotazamia kujiajiri wenyewe zinakufa kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano kutokana na upungufu wa mafunzo ya stadi za biashara miongoni mwa vijana, elimu ndogo miongoni mwa wajasiriamali vijana na isiyojitosheleza, utamaduni wa watu wengi kupenda ajira rasmi zaidi ya kujiajiri na kutovutia au kutelekezwa kwa kilimo, ambayo ni sekta kuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofanikiwa wakati mwingine kwa biashara hizi pia kunatokana na mali/mitaji ya vijana hawa kuharibiwa au kupotea na wao wenyewe

kuishia mikononi mwa polisi kama wahalifu. Wakati mwingine tunawahamisha waende maeneo ambayo hayafikiki kirahisi na hivyo kuwakosesha wateja. Kwa misingi hii hatujengi taifa bali tunabomoa taifa hili ambalo ni changa bado kiuchumi na linalokuwa kwa tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatambua mipango sahihi ya miji yetu, lakini lazima tuzingatie maslahi ya watu wetu na ugumu wanaoupata hawa vijana katika kujitafutia shughuli ya maana ya kujipatia kipato. Swali ni kwa nini Serikali inashindwa kuweka taratibu nzuri katika mipango yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani sasa ni wakati mwafaka kwa serikali kuangalia upya taratibu na mipango yake ili fedha hizi zitumike vizuri na ziwasaidie walengwa. Ipo haja ya kuwapa vijana wajasiriamali mafunzo ya jinsi ya kuendesha biashara zao vizuri. Hilo likishafanyika ndipo dhana ya kujiajiri itakuwa na maana kwa vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Vijana ni sehemu muhimu sana ya nchi yetu. Ni muhimu kwa sababu ya nafasi yao katika uchumi wa taifa na uhai wa taifa kwa siku za usoni. Kiuchumi, hii ndiyo nguvu kazi ya taifa ambayo inatarajiwa kuzalisha na kuleta tija. Ili waweze kushiriki vizuri lazima wawekewe fursa katika uchumi ili waweze kujiajiri na wengine kuajiriwa. Taarifa za tafiti na takwimu mathalani, MKUKUTA zinatuonyesha kuwa suala la vijana kutokushirikishwa katika uchumi wa nchi ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maendeleo ya Vijana, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 vijana wa kati ya miaka 15 mpaka 35 ni takribani 11,775,259. Hivyo, hili ni kundi ambalo halipaswi kupuuziwa. Na zaidi ukitazama hali ya vijana nchini wengi wao hawana ajira, wengi wao wamekata tamaa, wao ndio waathirika zaidi wa UKIMWI na mambo mengine. Kwa vyovyote vile tusipoweka kipaumbele kwa kundi hili taifa lipo katika bomu la wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapaswa kubadili mtazamo wetu kuhusu vijana na kuwatazama kama suluhisho badala ya tatizo. Kwa asili vijana ni kundi muhimu kiuchumi kama wazalishaji wakuu; kwa asili vijana ndio wenye kuweza kulisukuma taifa mbele kutokana na nguvu, nishati na ubunifu wao. Ndio maana maendeleo ya vijana yanapaswa kuwa ajenda mtambuka *(cross cutting agenda)* kwa sekta zote. Kwa kuwawezesha wazee tunajenga taifa lipitalo, kwa kuwalea watoto tunajenga taifa la kesho, kwa kuwezesha vijana tunawekeza katika Tanzania ya leo na kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufike huko tunahitaji sera mwafaka ya maendeleo ya vijana. Kwa muda mrefu tumekuwa tukitumia sera ya maendeleo ya vijana ya mwaka 1996. Kwa vyovyote vile sera hii imepitwa na wakati. Kwa miaka kadhaa sasa serikali imekuwa ikitoa matamko kwamba iko katika mchakato wa kuibadili sera hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako, tayari sera mpya ilikwishaandaliwa. Hata

hivyo, vijana katika maeneo mbalimbali wanalalamika kuwa hawajaiona sera hii mpya. Kambi ya Upinzani ingependa kuelewa ni lini sera itawafikia vijana walau katika vikundi vyao ikiwemo vijijini ili washiriki kwa nguvu katika kuitekeleza? Serikali lazima itimize wajibu kwa kasi mpya ama sivyo wananchi na wadau wetu wa maendeleo, mathalani shirika la kuhudumia watoto *UNICEF* ambao walichangia katika mchakato wa kukusanya maoni katika kanda mbalimbali kuhusu sera hii watatushangaa na kupunguza imani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea kuhusu Baraza la Vijana, kwa sababu ya uwingi wao na nguvu zao, kundi hili la vijana ni lazima liwe na chombo kinachowaunganisha bila ya kujali itikadi za vyama vyao. Mbinu nyingi zinafanywa na watendaji Serikalini kuhakikisha kuwa Baraza hilo haliundwi kwa misingi ya vijana wenyewe yaani ushirikishwaji wa makundi ya vijana wenyewe na asasi mbalimbali za vijana ni mdogo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kuwa kwa miaka kumi sasa Baraza limekuwa ahadi, litaendelea kuwa ahadi mpaka lini? Jitihada za vijana za kujiunga na kuwa na baraza lao huru zilitokana na nchi yetu kurudi katika mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. Baada ya kurudi kwa vyama vingi Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) ukakosa uhalali wa kuwa chombo cha vijana wote nchini. Jitihada za vijana kujiundia chombo chao mpaka leo hazijafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzisha Baraza hili, serikali yetu itakuwa imetekeleza makubaliano ya kimataifa ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusu Vijana ambayo nchi yetu imeridhia. Chombo hiki kitakuwa mhimili muhimu katika utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana Tanzania na kuwa chombo cha kuwaunganisha vijana katika hekaheka zao za kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu ni lini muswada huo utaletwa bungeni ili uweze kujadiliwa na ni kwa kiasi gani wadau wa muswada huo watashirikishwa katika mchakato mzima wa kuanzishwa kwa Baraza husika. Aidha, tunaitaka serikali iwaeleze vijana ambao wamekuwa wakilalamika, ni vigezo gani vilitumika kuwapata vijana ambao walishiriki katika mkutano wa vijana ulioandaliwa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana katika ukumbi wa Hoteli ya Bandari, Tanga ambao pamoja na mambo mengi ulijadili mchakato wa uundwaji wa Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka katika asasi mbalimbali za vijana kwamba hazikushirikishwa katika mkutano huo muhimu. Je, Serikali ina nini cha kuwaambia vijana hao ambao kimsingi wamekuwa mstari wa mbele katika kuwawakilisha vijana katika masuala ya kitaifa na kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kulingana na hotuba ya kufunga kongamano hilo, Mkurugenzi wa Idara ya Vijana alisema kuwa uundaji wa Baraza la Vijana unahitaji kwenda polepole. Kamabi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni lini uundwaji wa Baraka utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nawashukuru wabunge wote na watanzania kwa ujumla kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifa, kwa kweli wewe ni hodari, maana unasoma kama mashine. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nadhani makundi yetu maalumu yamemalizika. Sasa nitamwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dorah Mushi na Mheshimiwa Eng. Laus Mhina. Nadhani kwa asubuhi hii hawa watatosha. Waheshimiwa Wabunge nawaombeni wengine ambao mngependa kuchangia hapa mwandike, kwa sababu nina orodha kubwa kabisa, na mimi hata kundi waliochangia mara moja halitakwisha. Kwa hiyo, naomba wote mlioomba changieni kwa maandishi na mkiandika asubuhi hii itakuwa vizuri Mheshimiwa Waziri atajibu. Mheshimiwa Sakaya karibu!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kwanza ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii iliyoko hapa mbele yetu. Naomba nichukue fursa hii pia kukushukuru wewe mwenyewe, Spika, na Wabunge wenzangu kwa kuungana na mimi kufurahia zawadi nzuri ambayo Mwenyezi Mungu amenipa, nawashukuru sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu kwanza kuchangia kwenye Bunge hili la Bajeti, naomba nichukue nafasi hii pia kuungana na Wabunge wenzangu kutoa pole zangu za dhati kwa familia ya Mzee Chifupa, jamaa na marafiki wake wa karibu, kwa msiba mzito uliowapata kwa kuondokewa na Mheshimiwa mwenzetu, marehemu Amina Chifupa. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amina! Naomba pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kutuandalia hotuba hii na kuweza kutuletea hapa Bungeni ili tuweze kuijadili. Pamoja na mikakati mizuri ambayo imeandaliwa kwenye hotuba aliyowasilisha Mheshimiwa Waziri lakini bado tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini ni tatizo sugu na ni kubwa sana.

Vijana wengi sana wanatapakaa mitaani, mijini na wapo kwenye magenge mbalimbali hawana la kufanya kwa sababu hawajawekewa mikakati imara, miundo ambayo itawasaidia waweze kuwajibika inavyopaswa. Ningependa kujua kwamba Wizara au Serikali kwa pamoja inaandaa vipi vijana kuanizia ile ngazi ya kumaliza Sekondari kwa maana ya kufikisha miaka kumi na nae, wameandaliwa utaratibu gani wa kujisaidia kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali imesema kwamba itakuwa inawachukua *division one* na *two* kwa ajili ya kuwalipia vyuo vikuu. Wale wengine wa *division three* na *four* wameandaliwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, tusipoweka mikakati thabiti tutajikuta kwamba vijana wetu wengi wataishia kwenye kuvuta bangi, kwenye kujiingiza kwenye mauvo mbalimbali na

hivyo kulipeleka Taifa hili mahali ambapo sipo. Vijana wengi wamekuwa wakikimbilia mijini kwa sababu wanaona labda pengine mijini ndiko wanaweza kupata ajira. Lakini wanapofika kule mijini na kukuta kwamba uwezekano wa kupata ajira hakuna, hawana la kufanya wanataka wawe wamachinga na umachinga hauwezekani, hawajaandaliwa mikakati mizuri wanajikuta wanakaa bila kazi na hivyo kuwepo na hali ambayo ipo sasa hivi. Tatizo kubwa la kukosekana kwa ajira hapa Tanzania limesababishwa na Serikali kubinafsisha viwanda wakati huo huo sekta binafsi zikiwa hazijaimarishwa. Kwa hiyo, wapo vijana wengi waliokuwa wanafanya kazi kwenye viwanda vilivyobinafsishwa wamerudishwa nyumbani, hawakuandaliwa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tungependa kujua Serikali inalichukuliaje suala hili? Mimi napenda kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo: Kwanza, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara nyingine ianze kutoa mafunzo ya ujasiriamali kuanzia ngazi ya chini kabisa. Isisubiri vijana waende mijini wakae kwenye makundi mbalimbali ndiyo ianze kuwakusanya hapana! Ianze kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wale wadogo wadogo kuanzia miaka kumi na nane ili waweze kujua jinsi ya kujiajiri wenyewe mara wanapotoka *shule.S*traight toka shule wajue wanachoenda kufanya badala ya kwenda kujiunga kwenye makundi mbalimbali ambayo yanapelekea wakawaza kubadilika tabia na kuweza kuwa na tabia ambazo hazistahili, hasa ikizingatiwa kuwa vijana hawa ni nguvu kazi ambayo inatakiwa kusaidia taifa hili liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo *t*umekuwa tunalizungumzia sana hapa Bungeni, ni kwamba naomba Serikali ipeleke maendeleo vijijini kwa kuhakikisha kwamba kuna miundombinu ya kutosha na kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wamekuwa wakilima na wakilima wamekuwa hawana zana za kutosha, na wanategemea mvua, mvua zenyewe hakuna. Wakilima mwaka wa kwanza wakiona hawajapa, mwaka wa pili hawajapa, wanasema wakimbie kijijini waende mijini. Kijana anaamini akienda huko pengine atapata riziki katika maisha yake. Kwa hiyo, naomba maendeleo yapelekwe vijijini, miundombinu iboreshwe na nishati ziwepo. Umeme ufike mpaka vijijini ili viwanda vidogo vidogo kama vya useremala viweze kufanya kazi kwa ufanisi vijana waweze kujiajiri; na kama maendeleo yatapelekwa vijijini, nina imani kabisa vijana walioko mijini watashawishika kurudi vijijini wakijua kwamba wakienda kule wanaweza kuwa na maisha yaliyo bora kwa sababu hali hali inaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali iweke mikakati ya dhati na madhubuti kuangalia wale vijana wasiokuwa na kazi labda baada ya kufikisha miaka kumi na nane inawasaidiaje kuweza kumudu maisha yao. Kwa nchi za wenzetu wana utaratibu baada ya miaka kumi na nane wanakitu wanaita *sustainable allowance*, kuna hela kidogo anayopewa kijana badala ya kwenda kukaa mitaani. Anakuwa na namna ya kujiendeleza wakati huo anatafuta ama aende chuoni au shuleni au atafute kazi. Kwa hiyo, kuna kiasi cha fedha kinachotolewa kuwezesha kuishi. Je, Serikali yetu yenyewe inaangaliaje wale vijana ambao wanatoka shule lakini hawajawezeshwa jinsi ya kuishi haya maisha. Wanawasaidiaje waweze kujiandaa wakati wanatafuta kazi au shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubali kabisa kwamba sasa hivi tunaingia kwenye soko la *East Africa*, soko la pamoja. Je, Serikali inawaandaje vijana wetu, kielimu, kibiashara na kikazi? Tungependa kujua Wizara sasa hivi imeandaa utaratibu gani vinginevyo wenzetu wamewaandaa vijana wao vizuri sana, wengi ni wasomi wazuri, wengi wana kazi zao, wakija hapa vijana wetu watakuwa ni vibarua kwenye nchi yao. Je, Serikali imewaandaje hawa vijana wetu kwa kuingia kwenye hili soko la pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni wakati muafaka, naiomba sana Serikali iwafikirie sana wale vijana ambao wamekwenda shule lakini hawakufaulu kwa kiwango cha kwenda Chuo Kiuu. Kwa sababu tumekuwa tunasikiliza hata hotuba za Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, wanawataja wale tu wenye *division one* na *two*, wale wengine jamani wanakwenda wapi? Tuambiwe wameandaliwa utaratibu gani. Hili taifa kila mwananchi anatofautiana kiuwezo na mwenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huu mfuko wa *NSSF*, ambao ni michango ya wafanyakazi wote Tanzania. Kwa hiyo, ni mfuko wetu na mfuko wa vijana pia. Kwa nini mfuko huu usitoe mikopo ya riba nafuu kwa vijana ambao hawana kazi? Kwa nini Serikali isifanye hilo suala kwa wale vijana ambao wanatapakaa hawana kazi? Kwa sababu wanajenga majengo? Kwa kweli wana fedha za kutosha niseme kutokana na kazi wanazozifanya. Mfuko unazo hela za kutosha zinazoweza kuwasaidia vijana wetu. Kwa nini wasitoe fungu kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana wetu ili waweze kujisaidia na kujikomboa katika maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue jukumu la *social responsibilities* kwa wananchi wake. Isiwaache mwananchi wake tu kwa kuwa labda hakufaulu vizuri au hana kazi, ikamwacha tu awe anatapatapa, hapana! Kila mmoja anaipenda nchi yake, kila mmoja ana wajibu na ana haki zote za kupata huduma zilizo nzuri na salama. Kwa hiyo, Serikali ichukue *responsibilities* za kuhakikisha kwamba kila mwananchi anaishi vipi na asiyekuwa na kazi anaishije na mwenye kazi anaishije. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana ambao wanafanya kazi kwenye sekta binafsi, wengi wao wameacha kufanya kazi kule kutokana na kunyanyaswa, wengi wao wameacha kazi kutokana na mishahara midogo haikidhi hata mahitaji. Unakuta mtu anafanya kazi, lakini anaishia kulipa nauli, pengine hata chakula cha mchana hapati. Kwa hiyo, ningependa kujua Wizara inaangaliaje suala la vijana ambao wanafanya kazi kwenye sekta binafsi ambao hawatendewi haki, wengi wao wamekuwa wanaishi maisha magumu sana. Mtu anafanya kazi lakini kama vile hafanyi kazi. Sasa hili nalo linachangia vijana kuwepo mitaani, anaona kwa nini apoteze muda wakati akitumia nguvu zangu nyingi kwenye kazi ambazo hazimpatii kipato kinachotosheleza, kwa hiyo, anaona bora akae. Sasa kule kukaa matokeo yake ndiyo kujiingiza kwenye makundi ambayo ndiyo tunawaita wamachinga. Wengine ni wasomi, lakini wamachinga, ana vyeti vyake, lakini ni mmachinga, hana kazi, amekuwa kijana wa kijiweni. *(Makofi)*

Wapo wengine kutokana na mazingira mazuri wanafaulu vizuri, wengine wanafaulu kwa kiwango kidogo. Lakini pia yule ambaye amefaulu kidogo pengine kuna

sababu ambazo zimesababisha kufaulu kwa kiwango kidogo yakiwemo mazingira, familia na mambo mengine kama hayo lakini hawa wasiachwe. Wameandaliwa utaratibu gani wa kuwawezesha kuishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kujua Wizara hii inawasaidiaje vijana kuweza kukwepa vitendo ambavyo vinawapelekea kufanya mambo yasiyostahili na hivyo kuwapelekea kwenye janga kubwa la UKIMWI. Sasa hivi tunapambana sana na suala la UKIMWI, tumejizatiti. Serikali imejizatiti na kuna miradi mbalimbali inayopambana na masuala ya UKIMWI. Lakini cha kushangaza ni kwamba vijana tunawaona wengi wao wanatembea *almost* nusu uchi barabarani tumewaacha! Tumewaona vijana wanajiingiza kwenye kumbi mbalimbali ambazo kwa kweli yanayofanyika ni kama kwenye sinema, hayastahili. Ukienda *beach* unakuta ni vituko! Vituko! Vituko! Haya yote tunayaangalia, lakini wakati huo huo tunapambana na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua Wizara hii, je, inawaangaliaje hawa vijana kwa sababu hata leo ukitoka hapa mjini utakuta kijana ambaye amevaa nguo ambayo kwa kweli inaashiria kabisa kwamba huyu kimaadili amepotoka. Lakini Wizara wanaangalia, viongozi wanaangalia, hapo hapo tunaongea mara zote kwamba tunapambana na UKIMWI! Tuanze kwanza kuwafanya hao vijana waingie kwenye mstari mmoja, tuwarekebishe. Vijana wetu wamekuwa wanaiga sana na tunawaacha tu wanaiga. Tunaona vijana wanatembea na nguo za *swimming pool,* tunawaacha tu kwamba ni utandawazi. Utandawazi unatupeleka pabaya! Kwa kweli tunaomba Wizara hii iwasaidie vijana, vinginevyo kazi tunayoifanya ya kupambana na suala la UKIMWI inaenda *against* na mambo ambayo vijana wanayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa Wizara ilete mapendekezo Bungeni na kuliwezesha Bunge kutunga sheria itakayodhibiti vijana waondokane na masuala ya kuingiaingia kwenye sinema za ajabu, kuvaa nguo zisizostahili, kufanya vituko barabani. Sheria ambayo itawadhibiti ili waweze kuishi kwenye maadili ya Kitanzania na hivyo kuweza kuwasaidia, kuweza kufanya shughuli zinazowapasa na waondokane pia na na janga kubwa la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, bada ya hapo, naomba nishukuru kwa nafasi hii, asante sana! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana kwa uchangiaji mzuri! Sasa nitamwita Mheshimiwa Missanga na Mheshimiwa Dorah Mushi ajiandae!

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii mapema kuchangia katika hoja hii muhimu. Baada ya kushukuru, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo wameileta, yeye, Manaibu wake wote wawili nawapongeza, Katibu Mkuu pamoja na wote ambao wanahusika na Wizara hii, nawapa pongezi sana na nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia habari za kazi. Masuala ya kazi ni masuala ya utatu. Ni masuala ya utatu; ni Serikali, waajiri na waajiriwa. Wote hawa ni muhimu, wote hawa wanapaswa kuheshimiana. Mmoja asipomheshimu mwenzake, basi utekelezaji wetu wa utulivu na amani katika sehemu za kazi hautakuwepo. Kwa hiyo, Serikali kama mwajiri mkuu lazima iheshimu, waajiri wenyewe na waajiriwa pia lazima waheshimu sheria za kazi. Hilo ndilo la msingi ambalo ninataka nianze nalo. Na tukifika huko, kama wataheshimiana na kila chombo kitafuata sheria na taratibu, nina hakika tutaendelea kuishi kwa utulivu na mani katika sehemu za kazi kama nchi yenyewe Tanzania ilivyo na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine napata tabu kwamba Serikali yenyewe ambayo inatunga sheria za kulinda mambo kama hayo, inakuwa mstari wa kwanza kuvunja sheria. Kwa mfano, iko sheria ya *Public Service* (nadhani inamhusu sana Mheshimiwa Waziri wa *Management*, lakini Serikali ni moja) ambayo inataka Serikali ipeleke mambo yake katika Baraza lile ambalo limeundwa kwa mujibu wa sheria ile ya kuangalia pamoja na maslahi na mishahara mbalimbali. Ningekuwa na muda ningeweza nika-*quote*, lakini muda wenyewe haupo.

Kifungu Na. 6, *Functions of the Services Joint Staff Council:- To advice the Government, to discuss recommendations, to negotiate matters relating to the terms and condition of service with respect to the public servants* na mengine mengi tu. Lakini taarifa nilizonazo, hotuba ya bajeti ambayo ilitolewa na Serikali hapa wakati wa hotuba ya Wizara ya Utumishi, haikufika kwenye Baraza hili. Sasa vipi wewe kama Serikali unatunga Sheria na wewe ndiye unakuwa mtu wa kwanza kuvunja sheria.

Ombi langu hapa ni kwamba wote watatu au hasa waajiri na waajiriwa na Serikali kwa maana ya kwamba ni mwajiri, lazima tuheshimu sheria, tumetunga wenyewe, hizi ndizo zitakazotuletea utulivu na amani katika sehemu za kazi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mwaka 2004 tulitunga sheria nyingi, lakini za kazi mbili: Ile Na.6 na Na.7, *Employment Labour Relations No. 6, 2004 and Labour Institution Act No.7, 2004.* Kwanza, Sheria zenyewe zimechelewa, zimetungwa mwaka 2004 na hapa ninayo sheria moja ambayo inaonyesha Mheshimiwa Rais ameisaini mwaka huo huo wa 2004, wala hakuchelewa. Kwa hiyo, hakuwezi kuwa na kisingizio kwamba Rais alichelewa kutia saini, kisingizio hicho hakipo. Mheshimiwa Mkapa, Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Tatu, alisaini mwaka 2004. Saini yake hii hapa, Benjamin Mkapa, tarehe 4 Juni, 2004. Lakini sheria hizi zimeanza kutumika Mei, 2007, takriban miaka mitatu, kwa nini? Wakati mwingine miswada inaletwa hapa haraka haraka, tunapitisha haraka haraka, lakini sheria zake hazitumiki haraka haraka. Kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka *SUMATRA* ilikuja tukaipitisha hapa haraka haraka, lakini ilikaa mpaka ikaanza kufanyiwa marekebisho hata kabla haijaanza kutumika. Tatizo liko wapi? Mimi ningeomba kama kuna uharaka wa kuleta hapa na vilevile tukishapitisha tunataka zitumike haraka ili ziwasaidie na zitatue matatizo ambayo tulikuwa tumekubaliana kwa mujibu wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na.6 kwa maoni yangu ina upungufu kadhaa. Upungufu wa kwanza ambao naweza nikasema ni kwamba hadi sasa hizo sheria hazijatafsiriwa, ziko katika lugha ya Kiingereza. Hivi mwananchi gani, mfanyakazi gani, mvuja jasho gain huku chini anayejua Kiingereza? Kiswahili tu!

Unapoandika sheria kwa lugha ya Kiingereza maana yake unataka kumnyima mfanyakazi Mswahili sheria kwa njia moja au nyingine. Kuna sababu gani za kutokutafsiri hizi sheria mpaka leo? Zimetungwa mwaka 2004 mpaka leo hazijatafsiriwa, zipo katika lugha ya Kiingereza kwa nini? Huo ndio upungufu wa kwanza, naomba zitafsiriwe haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa pili ambao mimi nauona ni kwamba hata zile taasisi au *Institutions* za kutekeleza hizo sheria zenyewe bado hazijakamilika. *Labour Court*, na *Commission for Mediations and Arbitration*, sana sana iko Dar es Salaam. Wananchi wako Mtwara, kule Mikindani, unategemea atoke Mikindani aje Dar es Salaam au atoke Singida aje Dar es Salaam? Wapi na wapi? Sasa hiyo yote hiyo ni kuchelewesha, matokeo yake sasa sheria hii imesababisha mlundikano wa kesi nyingi. Hapo zamani tulipokuwa tunatumia sheria ya zamani, tulikuwa na *Labour Officer* kila Wilaya, ambapo kesi chungu nzima zilikuwa zimejaa. Je, leo ambapo *Labour Court* ipo Dar es Salaam na *Commission* hazijaundwa katika mikoa na wilaya hali ikoje? Huo ni upungufu mwingine ambao upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu mwingine ambao tuliuzungumza sana wakati ule wa kutunga sheria hizi ni kwamba zina matatizo, zimeondoa ule udhibiti wa kumfukuza mfanyakazi kwa haraka. Ile Sheria Na. 62 iliyoundwa baada ya Ukoloni ilikuwa na maana ya kumzuia mkoloni, kwamba mwajiri yeyote yule asimfukuze mfanyakazi kiholela holela tu. Lakini hii kama tulivyobishana mpaka ilivyo sasa kuna uwezekanao nikaamka leo Missanga nikasema, "wewe nani? Juma! *alright* acha kazi nenda nyumbani kwako, basi!" Huo ni upungufu ambao upo, nadhani ni vizuri ungeangaliwa huko mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba sheria hizi bado hazijaanza kutumika sawa sawa ingawa zimetungwa muda mrefu zimeandikwa kwa Kiingereza, kwa hiyo, wananchi bado hawawezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba: kwanza, zitafsiriwe haraka. Pili, hao *CMA Officials* na *Labour Officials* Mikoani na Wilayani nao waweze kuwa *trained* na wapelekwe huko Mikoani. Kwa kweli haiwezekani mtu atoke Musoma aje afuate haki yake Dar es Salaam. Hilo naomba nilisisitize. Kama kweli tunataka tutoe haki, lazima wananchi wawezeshwe kuipata haki yao bila ya matatizo yoyote.

Tatu, sambammba na sheria hizi tulizungumza hapa habari ya *Workmans' Compensation* kwamba imepitwa na wakati, na tukaahidiwa tulipokuwa tunashika vifungu, wakati huo Waziri Kapuya akiwa katika Wizara hii kama nakumbuka sawa sawa, alisema itakuja mara tu baada ya hizi! Sasa tangu mwaka 2004 mpaka leo, hakuna

hata dalili. Hata ukisoma hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri, hakuna hata dalili kuonyesha kwamba inakuja hiyo sheria, yako maneno tu ya *blah blah,* maneno ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli mfanyakazi kafariki unamlipa shilingi 84,000/= na wewe unakwenda pale unasema kwa niaba ya Serikali nimekuja hapa kuwasilisha mchango wangu wa shilingi 84,000/=, wewe huoni aibu? Ni aibu shilingi 84,000/=. Mtu amefariki ndani ya kazi au mtu amekatika mikono au amekatika miguu analipwa shilingi 108,000/= leo hii! Sheria yenyewe hata kwenye kitabu chake Mheshimiwa Waziri ameandika ni sheria ya mwaka 1949! Hiyo si aibu? Hivi sisi toka tumejitawala mpaka leo tunashindwa kweli kukaa chini na kutunga sheria ya *Workmans' Compensation?*

Mbona mengine tunayaleta hapa? Yale yanayowafaa wafanyakazi na wananchi mbona hatuna haraka kama yale mengine ambayo yanatufaa sisi? Huu ni uonevu! Hata Waziri wa Maliasili juzi kaeleza kuwa wamebadilisha fidia ya mtu anayeuawa na ndovu na simba kutoka shilingi 50,000/= mpaka shilingi 200,000/= - kauwawa na ndovu na simba, lakini huyu aliyekufa kazini shilingi 84,000/=! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimejieleza vizuri, Serikali hasa Serikali ya CCM ambayo inawajali watu, inawapenda watu, inawathamini watu, ni vizuri sana ikaliona hili na ikaondoa hii dosari ambayo inaweza ikawapa rafiki zangu nafasi ya kusema sema bure wakati hawana sababu ya kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi wakati wa kujumuisha, kama Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu, ndugu yangu, lakini kama hatanipa tarehe maalumu, pengine shilingi au nusu naweza nikaipunguza kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *NSSF*, bahati mbaya muda haunitoshi, *NSSF* wamefanya kazi nzuri na tumeambiwa kwamba watu wanatoka nje wanakuja kuiga hapa! Bahati mbaya sisi watu wanaotufanyia kazi nzuri hatuwaoni, badala ya kuwasaidia, tunawapiga vita n.k.! kwamba watu wanatoka nje kuja kuiga mifano, nasema wapongezwe na wasaidiwe katika kila hali. Lakini pili iko dhana ambayo inaingia kwamba inaonekana hii Mifuko ya Wanachama inakwenda kihazina hazina hivi. Hii ni Mifuko ya wanachama, wananchi, wavuja jasho, ni mifuko yao, wao ndio wanufaike zaidi kuliko mtu mwingine! Hii ndio sababu tunazungumzia mambo ya kazi ambayo yako chini ya *ILO*, anayehusika hapa ni Waziri wa Kazi.

Unaponiambia hizi *social security* ziende Hazina, mimi sikuelewi kwa sababu anapokwenda Mheshimiwa Waziri Chiligati kule *ILO*, yeye ndiye anatakiwa kueleza ile *Convention* yetu mmeitekeleza namna gani na kadhalika na kama ni kusulubiwa, yeye ndiye anayesulubiwa! Dhana kwamba Serikali inaonekana inapeleka zaidi *social security* Hazina badala ya kuachwa kwenye Wizara ya Kazi na kufanya kazi katika hiyo naomba hiyo iondolewe, kwa sababu Wizara ya Kazi na Wizara ya Fedha zimefanya *study*. Kwanza, mnatupotezea hela zetu bure hapa badala ya kufanya kazi nyingine, *study* chungu nzima hazina sababu. Kuna *study* gani wakati dunia nzima hizi *Social Security* ziko chini ya Wizara ya Kazi na zinaenda kwenye *ILO*, wala haziendi sehemu zingine. Kwa hiyo, naomba sana hilo liangaliwe ili kusudi lisiwe linajirudia rudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Financial Institutions* kwa mujibu wa tafsiri ya fedha ni zile ambazo sijui *deposit* na kadhalika, lakini hii ni michango ya wafanyakazi, utaipelekaje kwenye *Financial Institution?* Hii ni michango siyo *deposits*! Mimi naona hii ni tofauti kubwa na kwa ninyi wasomi mnajua zaidi kuliko hiyo. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba ibaki Wizara ya Kazi na watu wa Wizara ya Kazi ndio wasimamie tena yote. Na hii habari ya kusema moja huku, nyingine kule, ndiyo hiyo sera mnaichelewesha bure bila sababu. Naomba muilete ili kusudi kuondoa hii dosari ambayo iko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho niseme, tumsaidie Mheshimiwa Rais. Naomba ninukuu kwa mfano hotuba yake ya Mei Mosi, ambayo Mheshimiwa Rais anasema: "Zamani Serikali ilikuwa inaamua, hivyo kwa wafanyakazi wote nchini hata wale wa sekta binafsi, siku hizi utaratibu umebadilika, maamuzi ya kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi wa sekta binafsi hufanywa na Bodi za Kisekta. Serikali inalo jukumu la kuhakikisha kwamba Bodi hizi zinaundwa haraka". Mheshimiwa Rasi amezungumza, lakini mpaka leo kwenye *speech* hii sijasikia kima cha chini. Mmekubaliana kwamba kutakuwa na vima vya chini vya sekta sijui nane, ngapi…! Mbona hamna kitu! Na kuna mahali Mheshimiwa Rais anasema kabisa kwamba siridhishwi, siridhiki na kasi hii.

Mheshimiwa Rais anasema kuwa "Serikali itahakikisha kuwa Mabaraza ya Kisekta ya Mishahara ya kima cha chini yanaendelea kuundwa, kwa ajili hiyo naiagiza Wizara ya Kazi kuongeza kasi ya uundwaji wa Mabaraza hayo, kasi ya sasa hairidhishi!" Jamani tumsaidie Mheshimiwa Rais, anapotoa maelekezo kama haya anajua, ndio maana siku ile mimi nilisema wakati mwingine kuna watu wanampiga piga vita Rais wetu mpendwa hapa, maana kwenye barabara, "tengenezeni barabara", "hela hakuna," "sijui hela hakuna!" Haiwezekani Rais aendelee kutoa magizo na maelekezo, halafu ninyi watekelezaji Serikalini mshindwe kuyatafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nitoe rambi rambi zangu za dhati kwa familia ya marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Mungu aiweke mahali pema peponi roho yake pamoja na wote waliofariki katika miezi hii ya nyuma mpaka katika kipindi hiki cha mwezi huu wa nane katika Bunge letu la Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la ajira kwa vijana wetu, lakini nianze kuwapongeza Mawaziri wetu watatu kwa jinsi ambavyo wameleta hoja yao nzuri mbele ya Bunge lako Tukufu. Tunawapongeza sana kwa hoja yao nzuri na pia wataalamu mbalimbali ambao walifanya kazi hii kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 iliahidi kutengeneza ajira milioni moja. Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi ilitambua kwamba sehemu kubwa ya Watanzania walio wengi ni vijana na hawa ndio wanaoathirika zaidi kukosa ajira. Changamoto iliyo mbele yetu ni kwamba Serikali yetu inatakiwa sasa iweke mazingira mazuri ili tuweze kuangalia jinsi ya kuwasaidia vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana kwa jinsi ambavyo wameweza kujali watoto wanaolelewa katika mazingira magumu. Msemaji aliyepita ameuliza kwamba, "je, Serikali yetu inawaandaje vijana, inawasaidia vipi wale vijana wa miaka 18?" Lakini naona kwamba Serikali inafanya mambo mazuri, maana kuanzia vijana wa umri wa miaka 12 na kuendelea, wengine inawachukua na kuwapeleka kuwapa stadi za kazi mbalimbali.

Zaidi ya hapo, hata wale ambao wako chini ya umri huo ambao hawajui kusoma na kuandika, bado Serikali yetu imechukua jukumu la kuwaondoa waliko katika mazingira magumu na kuwapa stadi za kazi na wengine wanarudishwa shuleni kuanza MEMKWA. Hivyo, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Tanzania kwa kazi nzuri inayofanya na tunaiomba iendeleze na iwaendeleze pia wale vijana wanaojifunza stadi za kazi mbalimbali iweze pia kuwapa vitendea kazi na mitaji wanapomaliza waweze kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa ule mpango wa shilingi bilioni moja moja kwa kila Mkoa. Kwanza kabisa, ningeomba Serikali ichukue majukumu ya kutoa elimu ya ujasiriamali kwa ajili ya wale walioko vijijini waweze kupata ile elimu waweze pia kunufaika na mikopo hii na zaidi sana waweze kupewa elimu ya kuweza kukopa na kurejesha mikopo yao sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuangalia ni jinsi gani Serikali yetu inaweza kulinda ajira za vijna wetu. Kwa mfano, ukitembelea maeneo ya Kariakoo, utakuta vibanda vingi ni vya Wachina. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha kwa sababu vibanda vingine ni vya *salon* na vingine ni vya kuuza urembo wa akina mama. Sasa utaona kuwa zile kazi au biashara ambazo Wachina wanafanya kule, ndizo zingefanywa na watoto wetu hao wanaolelewa katika mazingira magumu. Mimi sijui kwamba Serikali inawapa wageni maeneo makubwa ya kuchimba madini, inayapa makampuni makubwa wanaendeleza, bado kule chini kabisa wanaachia zile ajira ndogo ndogo za watoto wetu! Hivi tutawapeleka wapi watoto wetu? Naiomba sana Serikali iweze kuona hilo na pia iweze kuangalia ni jinsi gani watakavyoweza kuangalia vile vibali ambavyo vimekwishatolewa na pia ile Tume ambayo imewekwa kwa ajili ya kufuatilia vile vibali, iangalie vile vibali ambavyo ni sawa vile ambavyo si sawa viondolewe, viachiwe watoto wetu waendeleze shughuli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalopenda kuzungumzia ni suala la la usalama mahali pa kazi, kwa mfano viwandani. Kwa kweli tunamshukuru Mungu kwamba tumetembelea maeneo mengi. Viwanda vingi hapa nchini, baadhi yao

wanafanya vizuri, lakini kuna viwanda vingine akina mama hawaruhusiwi kupata mimba. Wasichana wakipata mimba wanafukuzwa. Hivi unapomfukuza mama kwa sababu amepata mimba, akijifungua anakula nini? Naomba hilo nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwanda kingine kule Arusha cha *Sunflag*. Hao nawapongeza sana kwa sababu wanajali akina mama, wanawapa kazi na akijifungua anapewa muda wa kwenda *maternity leave*, halafu baadae wakati anarejea kazini, na bado kuna basi la kiwanda la kuweza kuwapeleka nyumbani kwenda kuwanyonyesha watoto wao. Ninatoa wito kwa viwanda vingine, kwa sababu sasa hivi tunatekeleza falsafa ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, kwamba wanaweza pia kuweka kituo kwenye kiwanda chao ili akina mama wanapokuja kazini asubuhi, wanakuja na watoto wao mgongoni. Wana nguo za kubadilisha na kila kitu.

Kile kituo kinakuwa na *facilities* zote, watoto wanalelewa pale kama vituo vya kawaida ilimradi wakati mama anapojisikia kwenda kunyonyesha au kumwona mtoto wake mara kwa mara inakuwa rahisi. Kwa hiyo, mimi ningeshauri viwanda hivi vikubwa vinavyoajiri watu wengi pamoja na akina mama, waone uwezekano wa kuanzisha vituo kama hivyo na kuweka *facilities* zote na wahudumu wa afya wawepo na watu wa kuwatunza watoto. Nafikiri itakuwa ni vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea na mpango wa *NSSF* ambao kila mmoja anauzungumzia. *NSSF* kwa kweli ni watu wa kupongezwa na tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hebu angalia mji wa Dar es Salaam unavyopendeza, majumba makubwa ukiuliza hili utaambiwa ni *NSSF*, ukiuliza lile unaambiwa ni *NSSF*, ukiangalia na Bunge letu zuri hapa, *NSSF* nayo imejitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusu daraja la Kigamboni. Kwa kweli *NSSF* wamejiandaa kwa muda mrefu, wamekwishanunua viwanja vingi kwa ajili ya kujenga nyumba za bei nafuu kuwakopesha wananchi.

Sasa sielewei kuna sababu gani za msingi miaka mitatu sasa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilikwishatamka wazi kwamba hilo daraja litajengwa na *NSSF*, inakuwaje miaka mitatu tunavuta kamba, huku na kule, hivi kuna siri gani? Naomba sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa *NSSF* waweze kufanya kazi hiyo na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naishia hapo, asante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ningependa nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa hotuba yake nzuri ya kusisimua na vilevile niwapongeze na Naibu Mawaziri, Katibu wa Wizara hii pamoja na wote waliofanikisha hotuba hii hadi kuisifu kuwa nzuri kiasi hiki. Pia ningependa

nisisahau kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwani makusudio yake ya dhati ya kukabiliana na tatizo la ajira yanaonekana wazi wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa nianze mchango wangu katika Wizara hii kwa kuugawa katika makundi matatu:- Idara ya Kazi, Idara ya Ajira na Idara ya Maendeleo ya Vijana. Kwanza kabisa, tuelewe wazi kwamba jukumu la Wizara hii ni nini. Nadhani tumekwishasikia imeelezwa wazi wazi kwamba ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na vilevile Sera ya Taifa ya Usalama na Afya mahala pa kazi.

Mchango wangu niuanze na hii Idara ya Kazi. Jukumu la Idara ya Kazi kwamba ni kuratibu na kusimamia sera na sheria za kazi au kwa lugha iliyo nyepesi hawa ndiyo wanaotusaidia katika kuzuia na kutatua migogoro sehemu zote za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi kwa kweli tunaelewa yanafanywa na Wizara hii kwa ujumla, tunafahamu wazi kazi zinazofanywa huko Mikoani, majengo chungu nzima yamekarabatiwa. Mifano hai tunayo Arusha, Mbeya, nadhani kama sikosei hata Mtwara na Dar es Salaam, kwenyewe tunafahamu wazi kwamba ongezeko la ushughulikiaji wa migogoro kazini limeongezeka kwa kasi. Tunafahamu wazi kwamba rufaa zinazopelekwa kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Idara hii zimepatiwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hapa nimetoa pongezi na sifa lakini mahali popote penye sifa na pongezi pia kasoro hazikosekani. Katika idara hii kuna kero nadhani inanigusa mimi mwenyewe na nina hakika inawagusa wazazi wengi. Kero hii ni ongezeko la ajira kwa watoto. Hii ni kero na inamkera karibuni kila mzazi. Tunayafahamu wazi maeneo ambayo yana kero hii.

Tunaelewa wazi kwamba kuna maeneo ya mashambani hususan wale wenye kilimo cha biashara, kuna sehemu za migodini ambako huko siyo kufanyishwa kazi tu peke yake, tumesoma hata kwenye magazeti baadhi ya watoto wetu wanatumika kama kafara katika sehemu hizo. Kuna sehemu ambazo ni mbaya zaidi za madanguro. Ni hivi majuzi nadhani tumesoma kwenye magazeti, vijana wetu wa darasa la saba waliotoka Morogoro kwenda kufanya biashara hii ya ukahaba Dar es Salaam. Hebu Wizara hii iangalie ni jinsi gani ya kuitatua hii na kuipatia ufumbuzi endelevu. Tufahamu wazi kwamba watoto hawa tunaowazungumzia ndiyo taifa letu la kesho. Sasa tunapowaachia waharibike leo hapo kesho nani ataongoza?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ambalo napenda niongelee ni idara ya ajira. Katika idara hii mimi nimejaribu kuigawa katika maeneo mawili: ajira zilizo rasmi kwa maana ya kuajiriwa na ajira ambazo siyo rasmi kwa maana ya kujiajiri wenyewe. Katika hizi Idara ambazo ni za kuajiriwa tunafahamu kabisa juhudi zinazochukuliwa na Wizara hii kwani tunaelewa ni kwa jinsi gani ongezeko la vituo vya ajira limeongezeka kwenye miji ya Mikoa mbalimbali.

Tunaelewa wazi udhibiti unaofanywa kuhusu ajira za wageni wanaovamia nchi hii. Ni juzi tu, siku chache zilizopita hata Mheshimiwa Naibu Waziri wa Idara hii

ametuhakikishia kwamba kuna watu au wafanyakazi wasiopungua 400 wageni ambao wamefukuzwa na kurejeshwa makwao. Tunaipongeza sana, idara hii kwa hilo. Tatu, pia ni hili ongezeko la kazi za ufundi za ujuzi kwa maana ya *VETA*. Sote tunaona jinsi linavyoongezeka. Kwa kweli haya yanastahili pongezi kwani huu ndiyo utekelezaji kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu cha CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira nyingine ni hii tunayosema, ajira zisizo rasmi. Tunafahamu wazi ajira zisizo rasmi zinachukua nafasi ya karibu asilimia 90 hapa nchini. Kati ya hii asilimia 90 karibu 84 iko katika sekta ya kilimo. Sasa japokuwa kilimo iko kwenye idara nyingine lakini nitahusisha sana Wizara hii iangalie masuala ya kilimo. Tunapozungumzia suala la kilimo kwa kweli tunazungumzia uhai au maisha ya vijijini kwa sababu vijijini kazi zao kubwa ni kilimo na rasilimali zilizoko kule. Ili Kilimo hiki kiwe na thamani kwa kuitumia Wizara hii tungeomba kiwe na thamani, ardhi iwe na thamani kwa mkulima. Nina imani kabisa kwa sababu nazungumzia ajira hapa ambayo tumemhusisha mkulima basi Wizara hii itasaidia ardhi ya mkulima ipate thamani.

Mheshimiwa Waziri ameongelea kuhusu mikopo tumwezeshe mkulima huyu apate mikopo. Mikopo hii isiishie mijini au isiishie kwa wafanyakazi wa kuajiriwa. Mikopo hii iwafikie hata wale waliojiajiri wenyewe kwa maana ya wakulima. Ninapoongelea hapa wakulima hasa hasa ninamaanisha wale wakulima wadogo. Pia ningeomba Idara hii isisahau pia mkulima huyu anahitaji soko la uhakika. Kwa hiyo, japokuwa haya yanayohusu Idara ya kilimo lakini kwa sababu tunazungumzia ajira katika sekta ya kilimo basi Wizara hii isisahau kumhakikishia mkulima yule wa kijijini hususan mkulima mdogo soko la uhakika la mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiwango fulani naelewa wazi Serikali yetu inavyojitahidi kumsaidia mkulima huyu. Lakini mimi binafsi ningejaribu kuisihi imwangalie mkulima huyu ananyonywaje katika suala la bei. Serikali kidogo imejiweka pembeni kwa suala la bei ya mazao. Tuna mifano hai wenzetu wa korosho walivyokuwa wanalalamika hapa na siyo wa korosho tu mazao yetu kumnufaisha mkulima itabidi tumfikirie bei za masoko. Tunaiomba Wizara hii iingilie kati ili mkulima huyu afaidike katika kuuza mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niongelee kidogo kuhusu pia Idara ya Maendeleo ya Vijana. Kwa kweli huyu ni msimamizi mkuu wa sera na taratibu za kuwajenga vijana wetu katika maadili, kiuchumi na kijamii pia. Tunao vijana wengi wanaomaliza darasa la saba. Lakini karibu asilimia 34 ya vijana hawa huwa hawana bahati ya kuendelea na masomo ya sekondari. Sasa umefika wakati wa kufikiria nini tuwafanyie vijana hawa. Inawezekana kabisa tukawaweka katika makundi ya kuwapa mbinu mbalimbali za kujenga maisha yao ya baadaye. Vikundi hivi vinaweza vikawa ni vya kimichezo, vya kielimu, vya kiufundi, vinaweza vikawa pia vya uzalishaji mali.

Ongezeko kwa mfano la shule za ufundi au vyuo vya ufundi litasaidia sana katika kutatua tatizo hili katika kuwawezesha vijana wetu kiuchumi, kijamii na kimaadili. Pia mifano hai tunaiona katika nchi za wenzetu labda mashariki ya mbali walivyotumia kuwekeza kwenye ufundi na leo hii kuna nchi kama Malasiya, Indonesia, India

zinafaidika kwa hiyo ningeomba idara hii ikazane kwa kweli katika kuwekeza katika vyuo vya ufundi. Au uanzishwaji wa vilabu ungesaidia sana pia kuwawezesha vijana hawa kiuchumi na pia katika kuondoa badala ya kukaa vijiweni wakawa na sehemu za kupotezea muda.

Isitoshe pia mimi ningependa niipongeze sana Serikali yangu hii ya Awamu Nne, kwa maamuzi yake ya kufufua Jeshi la Kujenga Taifa. Huyu kwa kweli atakuwa mkombozi wa vijana wengi. Tunaelewa kabisa ni nini kinafanyika kwenye Jeshi la Kujenga Taifa, hususan kwa sisi ambao tumepitia maeneo hayo. Pale hufundishwi silaha tu, pale unafundishwa mbinu mbalimbali, unafundishwa ufundi, unafundishwa kulima. Kwa hiyo, vijana hawa nina imani watakapomaliza masomo pale au miaka yao miwili au mmoja watakuwa na ujuzi tayari katika sekta ya kilimo au ya ufundi na hivyo wataweza kujiajiri wenyewe au kupata ajira kwa urahisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa nigongewe kengele ya pili, nina hakika kabisa ajira ya watu milioni moja inawezekana kabisa ifikapo 2010. Baada ya hapo naunga mkono hoja hii. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kutoa rambi rambi zangu kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, naiombea familia yake iwe na subira na Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani na pongezi zangu kwa Waziri wa Kazi na Manaibu wake wote wawili, kwa kazi nzuri wanayoifanya na mipango mizuri waliyotuletea. Kwa nguvu za Mwenyezi Mungu ningeomba mipango hii itekelezeke na isiishie kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuongelea ajira za kujiajiri, yaani vijana wanaojiajiri ajira binafsi. Kumekuwa na mpangilio wa baadhi ya Halmashauri nyingi, hawa vijana tayari baadhi wanakuwa wamekwishapata mikopo, baadhi yao hawana mikopo, baadhi yao wanachukua mikopo sehemu nyingine kama *FICA, PRIDE, SEDA* na wanakwenda kujiajiri. Lakini inapofika baadhi ya Halmashauri nyingi zinawachukua vijana hawa na kuwahamishia maeneo ambayo ni nje ya mji ambapo hata hawawezi kufika kule kwa wakati wowote. Kwa hiyo, vijana hao kazi yao inakuwa ni kutembea na mizigo, asubuhi anapeleka mzigo porini nje kabisa ya mji na jioni anarudisha ule.

Sasa tunaposema kazi, ajira na maendeleo ya vijana, kwa stahili ya kuzunguka na mizigo, asubuhi unapeleka, jioni unapeleka huna unachokiuza, hawa vijana haya maendeleo watayapata wapi na lini. Kwa hiyo, ningeishauri Wizara hii kushirikiana na Halmashauri za miji watenge maeneo ambayo hata kama ni mtu anaweza akapita kwa bahati mbaya akaona kiatu kizuri akanunua, kijana yule tayari atakuwa ameshajipatia riziki na akaweza kuhimili ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hawa ambao wanajiajiri wenyewe pia kuna vijana ambao tayari wamepata ajira. Lakini kwa vijana hawa sio ajira inakuwa ni madhila, kwa sababu kijana ameajiriwa lakini inapita ndani ya miezi minne au mitatu kijana huyu hajapata mshahara wake, wakati kijana huyu yuko mbali na makazi na ndugu zake.

Serikali kwa kupitia Wizara hii inawafikiriaje vijana hawa? Vijana wengine ni waajiri wa Serikali yenyewe tayari wana ajira. Kwa mtindo huu ni kwamba tutawavunja moyo hata hao vijana ambao tayari wameshakubali kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kutolipwa mishahara kwa muda mrefu.

Baadhi yao hasa wasichana ndiyo hulazimika kuwa changudoa. Kama ni msichana miezi minne hajalipwa mshahara na hayuko kwao, yuko nje mbali kabisa na kwao, unatarajia nini? Je, unatarajia ataishije msichana huyu?

Matokeo yake atandanganywa na vitu vidogo vidogo na kukiuka maadili. Kwa hiyo, Serikali iangalie, isiwe kichocheo cha kuwafanya wasichana wetu kuvunja maadili kwa ajili ya kucheleweshewa mishahara yao. Tukitoka hapo tukirudi upande huo huo wa kazi kuna viwanda binafsi, hivi ndivyo vimekuwa kero kwa hasa kwa vijana wetu na si kero tu, naweza kusema kwamba hivi viwanda binafsi vinamaliza nguvu za vijana wetu bila mafanikio na faida yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo nikiwa na maana kwamba vijana hawa wanafanyishwa kazi kwa muda mrefu sana. Kwanza huanza kufanya vibarua zaidi ya miaka miwili mitatu, na bado mfanyakazi anaitwa kibarua tu. Baada ya kuwa kibarua kwa miaka mitatu anaajiriwa kwa mshahara wa shilingi 40,000, anamaliza kuajiriwa kwa mshahara wa shilingi 40,000 kwa kazi ngumu na muda mwingi wa kufanya kazi anatoka hapo akiwa tayari amekuwa mtu mzima.

Sasa amefanya miaka kumi ya kuajiriwa na miaka miwili ya kibarua analipwa kiinua mgongo laki mbili. Kwa hiyo, tunatakuwa hakuna tunachowajengea wananchi wetu wa Tanzania, ni kwamba tunawatafutia kwanza maradhi, mtu anafanya kazi katika hali ngumu kwa muda mwingi lakini kipato chake ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba Wizara hii ichunguze hasa viwanda vya samaki kote nchini hususan Kanda ya Ziwa viwanda vinawafanyisha vijana kazi ngumu. Kijana anakwenda kufanya kazi kwenye chumba cha barufu bila ya vifaa vya kuweza kumkinga baridi lile. Je, kijana huyu anapotoka pale anapewa kitu gani na mwajiri wake cha kuweza kumrudishia ile afya yake aliyoipoteza kwenye chumba cha barafu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara na Waheshimiwa Wabunge wanapoamua kufanya ziara kwenye viwanda kama hivi wasitoe taarifa wafanye kuvivamia kwa sababu ziara hizi sisi wengine tumefanya kwa kuzivamia, na kukuta watu wanafanya kazi bila vitendea kazi.

Lakini pale unapotoa taarifa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri anakuja lazima waweke mambo yao sawa kwa sababu wanajua kwamba watakuja kuumbuka kwa kitu fulani. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara hii iwajali wananchi, tusijali zaidi wawekezaji kwani wanakuja kutuumizia vijana na si kwamba wanawapa vijana ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kijana anakuwa anafanya kazi kwa muda mwingi, lakini pale anapotaka kusema kwamba wawe angalau na chama chao cha wafanyakazi, hasa wenzetu hawa wahindi wenye viwanda wanakuwa wakali sana. Wahindi watakapoona kwamba kuna kijana ambaye ameshikilia msimamo huo wa kuanzisha chama cha wafanyakazi ndani ya kiwanda kile anaweza akaambiwa na mhindi kuwa kazi basi.

Hakuna cha swali wala cha jibu, na kijana huyo atakapoachishwa kazi binafsi hajui aanzie wapi kwa sababu vijana wetu tunafahamu wanaofanya kazi katika viwanda hivi, elimu zao kwa kawaida zinakuwa ndogo, wanakuwa hawaelewi sheria ya aina yoyote, anaposimamishwa na yeye anakubali, hiyo kazi anaiacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee mikopo ya Halmashauri ya miji ya vijana. Ningeiomba Wizara iweze kutoa matangazo, kutoa maelekezo kwa sababu vijana wengi hawafahamu kwamba Halmashauri kuna mikopo ya vijana. Wanaofaidi mikopo hii ni wale jamaa zao wanaofanya kazi katika Halmashauri. Mfanyakazi anaweza akachukua ndugu zake, familia yake, wakaja kama vijana au kama kikundi wakapata mikopo hii wakati vijana walengwa mikopo hii haiwafikii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa niongelee mfuko wa uwezeshaji. Mfuko huu umetolewa kwa kila mkoa shilingi bilioni 1, lakini tunashindwa kuelewa jinsi tunavyotoka hapa Dodoma na kufika mikoani. Kila Wilaya unayozungukia wanakuuliza mkopo huu amepewa nani mpaka unatuwia vigumu kuanza kuzungukia wilaya zote. Kama sisi tunaoambiwa Wabunge wa Mikoa tunashindwa, utaanzia wilaya, kila wilaya unayokwenda kilio ni hicho hicho.

Sasa naiomba Serikali kama haikuwa tayari kuwawezesha kuwapa mikopo wafanyabiashara ndogo ndogo au kuwawezesha watu wenye maisha magumu zaidi, iweke utaratibu wa kuwawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana kuwa mikopo hii imechukuliwa na watu wachache wenye maisha nafuu kidogo, kwa sababu hiyo, ni bora Serikali ingewekeza katika viwanda au vijijini au katika matrekta ikawakodisha watu, wakalima, baada ya kulima na wakishavuna, Serikali ije kudai marejesho, lakini si hivyo walivyofanya. (*Makofi*)

Mikopo hii imefikia sehemu wanawake wamepigana wakaachana wazi barabarani. Mwanamke anakwenda kuchukua akiba yake aliyokuwa ameiweka chini ya

godoro akijua kwamba nichangie kutengeneza Katiba; nichangie kikundi changu kisajiliwe ili niweze kupata mkopo. Lakini dhamira na malengo yanakuwa si hayo.

Wanatokea watu wanamweleza kwamba ni wewe ndiyo uliyekuja kutukusanyisha pesa zetu na pesa hatujapata tumefika kwa mtendaji katufukuza. Tumefika kwa mtendaji naye anataka kitu kidogo ili aweze kupitisha hii Katiba yetu au rasimu yetu ya Katiba ili tuweze kusajiliwa, pesa ya kuendelea kutoa kwa mtendaji.

Kwa hiyo, kama huu mfuko unaendelea ningeomba usipitie mfumo ulioanzia nao mwanzo. Bora hata kama hii pesa irudi Halmashauri ya Mji au kwenye *SACCOS*.

Watu waelimishwe kwa sababu mtu mwingine ukimwambia *SACCOS* anajiuliza, kwanza, nini hiyo haelewi hata jinsi ya kufika kwenye ile *SACCOS* apate mkopo.

Haelewi wa kumwelimisha hayupo, hao wenyewe wenye *SACCOS* jinsi ya kuwaelimisha wananchi hawawezi kwa sababu na wao wenyewe wanazitaka pesa hizo.

Basi mradi ni mzunguko tu kwa sababu yule mlengwa aliyelengwa hakufikiwa na mkopo huo, na pia hata wale wanaofikia mkopo huo hao wachache wanakuwa hawana elimu ya mkopo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba Serikali kwanza itoe elimu kwa vijana kutoa, kwa kina mama, iweze kurudia mkopo huu na si kusema wapeleke kwenye *SACCOS* peke yao kwa sababu kuna watu wengine *SACCOS* hawaelewi, mtu unaweza ukamkuta kule yuko labda wilaya ya Ilemela, Isisebudaba umwambie *SACCOS* haelewi ni kitu gain.

Kwa hiyo, huyu mtu bado anahitaji mkopo huu ili na yeye ajivute kimaisha. Sasa hivi tunakuwa na malalamiko kwamba watoto wa mitaani wamezidi watoto wanaoishi katika mazingira magumu kulingana na maisha magumu ya wazazi wao.

Mzazi anakimbia familia, baba anamwachia mama, mama huyu labda kapata kutoka kwa mjomba wake shilingi 1,000 ai 2,000 akanunua labda biashara ndogo aende kuuza, akija mgambo wa Jiji au Halmashauri anapitia na kumfukuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mama huyu anakuwa hana uwezo tena wa kutunza wale watoto, na hajui aanzie wapi, matokeo yake anawaacha watoto wake wanazagaa mitaani, tunamwongezea Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mama Sophia Simba, mzigo wa watoto wenye mazingira magumu, lakini chanzo ni kazi ajira na maendeleo ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanasema kilimo ni uti wa mgongo, na mimi nasema Wizara hii ndiyo uti wa mgongo. Kama hawataweza kuwatetea wafanyakazi, vijana, wanawake katika mikopo yao, hakuna kitakachoendelea zaidi, badala yake badala ya wananchi kuwa mbele watazidi kurudi nyuma siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali irudie tena kulifikiria suala hili upya na isifikirie kwenye *SACCOS* kama nilivyoongea, iwafikirie na wale watu ambao kuna watu wengine ukimwambia hata *SACCOS* hakuelewi, lakini na yeye mkopo huu anauhitaji vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala mengine mfanyakazi anaweza, tusiseme tu wafanyakazi wa kawaida, anaweza tu mfanyakazi akawa amepata matatizo kidogo na kuna mfano hai ambao naweza nikautoa.

Kuna dada mmoja amepata matatizo kidogo ya kuugua kama miezi mitatu, minne, hivi. Yeye alikuwa akifanya kazi katika kiwanda cha *TFP*, alifanya kibarua kwa muda wa miaka miwili, kafanya kazi Mikumi na akaugua kwa miezi miwili lakini akawa ameambiwa kwamba amefikia muda wa kustaafu.

Lakini kitu cha ajabu dada huyu amelipwa kiinua mgongo laki mbili kwa miaka kumi na mbili yote aliyofanya kazi, hajui aanzie wapi kufuatilia haki yake, hajui ni nani atakayemsaidia au ni sheria ipi itakayomsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado naiomba Wizara Wizara hii angalau ijaribu kuweka bayana, iongeze vipindi vya matangazo kwa sababu matangazo ya UKIMWI ni mengi. Hata matangazo ya kazi yangekuwa mengi kama ya *VODACOM*, kila mtu asikie aelewe ili aweze kujitetea na kujua haki ya kazi yake iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kwa kuchangia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuchangia, Mheshimiwa Mpina yeye amekupisha, kutokuwepo kwake basi wewe umefanikiwa.

Wizara hii ni ile ambayo ina Naibu Mawaziri wawili. Naibu Waziri mmoja tutampa nafasi ya kuchangia kama kawaida dakika kumi na tano, Naibu Waziri mwingine atashirikiana na Waziri wake dakika sitini, na tutabakia kwenye Kamati ya Matumizi dakika sitini. Kwa hiyo, kwa sababu hizo dakika tano haziwezi kutosha kumpa mchangiaji mwingine. Waheshimiwa Wabunge watakaochangia tutakaporudi atakuwa, Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Abbas Mtemvu.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 12.57 Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Tulipositisha Shughuli za Bunge nilisema tutakuwa na wachangiaji wawili, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina ataanza na Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu atamalizia.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri pamoja na utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutoa salamu za rambirambi, kwa ndugu, jamaa na marafiki wa aliyekuwa Katibu wa Umoja wa Vijana, Mkoa wa Kilimanjaro, aliyekuwa Katibu wa Umoja wa Vijana Wilaya ya Chamwino, Bwana Bundala na aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana, Kata ya Mwanjolo, Wilaya ya Meatu. Kwa ujumla, Umoja wa Vijana na CCM imepoteza wapiganaji wake wazuri na Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona fahari kubwa sana, kuchangia leo katika Wizara hii. Katika uchaguzi wa mwaka 2005, Wenyeviti wa Vijana walioingia kugombea Ubunge na kuchaguliwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Taifa, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi. Lakini vilevile pamoja na Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Wilaya ya Meatu. Ninaona fahari kubwa na vilevile nichukue nafasi hii pia kuwapongeza vijana waliochaguliwa kwenye nafasi mbalimbali na wengine wamechaguliwa kuwa Madiwani, Wenyeviti wa Halmashauri, *DCs,* Mawaziri na vijana wengine ambao ninao humu, wamechaguliwa kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwahakikishie tu vijana wenzetu ambao wako nje ya Bunge hili kwambam tutaendelea kuwawakilisha vizuri sana hapa Bungeni na hata nje ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishukuru Kamati yangu ya Utekelezaji, pamoja na Baraza la Umoja wa Vijana la Wilaya ya Meatu, kwa sababu ndiyo hasa waliokuwa wakinipa nguvu hata kuthubutu kuchukua fomu ya Ubunge. *(Makofi)*

Mimi ningefikiri ili ikae *cronologically,* ingefaa zaidi iwe Wizara ya Maendeleo ya Vijana, Ajira na Kazi, kwa sababu huwezi kupata kazi kama huna *labour.* Lakini pia kupata *labour* lazima umwandae na anayeandaliwa sasa ndiyo huyu kijana. Kwa hiyo, ikikaa Vijana, *then* Ajira, halafu Vijana, Ajira halafu Kazi, nadhani itakuwa imekaa vizuri zaidi. Ninachotaka kukisisitiza sasa, ninatoa wito kwa vijana wetu ambao wako mashuleni, wako vyuoni, wanaosoma, wasome kwa bidii kwa sababu Taifa hili linawategemea sana. Waachane na migogoro isiyo ya lazima na migomo isiyo ya lazima. *(Makofi)*

Nilipokuwa nazindua Serikali mpya katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, nilitoa wito kwa wanafunzi wote nchini kwamba, waachane na migomo isiyo ya lazima, zaidi waingie kwenye mashauriano kutatua migogoro yao na badala ya migomo. Nikawakumbusha kama mnasema mnatoka kwenye familia maskini, lazima mjue wananchi maskini hawawezi kuzaa Serikali tajiri. Kwa hiyo, kuweni watulivu wakati

Serikali inashughulikia matatizo yenu. Hata hivyo, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla, ushauri tulioutoa wakati tunachangia Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia mwaka jana, ameufanyia kazi kwa karibu asilimia 100. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Kuhusu uwezeshaji kupitia Benki za *NMB* na *CRDB* sasa unalalamikiwa na watu wote. Wananchi wanalalamika, viongozi wanalalamika na watendaji wanalalamika. Fedha ni zetu, lakini tatizo lililoko hapa sasa anayeamua ni nani apewe mkopo na kwa kiasi gani ni benki. Sasa kama anayeamua ni benki, tutawezaje kufikisha hizi fedha kama tulivyowaahidi Watanzania kwamba, fedha hizi tutahakikisha zinafika kwa walengwa? Sasa huruhusiwi hata kuziona zile kumbukumbu tu. Mbunge hajui, *DC* hajui, Afisa Ushirika hajui. Utasimama lini uwaambie wananchi kwamba, fedha zimewafikia walengwa? Ni tatizo kubwa na tunahitaji tuliangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, anayeamua ni mfanya biashara na si viongozi. Mimi nakubaliana na Kamati ilivyoshauri kwamba, fedha hizi ni bora sasa ziende kwenye *SACCOS* moja kwa moja. Tufanye ule utaratibu kwamba, Vikao vya Kata na Wilaya, *actually* wale ndiyo wanawajua watu, wakisema wanakopesha wanawajua, lakini huyu mfanyabiashara wa benki, yeye atasoma tu masharti yake ya kwenye benki *then full stop.* Kwa hiyo, matokeo yake, fedha hizi zitaenda kwa watu wachache sana na wengi kukosa kabisa. *(Makofi)*

Mimi ninashauri fedha hizi ziende kwenye *SACCOS* moja kwa moja, lakini tuimarishe Kitengo, Idara ya Ushirika, Idara ya Vijana, pamoja na Maendeleo ya Jamii, kwa maana ya kuwapatia vifaa kama pikipiki waweze kufuatilia kwa karibu fedha zinazotolewa kwa wananchi kama zinafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Lakini kinachotupeleka benki ni kwa sababu benki wana Afisa Mikopo na sisi kwenye Halmashauri yetu, tuweke Kitengo cha Maafisa Mikopo, kazi yao ni kuratibu mikopo tu, hatuwezi kushindwa tunaweza, tuanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya fedha ambazo zinatolewa na Wizara kwenda Halmashauri kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Vijana na Akina Mama, lakini vilevile kila Halmashauri pia inalo jukumu la kutoa sehemu ya mapato yake kuchangia Mfuko huo. Tatizo kubwa tulilonalo sasa ni nani anayeratibu shughuli hizi. Je, Wizara inajishughulisha kuhakikisha kwamba, kila Halmashauri inachangia fedha hizo ili kutunisha huo Mfuko? Je, kwa utaratibu tuliouweka, zile Halmashauri ambazo hazichangii zinachukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama tungekuwa tumeji-*tune* kusimamia huu Mfuko vizuri kwenye Halmashauri, fedha zinazotoka Wizarani na zile za kwenye Halmashauri, nadhani hizi fedha za uwezeshaji zingetukuta tukiwa kwenye hatua nzuri sana na tusingebabaika katika utekelezaji wa suala hili kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SACCOS* za vijana kila Wilaya. Mheshimiwa Waziri, kwa kipindi kile wakati anawasilisha bajeti yake alisema kwamba, zitaanzishwa *SACCOS* za vijana kila Wilaya. Tatizo lililopo sasa hivi ambalo ninalihofia ni kwamba, sijui kama kuna utaratibu mzuri uliowekwa kuhakikisha kwamba, kila Halmashauri imeanzisha hiyo

*SACCOS* ya vijana. Sasa tujiulize ni *SACCOS* ngapi za vijana zilizoanzishwa kwenye Wilaya? Kwa sababu unaweza ukakuta *SACCOS* ya vijana ya Wilaya lakini mtandao wake ni pale mjini tu, inaitwa *SACCOS* ya Wilaya, haina mtandao halisi unaoiwezesha kuitwa *SACCOS* ya vijana ya Wilaya. Kwa hiyo, naiomba Wizara ifuatilie ione uanzishaji wa suala hili ni suala zuri na ni suala ambalo litasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi ihakikishe basi inaboresha mazingira ya wafanyakazi ili waweze kufanya kazi vizuri, waweze kutumika vizuri na waweze kuleta ufanisi wa utendaji kazi katika sehemu zao. Watendaji wa vijiji na kata tuliwaahidi, tulisema kwamba, watendaji wetu wengi wana elimu ya darasa la saba. Tujitahidi, tuwasomeshe wafike kidato cha nne. Tatizo lililopo ni kwamba, sijui Wizara inajishughulisha vipi kuratibu shughuli hizi, kujua watendaji hao ni wangapi sasa waliomaliza kidato cha nne na wangapi wako masomoni.

Sasa naongelea kuhusu watumishi kuhamishwa toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa. Watendaji wetu wengi waliohamishiwa Serikali za Mitaa, wengine hawajarekebishiwa mishahara yao mpaka sasa na hawapandi vyeo. Wizara ijishughulishe kuona hili. Kule kwangu kuna mgogoro mzito, yuko Irekebu na wenzake ambaye ni Afisa Kilimo kule Lingeka, wanalalamika sana kwamba, miaka 10 sasa hawajarekebishiwa mafao yao. Wizara ijishughulishe kuondoa migogoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vibali vya ajira vinachelewa sana, hata kama sababu za kujaza nafasi zinaridhisha lakini vibali vinachelewa. Miezi sita, miezi mitano, wakati labda imetokea mtu amefariki au amefukuzwa kazi, lakini kibali cha ajira kinachukua miezi sita mpaka mwaka; kwa nini? Sheria ngumu za ajira, Maendeleo ya Jamii tunapashwa kuajiri sasa hivi Maafisa Maendeleo wa Jamii kila Kata, sasa unaambiwa uajiri mwenye digrii utamtoa wapi? Tunaomba turuhusiwe tuajiri wenye *Certificate.*

Mwisho, gari la wagonjwa Mwandoya. Ninatoa wito kwa Wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa kwamba, gari la Mwandoya sasa liko bandarini na nitakuja muda si mrefu kulikabidhi. Nampongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kushughulikia matatizo ya Wananchi wa Kisesa na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Mheshimiwa Rais, siku moja nilim-*quote* alikuwa akisema kwamba: "Nahitaji viongozi wenye dhamira ya kweli, kuondoa umaskini wa Watanzania." Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, viongozi wenye dhamira ya kweli ya kuondoa umaskini wa Tanzania tupo na tutamuunga mkono mpaka ukamilifu wa bahari. Wanaobeza kasi mpya, hawako tayari kufanya kazi. Acha kasi mpya iendelee na tutaiunga mkono mpaka mwisho. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana kwa kuniachia dakika nne. Sasa nitamwita Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri, Naibu Mawaziri wote wawili, pamoja na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwanza kwenye eneo ambalo wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nililieleza kidogo na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati anajibu alisema masuala yanayohusu Wizara mbalimbali, basi wahusika Mawaziri watajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilizungumzia Sekta ya Ajira Binafsi. Nilizungumza kwamba, Serikali iangalie sasa ni namna gani tunasaidia Sekta ya Binafsi. Mara nyingi tumekuwa tukitamka nyongeza ya mishahara kwenye Mashirika ya Umma na Serikali, lakini tumekuwa tukiisahau sana hii sekta ya ajira binafsi. Nilitoa mifano mahotelini, makampuni ya ulinzi na maeneo mengi tu ya sekta ya ajira binafsi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, alilizungumzia sana hata Mheshimiwa Rais, kwenye Mei Mosi aliwahi kulizungumzia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri, umefika wakati kama Serikali, kulitazama hili eneo la sekta za ajira binafsi, kwa sababu kwa kweli kima chao cha chini kinatisha sana. Lakini si hivyo, nilizungumzia suala la pili kwamba, sasa Serikali ina mpango wa kutoa vitambulisho vya Kitaifa. Ni muhimu wakati tunatoa vitambulisho hivyo basi tukasajili wafanyakazi wote wa sekta za ajira binafsi ili wakati wanapata vitambulisho na ikiwezekana tukahakikisha mishahara yao wanalipwa kupitia benki. Hii itasaidia sana na wao kushiriki kuchangia katika pato letu la kodi la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi zilizoendelea, wafanyakazi wake wote hulipwa kwa njia ya benki. Kwa kweli tutapata pato kubwa sana, kwa sababu sekta ya ajira binafsi ina watu wengi sana na mimi nirejee kama wenzangu walivyozungumza kwenye mkopo wa JK. Kwanza, naipongeza Serikali, Rais, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wabunge, kwa mpango ule mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia katika Wilaya yangu ya Temeke. Zoezi lilikwenda vizuri kiasi na hasa kwenye benki ya *NMB*. Utaratibu haukuwa mzuri sana. Mheshimiwa Waziri, wewe ulikuwa Mkuu wa Wilaya ya Temek, na uliunda vikundi vingi sana pale Temeke na unajua Wananchi wa Temeke wanavyokupenda, kuna bustani ya Mwembe Yanga pale mpaka kesho ina heshima yako, kwa kupanda miti mizuri na inakua vizuri. Lakini nataka kukuhakikishia, vile vikundi ambavyo wewe mwenyewe ulivianzisha, vingi havikupata mkopo kutokana na urasimu mkubwa uliokuwepo katika benki hiyo ya *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano Mheshimiwa Waziri, kuna kikundi tulikisajili kwa nguvu sana pale Kurasini, *OMASCO,* wakapata usajili tarehe 22 Machi, 2007. Kikundi kina akina mama karibu 50, wakafungua pale benki ya Temeke kwa shilingi laki tano. Lakini ninakuhakikishia akina mama wale wamesumbuka mpaka leo wanataka kuvunja kile kikundi. Lakini si hivyo tu, nakupa mifano tu michache; wapo

wengi, yuko kijana anaitwa Nasibu yupo Tandika pale, ana duka lake zuri sana. Yule kijana ni hodari, mimi mwenyewe nilipata kumwazimia mahali dola 3,000 kutokana na uhodari wake na alilipa kwa wakati. Alikwenda ile benki alizungushwa kweli kweli na mahitaji yote yaliyohitajika aliyapeleka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo, nimalizie kuna kikundi kingine cha *Amkeni Women Group,* kiko Kurasini, kilifungua akaunti pale kikaweka karibu shilingi milioni mbili, lakini hadi leo kupata mkopo kwa benki hii ni tatizo sana. Mpaka wengine wakahamishiwa *Morogoro Road* na mimi pale nina *account* kusema kweli pale *Morogoro Road* wanafanya kazi nzuri sana. Lakini pale Temeke tumepata matatizo makubwa sana. Mkuranga hawana benki, watu wao walikuwa wanatoka Mkuranga wanakuja Temeke lakini cha ajabu wote walikuwa wanarudishwa bila ya kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mimi katika hili, naipongeza sana *CRDB* na nasema ndugu yangu Dr. Kimei udumu. Wako akina mama zangu pale Wateu, mfano mmoja tu walipeleka mahitaji yao, wakaambiwa *documents* zinazohitajika wakafikisha, walichukua mwezi mmoja tu kikundi cha watu 2006 wakapata milioni 165 walizohitaji, mwezi mmoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hili ulitazame na kwa Temeke utazame kwa macho ya huruma. Unajua Temeke unavyopendwa ikiwa 2010 ukiamua fomu Temeke hata mie sichukui fomu. Najua mapenzi yako kwa watu wa Temeke ulivyokaa nao vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba uitazame Temeke kwa jicho la huruma katika hili, vikundi vyake vyote havikupata pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine Mheshimiwa Waziri, Dar es Salaam tulipata shilingi bilioni moja. Naomba Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri, mjaribu kutazama Dar es Salaam, sasa tunafikia karibu watu milioni 4.5. Unatupa shilingi bilioni moja na usisahau sasa hivi vijana wote, Mikoa yote, wakimaliza la saba, mahali pa kukimbilia kutafuta kazi ni Dar es Salaam. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba na hilo ulitazame kwa jicho la huruma, hatukatai vijana wasije Dar es Salaam, tunawakaribisha kwa mikono miwili lakini mtupe basi stahili zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye eneo la *NSSF.* Wabunge wenzangu waliotangulia, walilisifia sana Shirika hili kwa kazi nzuri na mimi niungane nao kulisifia kwa kazi nzuri inayofanywa na *NSSF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Mtu akifanya vizuri, anastahili sifa na mtu akifanya vibaya basi anastahili kuzomewa hata ikiwezekana. Lakini *NSSF* kusema kweli kuanzia Waziri mwenyewe, Bodi na Menejimenti wanafanya kazi nzuri, tunawasifia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi niliona Shirika hili likiingia makubaliano na Jeshi la Polisi, kuhusu ujenzi wa nyumba za Polisi na nikamsikia *AGP* anasema hiki kidogo tunaomba kingine kiongezwe. Naamini kile walichopewa tayari kimepangiwa, lakini ikitokea wakaongezwa tena, naomba basi *NSSF* Mheshimiwa Waziri na *AGP*

muangalie uwezekano wa nyumba za Polisi za *Kilwa Road*, hali yake mbaya sana. Tuna eneo kubwa la kubomoa zile nyumba ndogo tujenge nyumba kubwa za ghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuangalie uwezekano wa nyumba za Chang'ombe Polisi za siku nyingi sana. Leo msisahau jamani Uwanja wa Kimataifa umejengwa pale Temeke. Kila aina ya wageni watapita maeneo hayo, wataziona zile nyumba za ndugu zetu. Kwa hiyo, naomba kama wataongezewa pesa, basi tuangalie umuhimu wa nyumba zile za *Kilwa Road* na Polisi Chang'ombe. Lakini pia niipongeze *NSSF* lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais na nimpongeze sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uamuzi wa jengo la Wachinga, ambalo litagharimu karibu shilingi bilioni kumi pale Ilala Dar es Salaam. Tunapongeza sana. Litasaidia sana kuwafanya hawa wafanyabiashara ndogo ndogo wafanye kazi zao vizuri, wafanye kazi zao kwa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili nitamke na Mheshimiwa Waziri Mkuu, liko suala la Daraja la Kigamboni. Suala hili sasa limekuwa linasemwa sana na watu wasiohusika, maana yake wanaohusika na suala hili ni CCM. Imo kwenye Ilani, naomba ninukuu ukurasa wa 54 eneo la (f).

Mheshimiwa Naibu Spika, inasema: "Kuhimiza maandalizi na ujenzi wa Daraja la Kigamboni chini ya Uongozi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* ili kuunganisha Kigamboni na Dar es Salaam. Sasa Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tusipoangalia suala hili liko kwenye Ilani ya CCM. Lakini linaweza likachukuliwa na wasiohusika likawa suala lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alisimama hapa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu akasema daraja litajengwa. Alisimama hapa Waziri wa Kazi aliyepita, Mheshimiwa Profesa Abdallah J. Maghembe, akasema daraja litajengwa. Sasa hadi leo hatujui kama daraja litajengwa lakini kwenye Ilani limo na kwenye kitabu limo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri japo atoe tamko basi, daraja litajengwa au halitajengwa. Ni vizuri kwa sababu tayari *NSSF* imeshaonesha nia na leo watu hapa wameisifia kwa kila namna, jinsi inavyofanya kazi, inavyoboresha na inavyoweka majengo ya kisasa. Tumeambiwa hapa na Mheshimiwa Waziri aliyepita kwamba, yale mambo yote yanayofanyika, yanafanyika kwa mkopo na hela zinarejeshwa.

Sasa eneo hili la daraja kuna tatizo gani? Si vyema kusema, lakini hali ya vivuko pale Kigamboni ni mbaya sana. Hatuombi, Mwenyezi Mungu atujalie na kitu chochote kibovu ukikiweka mahali iko siku kinaweza kufanya mambo ya ajabu, sijui tutaambiana nini? Mimi naomba Mheshimiwa Waziri, tupate tamko daraja litajengwa lini na kama halijengwi tuambiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na sina la kuongeza. Asante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iweke *job centers* kila Mkoa ili kuwe na kituo kinachounganisha wanaotafuta kazi na wanaotafuta wafanyakazi, pia kuwepo na *job agencies*. Hadi leo tunazo *job centers* ngapi nchini Tanzania mikoani hasa mkoa wa Iringa?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti na ina changamoto kubwa hasa kwa kuwa tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya kijana ni miaka 18 hadi 35, na vijana ni wengi kuliko watu walio na umri zaidi ya miaka 35, na mbaya zaidi *life expectancy* yetu inaendelea kushuka siku hadi siku na sasa ni miaka 47. Kwa hivyo, nguvu kazi ya Taifa hili iko katika umri a miaka ya ujana.

Mheshimiwa Naibu Spika, umri wa kijana aliyebahatika kusoma vizuri atamaliza *degree* yake ya kwanza akiwa na miaka 21 hadi 23. Kijana huyo akienda kwenye soko la ajira anaambiwa lazima awe na uzoefu wa miaka 5 hadi 10, je, amepata wapi uzoefu nje ya kazi wakati akiwa shuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni kuwa vijana wengi wanakosa ajira kwa kigezo cha uzoefu zaidi ya miaka miyano hadi 10? Je, Wizara inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tathimini ya nguvu kazi ya mwala 2002 kati ya nguvu kazi ya Taifa ya watu milioni 17.9 ni 65% ni vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35, ambayo kwa sasa Waziri amesema imefika 11% maana yake imepungua kwa asilimia moja ndani ya miaka mitano. Kweli tutafika? Hii ni aibu, kasi mpya iko wapi? Hii ina maana nyingi, ukosefu wa ajira ni 25.5% na Jiji la Dar es Salaam ni 46.5% hii ni hatari. Maana yake katika vijana wawili, mmoja hana ajira kwa hiyo, vijana wengi hawana ajira ni *mission town* na wengi wako vijiweni na wengi wao hutumika kipindi cha chaguzi kama ngazi ya kupata nafasi kwa ahadi tamu halafu wanaachwa kwenye mataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaleta matatizo kwa vijana, wanapata msongo wa mawazo *(depression),* wanajiingiza katika matendo ya wizi, ujambazi, unyang'anyi na wengine wanajihusisha kwenye biashara ya ngono kwa vijana wa kike na wa kiume, wengine wanaangamia kwenye ulevi wa kupindukia ikiwemo dawa za kulevya na wengi kufa mapema kutokana na matokeo ya matendo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ichukue hatua za haraka juu ya matatizo hayo, *we need sense of agency, its emergency to our country*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *vision 2025* itafanikiwa kama Serikali itajali vijana wake na lazima vijana washirikishwe katika mchakato mzima wa kuwaondolea matatizo yanayowahusu. Uchambuzi wa MKUKUTA umeonyesha wazi ni hatari kuwaacha nyuma

vijana kwani wao ndio wengi na kama kweli tuna lengo la maendeleo ya milenia na endelevu ya kiuchumi, kijamii na hata ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Vijana, naamini vijana wakipata chombo chao tutakuwa na sehemu moja ya kutolea sauti zetu kwa umoja, chombo hiki kitasaidia kutoa maoni mazuri yahusuyo sera za vijana na matakwa ya vijana kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya waanzilishi wa baraza hilo tayari wamepoteza sifa ya ujana, tatizo lipi limefanya uchelewe? Historia inaonyesha baada ya vyama vingi mwaka 1996 asasi mbalimbali mfano *National Youth Forum (NYF)* na baadaye *TYVA* Tanzania zimekuwa zikipigania uanzilishi wa Baraza hilo lisilokuwa na itikadi lakini hawakupata kitu, je, ni lini sheria ya uundwaji baraza hilo italetwa Bungeni kama Muswada hatimaye ipite kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaelewa bado *solution* ipi imewekwa kwa vijana hao, Waziri amesema wanajengewa eneo maalumu la biashara, je, wameshirikishwa, maana mwaka jana walitumuliwa mijini eti miji iwe safi na baadaye wakapewa nafasi eneo la Kigogo ambalo liko Ukanda wa Msimbazi, mvua ikinyesha maji yanajaa na mabanda yapo katika hali duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa sasa wa kutoa mikopo mfano ile ya bilioni moja kila Mkoa inayoletwa kwa *SACCOS* na mtu mmoja mmoja ambao wengi hawana mitaji, hivyo mikopo hiyo ndiyo mitaji mibaya zaidi hawana ujuzi wa biashara na wengi hugeuka kuwa wamachinga hivyo Serikali inaongeza tatizo la wamachinga badala ya kutatua tatizo la ajira na matokeo yake watashindwa kulipa madeni ya mikopo hiyo kwa kuwa wamachinga hawana maeneo maalumu katika miji mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ibadili utaratibu wa utoaji wa mikopo kwanza riba ni kubwa na vile vile mikopo ni dhana nzuri lakini si njia ya haraka ya kuondoa matatizo na kujiletea maendeleo hasa ile mikopo midogo midogo haileti mafanikio bali mtatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ni zaidi ya kuuza na kununua, Serikali ianze kutoa mikopo kwa wanataaluma mbalimbali na wazalishaji mali ikiwemo watoa huduma. Mfano, Serikali ikiwakopesha vijana wakulima katika kikundi, soko lao basi ajira inakuwa imepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wanataaluma mfano wanasheria wakopeshwe *as a group* kuanzisha kampuni ya uwakili na msaada wa kisheria. Waliosoma biashara wawezeshwe *as a group* kuwa washauri wa masuala ya biashara wataleta ufanisi kwa jamii watakaopata ushauri na mafunzo hayo. Tubadili *mind set* zetu, yawezekana kupata ajira zaidi ya milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wafanyakazi kiwanda cha chumvi Uvinza, Serikali iliagiza *PSRC* kutangaza uuzwaji wa hisa asilimia 81.33 kutoka katika kiwanda

kiitwacho *Great Lakes Mining Cooperation Limited* na kununuliwa na *Nyanza Salt Mines,* tangazo hilo lilitoa uhakika kwa wafanyakazi kuwa wanaendelea na kazi na wakipunguzwa basi watapata maslahi yao, wafanyakazi 383 walipunguzwa lakini hawajalipwa mafao yote, tatizo ni lipi? Naomba jibu kwenye hitimisho la Waziri pamoja na mengi niliyouliza. Miaka nane imepita sasa wafanyakazi wa kiwanda cha chumvi hawajatatuliwa tatizo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake wote kwa hotuba nzuri na yenye ufasaha mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii, baada ya hayo ninaomba kutoa maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la hela za uwezeshaji zinazojulikana kama hela za Rais Kikwete, hela hizi zinaonekana kama utekelezaji wa utoaji wa mikopo inayotokana na hizi hela hairidhishi, kwa mfano katika Mkoa wa Morogoro wananchi wa vijijini wanakosa hii huduma kwa kisingizio cha umbali.

Je, hizi ni hela za Benki au ni za Serikali kwa ajili ya wananchi maskini ambao wengi wao wapo vijijini? Hali hii isiporekebishwa hatutaweza kuwadhibiti vijana wasihame vijijini kwenda mijini.

Mheshimwa Naibu Spika, nashauri Serikali itumie Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambao wanauzoefu wa kutoa mikopo midogo midogo kwa wananchi vijijini, hizi *NGOs* zifanye kazi na *SACCOS* na vikundi vidogo vidogo huko vijijini. Pia *NGOs* hizi zipewe jukumu la kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake ili waweze kuwa na stadi za kubuni na kuendesha miradi kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia ajira ya wafanyakazi wa majumbani, je, Serikali ina mpango gani wa kurasimisha eneo hili kama inavyotambulika? Hawa wafanyakazi wangepewa nao *priviledge* ya kutambulika pamoja na hali ya kufanyakazi katika mazingira salama, wapewe heshima na haki zote za ajira kama kulipiwa *NSSF* na matibabu wakiumwa. Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani bado hawajafanya kazi ya kutimiza wajibu wao vizuri, kwa mfano ajira hii inawashirikisha watoto na pia kuna unyanyasaji wa kijinsia kwa kiwango kikubwa. Je, Wenyeviti wa Mitaa hawataweza kuisaidia Serikali katika kudhibiti hali ya unyanyasaji wa watoto hawa wanaoitwa *house girl,* Serikali iwape agizo na msisitizo wa uwajibikaji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ajira za akinamama wanaofanya kazi katika sehemu za burudani na *Guest Houses*, hawa akinamama bado hawajapewa heshima ya kazi yao pamoja na malipo yanayostahili, afya zao zipo hatarini kwa sababu wengine wanaambiwa kuwa malipo yao yanatokana na wateja. Hali hii imesababisha

hawa wahudumu kuwa kwenye mazingira ya kunyanyaswa kijinsia. Serikali ina mpango gani wa kurasimisha na kuipa heshima ajira hii?

Kuhusu huduma za burudani kwa vijana na jamii yote hususani katika maeneo ya vijijini pia hili ni tatizo kubwa. Ajira ya vijana katika sekta ya vijijini naomba Serikali itoe mkakati pamoja na mipango kabambe ambayo imechelewa kwa ajili ya kuwawezesha vijana walime mazao ya chakula na biashara na wanaweza kulima vitunguu, wakafuga nyuki, mabwawa ya samaki na aina mbalimbali za mboga mboga na wasaidiwe kupata elimu na masoko kwa ajili ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama katika sehemu za kazi pamoja na kero ya rushwa za aina zote, vijana wanaumia kazini lakini hata matibabu hayapo licha ya *compensation,* naomba Wizara iwaangalie na kuwafuatilia maofisa kazi hasa wale ambao wanashirikiana na waajiri wengine hasa kwenye *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuipongeza *NSSF* kwa kazi nzuri, naomba *NSSF* iwaelekeze vizuri maofisa wao mikoani kuhusu ushirikiano wao na mahusiano na waajiri *special* kama *NGOs* zinazofanyakazi na *volunteers* kwani inapokuwepo fursa ya kumpata mfadhili wa kulipa mishahara ya baadhi ya *volunteers* basi hao maofisa wasiwape uongozi shida. Hali hii ipo na inafanya waajiri wengine waone *NSSF* kama ni wachache na naamini kwamba Wizara na uongozi wa *NSSF* watashughulikia hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba *NSSF* hapo baadaye itaangalia uwezekano wa kuwasaidia vijana wetu waweze kupata mikopo kupitia *SACCOS* zao. Hii ni njia mojawapo ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri kwa kazi anayoifanya pamoja na Manaibu wake wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe shukrani sana kwa msaada mkubwa kwa vijana ambao mmewawezesha kwenda kwenye mafunzo ya *demand driven skills* kama ilivyoonyeshwa katika ukurasa wa 56 wa hotuba yako, idadi inayoonyeshwa ni 20 lakini ukweli waliopelekwa ni vijana 40 ambao bado wako chuoni, lakini pamoja na shukrani nilitaka niulize, je, mmebuni mkakati gani au vitendea kazi vya kuanzia shughuli husika ili wasije wakabaki na elimu ambayo wanashindwa kuifanya kazi? Hakika hapatakuwa na *impact* yoyote, naomba jibu.

Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 62, kiambatisho Na. V-B kuhusu kiasi cha fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi katika Mkoa wa Tanga, Wilaya zote za Mkoa zimepata huduma hiyo isipokuwa Wilaya ya Kilindi, je, sababu ni nini hata kama tutengewe fungu kidogo ili kuhakikisha fursa sawa kwa kila Wilaya zote? Je, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha angalau fedha kidogo katika Wilaya ya Kilindi ili kurudisha imani kwa wanakilindi kuhusu *SACCOS* iweze kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jibu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, kwa kuandaa hoja ya Bajeti vizuri na kuwakilisha kwa umahiri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitazungumzia eneo moja, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa nia nzuri aliyoiweka na kuitekeleza kwa kuanzisha mfuko wa kuwezesha wajasiriamali kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tangu uanzishwe mfuko huu wa bilioni moja kila Mkoa nadhani ni wakati muafaka wa kuangalia katika maeneo yote mafanikio na matatizo wakati tunaendelea na awamu ya pili ya uwezeshaji. Ni muhimu kufahamu katika maeneo yaliyo na matatizo tufanye nini na matatizo yenyewe ni yapi ili tupate jibu la haraka na kuyapatia ufumbuzi utakaoleta faraja kwa walengwa na hivyo kufanya lengo lililokusudiwa kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wilaya ya Namtumbo wananchi wake asilimia 90 na zaidi ni wakulima na ndiyo wajasiriamali wetu, *income* ya kuendeshea maisha yao inategemea kilimo, ukitaka kumsaidia mjasiriamali wa Namtumbo unamsaidia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika awamu ya kwanza ya mkopo huu wa bilioni moja kila Mkoa katika mwongozo uliotoka ilitafsiriwa wajasiriamali ni wale wenye biashara ndogo ndogo, katika Wilaya ya Namtumbo mkulima hakupata mkopo. Katika Wilaya yetu wajasiriamali 680 waliomba mkopo na waliopata ni 45 tu hadi kufikia tarehe 26 Juni, 2007 na pesa iliyotolewa mkopo ni shilingi 18,700,000 tu. Kati ya wajasiriamali 1,079 na shilingi 569,000,000 zilizotolewa na Benki ya *CRDB/NMB* ni watu 45 tu na shilingi milioni 18.7 tu ndizo zimetolewa Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo na sababu kubwa ni hakuna Benki. Lakini kuna mtandao wa *SACCOS* za Dunduliza ulioimarika wenye wanachama 8,015 wa Namtumbo kati ya wanachama 17,133 katika Mkoa wa Ruvuma na wanachama 52,591 nchi nzima na pia kuna *SACCOS* tatu za Namabeyo, Lusewa na Mkongo Gulioni ambazo zimeimarika na kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtuingizie *SACCOS* za Dunduliza katika awamu hii ili waweze kutoa huduma hii vizuri na wanachama wake ambao wengi wako katika *SACCOS* za Namtumbo.

Kwa mtazamo wa nchi, *Dunduliza Saccos Network* wapo katika Mikoa ya Mwanza ambako kuna wanachama 10,080, Mara wanachama 12437, Dar es Salaam wanachama 12,941, Ruvuma wanachama 17,133 ambapo jumla yake inakuwa ni wanachama 52,591.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa mtazamo huo *SACCOS* hizi zina uwezo wa kuwafikia wananchi wa kutosha walio wanachama na wanaimani nao kwa kuwa wanawafahamu kuliko *NMB* ambao inawawia vigumu kufanya maamuzi ya kutosha na kwa waombaji wengi pale ambapo hawana *branch* na hivyo kukosa imani na waombaji ambao sio *customers* wao. Kwa mfano huu wa Namtumbo, walioomba *NMB* - Songea Mjini kutoka Namtumbo ni 680, waliopata ni 45 tu. Tunaomba mtuingizie katika utaratibu wa awamu ya pili, *Dunduliza Saccos* ili waifanye kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga hoja mkono.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema siku ya leo na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kunifikisha hapa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wa Wizara hii kwa kutekeleza na kusimamia vyema majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa hifadhi ya jamii *NSSF* ni muhimu sana kwa maslahi ya wastaafu, ufanisi wa mfuko huu ni kutunza vizuri fedha za wafanyakazi na hivi sasa ili kuongeza tija zaidi kwa wafanyakazi na hivi sasa ili kuongeza tija zaidi kwa wafanyakazi inawekeza miradi mingi ya maendeleo kutokana na hili hatuna budi kuipongeza *NSSF* kwa hilo kwa sababu kufanya hivyo ni kuongeza mfuko wa wafanyakazi wote katika nchi pia kujiimarisha zaidi kutoa misaada kwa watu wengi zaidi na kutimiza majukumu waliojipangia kwa mujibu wa sheria na haki za wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kuondosha vizingiti katika miradi ambayo imeanzishwa na *NSSF*, pia suala la wafanyakazi wa *NSSF* kuwa wanachama wa mfuko mwingine, naomba lifikiriwe upya kwani kufanya hivyo ni kuwanyima haki wfanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango wangu mfupi na kwa kuwa mengi yamechangiwa na wasemaji wengi. Naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nimshukuru Mola kwa kuniwezesha kuishika kalamu nami nikatoa mchango wangu katika hotuba husika.

Pia nikupongeze wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa umahiri wenu wa kutuongoza vema hapa Bungeni. Pia namshukuru Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kutuandalia hotuba ambayo itamfanya kijana apate mategemeo ya maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba niende katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa vijana, napenda kusema mwenye macho haambiwi tazama, natumia msemo huu nikiwa na maana bado vijana wetu hawana ajira Serikalini, Mashirika na kwa watu binafsi. Hali hii hupelekea vijana wetu kuingia katika matendo maovu, tunaposema Halmashauri zitoe mikopo kwa vijana tunajidanganya kwani haziwafikii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vijana kukimbilia mijini ni alama tosha kuwa wanaamini huko ndiko kunakopatikana ajira. La kusikitisha kabisa ni kitendo cha baadhi ya miji mikuu kama vile Dar es Salaam, kijana anapoamua kujiajiri binafsi hupata matatizo makubwa kana kwamba ni mkimbizi, je, hii ni haki? Nani ni mmachinga, kijana hana uwezo wa kuwa na ofisi yake, ofisi yake ni mgongo wake akifanya jambo la kujiendeleza hufukuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kubinafsisha viwanda vyetu ndiyo sababu kubwa ya vijana wetu kukosa ajira. Kuna umuhimu wa Serikali kutoa tamko rasmi juu ya ajira za wageni ili watu wetu wapate nafasi za kazi, ni vema Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana iitake Wizara inayoruhusu kuingia kwa wageni na kufanya biashara ndogo ndogo hapa nchini kwani kitendo hicho kinawanyima ajira vijana wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo naitakia Wizara mafanikio mema.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, kwanza nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wa *NSSF* na *NIP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatueleza kuwa daraja la Kigamboni wahusika wakuu ni *NSSF* na wanaweza, lakini panaonekana pana mchezo mchafu unafanyika kwani hadi leo Shirika la *NSSF* wanaweza na tuwe na utamaduni kutumia mashirika yetu kwani *NSSF* wana kila sifa kuwa wanaweza kulisimamia daraja hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha Shirika letu kunyan'ganywa kiwanja kwa ajili ya kupewa wageni wakati *NIP* walishaanza kuwekeza na shirika hili ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Kuhusu shirika la Tija, Serikali itoe kauli kwa Wizara pamoja na Halmashauri zote wawapeleke maofisa na wafanyakazi wakawasomeshe. Shirika la Tija ukweli linastahili sifa kwa sababu Mkurugenzi amelikuta shirika wakati mgumu sana (karibu ya kufa) inafaa shirika hili liongezewe au kupatiwa ruzuku Serikalini ili lijiendeleze kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima iliangalie suala la wageni wanaotaka kuwekeza, mfano wa Wachina wa Kariakoo; ile kazi wanaofanya Watanzania wanaweza kuifanya. Naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE. Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza kuhusu suala la *BAVITA* na nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili naomba Waziri ashughulikie mwananchi huyu ambaye alikuwa mfanyakazi wa *TRC* nimeambatanisha barua yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja hii.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wake kwa umahiri wao katika kazi zao za kuendeleza kazi, ajira na maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu ajira ya vijana, kuna vijana wengi ambao wanajiajiri katika biashara zao lakini Halmashauri za miji zimekuwa kero kwa kuwapatia maeneo ambayo yapo mbali na makazi ya watu, kwani huwezi kufanya biashara ambayo hakuna wanunuzi. Tunaiomba Wizara hii iangalie suala hili kwa umakini makubwa.

Pia wale walio na ajira nao ni taabu tupu, mishahara yao ni taabu sana, kijana huyo karibu miezi minne hana au hajalipwa mshahara, ni vipi atapata maendeleo hata kama atalipwa basi atapewa pesa ya mwezi mmoja na mingine hajui atapewa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iliambie Bunge hili ni lini tabia ya mishahara ya wafanyakazi italipwa wakati husika hasa wale wa Serikalini ambao wanafanyakazi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna vijana ambao hufanyakazi na kuwa vibarua zaidi ya miaka miwili, hapa naomba maelezo kama ni halali au ni kuwachosha vijana wetu? Tabia hii hujitokeza katika viwanda vya watu binafsi na pia mishahara yao huwa duni sana, naiomba Serikali ifuatilie kwa karibu sana ili vijana wetu waweze kupata maendeleo na maisha bora kwa kila Mtanzania yaweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya makampuni huwafanyisha kazi wafanyakazi wao bila vifaa vya tahadhari, mfano makampuni ya kuzoa taka hawapewi *gloves* wala *gam-boot,* kitendo hiki Wizara haioni kama ni tatizo kubwa? Hivi *OSHA* hawaoni tatizo hili na kulichukulia hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji haukuwafikia watu wengi na pia tulipata taarifa hapa Bungeni toka kwa Mheshimiwa Grace Kiwelu, baada ya ziara zake kuwa uligawiwa kisiasa, sasa tunaiomba Serikali itufahamishe hiyo ni halali au si halali na kama hayo si maelekezo ya Wizara, ni hatua gani watachukuliwa watendaji hao ili suala hilo lisijirudie?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara iwe makini na iweze kufuatilia mikopo hiyo kwa karibu ili kuondoa manung'uniko kwa wananchi wetu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kutoa elimu kwa wananchi ili kujua juhudi za kujiajiri pamoja na *SACCOS* za kikundi nchini.

Pili, napenda kushukuru Wizara kwa kutupokea wakati tukija Wizarani kwao, Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ni miongoni mwa Wizara ambazo tukija kwa shughuli za wanachi tunapata mapokezi na kusaidiwa shida za wananchi. Naomba mzidi kuwa na moyo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo ya Wilaya za vijijini kama Longido elimu ya *SACCOS* ni ndogo sana kutokana na Afisa Ushirika kuwa na kazi ngumu kwani Wilaya ni kubwa na usafiri haipatikani kwa afisa huyu kwenda vijijini mpaka sasa Wilaya ya Longido hatukupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taasisi kama *NSSF* waende katika Wilaya za vijijini kujenga nyumba kwa ajili ya kuleta maendeleo huko kama wakijenga taasisi za kimaendeleo watapangisha. Nawaomba sana waje Longido.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kuongelea suala la shamba na kambi ya vijana Sasanda - Mbozi, mwaka 2006/2007 kwenye Bunge la Bajeti na kupitia Kipindi cha Maswali na Majibu hapa Bungeni niliwahi kuhoji juu ya eneo kubwa la ardhi linalomilikiwa na Wizara hii katika kambi la Sasanda lakini matumizi yake yakiwa madogo sana wakati wananchi wanaoishi jirani na kambi hiyo wakiwa hawana ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi la Sasanda ina ukubwa wa ekari zisizopungua 800 hivi. Niliwahi kuomba kupitia Bunge hili kwamba ingekuwa busara kama Wizara ingetoa eneo japo kidogo kwa wananchi wa vijiji vya Nyimbili, Hasamba na Masangula ambalo wanaishi pembezoni mwa kambi hiyo, hata hivyo majibu ya Serikali yalikuwa kwamba Wizara haitatoa sehemu ya shamba hilo kwa wananchi hao eti kwa sababu Wizara ilikuwa na mpango mahsusi wa kulitumia eneo hilo kikamilifu na kwamba mpango huo ungekuwepo kwenye Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa ni namna gani Wizara itatumia eneo lote, nimesoma hotuba ya Bajeti aidha, nimemsikiliza Waziri vizuri, hata hivyo sijaona mahali panapoonyesha mkakati wa matumizi ya eneo hilo. Nilichosoma na kusikiliza ni ukarabati wa nyumba na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kambi hiyo. Angalia

ukurasa wa 29(h), 30(e), 24(f) na *Youth Camp* iliyofanyika hapo Sasanda ukurasa wa 22(g).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hoja yangu ya matumizi ya eneo hilo kubwa ijibiwe kikamilifu na kigugumizi ni nini ambacho kinafanya Wizara isiache eneo walau kwa wananchi hao wenye shida kubwa ya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha naomba nijulishwe ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa maendeleo ya kambi ya Sasanda kwa mwaka 2007/2008 maana kwenye kitabu cha nne cha maendeleo ukurasa wa 99 - *Vote 65, Sub-vote 1003, Item 6380* nimeona zimetengwa shilingi 1,800,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa ofisi za kazi na kambi za vijana nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni mikopo ya wajasiriamali, bado upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wajasiriamali bado siyo mzuri hasa kwa wananchi wa vijijini na hasa wakulima. Utaratibu wa mikopo hiyo unamtaka mkopaji awe na uwezo wa kurejesha mkopo huo kila mwezi, je, mkulima ambaye huvuna mara moja kwa mwaka, atapata wapi uwezo wa kurejesha mkopo kila mwezi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali kupitia Wizara hii iweke utaratibu utakaomwezesha mkulima aweze kukopa na mashamba yake au ardhi yake ndiyo iwe dhamana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi nyingi zinazohusiana na kazi kati ya wafanyakazi na waajiri huwa zinachelewa sana kusikilizana na hasa zinapofika kwenye mabaraza ya kazi yaani *Conciliation Boards,* sababu za kuchelewa ni nyingi lakini kubwa zaidi inatokana na upungufu wa maafisa wa kazi *(labour officers)* kuwa wachache sana ukilinganisha na kesi zilizopo, sababu nyingine ni ofisi hizi kuwa mbali zaidi na walipo watumishi wengi. Ofisi nyingi zipo Makao Makuu ya Wilay, tatizo lingine ni rushwa na hicho ni kigezo cha kuchelewesha kesi lakini pia huwanyima haki watumishi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kushauri Wizara iajiri maafisa wengi wa kazi ili uendeshaji wa mashauri uharakishwe, pili, Wizara ijenge ofisi za kazi katika Wilaya zote ili kusogeza huduma hii karibu na watumishi na waajiri na tatu, Wizara iwabane maafisa wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya mbio za Mwenge ni nzuri sana, kwa sababu mwenge huchochea shughuli za maendeleo katika maeneo unapopita, hata hivyo miradi mingi inayozinduliwa huwa haiishi, nashauri kuwe na utaratibu wa kufuatilia ahadi zote na kuona kwamba zinakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linaloambatana na mbio za Mwenge ni maambukizi ya UKIMWI, naomba kujua hivi Wizara ina mkakati gani wa kupambana na maambukizi yanayosababishwa na kuwepo kwa mikesha ya mwenge?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa moyo wangu wa dhati kabisa kumshukuru Waziri kwa kuonesha kwenye hotuba yake ya Bajeti ukurasa wa 30(d), uwezekano wa kujenga ofisi yake ya kudumu Mjini Dodoma. Sikumbuki kama kuna Wizara imeonesha nia kama ilivyofanywa na Wizara hii nawapongeza sana. Hata hivyo naomba azma hiyo iwe ya kweli na isije ikabaki kwenye kitabu hiki cha Bajeti tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba maelezo ya kutosha kuhusu uendelezaji na matumizi ya mashamba/kambi la Sasanda kule Mbozi na mengine niliyoyaandika. Naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la ukiukwaji wa sheria inayolinda haki ya watumishi kazini ambapo maamuzi mengi ya Waziri kuhusu rufaa za watumishi hayazingatiwi na waajiri na katika maeneo mengine, maamuzi ya Waziri yanapuuzwa. Ipo mifano mingi hai ambapo watumishi wamerudishwa kazini na Waziri baada ya kufikisha mashauri yao kwake na kuamua warudishwe kazini, taasisi zimedharau uamuzi wa Waziri na kutupilia mbali maamuzi ya Waziri ambayo ni ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watumishi wengi wa Hifadhi za Taifa ambao wamekumbwa na tatizo hili je, tatizo ni nini? Je, sheria inampa mamlaka Waziri kumrejesha kazini mtumishi ambaye amefukuzwa kazi baada ya kuridhika na ushahidi ina mapungufu? Kama yapo Serikali ina mkakati gani wa kuyaondoa mapungufu hayo? Hali ilivyo sasa ni ya kukatisha tamaa kwa watumishi wengi ambao sheria imewatendea haki lakini wachache wanaendelea kuikalia haki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tatizo la watumishi wengi wa *TANAPA* ambao wamerudishwa kazini na menejimenti kukataa kutii maamuzi ya Waziri lishughulikiwe ili haki itendeke na kuwaondolea watumishi hawa matatizo na taabu inayoendelea kuwapata watumishi hawa.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia tena kwa maandishi hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na wataalamu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira mbaya kwa watoto, tatizo hili limekuwa sugu sana ni vema Serikali ikaongeza sheria kali kwa wote ambao hadi sasa bado wanatumikisha watoto kazi ambazo ni ngumu na za kudhalilisha mfano ni watoto kugonga mawe ili zipatikane kokoto, kazi za mashambani na wengine kuanzisha madanguro ambayo vijana wadogo hufanyishwa kazi ya ngono na kadhalika. Hii ni aibu kubwa kwa jamii na Serikali na hasa ikizingatia ugonjwa wa UKIMWI na kukoseshwa kuendelea na masomo, sheria zirekebishwe kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa vijana uangaliwe zaidi katika kuwapangia mipango imara ya ajira ya vijana kuanzia Wilayani kwa kuwapa semina na mafunzo ili wajitegemee kiuchumi na kupunguza wimbi la ongezeko la vijana kuingia

katika Jiji la Dar es Salaam kwa wingi na pia vivutio vya kutoa mikopo ambayo wataimudu katika kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naupongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kijamii chombo hiki kiangaliwe jinsi ya kuongeza ujenzi wa nyumba za bei nafuu pamoja na jitihada zinazoendelea kwa sasa, ujenzi wa nyumba hizo bado mahitaji ya nyumba hizi ni kubwa na ndiyo njia pekee ya kuwaondolea adha ya makazi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za kulevya ni janga kubwa hapa nchini pamoja na baadhi ya Wilaya zimeaanza kuwakusanya vijana walioathirika na dawa za kulevya na kuwapa ushauri nasaha pamoja na tiba. Nashauri kwamba ni vema sasa likatolewa somo la athari ya dawa ya kulevya mashuleni ili somo hili lijenge kwenye akili za watoto kujua hili jambo zuri kwa binadamu na kuliokoa Taifa kupoteza nguvu kazi ya wanachi wake.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri, ili kuongeza ajira nashauri yafuatayo yafanyike, kwanza kuimarisha suala la ajira kwa vijana budi liwe mtambuka, pili, kwa mfano madini, Wizara ya Nishati na Madini itoe maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa mfano eneo la Matabe wachimbaji wadogo wapewe eneo hilo, walishapeleka maombi yao ila Wizara ya Maliasili na Utalii inawakwamisha, Waziri anayo taarifa, eneo linaajiri watu wengi na wanaiingizia Serikali kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii iingilie kati kuwasidia vijana wachimbaji kwa nini Wizara ya Maliasili na Utalii haitaki kuwaruhusu wachimbaji wa Matabe ambao wameomba kiuungwana na kuendelea kusubiri muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaweza kuongeza ajira kama itakuwa na mikakati mizuri ya kusaidia vijana wakulima. Kwa mfano wakulima wa matunda wa Geita, Lushoto na Tabora, Morogoro na Ukerewe, wakasaidiwa kupata mwekezaji anayeweza kusindika matunda yao ili waweze kufanya kazi zaidi ya uzalishaji na kuingiza pesa za kigeni?

Mheshiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni jukumu lao pia kuliona hili, Geita tunahitaji kiwanda cha matunda ili vijana waweze kujiajiri. Nina imani itawawezesha kufanya biashara ya uhakika. Naomba vijana wanaojiajiri kwa kutumia pikipiki na baiskeli waruhusiwe mara moja kwani hata polisi wanaowazuia, wanawafukuza wakiwa wamebebana kwenye pikipiki wakati sheria haibagui kuwa mwendesha pikipiki awe askari tu. Suala la baiskeli na pikipiki ni sawa na mtu anayekunywa gongo kumfukuza mpika gongo? Naomba waendesha baiskeli na pikipiki wasibughudhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi naomba yafuatayo, kila Wizara ioneshe inalichukuliaje suala la ajira na vijana ni suala la mtambuka, isiachiwe Wizara moja tu. Pia kuwekwe utaratibu kwa vijana waendesha pikipiki na baiskeli waruhusiwe haraka

kufanya biashara hiyo. Kuweka kiwanda cha kusindika mazao ya matunda badala ya kunywa *(juice)* kutoka Kenya na Uganda au Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wachimbaji wa Matabe, Biharamulo na maeneo mengine kupewa maeneo ya kuchimba, Waziri wa Nishati na Madini analifahamu hili na ambaye analo sasa ni Waziri wa Maliasili na Utalii, maombi yao ni ya muda mrefu.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi kama wakulima, waajiriwa na wafanyabiashara, pia kuna kundi ambalo halifanyi kazi kabisa licha ya kuwa na nguvu na umri wa zaidi ya miaka 18. Katika kundi la waajiriwa hasa wa Serikali kuna kundi ambalo halifanyi kazi lakini wapo kama picha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu ambao wakienda kazini ni gharama kuliko angebaki nyumbani. Mfano ofisa anayetumia gari ya Serikali na dereva anaenda ofisini kuwasha taa na kiyoyozi lakini anabakia kusoma magazeti, mtu huyo gharama yake ni kubwa bora angebaki nyumbani, watu hao wapo naomba Wizara iwathibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanapaswa kujipima kwa kiwango cha utoaji tija. Kila mtu aelewe anapaswa kufanya kazi kwa saa ngapi na ni kweli anatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, daktari anapochelewa kwenye foleni na siku hiyo alikuwa na wagonjwa watatu wa kuwafanyia upasuaji na kuwafanyia wawili tu ni hatari kwa wagonjwa. Huu ni mfano tu wa kuonyesha jinsi wakati wa kazi unavyopotea na athari zake. Naomba tutafute jawabu lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri ashughulikie suala la vijana wapanda Mlima Kilimanjaro kwa kasi kama alivyoahidi hapa Bungeni. Hii ni ajira nzuri inayopaswa kusimamiwa ili vijana hawa wapate malipo kwa nguvu zao wanazotumia. Suala hili ni nyeti naomba ufumbuzi na Serikali itambue kuwa vijana hawa wako makundi mawili. Kundi la kwanza ni la waongoza watalii na wapishi. Kundi la pili ni la wabeba mizigo yaani (*portes*) naomba uwekwe utaratibu wa ni nani aratibu shughuli zao.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri na pia naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa fedha zilizotengwa na Serikali shilingi bilioni 21 kwa ajili ya mikopo kwa wajasiriamali, shilingi bilioni moja kila mkoa imesaidia sana mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali ambao wameanzisha miradi midogo midogo ya kujipatia kipato na kuboresha maisha yao. Kwa kuwa fedha hizo zilipelekwa kwenye mabenki ya *CRDB* na *NMB* ambako masharti ya benki ni nguvu ya kupata mikopo hiyo. Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa mwaka 2007/2008 kwa ajili ya mikopo kwa wajasiriamali na kwa kuwa wilaya ya Mpwapwa imeanzisha *SACCOS* kila Kata zikiwemo Kata za Vinghawe, Mpwapwa Mjini, Matomondo, Pwaga, Kibakwe, je, Serikali itakubaliana

nami kwamba fedha hizo za mikopo zipitishwe kwenye *SACCOS* badala ya mabenki ili wajasiriamali wengi wapate mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, wajasiriamali waliokopa ni wangapi na fedha kiasi gani na marejesho ni asilimia ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri ya kutayarisha Bajeti hii. Baada ya pongezi hizo napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema ifahamike wazi kwamba ongezeko la ajira lina uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa uchumi wetu na ongezeko la shughuli nyingi katika sekta mbalimbali za uchumi. Kwa hiyo, katika kulishughulikia tatizo la upungufu/ongezeko la ajira nchini ni lazima Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ishirikiane kwa karibu sana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ili kubaini maeneo ya uchumi wetu yanayoweza kuwa ndiyo chimbuko la ajira nyingi hapa nchini.

Aidha, katika eneo la ajira za kujiajiri, Wizara haina budi kutafakari umuhimu wa kuhimiza elimu ya ufundi wa stadi mbalimbali kwa vijana wetu *VETA* na hatimaye kuwa na utaratibu wa kuwawezesha wahitimu kuanzisha miradi yao. Kwa bahati mbaya hata utaratibu wa mikopo ya shilingi bilioni moja inaelekea haujatoa matunda mazuri yaliyokusudiwa na Serikali. Kuna haja ya kuendelea na utaratibu huu lakini baada ya tathmini ya kina ya utekelezaji ya mpango wa shilingi bilioni moja kila mkoa. Katika kuwasaidia vijana wetu (wanawake na wanaume) kuna haja kwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kujifunza utaratibu wa *Grameen Bank* ya *Bangladesh* na kuona jinsi uzoefu wake unavyoweza kutumika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa sheria moja ya hifadhi ya jamii hapa nchini ni moja ya vikwazo vikubwa vinavyoathiri uendeshaji wa mifuko ya jamii kwani kumekuwepo na ushindani usiyozingatia ustaarabu na hasa kwa vile hakuna msimamizi *(referee)* anayeweza kukemea ushindani usio wa haki. Nina ihimiza Serikali (Wizara) iharakishe ukamilishaji wa sheria mama ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa mradi wa daraja la Kigamboni na Shirika la *NSSF* baada ya matayarisho ya muda mrefu na kupata msaada wa fedha toka Serikali ya Uholanzi. Serikali itoe uamuzi wake haraka ili daraja lijengwe kwa manufaa ya maendeleo ya eneo la Kigamboni kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Nashauri Wizara ifanye utafiti ni kwa nini vijana hukimbilia mijini hususani Dar es Salaam kutoka vijijini vijana hawa huingia Dar es Salaam karibu kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mategemeo ya kila Taifa ni vijana ambao wana afya ya kutosha katika kuzalisha mali, vijana hawa kama wangefanya kazi ya uzalishaji mali mashambani, viwandani na kadhalika tungepiga hatua kubwa katika kuinua uchumi wetu, hali hii ikiendelea itakua ni tatizo kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie wafanyakazi viwandani ambao siku za hivi karibuni wamekuwa wakiathirika kiafya, wengi wamekuwa wakipoteza fahamu na kulazwa hospitali. Wafanyakazi wa Kiwanda cha Korosho Mtwara wanaathirika kwa mafuta ya korosho na Moshi, kiwango cha ujira wanaopata pia haukidhi haja. Naomba Waziri au mwakilishi wake awatembelee wafanyakazi hawa kiwandani na kuona hali zao, nashauri pia kuongea na waajiri ili wawahurumie wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *NSSF* ilipewa jukumu la kujenga Daraja la Kigamboni lakini hadi leo hakuna kinachoendelea licha ya Serikali kutoa kauli Bungeni mwaka jana kuwa daraja litajengwa suala hili ni kero kubwa kwa wakazi wa Kigamboni na Watanzania wote, hakuna sababu zozote za msingi zinazotolewa. Ningependa kujua gharama halisi ya ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ni kwa nini Hazina huwa na tabia ya kukwamisha maagizo yanayotolewa Bungeni kuhusu ujenzi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawapongeza *NSSF* kwa michango yao katika miradi ya ujenzi hasa Chuo Kikuu cha Dodoma.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuandaa Bajeti hii pamoja na kusimamia Wizara nyeti inayotazamwa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi naomba Serikali itakapoanza kutoa fedha za wajasiriamali (mabilioni ya Kikwete) naomba Serikali ipeleke kwenye *SACCOS* ya Ushirombo kwani Bukombe hatuna benki, Wilaya ina ukubwa wa kilomita za mraba zaidi 10,000. Kwa hali hiyo wananchi wanapata shida ya kusafiri kwenda na kurudi Kahama pengine wasipate mafanikio. Naiomba Serikali iwahakikishie wananchi wa Bukombe kama huduma hizi watapata kupitia *Ushirombo Saccos Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ihamasishe taasisi za fedha zikubali kuwakopesha wananchi wasiokopesheka kwa kukosa dhamana mfano wakulima, wafugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Bukombe tumebakiza mwezi mmoja kilimo kianze, ni vema *SACCOS* zilizopo za wakulima, *NMB*, *CRDB* au sehemu zingine washauriwe na wawapatie mikopo iwasaidie katika kilimo kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri kama *SELF, PRIDE, SCCULT* wasogeze huduma au wakubali kuanzisha huduma zao Mkoa wa Shinyanga hasa Bukombe ili waweze kusaidia utoaji mikopo kwa wajasiriamali na kuongeza ajira. Utaratibu wa fedha za uwezeshaji zitolewe kwa uwiano mzuri kila kata kwani pasipo kufanya uwiano huo suala hili litabadilika kuwa la kisiasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongezaa kwa mipango mizuri iliyoainishwa kwenye hotuba hii na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu asilimia mia moja. Pili, niwapongeze Mawaziri wote na wataalamu waliomo kwenye Wizara hii. Kwa kutambua dhima na azma waliyokabidhiwa na Taifa hili wao kwa kweli ndio majemedari ambao wanaweza kulizamisha Taifa au kulivusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kwa sababu kundi la umma wa Tanzania (vijana) viongozi wa kesho wamekabidhiwa wao, kama hilo halitoshi basi tumewakabidhi ufunguo wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za dhati zinatakiwa na zaidi nizielekeze kwa Mungu muumba ili alisaidie Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ni uhai, kazi ni maisha ya kila mmoja wetu, kazi ni utulivu. Tunaiomba Serikali na Wizara hii iendelee kuboresha mazingira ya kila mmoja awe ameajiriwa au amejiajiri tunaelewa fika kuwa Serikali haiwezi kuajiri watu wote lakini watu wote wanahitaji kufanya kazi, kwa hiyo, wajiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara hii mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ajira, kilimo, uvuvi,ufugaji hizi ni sekta pekee ambazo zina uwezo wa kutusaidia. Kinachotakiwa ni kupangwa mbinu muafaka wa kukusanya vijana katika makundi chini ya uongozi wa mmoja wao na kwa maana ya utaalamu na inafunza watakapoelimika wapewe mtaji na kutekeleza shughuli zao. Hii kwa upande mmoja itasaidia kuleta ajira, itapunguza uzururaji na itaondoa kabisa unyonge unaowaandama. Tatizo la kitaalamu zitumike au kwa lugha nyingine tuwatumie wanataaluma vyuoni mwetu tuone wangetushauri na kutupangia vipi. Kwa kuanza tungeanzisha maeneo maalumu *(Pilot Areas)* katika nchi na baada ya kuonekana ufanisi wake tukasambaza nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sasa umefika wakati Serikali ikajipanga kutoa taaluma shule za kilimo, ufugaji na uvuvi kuanzia shule za msingi ili kuwaandaa vijana kujua nini la kufanya baada ya kumaliza shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, vyuo vya *VETA* viongezwe nchini ili vijana wapate taaluma mbalimbali za ufundi na kama hilo litafanyiwa kazi itasaidia sana kila kijana atakapotoka chuoni kujua atakachofanya hasa ukizingatia dunia sasa inakoelekea. Pia Serikali kwa makusudi iwe na Bajeti ya kila anaemaliza chuo cha *VETA* wapatiwe mtaji wa fedha au vifaa ili wajue pa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuweka mpango thabiti wa kuwasaidia vijana wanapotoka shuleni moja kwa moja na kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, napenda kuwapongeza vijana wote ambao wanajituma katika kujiajiri wao wenyewe, kama tujuavyo vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa, bila vijana kuwa na ajira mambo kadhaa yanaweza kujitokeza ikiwemo wizi, ujambazi, uvutaji bangi na ulaji wa unga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa ajira ndiyo kichocheo kikubwa cha maasi kwa vijana wetu. Vijana wanajitahidi kufanya biashara zao katika maeneo mbalimbali wanamoishi, tatizo linalojitokeza ni vijana hao kuhamishwa mara kwa mara katika maeneo wanayofanyia biashara zao na wahusika kushindwa kuwapatia vijana hao sehemu mbadala ya kufanyia biashara zao. Kwa kuwa Serikali ina mikakati ya kuwajengea wamachinga Jijini Da es Salaam, naiomba Serikali ihakikishe jengo hilo litakapomalizika litumiwe na walengwa, isiwe bado vijana wanahangaika jengo hilo likawa linatumiwa na wafanyabiashara wachache kwa manufaa yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwajengea wamachinga jengo kwa biashara zao ni mzuri, naiomba Serikali ihamasishe Halmashauri mbalimbali kutenga sehemu kwa ajili ya kuwajengea vijana sehemu za kufanyia biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo ya vijana inayotolewa na Halmashauri, ziko baadhi ya Halmashauri ambazo haziwahamasishi vijana kukopa pia taarifa hizo za mikopo kupitia kwao na kama zinatolewa pia utoaji wake ni wa kimatabaka, walengwa sio wanaopewa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Tanga lina viwanda kadhaa ambavyo vimefungwa, mfano kiwanda cha chuma, kiwanda cha mbolea, kiwanda cha *plastic* cha Amboni na vingine vingi. Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuvifungua viwanda vilivyokufa ili kuwezesha kuongeza ajira kwa vijana na kupunguza wimbi la wizi, ujambazi, ulaji unga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana walioajiriwa katika uzoaji taka ngumu, vijana hawa wanatumia mikono yao bila ya *gloves*, hawana *masks* za kuziba pua na mdomo, hawana *gum boots*, mwisho wa siku mwajiri anapata pesa kutokana na kazi

walizofanya vijana hao, lakini vijana hao wanaambulia kupata magonjwa hasa ya kuambukiza kutokana na kufanya kazi bila kutumia vifaa vya kinga.

Kuhusu vijana wanokaa vijiweni sio kuwa hawakusoma ila hawana sehemu ya kuajiriwa, naiomba Serikali iaendae utaratibu utakaowawezesha vijana kupatiwa mafunzo mbalimbali wakikusanya kutoka katika hivyo vijiwe vyao na baada ya kupata mafunzo hayo wajengewe uwezo utakaowawezesha kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji la Tanga kuna viwanda vya watu binafsi, kuna vijana ambao wanafanyakazi viwandani humo kwa muda mrefu kama vibarua bila kuajiriwa rasmi na malipo yao kwa kweli yanasikitisha kulingana na uzalishaji mali wanaofanya katika viwanda hivyo. Wamiliki wa viwanda hivyo hawawajali hao wafanyakazi kwa kuwapa huduma kama vile anapoumia akiwa kazini hana anachokipata kwa vile anahesabika kuwa yeye ni kibarua, je kuna sheria gani ya muda wa mfanyakazi kutumika kama kibarua?

Je, kibarua huyo anayefanya kazi kwa muda wa miaka mitatu hadi minne ni kibarua wa vipi? Serikali haioni kuwa inamkosesha haki zake za msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iandae waraka kwa wenye viwanda binafsi taratibu za ajira kwa wafanyakazi wake badala ya kumtumikisha mtu kama kibarua kwa muda mrefu bila kuajiriwa na kumkosesha hali zake za msingi.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara hii kwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Asilimia kubwa ya nguvu kazi katika nchi yetu ni vijana. Vijana walio wengi wanatafsiri ajira kama ni kuajiriwa kwa mshahara. Suala la kujiajiri kwa vijana walio wengi halionekani kuwa ni ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara iwaelimishe vijana wengi hasa wanaokimbilia mijini kuwa kuna fursa nyingi za kujiajiri hasa kwa shughuli za kilimo, kwa mfano wale vijana wanaopambana na askari wa miji wafanyiwe mipango katika maeneo yenye ardhi nzuri *(green belt)* za miji wanakozuiwa kufanya biashara ya kutembeza ili wapate ardhi na kuanza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuanzia wanaweza kuwasaidia kwa kuwalimia kwa mwaka wa kwanza kama ilivyokuwa katika mpango wa *village settlements* mara baada ya Uhuru. Pamoja na hamasa kubwa tulivyoitoa mwaka jana kuhusu mfuko wa uwekezaji, kuanzishwa kwa *SACCOS* vijana wengi hawakupata fursa hii kutokana na benki nyingi kuwepo mijini tu. Benki kama ya *NMB* haipokei maombi yaliyopo umbali wa zaidi ya kilometa 25 kutoka mahali benki zilipo, hali hii imewanyima vijana wengi fursa ya kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba zifanyike jitihada za makusudi kukopesha *SACCOS* zilizo kwenye maeneo ya vijiji ili nao waweze kuwakopesha wajasiriamali waliopo huko vijijini kwa masharti nafuu. Aidha, awamu ya pili ya mfuko wa shilingi bilioni 10.5 uelekezwe kwenye *SACCOS* kuliko Benki za *CRDB* na *NMB*.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakupongeza wewe na Spika kwa kuongoza Bunge vema, pia nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana bado ni vijana wetu na ndiyo viongozi wa kesho hivyo Serikali inahitaji kuwalea ili kwa tegemeo la kesho kwa Taifa letu kwani vijana ndiyo baba wa maasi, wapate kuepuka wizi, dawa za kulevya, biashara haramu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie Bajeti hii kwa kutoa elimu zaidi kwa vijana ili Tanzania tuwe na wataalamu wazuri. Watu wengi wanalalamika kutokutendewa haki kazini na madai ya fedha husumbuka na kupata taabu hadi kufikia hatua ya kushindwa kupata mafao yao au hali zao, naomba Serikali kupitia Wizara hasa kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwenda na awamu ya nne na kujali na kunadi utekelezwaji wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wageni wanaofanya kazi mahotelini liangaliwe kwa makini kwani Watanzania wengi hawana kazi, hivyo nafasi hizo wapewe vijana wetu wa Tanzania. Nchi za jirani kama Kenya, Uganda na kadhalika ndio wanaojifanya wenyeji mahotelini na sehemu zingine, naiomba Serikali ishughulikie jambo hili kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Magogoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali naomba kutoa pongeza za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa bidii, upendo na ushirikiano miongoni mwao. Pia nawapongeza kwa Bajeti nzuri ambayo Waziri ameiwasilisha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, zipo changamoto ambazo naomba Serikali iziangalie ili kuondoa kero kwa wananchi. Kwanza usimamiaji wa mafanikio tarajiwa kutokana na fedha za uwezeshaji wajasiriamali naiomba Serikali, moja, iangalie upya viwango vya riba ili mkopaji wa mwisho asilipe zaidi au tofauti baina ya mkopo kupitia *NMB* na *SACCOS*/*CRDB*. Kwa muundo wa sasa mkopaji kupitia *NMB* anatozwa 10% kama riba wakati mkopaji toka *CRDB*/*SACCOS* anatozwa 12%, hili lirekebishwe.

Pili mikopo kupitia *NMB* iwafikie wananchi vijijini katika Wilaya ya Kahama kwa mfano, yenye majimbo mawili, mikopo imetolewa kwa wajasiriamali wa Mjini Kahama, wale wa vijijini katika Jimbo la Msalala hawakupata kitu. Wajasiriamali waliokopeshwa wengi wao wana miradi mipya na hawana taaluma ya elimu ya biashara na uhasibu, hivyo ni vizuri Serikali ikaweka utaratibu wa kutoa mafunzo kabla ya mikopo kutolewa bila hivyo kutakuwa na *default* kubwa sana na hili litaonekana baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali iangalie upya mikakati yake kukabiliana na wimbi la vijana wasiopenda kazi na kukaa vijiweni, naomba vijiwe hivyo vivunjwe. Katika mazingira ya sasa si sahihi kuwa na wimbi la vijana wasio na kazi na hivyo kutolipa kodi, hili linafanya wigo wa kodi uzidi kuwa mdogo na hivyo kusababisha mzigo wa kodi bora, ikibidi kodi ya kichwa irudishwe ili kila Mtanzania alipie huduma kama afya, elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utandawazi, naomba Serikali idhibiti vibali vya kazi kwa wageni hasa katika sekta ya madini na hotelini. Serikali isimamie sheria ya uwekezaji inayomruhusu kila mtu kuja na wafanyakazi watano tu. Kwa sasa *Bulyanhulu Gold Mining* ina *expertriates* zaidi ya 150 wakati *Resolute* (mgodi wa Nzega) una *expertriates* zaidi ya 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali izingatie ushauri wangu. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa pongezi nyingi kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii, Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kama *NSSF* yanafanya kazi nzuri sana. Mimi nathamini sana michango ya shirika hili katika kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu hii ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyuo, nyumba za polisi kwa bei nafuu na ukusanyaji wa michango unafanywa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana pamoja na kazi nzuri inayofanya lakini bado haionekani kufanya usimamizi unaofaa kwa ajira binafsi, bado waajiri wengi binafsi hawaongezi mishahara na posho hata pale nyongeza ya mishahara inapotangazwa na Serikali Kuu. Viwango vya mishahara bado ni vidogo sana katika ajira binafsi ilihali uzito wa kazi ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii iunde au iboreshe kitengo cha usimamizi wa malipo ya waajiriwa binafsi.

**MHE. DR.WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Serikali imetangaza nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa Serikali, na kwa kuwa watumishi walioko katika sekta binafsi mathalani hoteli, baa, mashamba makubwa na makampuni binafsi hadi sasa hakuna mwongozo au maelekezo yanayoeleweka toka Serikalini; na kwa kuwa watumishi hao wanapata mishahara kati ya shilingi 35,000/= hadi shilingi 54,000/=kwa mwezi; na ikizingatiwa kuwa watumishi wa Serikali wananunua masoko hayo hayo, watoto wao wanaenda shule hizo hizo, je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu uduni huu wa maslahi unaowafanya Watanzania hawa wajione wametelekezwa na Serikali yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anaweza kutamka sasa angalau asilimia ya ongezeko la nyongeza na kima cha chini ambayo lazima ifuatwe na waajiri hawa ili Watanzania hawa waishi nao kama binadamu?

Pia Kamati inayohusika kupanga mishahara kwa kada hii imetoa taarifa gani na kama imetoa taarifa hiyo itatolewa lini hadharani kwa waajiri wasiofuata maelekezo ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nafasi ya kwanza ya ajira katika nchi yoyote ni kwa raia wake na kwa vile Tanzania hatuna vitambulisho vya uraia na kwa vile taarifa ziko sehemu mbalimbali ya nchi hii kuwa wawekezaji na waajiri binafsi na sheria zetu je, Serikali itafanya sasa kampeni ya makusudi kubaini watu/ wageni hao waliotapakaa nchi nzima na wanaofanya kazi ambazo Watanzania wengi wana sifa kuzifanya na hivyo kuwanyima Watanzania hao haki yao ya kazi katika nchi yao wenyewe? Waziri anaweza kutoa ratiba kamili ya kmpeni hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, utaratibu wa zamani wa kuwa na wakaguzi wa makampuni umeishia wapi? Kwa nini utaratibu huo mzuri usirejeshwe na wakaguzi wakapewa majukumu mahsusi kukagua kama waajiri wote wanasifa zote zinazotakiwa kisheria hasa idara ya raia inayoruhusiwa kwa kila kampuni ya wawekezaji.

Kwa kuwa kuna ushahidi kuwa mikopo ya vijana inatolewa kwa misingi ya kisiasa na Waziri alikiri kuwepo kwa hali hiyo kama alivyonukuliwa katika maelezo yake kwa Kamati ya *LAAC,* je, anatoa kauli gani ili kuondoa ubaguzi huo wa wazi katika kugawa rasilimali chache za nchi hii ambayo sote kwa viwango vyetu tumechangia lakini inapofika kugawana inatolewa kwa misingi ya kisiasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Mwenge wa Uhuru ni mmoja kati ya mambo yanayounganisha Watanzania na kuwa wananchi wananyanyaswa sana wakati wa kukusanya michango ya mwenge ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa vyungu vyao, vitanda na vifaa vingine vya nyumbani, jambo ambalo ni kinyume na malengo ya mwenge, je, Serikali inatoa kauli gani kupiga marufuku utaratibu huu wa manyanyaso na udhalilishwaji? Mwenge ni wa hiari ni kwa nini watu wasio na uwezo wasisamehewe badala yake wanaburuzwa? Gharama za kukimbiza Mwenge ziko kwenye Bajeti ya Wizara, je, mwaka huu kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Mwenge?

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba na kwa niaba yangu binafsi, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na wataalamu wote wa Wizara hii. Ni hotuba nzuri kwanza kwa kuzungumzia maeneo mengi ya msingi na inaleta matumaini. Naunga hoja hii mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi nina mchango wangu katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilipongeze Shirika la Hifadhi ya Jamii kwa ubunifu wake mbalimbali wa kuibua na kushiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa na *possibilities* mbalimbali zitolewazo na Mfuko wa Hifadhi hii. Hii ni pamoja na mpango maalumu kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la *OSHA* liongezewe uwezo wa kifedha na utaalamu ili liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* ifanye (ifunge) mikataba na Halmashauri za Wilaya katika mpango maalumu wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya kama zile za Kinyerezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na mpango thabiti na wa dhahiri kwa vijana kuwaelimisha kuwa ajira hutafutwa kwanza kwa kufikia vigezo fulani fulani kwa kila ajira. Ajira haipatikani barabarani na kijiweni kwa kupiga soga. Wajipange vyema sana ili wafikie viwango vya kustahili ajira. Kulalamika pekeyake hakutawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgogoro wa kiwanja cha Shirika la Tija la Taifa lipewe uzito unaostahili kwa kulitolea maelezo ya wazi kuhusiana na kunyang'anywa kwa kiwanja hicho na fidia ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ya wajasiriamali ipitishwe kwenye *SACCOS* badala ya kupitishiwa kwenye mabenki. Hii itakuwa na manufaa zaidi kwa wananchi kuliko mpango wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uzima nikaweza kuwepo hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kutoa rambirambi zangu za pekee kwa familia za Marehemu wote waliofariki katika kipindi chote hiki kuanzia Januari hadi sasa. Rambirambi zangu za pekee kwa aliyekuwa Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Juma Akukweti pamoja na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Vijana Taifa, Mheshimiwa Amina Chifupa, Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba yao nzuri ambayo wameiwasilisha hapa Bungeni leo. Zaidi sana kwa wataalamu wa Wizara kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao kwa kuzingatia falsafa ya ari mpya kasi mpya na nguvu mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 iliahidi kutengeneza ajira milioni moja kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Ilani hii ilitambua kwamba sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania ni vijana. Katika kundi hilo ndiyo wanaoathirika zaidi kwa kukosa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira mazuri yanayoweza kukuza ajira katika makundi mbalimbali yanayoathirika ikiwa ni pamoja na vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Serikali ikaweka mikakati madhubuti na kuhusisha wadau mbalimbali ili kuweza kupunguza tatizo la ajira katika nchi yetu. Ili mikakati hii iweze kufanikiwa Serikali ianzishe vituo vya ajira katika kila mkoa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ulioanzishwa na Serikali kwa kutenga shilingi bilioni moja kwa kila mkoa kama njia mojawapo ya kuwawezesha wananchi wenye vipato vya chini. Vile vile elimu ya ujasiriamali itolewe sanjari na kuhamasisha wananchi hususan walioko vijijini ili waweze kuchukua mikopo na kuirejesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali ione uwezekano wa kulinda ajira za vijana wetu kuliko kuachia zinachukuliwa na wageni. Kwa mfano, ukitembea maeneo ya Kariakoo utakuta Wachina wamefungua vibanda vya saloni, vibanda vya kuuzia urembo, hii ni aibu. Wageni tuwape madini wachimbe hata na saloni. Bado tutawaingiza sokoni waanze kuuza mboga na matunda, hivi tunakwenda wapi, hivi hatuwezi kufanya chochote bila kumhusisha mgeni? Hivi ni kwa nini hatujiamini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama kazini viwandani na mashambani, nimetembelea viwanda mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa kukamilisha taratibu zote ili sasa *NSSF* iweze kukabidhiwa majukumu ya kuanzisha ujenzi wa daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri binafsi, Naibu Mawaziri wake, pamoja na watendaji wake kwa hotuba yake nzuri yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami bila kusita naunga hoja mkono kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie kwa uchache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wafanyakazi waliokuwa wa kiwanda cha *MUTEX* Mheshimiwa Waziri analifahamu vizuri, binafsi nimefika ofisini kwake na wawakilishi wa wafanyakazi hao. Alinipokea vizuri na kukubali kulishughulikia ili wapate mafao yao haraka iwezekananvyo maana suala lina zaidi ya miaka kumi hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa afafanue suala la hao waliokuwa watumishi wa *MUTEX* ili wajue mchakato mzima wa suala lao umefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wengi viwandani wanachukua zaidi ya miaka mitatu wakiwa kazini pasipo kupata ajira za kudumu na siku zote wanaitwa vibarua. Ningependa kufahamu tatizo hili litaisha lini maana ninaamini Wizara yako inalitambua hili tatizo la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingi hapa nchini vinawalipa vijana wetu malipo ya chini sana ambayo hata hayakidhi mahitaji. Napenda kufahamu ni lini Serikali itaweka kima cha chini kwa watumishi wa sekta binafsi ili wapate malipo yanayolingana na kazi, ikiwa ni pamoja na marupurupu mengine anayostahili kama mtumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi wa hayo machache na pia naomba kuunga hoja mkono. Ahsante.

**MHE. MUSTAPHA H. MKULO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ilonga, Wilayani Kilosa kuna Chuo cha Vijana, kama Mbunge sina hakika kama Chuo hiki kinatumika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa wataalamu wa Wizara kwa wakati muafaka wanielimishe kazi za chuo hiki ili nijue kama naweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye Wizara hii na nipatiwe majibu ya kuweza kunisaidia na wananchi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini mkoani Kagera tutakuwa na ofisi ya ajira? Mikoa mingine kama Mwanza ipo, naomba kujua wanaopewa mikataba au wawekezaji kwenye shughuli mbalimbali za mikoani, ujenzi wa barabara, viwanda mbalimbali na kadhalika tunafaidika nao vipi, kwa sababu watumishi wengi watakuja, nao je, sisi tunafaidika vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wamachinga, vijana wetu wanafukuzwa lakini Wachina wenyewe wanaendelea kuuza au kutembeza vyombo, kweli hii ni haki. Vijana walijianzishia ajira yao Bukoba za pikipiki na baiskeli wakawa wana ajira nzuri. Baadae polisi wakawakamata, siku zote wakati wanaanza hiyo sheria ilikuwa haipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa vijana hao wamekuwa wezi kwenye mji wa Bukoba. Mambo ya wizi tulikuwa tumesahau, leo hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi vijana wengi walijiua na uvuvi wa samaki hata wenyewe wanakamatwa kwa ajili ya zana haramu na hizo zana haramu zinatoka wapi, naomba kujua? Kwa nini Serikali isidhibiti hizo zana haramu pamoja na kiwanda kinachotengeneza zana hizo? Ili badala yake kiwanda hicho kikatengeneza

zinazokubalika kuliko vijana wetu kuwaweka hatiani huku makosa yakiwa ni Serikali kutowajali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hawa Wachina wanaotengeneza barabara, kunyanyasa wafanyakazi, ni kwa nini sisi Watanzania tunaona wananyanyaswa na sisi tunaona? Naomba masuala haya niliyo uliza nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii itembelee Mtwara kwenye Kiwanda cha Korosho, ione watu wanavyonyanyasika, Wahindi wanatudhalilisha. Naomba ufike ukaone kiwanda cha Sukari Kagera, vijana wengi hawajalipwa pesa zao, nilileta malalamiko yao kwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Magembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipewe majibu na nitashukuru nikipewa majibu mazuri.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa maelezo bayana juu ya mikakati ya Wizara kuhusu kuibua na kuwaendeleza vijana katika maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana litaendelea kwa kasi kubwa mwaka hadi mwaka, kama Serikali haitachukua hatua za makusudi kupeleka wataalamu wa kubuni ajira vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni muhimu kwa sababu vijana wengi sana wanamaliza elimu ya shule za msingi wakiwa na umri mdogo, kwa hiyo hawana mawazo komavu ya kutambua fursa za kazi za ujasiriamali zilizopo katika mazingira wanamoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na binadamu kuyazoea mno maeneo anakoishi, mara nyingi ni vigumu kutambua kwa urahisi mambo yote yanayomzunguka. Kwa maana hii, ni vigumu kwa vijana na wananchi wasio na ajira vijijini kuona au kutambua *self employment opportunities* zinazomzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kutuma wataalamu waliobobea katika ujasiriamali na *job creation and job innovation* ili watoe semina na elimu mara kwa mara huko huko vijijini kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia hii itawahamasisha vijana na watu wasio na ajira kuwa na hamu au shauku ya kujiajiri kwa kutambua fursa zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na upanuzi wa ajira, naishauri Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ishirikiane na Wizara ya Miundombinu pamoja na TAMISEMI ili wafanye uchambuzi wa namna ya kuongeza ajira kwa kufungua *Road Maintenance Camps* (magenge) vijijini ambako mtandao wa barabara ni mkubwa sana. Makundi ya vijana hawa yakipewa mafunzo ya awali ya ku-*repair* barabara nyingi za vijijini na kusimamiwa vizuri, watapata ajira na kuboresha barabara zitakazosaidia sana usafirishaji wa mazao kwa urahisi zaidi na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, waajiriwa wa sasa ndio wastaafu wa kesho. Wastaafu wengi hupatwa na aina fulani ya *shock* ya kustaafu kutokana na mabadiliko ya ghafla ya mtindo na mfumo wa maisha yaliyozoeleka wakiwa waajiriwa. Kwa hiyo, ili kuwaandaa wastaafu watarajiwa nashauri Serikali iingize katika sera ya ajira, kuendesha semina ya mafunzo ya ujasiriamali *at elementary level* kwa waajiriwa, ili elimu hii iwasaidie kujiandaa kwa shughuli ndogo ndogo za kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia hii waajiriwa watakuwa tayari wameji-*tune* kisaikolojia kuweza kumudu maisha mapya baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango huu mdogo, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ni neno pana lenye maana ya shughuli anayofanya mtu ili kumuingizia kipato au chakula, mfano kulima, kuandika, kufundisha, kupika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni nyeti sana na bila Wizara hii hakuna maendeleo na wala Wizara ya Fedha isingekuwa na uwezo wa kusimama na hakuna sababu ya Wizara ya Fedha kulalama kuwa Bajeti haitoshi, kwani Wizara hii ikifanya kazi vizuri nchi hii haitakuwa tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kazi ni lazima uanzie katika familia. Familia ya wazazi wachapakazi na watoto wataiga. Vile vile familia ya wazazi wavivu, walevi, watoto wao wataiga mfumo huo huo na hii imepelekea wazazi tulalamike kuhusu watoto kukaa vijiweni toka asubuhi hadi jioni. Lakini tujiulize mzazi anakuwa wapi hadi kijana awe kijiweni?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara inatathmini ya wananchi wenye uwezo wa kufanya kazi na wanafanya kazi? Hatuna sababu ya kuitwa maskini wakati asilimia kubwa yenye uwezo haifanyi kazi ndio maana asubuhi, jioni utakuta watu wazima na nguvu zao wako vijiweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wale walioajiriwa hawathamini kazi zao. Hakuna *monitoring* lakini kibaya zaidi sheria za kazi hazifuatwi *(Public Service)*. Mtu anaingia ofisini saa 2:00 asubuhi, saa 4:00 asubuhi ameshaondoka wengine hutoka kabla ya wakati na wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Augustino Mrema alipokuwa Naibu Waziri Mkuu, aliamuru watu wafike kazini saa 2:00 asubuhi na vinginevyo viti vingechukuliwa, wafanyakazi walitii. Naomba Waziri Mkuu sasa atoe tamko hilo. Pia tuangalie nchi zilizoendelea ukiingia kazini una *slot card* yako ya kazi kujua muda ulipoingia na unapotoka. Mwisho wa wiki saa ulizofanya kazi yanajumlishwa na unapata ujira wako kutokana na saa ulizofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo *efficiency* na uhalali wa kipato. Haiwezekani mtu afanye kazi saa 20 kwa mwezi alingane kimshahara na yule aliyefanya kazi kwa saa 180 kwa mwezi, kwanza inakatisha tamaa kwa wachapakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira binafsi ni za muhimu na kwamba Serikali haiwezi kuajiri, katika ajira rasmi Watanzania wote milioni 20. Nawapongeza waajiri binafsi kwa kupunguza tatizo la *unemployment rate* ila tu naomba Serikali iwasimamie kwani kumekuwa na malalamiko mengi sana hasa ya kipato chao na pia mikataba. Serikali ndio mama na hivyo kutokuwajali na kusikiliza matatizo hayo kutafanya waajiriwa hawa kukosa imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la vijana kuhama mijini ni tatizo kubwa kwani vijana hao hufikiri mijini kuna starehe na ajira. Matokeo yake wanakuta hali tofauti na hivyo kuishia kwenye uchangudoa, kutumia dawa za kulevya, ujambazi, kukwapua vitu mbalimbali na hivyo kuishia kufungwa. Ni vyema Serikali ipeleke madaraka vijijini ili vujana wasije mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio siri kuwa ¾ ya wafungwa ni vijana lakini pia ¾ ya waathirika wa UKIMWI ni vijana kutokana na umri wao *(sexually active)*. Hivyo basi ni vyema Serikali iwasimamie vizuri vijana hawa kwa kuwa bila vijana hatuna Taifa. Hawa ndio wanaozaa, kwa maana hiyo ni lazima kuwe na mikakati ya kuwasaidia. Taifa linalopuuza vijana wake, lina jikana lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sakata la wafanyakazi waendeshaji wa vyuo vya elimu ya juu, ni jambo la ajabu kuona watu wenye sifa za kufanana wakipewa mishahara tofauti eti kwa kuwa mmoja ni *lecture* na mwingine ni *laboratory technician,* ni lini Wizara itawapa stahili zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni jambo la kawaida kwa kila mwajiri kudai mwombaji awe na uzoefu wa miaka mitano na zaidi. Ni jambo la ajabu kijana amemaliza *form four* na *form six* akiwa na *first class* na *university first class distinction* lakini bado anahitaji awe na uzoefu. Hivi uzoefu atapata wapi? Kuna chuo cha uzoefu? Matokeo yake waajiri wenye akili wamekuwa wakiwachukua *direct from university* wale wenye akili. Hivyo Serikali inabaki na wengine (waliofanya vibaya) mfano, *CRDB, Standard Chatered* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunamfahamu tajiri (bilionea) Bill Gates na yule wa Afrika Kusini, Tokyo Sexwel, hawa walitafuta vijana wenye uwezo mkubwa kiakili (vipanga) wakawaambia nataka niwekeze kwenye biashara itakayolipa haraka na kwa wingi. Vijana wakanoa bongo wakaja na miradi na ndio wamewafikisha hapa. Vijana wa leo si sawa na wa zamani, wana akili sana hivyo tuwatumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushindani wa kibiashara ni lazima Watanzania wafundishwe *hospitality* ili vijana wetu waajiriwe kwenye hoteli zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tutafute kwanza maendeleo ya vijana mengine yatafuata. Lakini pia Jeshi la Kujenga Taifa litasaidia sana maadili na kuwafunza kazi.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani za dhati kwa niaba ya viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu nchini, kwako wewe na Mheshiniwa Spika kwa kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kuhudhuria semina ya tarehe 28 Julai, 2007 pamoja na kwamba ilikuwa ya namna kama ilivyokuwa. Hii imeonyesha upendo na kujali sana hali za watu wenye ulemavu nchini, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliohudhuria semina hiyo ya tarehe 28 Julai, 2007 kwani walionesha kujali na upendo mkubwa kuhusu masuala ya jamii ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Jeremeah Sumari, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Dr. Komba, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri na inayoeleweka vizuri na ina taarifa za kina. Hongera sana

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nitachangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria Namba 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, nafahamu ndani ya sheria hii kuna kipengele cha upatikanaji wa ajira usio na misingi ya kibaguzi, ya kijinsia, rangi, kabila na ulemavu. Pamoja na sheria kudokeza tu kwamba wenye ulemavu wasibaguliwe kutokana na ulemavu wao, naomba ufafanuzi ili nijiridhishe ni kwa kiasi gani watu wenye ulemavu walivyoanza kufaidika na sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba pamoja na sheria kutungwa lakini katika hali ya ajira kuwa soko huria pasipokuwa na maelekezo bayana *(streamlined)* yatakayowavutia waajiri mbalimbali kuwaajiri watu wenye ulemavu waliokidhi vigezo vya ajira mbalimbali, itakuwa sheria hii haitawafaidisha watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali imekuwa ngumu zaidi kwa vile katika mazingira ya sasa Serikali sio mwajiri pekee bali kuwa waajiri wengi kwenye sekta binafsi ambao wanajali sana upatikanaji wa tija ya ziada kubwa ambayo huwa dhana potofu kuwa wenye ulemavu hawawezi kufanya kazi kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii dhana ni potofu sana kwa vile tafiti zimeonesha kuwa watu wenye ulemavu hawana tabia za kutoroka toroka kazini hivyo kufanya kazi kwa muda wote wa kazi na kuleta tija mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ajira kwa watu wenye ulemavu kuwa chache kutokana na ukosefu wa elimu, uzoefu na kadhalika, lakini basi ni chache zaidi kwa viziwi ambao wanakosa fursa ya kuwasiliana kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu wangeweza kujiajiri wenyewe lakini wengi wao hawana mitaji na uwezekano wa kupata mikopo kupitia ule mfuko wa vijana na ule wa uwezeshaji wa wananchi wa shilingi bilioni 21, watu wenye ulemavu ni ngumu mno. Sio mikoani, sio Wilayani, wahusika wa kuhamasisha watu wenye ulemavu kujiunga katika vikundi ili waweze kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ihakikishe kuwa maafisa kazi na maafisa vijana wanakuwepo katika ngazi ya Wilaya. Pili, natoa ushauri kuwa Serikali (Wizara) itoe motisha kwa mashirika na taasisi mbalimbali binafsi zilizoajiri au zitakazoajiri watu wenye ulemavu, kwa mfano kuwapunguzia kodi ya mapato kwa vile mashirika hayo yanaisaidia Serikali kuzalisha ajira kwa kundi la jamii ambalo lina nyanyasika katika kufikiriwa kwenye upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ajira na ulemavu yamefafanuliwa vizuri sana kwenye *Convention No. 189* ya *ILO,* lakini hapa nchini, bado azimio hili halijafikishwa Bungeni, tatizo ni nini? Je, katika hali kama hii hizo ajira mpya 201,390 zilizopatikana hadi Juni, 2007 ni watu wangapi wenye ulemavu wamefaidika na katika maeneo gani ya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi ili nipate hoja za kuwasaidia wenzangu wenye ulemavu, kuwapa ushauri wa aina ya kazi zitakazowapa nafasi katika soko la kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waziri na Naibu Mawaziri kwa matayarisho na uwasilishaji wa hotuba na Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ajira, Serikali inastahili kuimarisha shughuli mbalimbali ambazo zinaweza kuwawezesha wananchi kujiajiri. Baadhi ya hayo ni fedha za uwezeshaji haziwafikii wananchi wengi wa vijijini, kwa mfano Mbeya Vijijini, kwa kuwa hakuna mabenki. Fedha nyingi zinakwenda mijini au mahali penye benki. Kutokana na tatizo hili naomba fedha za uwezeshaji zipitie kwenye *SACCOS* zilizoimarika. Uwezo wa *NMB* na *CRDB* Mbeya wa kuweza kuwahudumia walengwa uimarishwe. *CRDB* Mbeya haina wafanyakazi wa kutosha kwa kutoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuwe na utaratibu wa mafunzo ya wajasiriamali wa vijijini kwa kupitia Halmashauri na *SACCOS* za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga tabia ya kujiajiri au kujitegemea **Wizara** ishirikishwe katika kuboresha elimu ya ufundi katika shule zote za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kupunguza rushwa kazini kwa kujenga mazingira mazuri ya ajira na baada ya ajira yaani mfanyakazi ambaye amestaafu. Hii inawezekana kwa kuweka *pension* nzuri ambayo inahakikisha kulinda hadhi ya

maisha ya mstaafu pamoja na kuweka utaratibu na mfumo mzuri wa kuwalipa wastaafu bila masumbuko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za wafanyakazi kwenye vyombo vyao vya fedha kama *NSSF, PPF, LAPF,* zitumike kutoa mikopo kwa Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa maghala na masoko vijijini ili kuwawezesha wakulima kulima kwa juhudi na kuwa na masoko. Masoko haya yatawasaidia wakulima na kuziwezesha Halmashauri za Wilaya kukusanya kodi kwa ajili ya kulipa mikopo kwenye vyombo vya fedha na kuongeza mapato ya halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya mpango na bajeti ya Wizara.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake wote wawili, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wao wote kwa kuwasilisha Bajeti yao kwa umakini na umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliowapoteza ndugu, jamaa na wapenzi wao. Nawaombea Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali kuandaa mipango maalumu ya kuhakikisha vijana wa nchi hii wanajikomboa kwa kuwa na ajira za uhakika, lakini bado tukubali vijana ni wengi na wote kuwapatia ajira za Serikali si rahisi kwani wako wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri hasa kwa upande wa Zanzibar vijana ni wengi sana, ningeiomba Wizara hii ikashirikiana na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji wakawashawishi wawekezaji *(donors)* ili wajenge viwanda Zanzibar angalau vitatu hasa ukizingatia udogo wa visiwa vyetu na mazao yanayozalishwa visiwani humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utapata kiwanda cha kusindika matunda, kusindika samaki na kiwanda cha sukari tutapunguza matatizo ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama na vijana Zanzibar wamekaa macho kwa muda mrefu kusubiri fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wetu mpendwa ili wananchi walio wanyonge waweze kujikwamua kimaisha kwa kufanya kazi, hadi hii leo hazijafika. Napenda nielewe tatizo liko wapi katika kupatikana fedha hizo kwani wananchi wapo wengi wanazisubiri fedha hizo kwa kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naunga mkono.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, akisaidiana na wataalamu wake na taasisi zote kwa maandalizi mazuri sana ya hoja hii ya Wizara. Naiunga mkono kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada Wizara inazofanya kuratibu ajira, bado sijaona jitihada za waziwazi kwa baadhi ya Wizara kuandaa mpango wa jinsi ya kuongeza ajira. Siyo lazima za kuajiriwa na Wizara zenyewe bali za kuweka mazingira ya wananchi kujiajiri wenyewe. Mfano, maliasili kuandaa mpango kabambe wa ufugaji nyuki au Wizara ya Nishati na Madini kuandaa vitabu maalumu kwa ajili ya wachimba madini wadogo wadogo. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuongeza maeneo ya umwagiliaji na kutoa mafunzo kwa wengi ya ukulima wa kisasa pamoja na kuhamasisha vijana wengi kuingia katika biashara ya kilimo na kadhalika. Wizara zisiendelee kudhani Wizara yenu itatoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tatizo kubwa la malipo ya wafanyakazi wanaopunguzwa kazi kukosa haki zao kwa kipindi kirefu. Hali hii inatuletea adha na usumbufu si kwa wafanyakazi tu, bali kwa nchi kuishi na wasiwasi wa hujuma mbalimbali. Kauli ya wafanyakazi popote pale walipo lazima isipuuzwe na mahusiano mema wakati wote mahala pa kazi yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nilipokuwa Wizara hii kama Waziri niliona kuwa usalama na afya mahali pa kazi katika kipindi hiki cha soko huria na viwanda huria, lazima upewe uzito wa kisheria. Pamoja na hilo lazima kwa makusudi Serikali itoe uzito wa hali na mali kwa taasisi hii ya *OSHA* ili itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *NSSF* bado naiomba Serikali ione namna ya kuishawishi *NSSF* itekeleze azma ya Rais wetu ya kuweka vitega uchumi katika mikoa iliyo nyuma kimaendeleo. Mkoa wa Rukwa ungefaidika sana na *NSSF* kwa kujenga nyumba za watumishi na kujenga ofisi, maana ofisi nyingi bado ni nyumba za watu binafsi ambazo zilijengwa kwaajili ya matumizi ya kulala, sasa ndio ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zaidi ya miaka mitano hadi hivi sasa suala la kuundwa Baraza la Vijana limekuwa kimya kabisa. Hivi tatizo ni nini, ukimya huu unaweza kudhaniwa kuwa mbinu za kutoanzisha Baraza hili. Lakini bado naamini maandalizi yake yanafanyika kwa uangalifu sana ili tusianzishe mzozo mwingine wa Kitaifa. Ni bora kuwa waangalifu lakini tuelezee kuwa hatua zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005 iliyoainisha mambo kadhaa yanayohusu Wizara hii, hivi kwa muda wote huu wa miaka miwili pamoja na kuandaa mkakati wa Taifa wa kukuza ajira, tumefikia wapi katika azma ya kufikia ajira milioni moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ukipitia kitabu cha Taarifa ya Uchumi 2006, kilichotolewa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji utakuta kuwa miradi mingi inaendelea kufunguliwa Dar es Salaam wakati mikoa mingine haina hata mradi mmoja. Je, Wizara inahusiana vipi na *PSRC* katika masuala haya ili kuzuia vijana wasiendelee kuhamia Dar es Salaam na kukimbia vijiji ambako ndiko kwenye ajira? Naunga hoja mkono. Nampongeza Waziri na timu yake yote hiyo.

**MHE.AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye huruma kwa kunijalia uhai na uzima na kunipa nguvu ya kuchangia hutuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake kwa kusimamia vyema utendaji na ufuatiliaji wa majukumu mazito yaliyo katika Wizara yao. Pia niwapongeze watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano mazuri waliyonayo na kumwezesha Mheshimiwa Waziri kuwasilisha hotuba yake mbele ya Bunge letu Tukufu, hotuba ambayo ina mwelekeo na dira ya maendeleo kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia hotuba hii kwa kuanzia na Shirika la Taifa la Tija *(NIP)*. Shirika hili lina majukumu makubwa ya kuboresha tija na ufanisi kazini na taasisi za umma, mashirika yasiyo ya Kiserikali na makampuni binafsi kwa kutoa huduma za mafunzo, ushauri, uelekezi na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika hili ni muhimu sana katika kukuza uchumi, lakini juu ya umuhimu huu naona Serikali haitoi kipaumbele kwa shirika hili kwa sababu shirika hili halipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini na hivyo kukabiliwa na hali ngumu ya uendeshaji, hali ambayo ilisababisha wataalamu wake kukimbia na kubakia watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, shirika hili lilikuwa na kiwanja namba 906/H. *Mbezi Beach* kwa ajili ya ujenzi wa ofisi. Kiwanja hicho kilipewa shirika la kibinafsi la Kihindi. Lakini pia baada ya kunyang'anywa kiwanja hicho shirika lilidai gharama zilizotumika kiasi cha shilingi milioni 213 kwa mujibu wa tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi milioni 49 zilitumika kuendeleza kiwanja hicho. Kama hiyo haitoshi, shirika baada ya kudai gharama hizo, Serikali iliamuru kulipwa shirika shilingi milioni 26 kama fidia na hadi sasa shirika limelipwa shilingi milioni 15 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hoja hii inaonesha wazi Serikali imelipa mgongo shirika hilo. Naiomba Serikali yetu Tukufu kuliendeleza shirika hili kwa kulipatia ruzuku ili kuweza kufanya kazi zake vizuri zaidi pia suala la kiwanja na malipo yao yaliyobaki warudishiwe wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mkurugenzi Mtendaji pamoja na watendaji wote wa mfuko huu kwa kazi kubwa, wanayoifanya kwa kusimamia vyema majukumu na maslahi ya wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko huu hivi sasa baada ya kukusanya michango ya wafanyakazi na kuhifadhi fedha hizo kwa malipo ya uzeeni, pia unajishughulisha na vitega uchumi vingi ili kuongeza mfuko na hivi sasa imemudu kutoa mafao yote ambayo yanatakiwa kutoa kwa wafanyakazi walioko makazini na wale wastaafu kwa wakati na bila ya usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na msaada mkubwa unaotolewa na *NSSF* katika kuendeleza jamii katika Taifa hili, naiomba Serikali kuzidi kuipatia vitega uchumi ili kuongeza tija pia kuiondoshea kodi katika miradi yake pamoja na miradi yote ambayo wameianza na bado wana nia ya kuiendeleza, wapewe ikiwemo daraja la kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* imewekeza fedha nyingi katika mradi huu wa ujenzi wa daraja na Serikali haina budi kujali fedha za wafanyakazi zilizotumika katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuchangia masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuanzisha mfuko wa mikopo ya wajasiriamali vijana. Hata hivyo mfuko huu ni mdogo kwa vijana wajasiriamali wa Tanzania. Fedha ziongezwe na fedha hizo zilenge zaidi katika kuwapatia mafunzo vijana hao ili kuweza kupata utaalamu zaidi wa kuendesha miradi yao na kuwapa uwezo vijana kukopa kutoka asasi za biashara za *NMB* na *CRDB Bank.* Kwa kuwa asasi hizi zinatoa mikopo ile ya mabilioni ya J. K. naiomba Serikali ifikishe fedha hizo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuanzisha *SACCOS* za vijana kwenye kata hautafanikiwa kama Serikali haitafanya kampeni kabambe kama ile ya ujenzi wa Sekondari kupitia wizara ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wananyanyaswa na waajiri wao kwa kutowalipa mishahara mizuri, kutowapa posho na hata kuwapatia vifaa vya kazi na kubwa zaidi ni lile la kunyanyaswa kijinsia hasa kwa wale wahudumu wanawake wa hoteli. Naiomba Serikali ifuatilie sehemu hizo ili kuweza kujua matatizo wanayoyapata vijana wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuongoza uhamasishaji wa kupima damu kwa kupambana na UKIMWI. Aidha, napenda kuwapongeza vijana wa Tanzania kwa kuhamasika kupima damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Serikali ifuatilie vijana wetu juu ya tatizo hili la UKIMWI ili iweze kuwanusuru na balaa hili na kuondosha au kupunguza unyanyapaa kwa watu walioathirika na iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yetu kwa mpango huu, lakini napenda kuiomba Serikali kuandaa *master plan* kwa kila mkoa hapa Tanzania na *master plan* hiyo iwe ni kigezo katika utekelezaji wa mpango huu ili iwe rahisi kufuatilia na kuwezesha vijana kupata ajira kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la wamachinga Dar es Salaam. Naipongeza Serikali kwa uamuzi huu. Napenda kuiomba Serikali ianze mara moja jengo hili. Kusiwe

na ubaguzi wa kijinsia katika ugawaji wa nafasi kwa wamachinga. Vijana wanawake na wale wanaume wapewe nafasi sawa. Baada ya hapo naunga tena mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja. Baada ya hilo napenda nitoa mchango wangu kwenye sehemu chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko ya hifadhi ina sehemu muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Naiomba sana Serikali ishirikiane na Wizara ya Fedha na TAMISEMI ili waunde mamlaka ya kusimamia mifuko hii. Sasa hivi mifuko inajiendesha yenyewe lakini itaboreshwa sana kama itakuwa na mamlaka ya kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa mifuko ya hifadhi ulenge zaidi kwa wanachama wa mifuko hiyo na miradi inayogusa jamii. Naiomba sana Wizara mifuko hii iimarishwe katika kuwekeza kwenye nyanja hizo tu na siyo zingine ambazo hazitengani na dira ya mifuko hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vijana wa Kitanzania hawawezi kushindana na wenzao wa Kenya na Uganda katika soko la ajira. Naiomba sana Wizara ifanye utafiti kuanzia shule za msingi mpaka Vyuo Vikuu kuwa tatizo ni nini? Jambo hili ni la muhimu sana maana vinginevyo ajira zote zitachukuliwa na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili pia naiomba Wizara isimamie sana vibali vya kazi kwa wageni. Idadi ya wageni wanaoruhusiwa kufanya kazi kwenye taasisi au mashirika iangaliwe na kusimamiwa kwa makini sana ili kulinda ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii kabla ya kutoa pongezi kwa Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuweza kuandaa hotuba hii ambayo imesomwa hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalmiko mengi toka kwa wafanyakazi waliopunguzwa kazi baada ya mashirika yao kuuzwa kwa watu binafsi. Kubwa wanalolalamikia ni ulipwaji wa mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke wafanyakazi hao walifanya kazi kwa moyo kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na kwa familia pia, kwa sababu hiyo basi tuna kila sababu ya kuhakikisha wafanyakazi hawa wanalipwa stahili zao kama ilivyoelekezwa na si vinginevyo. Tunataka kujua Wizara imefanya nini kuondoa tatizo hili ili wafanyakazi hao wapate haki zao bila usumbufu na kufuata sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wana haki ya kujiunga na chama ambacho watachagua na wataona kitalinda na kutetea maslahi ya yao. Pia wana haki ya kuanzisha vyama vingine katika maeneo yao ya kazi hata kama kuna chama kingine mradi wafuate taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako malalako toka kwa wafanyakazi kwamba upo urasimu au upendeleo katika kusajili vyama hivi, wapo wanaopewa na wengine kunyimwa na hii inwapa hisia kwamba vipo vyama vinaonekana vikipewa usajili vitaibana Serikali katika kudai maslahi ya wafanyakazi wao. Naomba majibu katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna watu walioathirika na suala hili ni vijana. Wapo vijana wengi mitaani pamoja na kuwa na elimu nzuri lakini hawana ajira na hii inawasababisha vijana kujiingiza katika mambo mabaya kama utumiaji wa dawa za kulevya, umalaya na hata wizi. Vijana hawa wanatakiwa kupewa nafasi kubwa katika suala zima la ajira na kuondoa kile kipengele cha sifa ya uzoefu. Kila siku huwa najiuliza uzoefu utaupataje bila kupewa nafasi ya kuonyesha uwezo wao katika nafasi hizo walizoshikilia baba zao na mama zao? Tunaomba sana vijana wapewe nafasi ili kuwanusuru katika hayo mambo niliyoyataja hapo juu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati kwa hotuba yake nzuri sana yenye takwimu muhimu na aliyoisoma kwa ufanisi mkubwa. Naunga mkono hoja yake kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwapongeza Naibu Mawaziri Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu Dr. Ladislaus Komba, Wakuu wa Idara na Watendaji Wakuu na viongozi wote wa taasisi chini ya Wizara hiyo kwa jinsi walivyomsaidia Waziri na kumwezesha kuwasilisha hotuba nzuri sana humu Bungeni. Endeleeni hivyo hivyo na mimi naunga mkono juhudi zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi wa Viwanda *(factory inspection)* iimarishwe na ipatiwe nyenzo za kazi za kisasa ili ifanye ukaguzi endelevu katika viwanda. Viwanda vingi havitimizi matakwa ya kinga za kiafya na mazingira hatari viwandani. Hata pale kinga zilipowekwa, wafanyakazi wenyewe wanazipuuza. Mfano Kiwanda cha Nguo cha *KTM.* Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilikitembelea na kuona mapungufu hayo

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ianzishe ukaguzi wa ajira nchini ili kuhakiki ukuaji wa ajira na upoteaji wa ajira zilizokwisha kupatikana. Kwa mfano kuna ajira mbalimbali zinazopotea wakati makampuni yanapouzwa bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ziwekewe taratibu za kisheria za kuzilinda na zinapofutwa basi taarifa rasmi itolewe Wizarani. Vile vile ajira zinapoongezeka kuwe na *form* ya *returns* za kipindi cha miezi sita sita. Zifuatiliwe maeneo ya kazi kwa njia ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze sana kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. Naomba kuchangia katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutafuta njia ya kusaidia wananchi kuepukana na umaskini kwa kutenga fedha za mikopo lakini mimi nashauri kama tunahitaji kusaidia wananchi hasa wale wanaoishi vjijini; kwa kuwa sasa hakuna benki hizo vijijini mikopo hiyo hupata watu wachache tu ambao wapo mjini na matokeo yake vijana hao hutoka vijijini na kuja mjini kwa wingi, ili kuja kupata mikopo hiyo na kujiunga na *SACCOS* ambazo ziko mjini. Tatizo la vijana kuja mjini halitoisha kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubali kutumia taasisi ambazo hufika vijijini na kukutana na wananchi, mfano *SIDO* ili waweze kushiriki vizuri katika kupata mikopo hiyo nao kuliko vijana kutoka vijijini kuja mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubali kuwa vijana wanapenda kuishi vijijini laiti kama vijana hao tutawajali kwa kuwasaidia wapate vitendea kazi mfano trekta, kwa kulimia kwa bei nafuu, hiyo inaweza ikatusaidia au hasa kusaidia vijana kupata kipato chao cha kutosha na wao wenyewe kuamua kubaki kulima kuliko kuja mjini. Naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Awali ya yote nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Capt. John Chiligati Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara kwa usimamizi mzuri na kuhakikisha kwamba mikopo ya bilioni moja inawafikia wananchi wote hapa nchini, ingawa sio rahisi wote kupata kutokana na hamasa kubwa waliyopata wananchi na ujasiriamali hapa nchini ni vyema sasa nitoe ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri, sasa Wizara iangalie jinsi gani itaweza kushirikiana na *SIDO* kwa kutoa mikopo awamu ya pili ambayo itasaidia kuwapatia wananchi mikopo hiyo kwa masharti nafuu, kwani *SIDO* uzoefu wao umeonyesha wananchi wanarudisha mikopo bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ushauri huo utafaa basi ni pamoja na umuhimu wa kuanzisha *SIDO* Wilaya zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi ambao wanasoma kwenye vyuo vyenye taaluma ya ufundi au kilimo ni vyema wakakopeshwa vitendea kazi ili waende kujiajiri wenyewe kufuatana na elimu yao waliyopata, kama vile vyuo vya Sokoine *(SUA),* hata wale wanaojifunza suala zima la ufugaji mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ishawishi shule zetu hasa za sekondari ziwe na masomo ya ufundi ya aina mbalimbali ili wasipopata nafasi ya kujiendeleza au kuendelea na elimu ya juu na hasa waendapo vijijini waitumie elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ishauriane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ianzishe vyuo vya mafunzo vya vijana kubadilisha tabia ya vinunda, wavuta bangi, na wanaotumia dawa za kulevya ili vituo hivyo viweze kubadili tabia ya vijana hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba niwatakie heri na mafanikio wote wanaofanya bidii na jitihada kuhakikisha kwamba ajira na maendeleo ya vijana wa nchi yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoelewa mimi kazi ni shughuli yoyote ambayo binadamu anaitekeleza kwa wakati aliojipangia na inampatia kipato cha kumwezesha kumudu maisha yake na familia yake, kama anayo. Si lazima mtu afanye kazi ya kuajiriwa na akae kitini na kushika kalamu, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ambayo Mwenyezi Mungu ameipenda sana, kwani tuna ardhi pana sana yenye virutubisho vya kuwezesha kilimo. Tunavyosema kilimo ni uti wa mgongo wa Tanzania, nguvu kazi ya vijana waliosambaa mijini ambao hawana shughuli ya kufanya, inatosha kabisa kuitumia, hautaweza kupata tija kama hujaitafuta kwa nguvu zote na hatutaweza kupata starehe kama hatuko tayari kupata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubali kutumia fungu la fedha hata kama kukopa tuwakusanye vijana wetu ambao hawajapata bahati ya kupata elimu yoyote ile wamejaa mijini na vijijini. Tutumie mabwana shamba tulionao ambao wanakaa bure, tutengeneze vijiji ambavyo wenyewe vijana watatumia nguvu zao kujenga hata nyumba za unafuu ambao wataweza kuishi humo kwa muda tuwatunze kwa mwaka mmoja tu. Tukiwa na vifaa vya kilimo, mbegu na bahati nzuri Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wameshafanya kazi ya kubaini ardhi ipi ni nzuri kwa zao lipi. Tuwasimamie vijana hawa walime zao la biashara na hapo hapo wanalima zao la chakula chao hapohapo wakiwekewa pia mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka mmoja tu wataanza kurudisha ule mkopo waliopewa na Serikali na wao watanusurika na kuishi kwa dawa za kulevya na kuwa

vibaka, kupigwa mpaka kufa na janga la UKIMWI kwani watakuwa wako *busy* na mashamba na mifugo. Serikali itapata na wao watapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zipo nyingi nchini mwetu, Watanzania ni watundu sana, kuna Watanzania wanotumia mikono yao na kubuni vitu mbalimbali. Udongo wa mfinyanzi hapa kwetu upo tele, kuna wakati kulikuwa na kiwanda kilichokuwa kinatengeneza vikombe, mabakuli na majagi ya maua na udongo walikuwa wanauchimba maeneo ya mkoa wa Pwani, udongo mzuri tu, sielewi kiwanda kile kilikufaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema kazi zipo nyingi, kinachotakiwa ni kukaa chini na kupanga mikakati na kuwa na fungu la fedha ambazo zitawekwa kwa ajili hiyo. Kama hutaki kutumia pesa basi hauko tayari kupata pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira tunazozizungumza hapa ni ajira ambazo wengi wanaozitafuta ni wale waliopata bahati ya kusoma. Hawa wako wengi mijini wanahangaika huku na huku kutafuta ajira. Magazeti yanaandika kwa anaetafuta kazi atume maombi, lakini cha kusikitisha vijana hawa huandika hata barua lukuki lakini hawapati jibu na hata wakijibiwa majibu hayaridhishi kwani siku hizi kama huna *god father* basi ni vigumu sana kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao wanaotangaza husema wanataka waombaji wawe na sifa za kufanya kazi kwenye taaluma hiyo isiyopungua miaka mitano yaani awe na uzoefu wa kazi husika. Je, suala linakuja hawa ambao wamemaliza elimu sasa uzoefu watautoa wapi? Hii si sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira zipo nyingi hasa kwenye makampuni ya watu binafsi, lakini ajira hizo hufanywa na wageni na ukizitafakari si ajira ambazo Watanzania wangeshindwa kuzifanya, ila hawa ndugu zetu wanatumia uwezo wao walionao kwa sababu kampuni ni yake anaajiri wageni kwa kisingizio cha uaminifu na utendaji.

Suala linakuja, je, Serikali na Wizara watapitia kwenye makampuni hayo mara kwa mara kujua akina nani ni wafanyakazi halali? Kwani naweza kusema rushwa nayo ni kizingiti kikubwa kwa tunaowaamini wanapitia na kuangalia, hayo wanadanganya tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwe waangalifu sana, wageni wanaofanya kazi ambazo Watanzania wangeweza kufanya wako wengi na sio wote wanajulikana na vyombo husika. Bado tuwe waangalifu na hao ndugu zetu wanaotoa *permit* za kufanya kazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ihakikishe vyama vya wafanyakazi vinapewa rungu la kuhakikisha wafanyakazi wanapata matarajio yao kwenye maeneo yao ya kazi, mafao yao yanalipwa kikamilifu wanapoacha au kuachishwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake waangaliwe wasinyanyasike likizo za uzazi zitolewe kwa jinsi utaratibu wa Serikali unavyotaka, maeneo ya kazi yawe na usalama wa kutosha na pindi mfanyakazi akipata ajali alipwe na aangaliwe vizuri wakati akiugua au

akiuguza kiungo alichopata ajali. Sheria zote zinazohusu utumishi zirekebishwe na ziendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya vijana si kuwapatia mikopo kwani mimi huwa nasema mkopo haumtoi mtu kwenye umaskini kama hakupata elimu ya mradi anaotaka kuufanya au soko la mazao yake ili aweze kupata tija na marudisho. Unampa mtu mkopo kesho unatarajia arudishe alichopata, je, anakopa ili afanye nini? Mikopo ya vijana itumike kama jinsi nilivyotoa rai hapo mwanzo wa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumwendeleza kijana si kazi peke yake inayohitaji muangalizi wa karibu sana, sio kijana kumkabidhi fedha umwambie kajiendeleze. Kumwendeleza kijana ni kumpa elimu ya ujasiriamali au ufundi wa kutosha, akimaliza elimu hiyo akopeshwe vyombo vya kazi ili akiondoka pale akajiajiri au wapatiwe na elimu ya kuanzisha ushirika wao wakakae pamoja, wafanye kazi yao kama ni mafundi seremala au fundi bomba au fundi umeme wakae pamoja waanzishe ushirika wao kwa kusaidiwa uanzishaji wa shughuli hiyo wakishazoea na wao wanaweza kuwasaidia vijana wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* ni mfuko wa fedha za wananchi wanaokatwa kwenye mishahara yao ambayo wanakuwa wameshakatwa kodi, sasa kama baada ya yeye kukatwa kodi kwenye mshahara wake na mshahara huo ndio unaokatwa mchango wa *NSSF* halafu tena anapolipwa mafao yake anakatwa tena kodi basi huo ni uonevu, kwa nini asilipwe mafao yake yote kamili?

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* inaingiza faida nyingi sana baada ya kukopesha au kufanya miradi yoyote ile. Hizo ni fedha za wafanyakazi wanazochanga kwa nini na wanachama wasipatiwe faida hiyo kwa kuongezewa kwenye fedha zao wanapolipwa? Hizo fedha za akiba za watu, faida inayopatikana anapewa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Kigamboni ni hadithi tosha kabisa na inasikitisha kuona Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilipelekwa mpaka eneo inayotaka kujengwa daraja hilo, tulichoambiwa Wanakamati na mie nikiwa mjumbe, mchoro, mipangilio yote tayari, kilichobaki ni Wizara ya Fedha waruhusu ujenzi uanze. Leo hadithi ziko nyingi mara bado hajapatikana mwekezaji wa kujenga daraja, wa nini mwekezaji kama *NSSF* watakuwa tayari kusimamia na tayari wameshapata *contractor* wa kujenga daraja hilo, *NSSF* wameshalipa mpaka kufikia kutambua wapi pa kujenga, leo tunasema tunahitaji mwekezaji ajenge halafu achukue fedha itayokuwa inapatikana ajilipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mie nikifikia hapo naona mambo si mazuri, fedha ingepatikana, *NSSF* wangejilipa na wanachama ambao ni Watanzania wangekuwa ni chombo chao, daraja lao wangelitunza na wangenufaika na viingilio si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuiomba Serikali/Wizara waangalie sana Shirika la Tija *(NIP)*, shirika hili linajitahidi sana kujiendeleza na kutoa elimu kwa Watanzania, shirika lipatiwe fedha ili liweze kujiendeleza mpaka hapo litakapojiweza. Kama tunataka kuendelea na kuishi kwa raha basi tutumie fedha pale tunapoona kwa

muda fulani, fedha husika itarudi. Tuendelee na kuitumia nguvu kazi iliyopo, tumia fedha upate fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, yapo mengi lakini kwa sababu hii ni Wizara yangu nitaendelea kuishauri.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi kwa Wizara kutoa hotuba ambayo inajitosheleza kwa ujumbe wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina malengo mazuri hasa inapowaamini vijana kuwapa mikopo ingawa ni kidogo ili kukuza mitaji yao. Matatizo yanayojitokeza ni pamoja na kukosa malengo ya kuweka mradi hadi kuutafuna mradi, kodi kubwa ya pango, Halmashauri kuhodhi maeneo mazuri na kuwauzia tena vijana kwa kutumia majina bandia, kupewa maeneo yasiyofaa kabisa kibiashara kukosa miundombinu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi nzuri ya kuanzishwa vikundi hivi vya *SACCOS* Wizara ifanye yafuatayo:-

Kwanza Wizara kupitia Halmashauri husika ziagizwe kufuatilia uhai wa *SACCOS* hizo baada yam bio za mwenge, pili, Wizara kupitia chombo hicho hicho wawapatie semina endelevu *SACCOS* husika. Hii ni kwa sababu *SACCOS* hizo zimeanzishwa ghafla kukidhi tukio na tatu, kuwepo na mrejesho nyuma wa uendelevu wa *SACCOS* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ni kujenga jengo la heshima hii mkoani Mwanza sababu vijana wa aina hii ni wengi sana katika jiji hili.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza *OSHA* kwa kupanua wigo na kuboresha utoaji huduma ya afya na usalama mahali pa kazi. Lakini bado zipo changamoto nyingi kwa waajiri, hasa sekta binafsi kutothamini hoja hiyo ya huduma ya afya na usalama mahali pa kazi. Je, inapotokea mfanyakazi kuathirika afya yake kwa uzembe wa mwajiri, Wizara inachukua hatua gani kwa mwajiri na mwajiriwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Wizara kwa hatua thabiti inazoendelea kuchukua kwa lengo la kuwaendeleza vijana. Katika mpango wa kuwajengea uwezo vijana wa kukua kiuchumi na hasa kujiajiri katika sekta isiyo rasmi, ni vyema mkakati wa makusudi uandaliwe kwa kuhamasisha vijana hasa wa kiume kwani *SACCOS* nyingi zilizoanzishwa wanachama wake ni wanawake. Hivyo ni dhahiri kama tutaendelea hivi, kundi kubwa la vijana wa kiume tutaliacha nyuma, jambo ambalo litakwamisha maendeleo ya vijana kwa ujumla wake. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa hotuba nzuri ambayo imetolewa asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini mipango aliyoainisha kwenye hotuba yake itasaidia sana katika suala zima la kuweka mazingira ambayo yatawezesha vijana kujiajiri. Hii ni pamoja na wale vijana wangu waishio katika Mji Mdogo wa Sanya Juu. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWINCHUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Wizara hii, Naibu wake Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Katibu Mkuu wa Wizara ndugu Dr. Komba pamoja na Wakuu wa Idara wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa katika kiwanda cha *KTM* kilichopo eneo la Mbagala, Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, wafanyakazi wanafanyakazi bila ya vifaa muhimu vya kazi hasa katika eneo la mchanganyo wa dawa na kusababisha mikono yao kuharibika na kuacha kazi baada ya muda mfupi kutokana na sumu kali. Naiomba *OSHA* kwenda kufanya kazi/ikaguzi wa kustukiza na pia kuomba fursa ya kuongea na wafanyakazi wakiwa peke yao na hasa mmoja mmoja kuepusha kusemeana kwa mwajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna mtiririko mkubwa wa maji machafu ambayo yanamwagika ovyo na kuleta wasiwasi mkubwa kwa wananchi wanaoishi jirani na kiwanda hicho na vile vile kuhatarisha maisha ya viumbe vya baharini, kwa kuwa maji hayo mwisho wa mwelekeo wake ni Bahari ya Hindi, pia yanaweza kuleta madhara kwa waosha magari wanaotumia maji ambayo yamechanganyika na uchafu wa *KTM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa daraja la Kigamboni lina umuhimu wa pekee. Wizara haina budi kutoa msukumo wa kutosha na kuharakisha taratibu za Kikao cha *IMTC* na Baraza la Mawaziri ili hatimaye tukamilishe taratibu za kibali na kuanza ujenzi. Naipongeza sana Wizara kwa kuanzisha bodi za ajira kwa kuzingatia sekta na ajira yenyewe. Hii itasaidia sana katika kufanya kazi kwa uafanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utoaji mikopo kwa wajasiriamali ni vyema Wizara/Serikali ikatumia utaratibu wa kupitisha fedha za mikopo kwa vyama vya kuweka na kukopa ili kwa nia ya kuhalalisha fedha hizo zinawafikie walengwa kwa urahisi zaidi kuepusha urasimu wa benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *NSSF* kwa mpango wake wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu, Kigamboni mradi ambao utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 10.8. Mradi huu kwanza utawezesha Kigamboni kuendelea na kujengeka kisasa na pia kutoa fursa kwa wananchi wenye kipato cha chini kuweza kukopa nyumba hizo na kulipa polepole kwa awamu/vipengele *(installment)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* walikuwa na mpango wa kupeleka baadhi ya Wanakamati wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ya Bunge sambamba na wajumbe wa bodi wa *NSSF* kujifunza kwa ndugu zetu wa China, naomba kutoa hima kwa Menejimenti ya *NSSF* kuendeleza lengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi. Kadhalika nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote. Ninao ushauri ufuatao kwa Wizara:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Wizara iainishe wazi umri halisi wa ujana ni upi unaotambulika kisheria. Kutambulika huku kutaondoa dhana ya kila mtu kutafsiri ujana kwa jinsi anavyoona yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mkakati wa Wizara kuhusu kuwaendeleza vijana wale wasio na elimu na maisha yao ni ya vijijini? Kadhalika naomba Mheshimiwa Waziri anieleze Tanzania kwa ujumla wake inao vijana wangapi na katika idadi hiyo wasichana ni wangapi na wavulana ni wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itakuwa na maafisa vijana kwa kila Wilaya lini Wilaya yangu ya Iramba iliyopo Jimbo la Uchaguzi la Iramba Magharibi itapewa afisa vijana?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mpango gani katika kuboresha sekta binafsi katika kuinua vipato vya vijana na kutoa elimu ya ujasiriamali kama hatua ya kumkomboa kijana kutotumbukia katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atoe ufafanuzi wa mbinu *(methodology)* inayotumika katika kuhakikisha zile ajira 1,000,000 zilizoahidiwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, Wizara inapata mafanikio ya kukamilisha idadi hiyo na hata kuzidi lengo na sio vibaya Waziri akilieleza Bunge letu Tukufu hadi sasa tayari ni ajira ngapi zimetekelezwa kupitia mpango huo na je, ni vijana wangapi wamefaidika kupitia mpango huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mfuko wa uwezeshaji maarufu kama mfuko wa J. K. mikopo inatolewa kwa kiwango kidogo sana na sio hatua ya kumkomboa mwananchi kutoka katika umaskini. Kiwango cha shilingi laki moja ama mbili bado ni kiwango kidogo mno, kwa nini viwango hivi vya Wilaya ya Iramba vimetofautiana na Wilaya zingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta binafsi kuhusu ajira kupitia wamiliki binafsi upo unyanyasaji mkubwa kwa wafanyakazi hasa kwa kufanyishwa kazi kuzidi saa za kazi, kutokulipwa *overtime*, kutokupewa likizo, malipo ya matibabu na marupurupu mengine yanayostahili hayatolewi. Waziri anaeleza nini kuhusu hii ambayo imeshamiri kwa kisingizio cha soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Wizara ipo vipi katika kupiga vita utumikishaji watoto katika sekta mbalimbali zikiwemo kazi za harubu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* utekelezaji wa majukumu yake pia uelekezwe ngazi za chini ili kutoa ushiriki zaidi kwa wananchi wetu hasa wakulima kushiriki kikamilifu katika kuhifadhi mapato yao kwa faida ya baadae.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa kupewa ufafanuzi wa maelezo yangu kama yalivyo juu.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe hongera kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na pia naunga hoja mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo napenda nichangie kwa maandishi kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la waajiriwa, Halmashauri za Wilaya kufukuza kazi waajiriwa kwa uonevu kama mwajiriwa Juma M. Munga, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Legeza Mwendo, Milola, Lindi Vijijini kufukuzwa kazi bila kusubiria utetezi wa mwajiriwa pindi alipoomba vivuli *(photocopy)* kutoka kwa ofisi ya *DED* ili akate rufaa kama alivyoshauriwa afanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu Juma M. Munga alishauriwa akate rufaa, lakini alipoomba vivuli kutoka ofisini kwake hakuvipata hadi muda wa kufukuzwa kazi ndipo akafukuzwa. Nina ambatanisha maelezo ya maandishi yote ya mjadala kati ya Juma M. Munga na mwajiri wake ili upate ufafanuzi zaidi ili maamuzi ya haki yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi kama sikutenda haki, hayo ni malalamiko ya wananchi ndani ya Mkoa wangu. Naomba uchunguzi ufanyike na haki itendeke, kama kweli ndugu Juma M. Munga ana kosa basi mimi sina mjadala, kama hana kosa basi haki itendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inasema nini kuhusu sheria ya kazi kwa mtu anayelipwa shilingi 200,000/= *gross*, je, mtu huyu anastahili pia kulipwa *overtime* au hastahili? Tupate ufafanuzi wake maana kuna utata katika kampuni za watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda na mashamba ya mashirika ya umma ambayo yalibinafsishwa na wafanyakazi wake bila kupewa malipo yao hadi leo. Serikali ina mpango gani juu ya suala hilo? Tunaomba ufafanuzi, maeneo kama Mbarali 170, *Hanang W. Complex* watu 400, Kilwa, *Mkata Saw Mills,* kiwanda cha Chuma Tanga, Kiwanda cha Mpira Muheza (Mashamba), tunaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu waajiri wa taasisi, mashirika binafsi, viwandani, kuona kuwa nao wanatendewa haki katika malipo yao ya ajira. Je, Serikali

inaangalia vipi juu ya ajira za taasisi binafsi, mashirika binafsi, viwanda binafsi juu ya mishahara ya watumishi, kufika na kuona kuwa wanalipwa kihalali?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utambuzi wa vijana wa vikundi vya kuzalisha mali viitwavyo *Youth Mapping* umeendelea kufanyika tayari? Je, katika mikoa ya Lindi katika Wilaya zake Ruangwa, Nachingwea, Liwale, Kilwa, Lindi, Lindi Vijijini tayari? Kama bado tunaomba sasa ni wakati muafaka wa kutambua shughuli za vikundi vya vijana.

**MHE. SAID A. AFRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na sasa naomba nijielekeze katika hoja iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya vijana ni Taifa la kesho kwa mtazamo wangu imetufanya kama Taifa kulitazama kundi hili kama halina nafasi kwa sasa, hivyo vijana kuachwa vijiweni bila kutambulika na kuibua vipaji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya makusudi sasa kuliangalia kundi hili kwa kubadili kabisa mtazamo wa dhana hiyo na kutambua vijana ni Taifa la leo pia. Nguvu kazi kubwa ya kusukuma maendeleo ya nchi hii ipo kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu letu la kwanza ni kuwajenga vijana hao katika maadili na kuwaelekeza vijana katika kuthamini kufanya kazi badala ya kukaa vijiweni, mahala ambapo tumewapeleka vijana wetu sisi wenyewe kwa kutokuwa na mipango sahihi kwa maendeleo na mustakabali wao. Kundi kubwa la vijana limejielekeza mijini kwa matarajio ya mafanikio katika maisha yao au kupata kazi, na wengi wao kuishia vijiweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sasa pesa zinazotengwa kwa ajili ya mfuko wa vijana ambazo mikopo yake inatolewa kwa upendeleo na pesa hazikidhi mahitaji ya vijana wote, ingekuwa ni busara pesa hizo kuanzisha *Youth Camps* na kuwapa zana za kilimo na pembejeo na vijana watakaokuwa tayari kwa hiyari zao kujiunga kwa lengo la kuendeleza kilimo na kuwafanya vijana wajitambue na kuthamini kazi na hasa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa uwezeshaji ulikuwa na bado una lengo na nia njema kabisa lakini utekelezaji wake umeleta kero kuliko faraja hasa katika Wilaya ya Mpanda na Jimbo la Mpanda Kati likiwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda sana kupata maelezo ni vikundi vingapi Mpanda vimenufaika na fedha hizo, kadhalika na mtu mmoja mmoja na hasa wanawake. Naomba kupata maelezo pia wananchi wangapi vijijini katika vijiji vya Wilaya ya Mpanda wamenufaika na fedha hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitapenda kufahamu ni sababu zipi ambazo zilifanya pesa hizo kuchelewa kufika Mpanda hata Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Mpanda alielezwa kero hii na kuahidi kuwaona wenye mabenki kujua sababu. Pamoja na ahadi na juhudi za Mheshimiwa Rais watu wangapi wamefaidika baada ya ziara ya Mheshimiwa Rais mwezi Mei/Juni, 2007? Nashukuru sana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili karibu 50% ya watu ni vijana na hapo hapo karibu 60% ya ajira zipo kwenye *informal sector* na hivyo vijana wengi wapo kwenye *informal sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuboresha *informal sector* ili kuboresha maisha ya vijana kwa kuzingatia shughuli nyingi katika *informal sector* ni za uchuuzi na sio za *production.* Vile vile kuna haja ya ku-*link* mfumo wa elimu ili kijana aweze kujiajiri katika uzalishaji na sio uchuuzi. Lazima Wizara hii iwe na mipango, ijihusishe na Wizara nyingine kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingi vilivyokuwa vinaanzishwa na Baba wa Taifa vilikuwa na sababu au malengo makuu mawili:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kupata ajira  na pili, kuitayarisha Tanzania kuingia katika dunia ya viwanda lakini sasa vyote vimebinafsishwa kwa mfumo wa ubepari wa kupata *maximum profit.* Hivyo wakati wa ubinafsishaji hatukuwa makini tukijua kwamba sisi tulikuwa kwenye *central economy* na vile vile *private sector* ilikuwa haijaimarishwa hivyo wale waliokuwa wanafanya kazi kwenye viwanda hivyo kubaki bila kazi. Sasa hawa waende wapi? Wakati hata *state* haiwatambui?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndio sababu kubwa inayopelekea vijana kutoka vijijini na kukimbilia mijini kujaribu kutafuta ajira sababu ya mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya nguvu kazi inasemaje? Kuhusu vijana wengi waliopo vijiweni? Vijana hawa hasa wakati wa *campaign* wanatumiwa sana na wanasiasa lakini baada ya uchaguzi wanatimuliwa, je, hii ni haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali ichukue *social responsibility* ya hawa vijana kuwa na mipango wakifika miaka 18  kuanzia ngazi zote vijijini mpaka mikoani waelewe matatizo yao na jinsi ya kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusanya kodi, iwekeze vijijini na katika mifuko ya *social responsibility* hizo fedha ziangaliwe ni jinsi gani ya kuwasaidia watu wasiokuwa na kazi sio kukusanya tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizi *International Organisation,* ningependa kujua je! Ni wawekezaji au ni wanakuja kutoa misaada. Sababu wengi wamekuwa wakileta wafanyakazi wa ngazi za juu hata za kati kutoka huko, kazi ambazo zinaweza kufanywa na watanzania. Je, Serikali haioni fedha wanazodai wanaisaidia Tanzania si zinarudi kulekule zilikotoka nah ii ni njia ya kuwapatia watu wao ajira na kuacha watanzania bila ajira? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wamekuwa wakienda *VETA* kujifunza ufundi lakini cha kusikitisha *garage* nyingi za Wachina katika mji wa Dar es Salaam wamekuwa wakileta vijana kutoka China hata wa kupiga rangi magari na kadhalika, kazi hizi zinaweza kufanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, hii ndio sheria ya kazi? Wachina walete wafanyakazi wao kutoka China? Hawa vijana wa Kichina wanapataje vibali vya kufanya kazi na wale vijana wa Kitanzania wanaomaliza mafunzo ya ufundi *VETA*, Serikali ina mipango gani nao?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa michango yenu. Sasa tuingie katika sehemu ya pili, ambapo Wahesihmiwa Mawaziri, wataanza kutoa ufafanuzi kwa yale mliyoyazungumza.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara yetu ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Ninaomba kusema kuwa, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri mia kwa mia. *(Makofi)*

Ninamshukuru, naomba na kumpelekea salamu rafiki yangu Miriam, aliyekaa pale *Speaker's Gallery,* amejionea mwenyewe Dodoma yetu hii, mchana joto, usiku baridi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miriam ni mke wake, msije mkadhani ni mtu mwingine. Miriam ni mke wake. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapelekee salamu vijana wetu Kisali, Sioi, Masomi, Nasiwa, Arip na Lengaree. Ninaomba pia kuwapelekea salamu maalum, Wananchi wa Arumeru Mashariki. *(Makofi)*

Ninaomba kuwapongeza sana kwa kupata Halmashauri Mpya, baada ya kungoja kwa muda wa miaka 43 na ninaomba salamu hizi maalum ziwafikie kwenye Kata za Ngarenanyuki, Lekuruki, King'ori, Kikatiti, Majiyachai, Maroroni, Makeba, Kikwe, Mbuguni, Nkoanrua, Akheri, Ndoombo, Nkoarusambu, Seela/ Sing'isi, Poli, Usa, Nkoaranga na Songoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, kwa kuhakikisha kuwa, Naibu Mawaziri, tunaofanya kazi naye tunahusika na tunashiriki kikamilifu katika majukumu ya Wizara. Ninamshukuru sana Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, kwa ushirikiano wake wa hali ya juu. Ninamshukuru Katibu Mkuu, Dr. Ladslaus Komba, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Edin Mangesho, Wakuu wa Idara na Watendaji wengine wote wa Wizara, ikiwa ni pamoja na Maafisa wa Kazi wote walioko Mikoani kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mdogo, naomba niende kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, nianze kwa kuwashukuru sana kwa hoja zenu Waheshimiwa Wabunge, pamoja na ushauri ambao mmeutoa. Nianze na Daraja la Kigamboni. Kauli ya Serikali ni kuwa Daraja la Kigamboni litajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Mussa A. Zungu na Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi. Kwanza, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, anasema Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *NSSF* imetumia fedha nyingi kufanya upembuzi yakinifu, *NSSF* iwe msimamizi mkuu wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa Daraja la Kigamboni na itahakikisha kuna ufuatiliaji wa karibu. Majibu yetu ni kwamba, mapendekezo ya Mradi wa Daraja la Kigamboni tayari yameshafikishwa Serikalini.

Ninakubali kwamba, ujenzi wa daraja hili umechukua muda mrefu. Lakini Serikali ilianza mazungumzo dhahiri na Shirika la *NSSF* mwaka 2003. Mwaka ule ule 2003 Shirika la Hifadhi ya Jamii likatumia dola 20,000, ambazo lilipwa kwa Howard Humfrey, kufanya upembuzi yakinifu. Mwaka uliofuata 2004, wakaendelea zaidi wakafanya upembezi kwa kina kwa gharama ya dola 230,000 lakini mwaka 2005, Chama cha Mapinduzi kikaweka kwenye ilani yake kwamba, litajengwa. Kwa kuwa chama kimeahidi na kwa sababu sasa hivi tunatekeleza ahadi zetu, daraja litajengwa na kudhihirisha kwamba litajengwa, juzi tarehe 1 Agosti, 2007, nilijibu swali hapa Bungeni na nilisema kwamba, tayari Waraka wa Baraza la Mawaziri umeshatayarishwa. Waraka huo tayari umeshapita kwenye ngazi ya sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kamati ya Makatibu Wakuu tayari imepitia Waraka huo na umeshakamilika na sasa tunachongojea ni huo Waraka ufike kwenye Baraza la Mawaziri na pale Baraza la Mawaziri litakaporidhika, litamshauri Rais, aagize kuanza ujenzi wa daraja hili, basi daraja litaanza. Leo ni 2007, tunatarajia kufikia 2010, kama Chama kilivyosema kwenye Ilani, daraja litajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mussa A. Zungu, alitaka kujua gharama za daraja lenyewe. Gharama halisi za ujenzi wa daraja hili kwa sasa ni *Euro* milioni 45, ambazo ni sawa kwa sasa na shilingi bilioni 91. Lakini kati ya hizo; *Euro* milioni 22.5 zitatolewa kama msaada na Shirika la Misaada ya Serikali ya Uholanzi.

Pili, Mheshimiwa Mussa A. Zungu alisema kwa nini Wizara ya Fedha inakaidi maagizo ya Bunge na kukwamisha ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Hiyo niseme kwamba, hatukubaliani na nadhani Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana nasi kwamba, Wizara ya Fedha haikaidi na haiwezi kukaidi maagizo ya Bunge na haikwamishi ujenzi wa Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Maulidah Anna Komu anasema, *NSSF* inapata faida kubwa sana; kwa nini faida hiyo wasipewe wanachama; je, hizo fedha analipwa nani na (b) na (a) iko

kwenye Daraja la Kigamboni, lakini (c) mishahara ya wafanyakazi inakatwa kodi halafu inakatwa michango ya *NSSF*, mfanyakazi anapostaafu pensheni yake pia inakatwa kodi na anadai kwamba, huu ni uonevu, Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa kodi kwenye mafao. Tunaomba kumjibu kwamba, faida wanayopata *NSSF* inatumika kuboresha mafao ya wanachama wake. Kwa mujibu wa Kanuni za Hifadhi ya Jamii Duniani, faida zinazopatikana kwenye Mifuko ya Jamii kama *NSSF*, hutumika kuboresha mafao badala ya kugawa fedha taslimu kwa wachangiaji au wanachama. Halafu tunapenda vilevile kusema kuwa, kwa hivi sasa, mafao hayakatwi kodi. Mashirika ya Pensheni, yanakatwa kodi kwenye mapato ya vitega uchumi lakini mafao yale yanayokwenda kwa wanachama, hayakatwi kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa anasema, uwekezaji wa *NSSF* ulenge zaidi wanachama wake na jamii kwa ujumla. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iimarishwe na iwekeze kwenye nyanja hizo. Tunaomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, uwekezaji unaofanywa na *NSSF* unalenga zaidi miradi inayogusa jamii. Kwa mfano, ujenzi wa Jengo la Wamachinga kule Dar es Salaam na mengine ambayo yatajengwa baadaye, ujenzi wa nyumba za jeshi, ujenzi wa nyumba za polisi, Chuo Kikuu cha Dodoma, Makao ya TAKURU na kadhalika.

Halafu Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini; *NSSF* itekeleze azma ya Mheshimiwa Rais ya kuwekeza katika mikoa iliyo nyuma kimaendelea. *NSSF* inayo azma ya kuunga mkono jitihada zote za Mheshimiwa Rais, kwa kuwekeza kwa mikoa iliyo nyuma kimaendeleo. Lakini hata hivyo, utekelezaji wa miradi utategemea sana matokeo ya upembuzi yakinifu na miradi ya maeneo husika.

Mheshimiwa Richard Nyaulawa ameshauri, fedha za *NSSF, PPF* na kadhalika zitumike kutoa mikopo kwa Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa maghala na masoko vijijini. Tunashukuru na tunasema kwamba, ushauri huu ni mzuri, hata hivyo, utekelezaji wake utategemea uwezo wa Halmashauri husika, kurejesha mikopo.

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed anasema, Shirika la Tija la Taifa *(NIP),* wapatiwe ruzuku waweze kufanya kazi zao vizuri. Rai hiyo pia imetolewa na Mheshimiwa Anna R. Lupembe na Mheshimiwa Maulidah Anna Komu. Tunaomba tuseme kwamba, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, inaandaa Sera ya Tija, itakayoliwezesha Shirika la Taifa kutimiza majukumu yake vizuri zaidi kwa kusaidiwa na Serikali na wadau wengine. Maandalizi ya sera hiyo yako hatua za mwanzo.

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir na Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, wanaulizia kuhusu Kiwanja Namba 906/H kule Mbezi Beach, ambacho *NIP* inasemekana walinyang'anywa. Tunaomba kusema kwamba, Wizara ina taarifa na jambo hili na tayari tunalifuatilia, tumeandika barua Wizara ya Ardhi na tunategemea kwamba, itatujibu inavyostahili na *NIP* watapata haki yao. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Juma H. Killimbah, amesema kwamba sekta binafsi inawanyanyasa wafanyakazi. Napenda kutoa agizo kuwa unyanyasaji wa aina yoyote

katika ajira unakatazwa chini ya Sheria Mpya za Kazi. Anayenyanyaswa ana haki ya kuwasilisha malalamiko yake kwenye vyombo vinavyohusika ili sheria ichukue mkondo wake. Sheria ya Ajira na Mawasiliano Kazini, inatoa mwongozo juu ya saa za kazi na ulipwaji wa saa za ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, aliongelea kuhusu Lindi kufukuzwa kazi kwa Ndugu Juma Munga, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Legeza Mwendo Mlola. Tunaomba tukuhakikishie kwamba, tutafuatilia jambo hili na tutampa taarifa Mheshimiwa Mbunge ya matokeo ya ufuatiliaji wetu.

Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, anaomba Wizara iharakishe ukamilishaji wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii ili kulinda ushindani wa mifuko usio wa haki. Napenda nimtaarifu kuwa, mchakato wa Baraza la Mawaziri kuhusu kutungwa kwa Sheria ya Hifadhi ya Jamii, uko katika ngazi ya Kamati ya Makatibu Wakuu. Ikitoka kwenye ngazi hiyo itakwenda kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, ameuliza watu wenye ulemavu wanafaidika vipi na Sheria Mpya ya Kazi Namba 6 ya 2004, kuhusu kipengele cha kuzuia ubaguzi katika ajira. Naomba nimwambie kwamba, sheria hii inamzuia mwajiri kwa mujibu wa kifungu namba saba, kifungu kidogo cha nne, kumbagua mfanyakazi katika ajira wakiwemo walemavu. Kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Naomba nimjibu Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, kuhusu mishahara ya watumishi wa umma kutopitia kwenye Baraza la Mashauriano ya Pamoja. Tukiri kwamba, Baraza lilikwishaundwa Mei, 2007, wakati huo Tume ya Kurekebisha Mishahara ya Umma ilikwisha kamilisha kazi yake. Kwa utaratibu wa sheria yenyewe, isingewezekana kurudi nyuma na kuitisha Baraza hilo. Hata hivyo, Baraza linakutana katika robo tatu, kufuatana na sheria hiyo kwa ushauri, ambapo wakati wake sasa bado. Kwa hiyo, tunategemea kwamba, katika bajeti ya mwaka 2008/2009, itawezekana sasa kuwahusisha Baraza hili.

Kuhusu tatizo lile la Sheria ya Fidia, nimhakikishie vilevile Mheshimiwa Mohamed H. Missanga kwamba, sheria yenyewe iko kwenye hatua nzuri, imeshapita kwenye ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Kamati ya Makatibu Wakuu na sasa inasubiri kufikishwa mbele ya Baraza la Mawaziri. Mheshimiwa Rais akikubali basi hiyo sheria itaanza kufanya kazi kama itakavyopendekezwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao na narudia kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA – MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza, kusema wazi kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Baada ya maneno hayo, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wetu, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, kwa malezi anayotupatia sisi wasaidizi wake. Lakini vilevile niwashukuru Naibu mwenzangu Mheshimiwa Jeremia S. Sumari, Katibu Mkuu wa

Wizara yetu, Dr. Ladislaus Komba na Naibu Katibu Mkuu, Mama Edin Mogesho, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nitumie nafasi hii, kuendelea kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Songea Mjini, kwa ushirikiano ambao wananipa katika kutekekeleza majukumu ya kila siku ya jimbo lile. Naomba vilevile niwahakikishie wananchi hawa wa Songea Mjini kwamba, kwa kweli nafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba, Waziri wa Nishati na Madini, anakosa usingizi mpaka umeme utakapopatikana Songea Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa niende moja kwa moja kwenye hoja...

**NAIBU SPIKA:** Washukuru uliowaarika hapa, mke wako na watoto. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA – MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliona Wabunge wanamuangalia sana mke wangu, kwa hiyo, nikasema nisitazame sana. Natumia nafasi hii kwa niaba yangu mwenyewe na maelekezo ya Naibu Spika, kumshukuru sana kwa kuacha kazi nyingine, kuja kushiriki zoezi la leo. Lakini vilevile nawashukuru wazazi wangu, kwa kutumia nafasi hii kuja kumwona mtoto wao akifanya kazi hii ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, niende moja kwa moja sasa kwenye hoja. Nitaanza na hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, yeye aliona tatizo la UKIMWI na kulihusianisha na mbio za mwenge. Nitumie nafasi hii kumhakikishia kwamba, mbio za mwenge zinafanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakumbuka miaka michache iliyopita, yalitokea malalamiko sehemu ambayo mwenge ulilala kwamba, siku chache baadaye watu walikuta maganda mengi ya kondomu. Nadhani huo ni ushahidi wa kutosha kwamba, mafunzo yalieleweka vizuri katika eneo lile. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nijibu hoja yake kuhusu kugawa eneo la Sasanda. Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, amekuwa na changamoto kubwa ya kutaka eneo la Sasanda ligawanywe ili wananchi wa kule waweze kulitumia kwa shughuli zao. Changamoto ya Mheshimiwa Mbunge imetokana na kuona eneo lile halitumiki ipasavyo na Serikali. Nataka nimwambie kwamba, changamoto aliyoifanya kwa Serikali, imefanya tufanye kazi kubwa kuhakikisha kwamba, kituo kile kinafanya kazi iliyokusudiwa na ndiyo maana mwaka huu unaoisha, tulitenga shilingi milioni 25.8 na ukarabati wa eneo lile unaendelea na mwaka ujao wa fedha tumetenga shilingi milioni 59,750,000 ili kuona kwamba kunatokea mabadiliko makubwa, ambayo yataboreshwa yatasaidia sio tu wananchi wa Mbozi, lakini pia wananchi wa maeneo mengine ya nchi yetu na hivyo kuwa na manufaa kwa nchi nzima badala ya kuwa na manufaa kwa eneo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, alitaka kujua namna tutakavyofanya ili Mfuko wa Vijana ufahamike zaidi. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake ya kuwasilisha bajeti, mpango wetu ni ule wa kuhakikisha kwamba, sio tu fedha zinawafikia walengwa, lakini zinawafikia walengwa ambao wameandaliwa vizuri na ndiyo maana tumechagua *option* ya kutumia *SACCOS* pia katika mpango unaokuja. Katika jambo hili, tutahakikisha kwamba, elimu inatolewa ya kutosha na Mfuko huo unaelimishwa vya kutosha.

Mheshimiwa Lucy F. Owenya katika mchango wake aliongelea umuhimu wa sekta isiyo rasmi katika uzalishaji mali. Nataka nikubaliane naye kwamba, sekta hii ni muhimu na hasa ikitumika zaidi katika eneo la uzalishaji mali, badala ya kuwa watu wa kati. Kwa hiyo, Serikali itashirikiana kikamilifu na wale wote wenye mawazo ya kusaidia katika kiwango hicho na hasa wadau wa elimu na kuhakikisha kwamba, elimu inayotolewa nchini inakuwa na uhusiano au inaoanishwa na mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Lucy F. Owenya, vilevile aliongea kwa uchungu kuhusu vijana wa vijiweni, ambao wamekuwa wakikaa bila shughuli za maana. Nataka niseme kwamba ni msimamo wa Serikali kwamba, vijana kukaa bila shughuli yoyote ni jambo la aibu, vijana wakishatambua hilo, mambo mengine yanafuata, hapo hamasa kuhusu shughuli za uzalishaji mali inawezekana na hapo inawezekana vijana wakaanza utaratibu wa kujiwekea akiba kidogo kidogo na wataweza pia kukopesheka. Kwa hiyo, changamoto hii tumeichukua na tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Lucy F. Owenya, ameongea kwa masikitiko, Wachina wanaofanya shughuli ambazo anaamini Watanzania wangeweza kuzifanya na hasa vijana waliosoma *VETA.* Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kufanya kazi kwa karibu na Kamati ya kugawa vibali kuhakikisha kwamba, zile nafasi ambazo Watanzania wana uwezo nazo, hazipewi watu kutoka nchi nyingine. Kwa hiyo, tutachukua hatua kila inavyowezekana, kuhakikisha vibali vinatolewa kwa umakini zaidi na wale ambao wamepata kwa bahati mbaya, utakapofika muda wa ku-*renew*, hatutatoa upya vibali hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Said A. Arfi, aliongelea haja ya kuwa na Kambi za Vijana ambazo zitawafundisha vijana kilimo na kuwafanya watambue umuhimu wa kazi. Kimsingi tunakubaliana naye moja kwa moja kwamba, hilo ni jambo la msingi na tutashauriana namna ya kulifanya kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Said A. Arfi, aliongelea habari ya vijana wa kijiweni. Naomba nirudie yale yale niliyosema kwa Mheshimiwa Lucy F. Owenya kwamba, tunatambua kwamba vijana kukaa vijiweni hakuna tija kwa taifa, tutafanya kazi ya ziada kuona kwamba, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali kulipunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, aliuliza nini mpango wa Serikali kwa vijana ambao hawana elimu ya chuo kikuu na ambao hawana elimu kabisa, ambao wakiachwa wanaendelea kupata madhala na hawawi na faida yoyote kwa Taifa? Nasema msimamo wa Serikali ni kama nilivyosema, tutaendelea kuimarisha mafunzo ya kati kama ufundi tuliyoyasema lakini vilevile tutaendelea kusisitiza uundwaji wa vikundi, pamoja na *SACCOS* na kuimarisha Mfuko wa Vijana. Lakini vilevile tutaendelea kutoa mafunzo kwa nguvu kuhusu umuhimu wa watu kutunza fedha, kujua mgawanyo wa fedha katika uwekezaji katika kuweka akiba na kujua eneo la kutumia, ili watu mwisho wa yote, wajue wanatumiaje rasilimali kidogo walizonazo kwa faida yao na kukuza kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya aliongea kwa uchungu kuhusu maadili ya jamii yetu kuporomoka. Naomba niseme kwamba ni msimamo wa Serikali kwamba, maadili ya jamii hayawezi kurekebishwa kwa nguvu ya dola. Maadili ya jamii yataweza tu kurekebishwa kwa watu kukubaliana kuendelea kuelimishana bila kuchoka na kutimiza wajibu wake kuelimisha mtu aliye karibu naye. Bila kufanya hivyo, hatutapata mafanikio yoyote. Hakuna sehemu duniani ambapo nguvu za dola zimefanikiwa kubadili maadili au utamaduni wa eneo hilo.

Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, aliongelea umuhimu wa vijana kuandaliwa kujiajiri na kupewa mafunzo yanayoweza kuwafanya wawajibike. Tunakubaliana naye moja kwa moja, tutashirikiana kuhakikisha kwamba, jambo hili linafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa aliongelea umuhimu wa elimu ya mafunzo ya ufundi kwa shule za msingi na sekondari. Nataka niseme tumeipokea hii changamoto, tutashauriana na Wizara zinazohusika, kuona wanaweza kufanya nini ili mitaala hii iweze kuingizwa katika utaratibu wao na kuleta faida kwa taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maulida Anna Komu, aliongelea umuhimu wa kuona kama tunaweza kuandaa vijiji maalum vya vijana na kuwapa mafunzo na waweze kukopesheka, ili baadaye waweze kulipa mikopo hiyo katika muda fulani. Nataka kusema, Wizara inaona wazo lenyewe ni jema tutalitafakari, kulifanyia kazi na kuona kama tunaweza kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, aliongelea kutenga maeneo ya vijana kwa ajili ya biashara. Nataka nimthibitishie kwamba, Wizara yetu itashirikiana na Halmashauri za Wilaya, pamoja na TAMISEMI, kuona namna ya kulitekeleza jambo hili kwa ufanisi. Jambo hili limekuwa likiendelea kutekelezwa, nadhani mkazo ni katika kufanya litekelezwe kwa kasi na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, aliongelea umuhimu wa Jengo la Wamachinga litakapokuwa limekamilika pale Dar es Salaam, kuhakikisha walengwa ndiyo wanapata nafasi katika jengo hilo. Nataka nimhakikishie kwamba, Waziri Mkuu wakati akiongelea ujenzi wa jengo hili, aliweka wazi kwamba, Serikali haitakubali utaratibu wowote wa ujanja ujanja katika jengo lile na kwamba walengwa ndio watakaopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, aliongelea pia taarifa za mikopo ya vijana na uhamaishaji ufanywe kwa nguvu zaidi. Tunakubaliana naye na tunakubalina naye pia katika umuhimu wa kutoa mafunzo kwa vijana.

Mhehsimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, aliongelea umuhimu wa masomo ya kuwawezesha vijana. Tunakubaliana naye moja kwa moja, ndiyo maana katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alisema wazi kwamba, moja ya mikakati yetu mwaka huu ni kuhakikisha kwamba, mafunzo yanapewa kipaumbele cha kutosha kutokana na Mfuko wa Vijana.

Mheshimiwa Pindi H. Chana, aliongelea umuhimu wa *Labour Exchange Centre* kuwepo katika maeneo mbalimbali na hasa katika Mkoa wa Iringa. Naomba niseme kwa sasa *Labour Exchange Centre* tumezijenga katika Mikoa ya Mwanza na Dar es Salam, kwa ajili ya Kanda ya Ziwa, pamoja na Kanda ya Mashariki. Kanda zitakazofuata ni Mbeya na Dar es Salaam. Mbeya kwa ajili ya Nyanda za Juu Kusini na Dodoma kwa ajili ya Kanda ya Kati. Kwa sasa wakati tukiendelea kujitahidi kuona kwamba huduma hii inafika kila mahali, watu wa Iringa watatumia Kanda ya Mbeya itakapokuwa inafanya kazi yake vizuri na imekamilika.

Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu na Mheshimiwa Lucy F. Owenya, wote kwa pamoja waliongelea kwa kina sana kuhusu vibali vya kazi, kupewa wageni kwa nafasi ambazo Watanzania wanazo. Naomba nisisitize tena kwamba, tutaendelea kusimamia kwa karibu, kuhakikisha kwamba, Watanzania ndiyo wanafanya kazi ambazo wana ujuzi nazo na wageni watakuja nchini kwa nafasi ambazo hatuna wataalam wake tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, aliongelea habari ya kata ya Ilonga kuwa na Kituo cha Vijana na yeye kuwa tayari kusaidia. Naomba nimshukuru sana kwa niaba ya Wizara, kwa kuwa tayari kusaidia kituo hicho cha Ilonga na tutashirikiana naye kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Michael L. Laizer, yeye aliongelea umuhimu wa kushirikiana naye katika kazi za jimbo lake na amepongeza ambavyo tumekuwa tukifanya naye kazi kwa karibu. Namhakikishia kwamba, ataendelea kupata ushirikiano wetu na tutafanya naye kazi kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Asha Mshimba Jencha, alitupongeza kwa kuhamasisha vijana wa kiume na wa kike kujiunga na *SACCOS.* Nasema tutaendelea kushirikiana naye na tutazingatia ushauri wake wa kuweka mkakati wa kuhamasisha vijana kujiunga na *SACCOS* zenye wanachama wengi wa jinsia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Juma H. Killimbah, alitaka Serikali itoe tafsiri sahihi kisheria kuhusu umri wa kijana. Kwa mujibu wa Sera ya

Vijana ya Taifa ya mwaka 2007, umri wa kijana wa Tanzania ni kuanzia miaka 15 hadi 35. Hivyo, umri wa kijana ni miaka kati ya 15 hadi 35 kwa mujibu wa sera hiyo.

Mheshimiwa Juma H. Killimbah, pia alitaka kujua vijana wasio na elimu na maisha yao vijijini ni wangapi. Kwa sasa ni vigumu kupata takwimu ya vijana wasio na elimu na wanaoishi vijijini, lakini vijana wengi wa Tanzania, wanaoishi vijijini elimu yao ni darasa la saba kwa walio wengi, japo wengi hawakufika darasa la saba na wengine wana elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, alitaka kujua pia lini Wizara itakuwa na Maafisa wa Vijana kila Wilaya na Wilaya ya Iramba itapewa lini Afisa wa Vijana? Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 34 Tanzania Bara ni 1,770,000 na wanawake 6,218,000. Kwa mujibu Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 34 Tanzania Bara ni 11,770,532, ambapo kati ya hao wanawake ni 6,218,238 na wanaume 5,552,294.

Wizara tayari imewasiliana na TAMISEMI, kuhusu ajira ya Maafisa wa Vijana wa Wilaya na tayari ilishaandaa *scheme of service* na kuiwakilisha Ofisi ya Waziri Mkuu. Mawasiliano baina ya Wizara yangu na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, yanaendelea. Aidha, baadhi ya ofisi zimeshaajiri maafisa hao mfano, Mufindi na Manispaa ya Shinyanga. Manispaa ya Shinyanga tayari imetangaza ajira ya afisa vijana. Wakati utaratibu huu unatekelezwa, Wizara zote zimeombwa kuteua ofisa anayeshughulikia masuala ya vijana kwa muda, wakati utaratibu ukiendelea kuwekwa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, aliomba kujua utaratibu wa zamani wa kuwa na wakaguzi umeishia wapi na ametaka urejeshwe ili waajiri waweze kukaguliwa ipasavyo.

Mhehsimiwa Naibu Spika, suala la ukaguzi lipo katika taratibu zetu za kazi. Kutokana na uhaba wa maafisa na vitendea kazi na hasa vya usafiri, ndio maana shughuli hii haikuweza kufanyika. Sasa Wizara ipo katika hali ya kuweza kufanya kaguzi hizo, kwa kushirikiana na taasisi nyingine. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba, kwa sasa tumejizatiti kikamilifu, kuweza kutekeleza kaguzi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, yeye aliulizia namna gani Wizara inaweza kushirikiana na *SIDO* kwa kutumia mikopo ya awali na ya pili. Naomba nimhakikishie kwamba, *SIDO* inahusishwa katika kutoa mafunzo mbalimbali kwa ajili ya wajasiliamali. Huu ni upungufu uliokosekana hapo awali, lakini sasa unafanyiwa kazi vizuri.

Mheshimiwa Castor R. Ligallama, alitaka kujua vijana wengi hawakupata fursa ya kukopeshwa kutokana na benki nyingi kuwepo vijijini na ametaka jitihada zifanywe. Ninakubaliana naye kwamba ni kweli vijana wengi hawakuweza kunufaika katika utaratibu wa awali na kutokana na matatizo mbalimbali yaliyojitokeza, upungufu huu utazingatiwa katika mpango wa pili, kwa kuhusisha mpango wa fedha ambazo zinaweza kufika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa William H. Shellukindo, alitaka uwepo utaratibu wa ukaguzi wa ajira zinazopatikana na jinsi zinavyopotea. Ushauri huu ni mzuri, kwa kuwa na taratibu za kuweka kumbukumbu za ajira zinazozalishwa na zinazopotea. Ni kwa njia hii, tunaweza kufahamu hali ya ajira na mwelekeo wake, wakati tafiti na chunguzi za ajira zitakapokosekana kufanyika, Wizara ya Kazi tayari imewasiliana na taasisi binafsi na Serikali za Mitaa ili waweze kuleta taarifa za ajira na uajiri.

Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, aliongelea habari ya wageni kufanya kazi mahotelini si halali, kwani wanachukua nafasi ya vijana wetu, Waganda na Wakenya wanajifanya hapa kama kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wageni kwenye mahoteli wameajiriwa kutokana na mahitaji halisi ya ujuzi unaotakiwa na vilevile kwa lengo la kuvutia watalii na kutoa ujuzi kwa wazalendo ambao hawakubahatika kuupata. Uajiri holela wa kigeni unadhibitiwa, kwani unapunguza nafasi za kazi kwa Wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis kwamba, tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu jambo hili kuhakikisha kwamba, mahoteli yanaajiri vijana wetu kwa kadri inavyowezekana na kwa sifa walizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, natumia nafasi hii sasa kurudia kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, hasa wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa katika kutekeleza majukumu yetu lakini vilevile nawashukuru Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, kwa jinsi ambavyo tunashirikiana kwa karibu katika kutekeleza majukumu ya nchi yetu. Ninawahakikishie kwamba, tutaendelea kuwapa ushirikiano kwa kadri inavyowezekana na tutashirikiana kufanya kazi za Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado napenda niwashukuru kwa dhati kabisa, Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii, kwa kusema moja kwa moja au kwa kuandika. Hoja tunazipokea tutazifanyia kazi na tutazijibu kwa maandishi, kwa sababu muda hapa hautoshi kujibu hoja zote zilizotokea. Sasa kabla sijawatambua wale waliochangia kwa maandishi na kwa kusema, nimalizie shukrani zangu ambazo asubuhi muda haukutosha.

Napenda niwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Dr. Komba, Naibu Katibu Mkuu, Bi. Mangesho, Wakuu wa Idara zote na watumishi wote wa Wizara, wakiwemo dereva wangu, Mr. Mushi na mhudumu, Bi. Zainab, kwa jinsi tunavyoshirikiana kufanya kazi katika Wizara ile na hasa mimi kwa sababu nilikuwa ni mgeni, wamenisaidia sana kuilewa Wizara kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuwashukuru Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu, yaani Dr. Dau kwa upande wa *NSSF*,

Bwana Kasenge - *NIP*, Bwana Kitumbo – (OSHA), Bwana Msigwa (CMA) na Bodi mbalimbali ambazo zinashirikiana na Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii, kuwashukuru washirika wetu wote ambao kwa namna mbalimbali, wametuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu na kwa njia ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Ushauri kwa masuala ya Kazi na Uchumi, yaani *LESCO*. Vilevile nawashukuru Shirikisho la Uajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi *(TUCTA),* kwa michango na ushauri wao mzuri wanaonipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kwa ushirikiano wanaonipa asubuhi walikuwepo hapa walitambulishwa. Nawashukuru kwa uchapaji kazi wao, kwa sababu katika muda mfupi wameweza kujenga Shule za Sekondari 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru vilevile kwa uvumilivu wao kwa sababu muda mwingi hawanioni, nikiwa nashughulika na masuala mengine ya Kitaifa lakini nataka niwahakikishie kwamba, nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kwa nguvu zangu zote. Nawashukuru wahisani mbalimbali, ambao wanatusaidia ikiwemo nchi ya Denmark, Benki ya Dunia, *ILO*, *UNDP*, *UNICEF*, *UNFBA*, *CYP* na *TACAIDS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, sasa napenda niwatambue Wabunge waliochangia ni wengi, naomba kengele isimame kwa sababu ni wengi kweli kweli.

**NAIBU SPIKA:** Muda hauwezi kusimama wewe endelea.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kusema ni Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Laus O. Mhina, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, vilevile Manaibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari na Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuandika wako karibu 60, nao ni Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Anna M. Komu,

Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Mwanne I. Mwachemba na Mheshimiwa Mohamed S. Sinani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Grace S.Kiwelu, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa James D. Lembeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Mustapha H. Mkulo, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Benadetha K. Mshashu na Mheshimiwa Juma A. Njwayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitazungumzia baadhi ya maeneo ambayo yameguswa na Wabunge wengi bila kuwataja. Eneo moja ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi ni suala la kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi. Hili ni tatizo la kweli na Serikali tunakiri kwamba, kima hiki cha sasa wanacholipwa wafanyakazi katika sekta binafsi cha Sh.48,000 kwa wafanyakazi wa mijini na Sh.35,000 kwa wafanyakazi wa vijijini, kiliwekwa mwaka 2002, kimepitwa na wakati na hakikidhi kabisa, hilo tunalikubali. Sasa sheria za sasa hivi za kazi zinasema, kima cha chini katika sekta binafsi kipendekezwe na bodi za kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kama Waziri mwenye Dhamana ya kuunda Bodi hizi, nimeshaziunda tayari na sasa hivi ziko kazini. Nimewaambia robo ya mwaka huu wa fedha ya kati ya sasa na Septemba, wawe wameshapita katika sekta zile nane, kila watu na sekta yao, wameshafanya utafiti, wameshazungumza na wadau wa sekta ile kwa maana ya waajiri na wafanyakazi na waniletee mapendekezo ili niweze kuyatangaza. Kwa hiyo, naomba wafanyakazi katika sekta binafsi, tatizo lipo kweli lakini tunashughulikia kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wao sasa hivi wajiandae kukutana na zile Bodi. Wajiandae kwa takwimu na *data,* wazungumze na hizi Bodi kama ambavyo waajiri nao watajiandaa, kwa sababu watatazama katika kila sekta, uzalishaji ukoje na tija ikoje. Wanaweza kulipana vipi ili huo muafaka waniletee mapema iwezekanavyo niweze kutangaza ili tuwaokoe wenzetu hawa ambao kwa kweli mishahara iko chini kabisa.

Kwa hiyo, hizi ndizo hatua ambazo Serikali tunazichukua kushughulikia marekebisho ya kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili limezungumzwa na watu wengi sana, nalo ni mikopo ya wajasiriamali, mikopo hii au Mfuko huu wa uzalishaji ni mpya mwaka uliopita ulikuwa ni mwaka wetu wa kwanza na kitu kipya wakati wote kinakuwa na matatizo. Kwa hiyo, naomba Watanzania wenzangu tuwe na subira, kwa sababu wengine wakizungumza huko mitaani, kwenye magazeti, inaonekana kana kwamba, utaratibu huu umeleta kero zaidi kuliko kutatua. Wengine wanasema sisi tutavunja hata *SACCOS* zetu, nasema huko ni kukosa subira, matatizo yapo lakini jinsi Mfuko huu tunavyoenda nao kwa sababu si Mfuko wa mwaka mmoja, huu ni mfuko endelevu tutaenda nao mpaka miaka mitano iishe, tutaenda tunaboresha Mfuko huu.

Tatizo moja kubwa limekuwepo la uelewa tu, walengwa wenyewe kuelewa taratibu za kukopa, wale maafisa wanaotakiwa kushughulikia kule kwenye vijiji na kata walikuwa hawaelewi wafanye nini. Maafisa wa benki wenyewe, kwa sababu ni jambo jipya vilevile mwanzoni kulikuwa na mkanganyiko, hata sisi kwa upande wa Serikali, lakini jinsi tunavyoenda, tumetoa elimu ya kutosha na tutaendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wote walengwa, watu wa mabenki na watu wa kata na vijiji na sisi kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo lingine lililojitokeza katika mwaka wa kwanza ni kwamba, baadhi ya maeneo hayakuweza kufikika kwa sababu mbalimbali na moja ni *NMB* katika baadhi ya wilaya hasa wilaya mpya hawapo. Kwa hiyo, wale watu wa wilaya zile ambazo hazina *NMB* wala *CRDB* katika mwaka wa kwanza limekuwa ni tatizo, japo tuliwaambia kwamba, waende kwenye wilaya ya jirani ambayo ina benki, lakini itakuwa ni mbali. Lakini vilevile hata pale penye *NMB,* katika mwaka huu wa kwanza wamekuwa na maofisa wachache wa mikopo, halafu wamekuwa wanashughulikia eneo kama kilometa 20 kuzunguka Makao Makuu ya Wilaya.

Kwa hiyo, maeneo ya vijijini katika mwaka wa kwanza hayakuweza kufikika. Nashukuru baadhi ya maeneo, walifanya ubunifu yule Meneja wa Benki akazungumza na *DC* na *DED,* wakampatia gari kwa sababu hawana magari hawa *branch managers* wakaenda mpaka vijijini mbali, lakini waliofanya maarifa hayo siyo wengi. Kwa hiyo, katika mwaka wa pili, eneo la wale ambao hawakufikiwa, tunaliboresha kwa kuingiza sasa katika utaratibu wa asasi ndogo ndogo nilizozisoma katika hotuba yangu pale asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila mkoa na kila wilaya kutakuwa na asasi ndogo ndogo za kifedha ambazo sasa hizi ndizo zitafika mpaka vijijini na Benki Kuu ambayo ndiyo inaratibu hizi asasi ndogo ndogo, imeomba Mamlaka za TAMISEMI kule kwenye wilaya ya mikoa, wapelekewe hizo asasi ndogo ndogo ambazo pengine watu wa benki hawazijui ili wazifanyie uchunguzi na wazitazame uwezo wao. Kwa hiyo, zikishateuliwa na sasa hivi wako katika hatua ya kuzitambua kukamilisha, watawapa mafunzo jinsi ya kufanya kazi hii na vilevile wataingia mkataba wa namna ya kufanya

kazi hii na na ziko shilingi bilioni 10.5 ambazo asasi ndogo ndogo zitapewa, zikakopeshe huko vijijini ambako mabenki katika mwaka wa kwanza hawakuweza kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine katika mwaka wa kwanza limekuwa ni hofu tu kwamba, tumesema wastani wa shilingi bilioni moja kila mkoa, kwa hiyo, kuna hofu kwamba, baadhi ya mikoa inaweza ikachukua hela nyingi zaidi kwa sababu wamezichangamkia haraka zaidi na baadhi ya mikoa kwa sababu hawakuzichangamkia haraka haraka wanaweza wakakosa. Tuliwaleta hapa mameneja wa benki zote mbili; Benki ya *NMB* na Benki ya *CRDB* katika Bunge hili hili katika semina maalumu na wakatuhakikishia kwamba, shilingi bilioni moja kila mkoa zipo, kwa sababu ndio kauli ya Serikali. Hivi tunapoongea kuna mikoa karibu sita wameshamaliza migao yao; Mkoa wa Mbeya wamepata shilingi 1.4, Mkoa wa Dar es Salaam wameshamaliza mgao wameshakopa shilingi 2.1, Mkoa wa Kagera wameshamaliza mgao wameshachukua shilingi 1.7, Mkoa wa Morogoro wameshamaliza mgao wao wameshachukua shilingi bilioni moja, Mkoa wa Mwanza wameshamaliza mgao wao wameshachukua shilingi bilioni moja na Mkoa wa Pwani wameshamaliza. Kwa hiyo, hawa kwa sasa hivi mikoa hii inasimama kwa sababu mgao wakiendelea kukopa watachukua na wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito katika ile mikoa iliyobaki kwamba, zile Kamati za Mkoa, Wilaya mpaka kwenye Kata, washirikiane na Mameneja wa Benki zinazohusika huko ili kuharakisha utaratibu wa kukopesha. Baadhi ya Mameneja wa Benki kwa kutokuelewa, tuliposimamisha pale kwamba sasa maombi yameshakuwa mengi zaidi wasimame, hata wale ambao walikuwa na maombi machache nao wakasimama. Tunasema hili ni kosa, kwa ile mikoa ambayo bado wana hela, waendelee kupokea tu maombi kwa sababu hela zipo, kwa mfano, Mkoa wangu wa Singida, mkiangalia kwenye jedwali mpaka sasa tumeshakopa shilingi milioni 230 tu, kwa hiyo kuna karibu milioni 800 ambazo zipo pale kwa ajili ya kukopa wakope. Nataka kutoa wito katika ile mikoa ambayo bado ina mgao wao, wakae na Mameneja wa Benki na tutaongea na Mkuu wa Benki yao vilevile ili na yeye asaidie kuharakisha mikopo. Kwa hiyo, ile hofu kwamba baadhi ya mikoa itapata nyingi mikoa mingine itakosa, Waheshimiwa Wabunge nataka kuiondoa kwamba hiyo haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo lilikuwa linalalamikiwa ni hili la kupeana taarifa. Waheshimiwa Wabunge wanasema, sisi tunaenda pale tunataka taarifa wangapi wameshakopa katika jimbo langu, katika wilaya yangu, hatupewi taarifa. Hili ni tatizo, ni kweli lipo tatizo na si Wabunge tu, hata Wakuu wa Wilaya vilevile wanalalamika, tulikubaliana nao walisema benki wana taratibu zao na maadili ya kibiashara kwamba, hawawezi wakatoa tu taarifa kwa kila mtu. Kwa hiyo, tulikubaliana kwamba taarifa zote kila mwezi watazitoa Benki Kuu, Ofisi ya Waziri Mkuu katika Wizara ya Mipango, Wizara ya Fedha na Wizara yangu.

Wizara yangu ndiyo itasambaza hizi taarifa kwa mikoa na wilaya na mimi nilikuwa nimejitahidi sana kila mwezi kuwapelekea hizi taarifa Wakuu wa Mikoa, ambayo inaonesha kiasi gani wamekopa katika tawi fulani katika mkoa wake, wangapi wamekopa, bado shilingi ngapi kila mwezi. Kwa hiyo, utaratibu wa kupeana taarifa ni kutoka Wizara kwangu, kwa Wakuu wa Mikoa halafu ndiyo inateremka kule chini, kwa

sababu mabenki walisema si vizuri hizi habari wakawa wanampa kila mtu, kwa sababu wana maadili yao ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hivi ndiyo hali ilivyo kuhusu mikopo ya ujasiriamali na kama nilivyosema, Wabunge wanasema tunaulizwa nani amekopa, kwenye taarifa tumeonesha mkoa kwa mkoa waliokopeshwa na jumla ya watu 27,000 wameshapata hiyo mikopo, hawa ni watu ambao bila utaratibu huu, wasingepata mkopo wowote kwa sababu hawana dhamana hawa. Ni mafanikio makubwa kabisa, hawa ni watu wamefika benki na wamepata mikopo kupitia utaratibu huu, kwa utaratibu wa kawaida hawa watu karibu 30,000 ni wengi, wasingepata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mwaka wa kwanza pamoja na matatizo yote haya, lakini bado nasema kwamba, jitihada nzuri zimefanywa, wananchi wasikate tama, huu mpango unaendelea na tunaendelea kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa hasa na Kambi ya Upinzani ni uundaji wa Baraza la Vijana. Kwanza, nataka kumhakikishia Msemaji wa Kambi ya Upinzani, maana katika hotuba yake alisema, nyie mlienda Tanga mkachagua watu wachache, mnaanza kuunda Baraza. Baadhi ya watu wakaeneza katika mtandao tena kwa lugha ambayo siyo ya Kitanzania, sasa unajiuliza huyu ni Mtanzania au mtu wa wapi huyu? Imeandikwa lugha ambayo siyo ya Kitanzania kabisa kuhusu ule Mkutano wa Tanga. Nataka kusema kwamba, Mkutano wa Tanga haukuwa wa kuunda Baraza la Vijana, ulikuwa ni mkutano wa kawaida, ambao ulikuwa umeitishwa na *UNICEF*. *UNICEF* wana mikoa tisa ambayo wanai-*support* katika miradi mbalimbali na katika kampeni mbalimbali za UKIMWI na miradi ya maendeleo, walikuwa ndio wameitwa pale na katika mkutano ule jumla ya wilaya karibu 19 zilienda ambazo ziko katika eneo la *UNICEF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya *agenda* pale walipewa taarifa kuhusu sera ya vijana, ambayo imeshapitishwa, sasa ndani ya ile sera upo uundaji wa baraza, lilitajwa tu kwa sababu ilikuwa ni moja ya mambo ambayo yapo ndani ya ile sera. Kusema kweli kile kikao hakikuwa kwa ajili ya kuunda Baraza la Vijana, Baraza la Vijana kama mnavyojua historia yake, Wizara tumeanza kulishughulikia tangu mwaka 1998 na 1999 lilifanyika kongamano la vijana, lililoshirikisha vijana wote na vyama vyote vya siasa vilishiriki. Vijana mbalimbali kule Iringa wakaunda kamati yao ya watu 15, wakapitia katiba ya hilo baraza na wakasema kwamba, baraza hili lipate nguvu ya kisheria, kwa hiyo, lifike katika Bunge na sisi tukakubali na Muswada ukaandaliwa wa kuunda baraza kisheria kupitia Bunge.

Tulivyoanza sasa ule mchakato wa ule Waraka ulipofika kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu, wakasema kwa nini sheria inatangulia kabla ya sera? Tungoje sera kwanza halafu sheria ije itekeleze sera. Kwa hiyo, hapo ndiyo ikasimama, sasa sera imeshapita tayari, tutakachofanya sasa hivi, tutawaita tena vijana, tutawashirikisha ule Waraka ambao tumeuboresha, ulingane na sera ya sasa. Tutawaita vijana katika *forum* mbalimbali, waujadili ule Waraka, tukikubaliana nao sasa tuanze mchakato wa kuuleta katika Bunge na sheria ipite na baraza liundwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili halina ujanja, wala uficho, litaenda kwa uwazi. Nataka niwahakikishie vijana wa nchi nzima kwamba, jambo hili tunalipeleka kwa uwazi kabisa na tutawashirikisha vijana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba utuweke sawa, vijana watajadili Waraka au rasimu?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, watajadili rasimu, haijaletwa kwenye vikao. Kwa sababu ndio wadau wakuu wa jambo hili, nataka kuwahakikisha kwamba, tutawashirikisha katika kukamilisha ile rasimu na tukishakubaliana sasa, ndio tutaileta katika vikao rasmi na baadaye mpaka kwenye Bunge sheria ipitishwe ili tuunde hilo Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la sheria mpya, baadhi ya Wabunge wamesema sheria hizi zilipitishwa mwaka 2004, kwa maana ya sheria Namba 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria Namba 7 ya Taasisi za Kazi kwamba, tangu 2004 zimechelewa kuanza kufanya kazi, zimeanza Mei, 2007. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba ni kweli sheria zile tulizipitisha 2004 na ni kweli kama kaka yangu, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga alivyosema, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais alitia saini mapema tu lakini kazi iliyofuata ilikuwa ni kutunga sheria na kanuni. Kanuni hizo ni nyingi, kila kipengele kina kanuni na kanuni ni nyingi kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hicho ndicho kilichochelewesha na mimi nilipoenda pale Wizarani Oktoba, 2006, nilikuta hilo tatizo ambalo wenzangu walishaanza kupambana nalo, Mawaziri walionitangulia, lakini nikakuta Mawaziri wenzangu wameshafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nilienda kumalizia tu. Kwa hiyo, mwezi Desemba tarehe 20, ndipo nikatamka kwamba, sheria hizi zitaanza kufanya kazi kama sheria inavyosema, siyo Mei, 2007 kama alivyosema msemaji, ni Desemba tarehe 20 na *GN* ikatoka Januari tarehe 2005, ndiyo sheria zikaanza kufanya kazi. Sasa hivi karibu Taasisi zote zinazotakiwa ili sheria ifanye kazi, tayari zipo na zimeanza kufanya kazi, pamoja na *CMA*, ile *commission* ya usuluhishi na uamuzi ni kweli Mheshimiwa Mbunge alisema, lakini sasa hii inaonekana ipo Dar es Salaam tu, hapana, ile *CMA* iko katika vituo sasa hivi 11 katika mikoa mbalimbali, kwa hiyo, si kwamba iko Dar es Salaam. Nia yetu katika mwaka utakaofuata, tutasambaza hivyo vituo ili walau mikoa ya jirani iweze kuchangia kituo kimoja, lakini nia yetu hatua kwa hatua, tuweze kufika katika mikoa yote ili mtu mwenye migogoro au malalamiko yake, basi ile *commission* iwe karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natika kutoa wito tena kwa wafanyakazi kwamba, sasa *commission* ipo, waanze kuitumia kwa sababu mimi bado napata migogoro, wananiletea kama Waziri. Kwa sheria ya zamani ni kweli migogoro ilikuwa inafika kwa Waziri na Waziri anakaa kama hakimu anaamua. Kwa sheria mpya, Waajiri na Wafanyakazi sasa hivi Waziri sihusiki moja kwa moja. *Commission* ipo kwenye mikoa mbalimbali na kwenye kanda mbalimbali.

Kwa hiyo, wapeleke katika hizo *commission* na sheria inasema *commission* ikishindwa kuleta suluhu moja ya pande mbili, sheria inasema yule ambaye hakuridhika apeleke jambo lake Mahakama ya Kazi, ambayo sasa hivi ni sehemu ya Mahakama Kuu ndivyo, sheria inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kupitia Bunge hili nitoe wito kwamba, wafanyakazi na waajiri, hiki chombo kipo tayari na *commission* ipo waitumie, wasipoteze muda kuleta mambo yao kwa Waziri. Mambo haya ya sheria yanaenda kwa muda, mpaka jambo litoke kwako lipelekwe kwa Waziri, kumbe siko kwenyewe mpaka linaporudi kwenye *commission,* wanaweza wakasema kwamba ,muda umekwisha. Kwa hiyo, naomba kupitia Bunge hili Tukufu, nitoe wito kwamba, watumie *commission* bila ya kuleta kila kitu kwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la ukuzaji wa ajira, nataka niseme tu kwamba, jambo la ajira Watanzania wajue kwamba, si la Wizara moja wala si la Serikali peke yake. Jambo la kukuza ajira ni la wote wazazi, sekta binafsi na kila mtu, maana baadhi ya magazeti ukisoma wanadhani kwamba, kuna mtu mmoja tu ambaye kazi yake ni kutoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli si sawa sawa na ajira ziko za aina mbili na hili naomba vijana walijue kabisa, maana yake vijana wengi wanajua ajira ni kuajiriwa tena ajira yenyewe iwe ya ofisini, hilo nalo linaleta matatizo makubwa sana. Ajira ni shughuli yoyote ya halali inayompatia kijana mapato iwe ya ofisini, iwe nje ya ofisi, popote pale ni ajira.

Ajira ya aina ya pili ni ile ya kujiajiri wenyewe, nayo ni ajira vilevile, una shughuli yako inakupa mapato unaishi. Sasa hili nalo vijana wengi bado halijaingia akilini sawa sawa. Serikali tunaweka mazingira ya kuwawezesha wajiajiri wenyewe, tumesema katika bajeti yetu kuhusu mafunzo kwa vijana, kuimarisha vyuo vya mafunzo ya vijana ili tuwape maarifa na ujuzi wafanye shughuli zao wenyewe. Tumesema tutaimarisha Mfuko wa Vijana na hata huu Mfuko wa Uwezeshaji ni Mfuko wa Vijana vilevile, hizi zote ni fursa mbalimbali za kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, tunalo tatizo la ukusanyaji wa takwimu za ajira, hili nalo naomba kabisa Watanzania wenzangu tusaidiane, kwa sababu ajira zinaweza zikawa zinazalishwa mahali Fulani, lakini kama taarifa zile hazitufikii, tutakuwa tunaripoti takwimu kidogo kumbe ajira kule ni nyingi zaidi.

Tumeongea na Halmashauri zetu kwamba, kila Halmashauri waweke mtu mahususi, ambaye atakuwa anafuatilia, anawasiliana na kata, anawasiliana na vijiji, anawasiliana na mitaa, kutazama ajira kiasi gani hasa katika sekta binafsi, hizi za sekta za umma ni rahisi kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tunaongea na wenzetu wa ofisi kuu ya takwimu kwamba, katika *survey* wanazozifanya kila mwaka, basi hili suala la ajira nalo walifanyie utafiti iwe vilevile njia mojawapo ambayo tutapata takwimu. Hii ni changamoto ambayo Wizara tunajaribu kutazama njia bora zaidi ya kupata takwimu sahihi na kwa wakati kuhusu ajira ambazo zinazalishwa wakati kwa wakati.

Mheshimwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, yote mliyoyasema tumeyazingatia na tutayafanyia kazi.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na kuungwa mkono, ili iweze kufikia mahali pake sahihi naomba Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 65 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kif. 1001 - *Administration and General* ……………...Sh.1,513,296,600

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.. *Vote 65,* program ya 10.

**MWENYEKITI:** Wote ni Mshahara wa Waziri, msitumie programu, kwa hili tunawaruhusu lakini *very brief*, kwa sababu la sivyo tutaingia kwenye *guillotine* bila sababu.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria Namba 6 ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, inatoa haki na wajibu wa waajiri na waajiriwa kazini, kwa lengo la kuleta tija; na kwa kuwa utafiti uliofanywa na Wizara hii kuna watu wapatao milioni 20, ambao wana uwezo wa kufanya kazi na milioni 18 ambao wanafanya kazi; na kwa kuwa walemavu wamo katika makundi yote haya mawili, wanaweza kufanya kazi na wapo ambao hawawezi kufanya kazi; na kwa kuwa katika muda mrefu walemavu wanalalamika juu ya haki zao katika kazi kwamba mazingira ya kazi hayafanani na hali zao; na kwa kuwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hajatoa maelezo yoyote kuhusu walemavu; je, Mheshimiwa Waziri atakubali sasa kueleza kuhusu kundi hili kubwa ambalo ni muhimu katika nchi hii juu ya haki zao za kazi katika Wizara yake?

**MWENYEKITI:** Asante sana. Mheshimiwa Waziri, kama una la kusema na pia majibu yawe kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo ya hoja ya Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, walemavu ni Watanzania na ni wananchi wenzetu. Kwa hiyo, wana kila haki ya kufanya kazi na pale ambapo wameshaajiriwa, sheria vilevile inawalinda, wasiweze wakaachishwa kazi au kunyanyaswa kwa namna yoyote, kwa sababu tu ya ulemavu wao. Sheria inakataza kuwabagua. Wale ambao hawana kazi, taratibu za uwezeshashaji zinazowahusu Watanzania wote na wao zinawahusu. Mara nyingi mimi ninapokutana nao, ninawaambia kwamba, itaturahisishia kazi wakiunda vikundi, kwa sababu baadhi yao wana ujuzi ili tunaposema kuna mikopo, basi walemavu vijana wana haki ya kukopa. Mifuko ya Uwezeshaji, walemavu ambao wana shughuli katika vikundi wanaweza wakakopa. Kwa hiyo, kwa kifupi ni kwamba, mipango yote ambayo inahusu watu wasio na ulemavu na walemavu vilevile inawahusu na tunawashughulikia.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, hakuna kurudia kwa sababu mko 15 mara 5 ni saa moja, tutaingia kwenye *guillotine*. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Luhaga J. Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia nilihoji kuwa, kuna baadhi ya watumishi ambao walihamishwa kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa, baadhi yao mpaka sasa hivi hawajarekebishiwa mishahara yao na hawajapanda vyeo kwa kipindi sasa cha miaka kumi. Je, Wizara imejipanga vipi kumaliza kero na malalamiko haya?

**MWENYEKITI:** Inakuwa hivi, kama kuna tatizo la namna hiyo, kwanza kabisa, yeye mtumishi mwenyewe anaweza kuandika malalamiko yake kwenye Wizara hii, lakini Wizara inayopaswa kujibu hili ni ile ya Utumishi. Kwa hiyo, nakuomba hilo swali nafikiri Waziri wa Utumishi, amelisikia kwa sababu Serikali ipo hapa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nimemsikiliza sana Mheshimiwa Waziri, akijibu ameeleza kwamba, mgao wa fedha za JK zimekwisha Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba anieleze ukiangalia viambatanisho vyake hivi Kiambatisho cha 5(a) ni vigezo gani walikuwa wanatumia katika kugawa hizi fedha kwa akina mama, ukiangalia Kiambatisho 5(a) Wanawake 164 tu ndiyo wamepewa lakini wanaume ni 924. Tukienda tena Kiambatisho cha 5(d), Wanawake wa Mwanza kwa mfano, Wilaya ya Kwimba, mwanamke mmoja tu lakini wanaume unakuta ni 28. Naomba Mheshimwa Waziri, anifafanulie ni kigezo gani walikuwa wanatumia kuwanyima akina mama ambao ni waaminifu sana katika kurudisha mikopo?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, hoja yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilikuwa hazigawanywi tu kwamba watu wamekaa mahali wanagawana, huyu mwanaume anapewa na mwanamke hapewi. Ukweli ni kwamba, tulitoa matangazo fedha hizi ni za wajasiriamali, tukasema wanaanza kuomba pale kwenye vijiji vyao au kwenye mitaa yao, kama ni mijini kwenye miji yao. Pale ndiyo wanamkagua kama kweli ni Mtanzania, anajishughulisha, maana wengine wanasema ni wajasiriamali lakini kumbe si hivyo. Wakishathibitishwa yote hayo, maombi yao yanakwenda kwenye Kamati ya Kata kwa uhakiki tu, kwa sababu wakati mwingine mtu anaweza akaonewa. Ikitoka hapo inakwenda moja kwa moja Benki. Kwa hiyo, kwa utaratibu huo, utaona kwamba, jinsi ulivyo hauna ubaguzi. Ila sasa katika kuomba, wale wajasiriamali inawezekana akina mama wameomba wachache.

Lakini nataka kumweleza Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa kwamba. jamani hili suala si la mwaka mmoja, linaendelea kwa miaka mitano, kwa hiyo, katika mwaka wa kwanza kama wengine walikuwa na mashakamashaka na utaratibu huo hawauelewi sawasawa, sasa wameuelewa. Kwa hiyo, naomba akina mama si wa Mwanza tu hata wa Manyoni kule kwangu na kwingine kote, kwa sababu mpango unaendelea na wenyewe wajiingize katika shughuli za ujasiriamali, waombe mikopo na ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, watapata.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mjini Musoma, tunacho Kiwanda cha MUTEX, kimebinafsishwa sasa ni zaidi ya miaka kumi na baada ya kuwa kimebinafsishwa, wale watumishi hawakulipwa mafao yao. Lakini kwa bahati nzuri nimemwandika Mheshimiwa Waziri, kwa sababu nimeweza kwenda ofisini kwake, pamoja na viongozi wa wale watumishi, tukazungumza taratibu zote walizopaswa kufuata walizifuata na zikawa zimekamilika. Mheshimiwa Waziri, aliniahidi vizuri kwamba, suala hili angekuwa amelishughulikia na lingepata majibu. Lakini ukiangalia sasa ni muda mrefu, wale watu hadi sasa toka kiwanda kibinafsishwe ni zaidi ya miaka kumi hawajajua hatma yao. Lakini vilevile hata fedha zao walizokuwa wameweka dukani, yaani fedha za duka ambazo iliamuliwa kwamba warudishiwe, hizo nazo imeshindikana kupatikana. Kwa hiyo, nimemwomba Mheshimiwa Waziri, aweze kunipa majibu ili nitakaporudi kule, niweze kuyafikisha. Sasa nashangaa, hakuyatoa labda kwa sababu ya muda, ningependa nipate majibu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namwomba radhi Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi ni kwa sababu tu ya muda hatukuweza kumfikia katika kumjibu, lakini kweli alileta katika maandishi tunayo hoja yake. Tunaomba radhi kwa sababu hatukumjibu pale. Suala hili liko Wizarani kwangu, ila ni la miaka ya nyuma kweli, kwa hiyo, lazima tuwasiliane na *PSRC*, tuone mafao ya hawa watu yamekomea wapi na kwa sababu gani. Kwa hiyo,

naomba Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, uwaeleze wale waliokuwa wafanyakazi wa *MUTEX,* wawe na subira wakati Wizara yangu inafuatilia na wewe kwa sababu ofisini kwetu unakuja mara kwa mara, tutaendelea kukupa mawasiliano kuhusu hatua gani tumefika. Kwa hiyo, bado tunalifanyia kazi.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Mshahara wa Waziri. Nazungumzia Mfuko wa Uwezeshaji. Mfuko huu ulianza mwaka jana na watu wachache waliouchangamkia kwa mfano, hiyo Mikoa sita aliyoisema ikiwemo na Kagera, tunaambiwa mgao wao umekwisha wakati ndiyo sasa watu walikuwa wamechangamka wamejiandaa pia. Nilikuwa naangalia kwenye majedwali hapa kwenye Mkoa wa Kagera, wenye watu zaidi ya milioni mbili ni *SACCOS* nne tu zimepata na watu karibu 1,000. Sisi tulifikiri huu Mfuko ni endelevu, watu wataendelea kufaidi kutoka kwenye huo Mfuko na waliokopa mwaka jana wameanza kurejesha; kwa nini hii Mikoa isiendelee kupata hiyo mikopo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa nini hii Mikoa isiendelee kupata baada ya watu kuwa wanarejesha?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile Mikoa sita ikiwemo na Kagera, tumesema imesimama si kwamba imesimama moja kwa moja, bali ni kwa muda tu wakati taratibu zinaandaliwa ili na wao waanze kukopa tena. Kwa hiyo, ni suala la muda mfupi tu wakati taratibu zinaandaliwa, kwa sababu ni kweli kwamba, wale ambao walikopa wameanza kurejesha na kama kwenye hotuba yangu nilivyoeleza, hawa wajasiriamali wadogo wadogo kwa kweli wanarejesha vizuri.

Kwa sababu, *NMB* wastani wa marejesho ni 91% na *CRDB* hawa wajasiriamali wadogo wadogo wanarejesha 100%, kwa hiyo, Mfuko huu kama ninavyosema ni endelevu, ile Mikoa imesimama kwa muda tu wakati utaratibu unaandaliwa ili waendelee tena kukopa.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu, nilihoji sana habari ya *workman compensation* kwamba, kiwango kimepitwa na wakati na sijaridhika ama sijapata maelezo ya kutosheleza. Ninapenda kujua tatizo ni nini kwa sababu kama ni umaskini tuelezwe ni umaskini, kama ni uroho tu kwamba maiti atapata hela nyingi tuelezwe, kama maiti atapata hela nyingi kwa sababu ya uroho. Lakini msaada ulishatolewa na mapendekezo mbalimbali.

Kwa mfano, tulisema inaweza ikahusishwa na asilimia ya mshahara kwa miaka aliyofanya kazi na kadhalika na kadhalika. Hiyo ni *option number one,* ushauri ulitolewa toka miaka ya 1990. Ushauri mwingine uliotolewa ni kwamba, badala ya kuweka kima kile katika Sheria yenyewe, iwekwe katika Kanuni ambayo Waziri ana uhuru au ana uwezo wa kuweza kufanya *revision* kila inapoonekana hela zile zimepitwa na wakati. Wenzetu Afrika Kusini, wakishaweka kila *amount* wanasema kabisa katika ile sheria

kwamba, kila baada ya miaka miwili itapanda kwa asilimia kadhaa. Sasa tatizo la hapa ni kitu gani kiasi kwamba, toka tumeanza kuimba wimbo huu sasa ni zaidi ya miaka kumi na kitu juu ya suala hili. Ninapenda nipate maelezo, kwa sababu kwa kweli mimi binafsi, nina hakika hata na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba, kuendelea kulipa shilingi 84,000 kwa mtu aliyefariki kazini na shilingi 108,000 kwa mtu aliyekatika mikono au miguu, naona kwa kweli ni dhuluma ya namna moja au nyingine kwa mwajiri anayehusika.

La pili, Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba, Sheria imetungwa mwaka 2004, lakini zimeanza kutumika 2007 Desemba, sasa hapa suala langu kwa ujumla kwa Serikali, hivi Serikali inapoleta Muswada hapa wameshafanya mambo yote na kwa kawaida mabadiliko katika Muswada yanakuwa ni madogo sana hivi kuna tatizo gani kwamba, wanapojiandaa kwa Muswada na vilevile Waziri muhusika anajiandaa kwa Kanuni zitakazo-*support* huo Muswada ili mara tu Mheshimiwa Rais, anapoanguka akasema anakubali basi na zile Kanuni ziwe tayari ili muda usiwe mrefu sana wa kupita kabla Sheria ile ambayo imepitishwa na Bunge iweze kutumika. Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**MWENYEKITI:** Suala ni kwa nini Kanuni zinachelewa, hizo habari nyingine naomba utujibu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, kama ifuatavyo:-

Ile fidia ya watu walioumia kazini amejibu vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba nirudie tu kwa sababu jibu alilosema ni sahihi. Tunakubali kwamba, vile viwango vya shilingi 108,000 na 84,000 vimepitwa na wakati. Waraka unaorekebisha dosari hii, unaoboresha jambo hili umeshaandaliwa kama alivyosema Naibu Waziri, umeshapita katika Sekretarieti ya Kabineti na umeshafika katika ile Kamati ya Makatibu Wakuu wakati wowote utajadiliwa katika kabineti na baada ya hapo, Sheria italetwa hapa Bungeni tuipitishe. Kwa hiyo, kwa kweli jambo hili limeshakamilika kwa kiwango kikubwa sana. Naomba sana Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, atuamini kwamba, kazi hii karibu inakamilika na uboreshaji ni mzuri sana, yaani Sheria ina mapendekezo mazuri ambayo yataleta manufaa kwa wafanyakazi.

Lakini vilevile kwa faida ya waajiri wengine, kuna baadhi ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii kama *NSSF*, sasa hivi moja ya mafao yao katika yale mafao saba ni ile ya kuumia kazini. Kwa hiyo, baadhi ya wafanyakazi wanaweza wakajiunga katika Mfuko ule na kule kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, wanatoa viwango vikubwa sana kuliko hata hivi vya Serikali.

Sasa *Regulations* niseme tu kwamba, kwa sababu tumechelewa, yote nitakayoyasema Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, anaona sisi tuna makosa tu kwa sababu tumechelewa. Lakini ukweli ni kwamba, nilipofika pale Wizarani kwa sababu na mimi nilikuwa silijui jambo hili, lakini nilipofika pale nikakuta Sheria ya mwaka 2004, bado haijaanza kutumika na mimi nilianza tu kufokafoka kama mwenzangu anavyofoka

pale. Kanuni za hii Sheria siyo Kanuni moja, mbili, wala tatu au kumi au ishirini ni nyingi zaidi ya 100, yaani ni kazi kubwa kweli na watu hao wamefanya kazi bila sikukuu bila *weekend* ni Kanuni nyingi kweli. Kwa hiyo, kazi ilikuwa ni nzito kwa hiyo, Maafisa wa Wizara yangu na Maafisa wa Mwanasheria Mkuu, wamefanya kazi ya ziada kweli na hasa nilipowaambia kwamba, mimi natangaza sasa kama ninyi hamjakamilisha shauri yenu ilibidi wakajifungie Bagamoyo kule na kwa kweli wamefanya kazi ya ziada. Lakini tumejifunza, safari nyingine Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, kosa hili hatutalirudia kwa hiyo, mshahara wangu tu kwa leo nianchie ndugu yangu kwa sababu nikikosa mshahara na wote tumetoka Singida, nitakuja kula nyumbani kwako na watoto. *(Kicheko)*

Lakini *point* tumeipata kwamba, hizi Sheria tunazozileta tusicheleweshe Kanuni, hili tutalizingatia.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Naongezea tu kidogo kwenye majibu ya Waziri wa Kazi ni kwamba, kilichocheleweshа utekelezaji wa Sheria za Mwaka 2004 hasahasa haikuwa Kanuni lakini ilikuwa ni kuandaa miundombinu ambayo inaendana na utekelezaji wa Sheria ile kwa sababu ilihitaji kutengeneza *infrastructure* mpya kabisa ili Sheria zile ziweze kuanza kutumika.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, niliongelea suala zima la wafanyakazi waendeshaji wa vyuo vya elimu ya juu, ambalo nina hakika Waziri analo kwa sababu ninazo barua kutoka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujua tatizo lililopo pale ni kwamba, wafanyakazi waendeshaji na wahadhiri wa vyuo vya elimu ya juu, wana tofauti kubwa sana ya mishahara na maombi yao walikuwa wameomba na wakaambiwa kwamba, watashughulikiwa. Lakini kwa bahati mbaya sana, wahadhili wameshapewa 100% ya nyongeza lakini wale wafanyakazi waendeshaji, hawajapata hata senti tano na bajeti ya mwaka jana walisema kwamba, suala hilo lingeshughulikiwa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atuambie hao wafanyakazi waendeshaji wa vyuo vya elimu ya juu watapatiwa lini nyongeza zao?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analozungumzia Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo ni la kweli. Katika vyuo vikuu kuna makundi mawili; kuna kundi ambalo linafundisha darasani ambalo ni Wahadhili na kuna kundi la waendeshaji.

Sasa mwaka juzi ilipoundwa ile Tume ya Rais ya kutazama mazingira ya kazi katika vyuo vikuu, ilipendekeza kwamba, wafanyakazi wale wanaofundisha waongezewe mishahara na wakasema katika ripoti yao kwamba, hawa waendeshaji suala lao litazamwe baadaye. Kwa hiyo, mapendekezo ya Tume yakatekelezwa, wale Wahadhili wakaongezewa mishahara. Kitendo kile kikaleta tofauti kubwa sana ya mishahara yao, yaani mtu mwenye *Ph.D* anayeingia darasani na yule ambaye yuko katika kazi za utawala, wakawa tofauti zaidi ya 100% au wote wana *Masters*, lakini huyu anafundisha na mwingine ni *research,* lakini wote wako katika Chuo Kikuu palepale wakawa wana

tofauti kubwa. Sasa ugomvi ndiyo ukaanzia pale na baadaye hilo jambo likafika kwa Mheshimiwa Rais, akasema tuzungumze nao jinsi ya kutatua hili tatizo. Wizara yangu imekuwa inawezesha yale mazungumzo kati ya Serikali kama mwajiri na wale wafanyakazi kupitia Chama chao cha *RAAWU.*

Sasa mahali ambapo tumefikia ni kwamba kwanza, Serikali imekiri kwamba, tatizo lipo la tofauti kubwa sana, hawasemi wafanane 100 kwa 100 hapana, wanataka tu ile tofauti iwe ndogo. Tumekubali hilo tatizo na sasa hivi linafanyiwa kazi kwa maana kwamba, kuna Wataalamu kutoka Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu, Watalaamu kutoka Idara Kuu ya Utumishi na Wizarani kwangu, wanaandaa Waraka ambao utakuja katika Baraza la Mawaziri na mapendekezo yatakayokubaliwa pale ndiyo yatakayotekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. MAGRETH AGNESS MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi sina la ziada kwamba natoa shilingi wala nini, lakini ninataka ni-*make observations.* Ni ukweli usiofichika kwamba, watu wenye ulemavu hata wakijiunga kwenye vikundi vya uzalishaji mali, inawawia vigumu sana kupata mikopo, wala siizungumzii hii ya ya bilioni moja, maana hiyo ni hatua ya juu sana hata hawaiwezi. Lakini basi mimi ninadhani mkopo ambao ungekuwa rahisi wao kuupata ni ule wa vijana, ambao unasimamiwa na Wizara zenyewe na masharti yake ni madogo sana lakini bado imekuwa ni matatizo mpaka leo.

Sasa nauliza je, Serikali au Wizara, haiwezi ikawa angalau na maelekezo mahususi kwa Watendaji wanaohusika na mikopo hii angalau kundi hili liweze kupata rehema hapo? Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, pendekezo lake ni zuri na tutalifanyia kazi. Ninaomba tushirikiane naye kama kweli kuna vikundi vya walemavu wanafanya shughuli zao au wana *SACCOS* zao, kuna mahali wanazungushwa zungushwa, naomba tuwasiliane ili kwa pamoja sisi na yeye, tuwasaidie hawa walemavu na wao wapate mikopo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sina tatizo na mshahara wake ila nataka ufafanuzi.

Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea katika Wilaya yetu ya Namtumbo tulipata matatizo katika mkopo wetu huu wa uwezeshaji wa wajasiriamali. Sisi kule Namtumbo 92% ni wakulima, ndiyo tunategemea mapato yetu kuendeshea maisha yetu ya kila siku. Katika mwongozo wa mkopo huu ulivyotafsiriwa na mabenki kule ni kwamba ni kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo, ambao ni Mamantilie, wenye vigenge, wenye maduka na kadhalika, wakulima hawaku-*qualify.*

Kwa hiyo, sisi kule Namtumbo hatukupata mkopo. Kati ya wakulima na wale wajasiriamali 680 walioomba kupitia Benki ya *NMB* Songea waliopata ni 45 tu. Kwa hiyo, tunachoomba ufafanuzi hapa ni kwamba, katika awamu hii ya pili, kama mtaweza kutusaidia tuweze kukopeshwa moja kwa moja kwenye *SACCOS z*etu, tuna *SACCOS* zetu zilizoimarika za Kata zetu za Mkongo, Mkongo Gulioni, Lusewa na Namabengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Asante sana. Lakini pia tuna *network* za *SACCOS* za Dunduliza. Kwa hiyo, tunaomba tupate ufafanuzi katika awamu ya pili, kama mtatuletea pesa moja kwa moja kwenye *SACCOS* zetu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Vita R. Kawawa kwamba, mikopo ya uwezeshaji ilipoanza mara ya kwanza ni kweli ilitolewa tafsiri potofu kwa baadhi ya mabenki na tulitoa hapa taarifa jinsi ambavyo Waziri Mkuu aliwaita wale *Managers* wa *Banks* na kuwaeleza kwamba, wamekiuka na wakakubali kwamba wamekiuka. Wakatoa wao sasa miongozo kwenye matawi yao kwamba, miradi ya kilimo imo, kilimo na ufugaji imo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, basi ni vizuri kama imo Mheshimiwa Vita R. Kawawa anasema pelekeni kwenye *SACCOS* zake. Yeye alikuwa anauliza wakulima wamo, kama wamo basi *SACCOS* zake zipewe *next time.*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia kwa maandishi na mara kadhaa nimekuwa niki-*raise* hoja hii ya riba inayotozwa. Mfuko huu wa wajasiriamali ulenge zaidi, pamoja na mambo mengine, lakini pia kupunguza riba kwa wajasiriamali wadogo wadogo walio maskini. Sasa kuna taratibu mbili; kuna wajasiriamali ambao ni *individuals,* wanakopa moja kwa moja kwenye *NMB* bila *intermediation,* ambao riba yao ni asilimia kumi. Wapo wale ambao ni maskini kabisa, wanaojiunga katika vikundi vya *SACCOS*. Kwa hiyo, kunakuwepo na *intermediation* ya *SACCOS* kwenda kukopa *CRDB*, *final Borrower* wanakopa kwa asilimia 12.

Sasa nimekuwa nikiuliza mara kwa mara kwamba, kwa namna hii hatuoni kwamba, tunawa-*discourage* watu kujiunga kwenye *SACCOS?* Kwa sababu wakiwa kwenye *SACCOS* watakopa kwa asilimia 12, akienda mwenyewe anakopa kwa asilimia kumi. Kwa hiyo, ili kuhamasisha *SACCOS*; kwa nini tusiweke mkakati na kuzielekeza benki kwamba, wakopeshe *SACCOS* kwa asilimia chini ya kumi ili mkopaji wa mwisho akope kwa hiyo asilimia kumi au kwa asilimia ambayo ni sawa na anayekopa moja kwa moja. Naomba kupata ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mwaka wa kwanza wa utaratibu huu, tulipata matatizo ya riba hasa kwenye *SACCOS. Banks* wakati ule zilikubaliana na Serikali kuhusu riba, sisi tulitaka iwe chini ya asilimia kumi, lakini katika kuzungumza nao, walipofika kwenye asilimia kumi wakasema hapo hawawezi kuteremka. Kwa hiyo, tukakubaliana asilimia kumi ndiyo makubaliano tuliyotia saini kati ya Benki Kuu kwa niaba ya Serikali na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye *SACCOS* wakasema kwamba, *SACCOS* yenyewe ikishakopa kwa asilimia kumi, inapotoa mikopo kwa wanachama wake na inapofuatilia marejesho, ina gharama. Tukazungumza na wenzetu wa Ushirika wakasema kwamba, kwa Sheria ya *SACCOS*, inaruhusiwa kuweka faida *up to two percent* katika shughuli zake. Kwa hiyo, tukaruhusu kwamba, *SACCOS* ili wasipate hasara katika kukopesha wanachama wao, waongeze iwe asilimia 12 ili wanaporudisha asilimia kumi na asilimia mbili ibaki kwa ajili ya shughuli zao. Lakini bado yakaja malalamiko kwamba, hiyo asilimia mbili vilevile haitoshi kugharamia shughuli za *SACCOS.* Tukatoa mwongozo mwingine, pengine haujafika. Nataka nirudie tena, tukasema zile *SACCOS* ambazo asilimia mbili hazitoshi, zinawapa hasara, zikae na wanachama wao wa *SACCO* ile wakubaliane ni *percent* ngapi ambayo wakitoza hawatapata hasara, watakachokubaliana na wanachama basi watoze itakuwa ni halali. Lakini ile asilimia kumi ndiyo makubaliano yaliyopo kati ya sisi na *Banks,* hii hatuwezi tukaipunguza.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Wakati tunachangia Kambi ya Upinzani, tumezungumza sana juu ya mchango wa *NSSF* katika miradi mbalimbali. Sina tatizo na *NSSF* kuwekeza, Mifuko mingi ya Hifadhi ndivyo inavyofanya. Kitu ambacho kinanipa tabu, napenda kupata maelezo kutoka kwa Waziri ni kuona kwa mfano, katika ukurasa wake wa 28, fedha ambazo ni za Miradi kwa *NSSF* zipo takriban shilingi bilioni 125 na zote ni kwa sababu ya kugharamia Bajeti ya Serikali. Fedha ambayo inaenda kuwekezwa sehemu nyingine ni kama shilingi bilioni 20.

Uwiano huu unanipa shida kwamba, Mfuko huu badala ya kuwa ni Mfuko ambao unajitegemea kwa ajili ya kutoa mafao kwa wafanyakazi, sasa Mfuko huu fedha zake zinachukuliwa kwa ajili ya kugharamia Bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, uwezo wa *NSSF* kulipa watu wake, utategemea tena uwezo wa Serikali kuilipa *NSSF.* Hali hii mimi naona ni hatari sana kwa Mfuko huu. Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, tumezungumzia sana juu ya fedha hizi shilingi bilioni 21 zinavyokwenda. Lakini kila nikiangalia vitabu vya Serikali, sioni nani anayewajibika na fedha hizi za Serikali. Nikiangalia kwenye Wizara hii hakuna shilingi bilioni 21; hizi fedha tumeziidhinisha kutoka kwenye bajeti gani na nani atahusika?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisikubaliane na Mheshimiwa John M. Cheyo kwamba, fedha za *NSSF* zinakwenda ku-*support* Bajeti ya Serikali. Hizi fedha za *NSSF* zinakwenda katika miradi ile kwa maana ya uwekezaji, si kuchangia Bajeti ya Serikali. Wanawekeza na Serikali inawalipa riba ili kutunisha Mfuko wa *NSSF* ili wafanyakazi wapate mafao makubwa zaidi na Serikali ni mlipaji mzuri tu.

*NSSF* wanalipwa vizuri tu na Serikali na wana uhakika kwamba, hapa watalipwa, wamewekeza mahali pa uhakika. Mahali ambapo hatari ya kupotea hela yao *(risk)* hakuna.

Nadhani tukubaliane na mzee wangu, Mheshimiwa John M. Cheyo kwamba, huu ni uwekezaji mzuri na ni mzuri zaidi kwa sababu kweli zinakwenda kusaidia wafanyakazi wale wale. Jamani askari hawa wanafanya kazi. Wakijengewa nyumba kule Jeshi la Wananchi ni wafanyakazi hao hao. Jeshi la Polisi wakijengewa nyumba, Jeshi la Magereza watajengewa nyumba, hosteli Chuo Kikuu kule ni watoto wa wafanyakazi. Kwa hiyo, kwa kweli fedha hizi zimewekezwa mahali pazuri na kwa nia nzuri tu ya kusaidia jamii na hasa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi shillingi bilioni 21 ni kweli kwenye Wizara yangu mimi ninaratibu tu mpango, pengine siku moja katika maswali yake anaweza akauliza Wizara inayohusika ya Fedha. Mimi ninajua fedha zipo, watu wanakopa na mimi ninafurahi wanakopa na Bariadi wanakopa. Sasa yeye kama kuna jambo linamkera kera kwa mikopo hii, basi anaweza kuuliza Wizara ya Fedha. Kwenye Wizara yangu ni kweli hazipo, kwa sasa mimi ninaratibu tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Mheshimiwa John M. Cheyo ni Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee,* angeweza akaona hata fedha zilizojenga Jengo hili la Bunge haziingi kwenye Akaunti ya Bunge ni kwa sababu Serikali yenyewe ime-*guarantee* kwamba, wakitoa hizo fedha watakuwa wanawalipa wenyewe. Mkiangalia kwenye *Consolidated Account* ile ya Hazina, mtakuta pengine hizo fedha zipo. Naomba afanye hilo zoezi halafu ajiridhishe. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Mimi ninaomba kupata ufafanuzi kidogo tu. Mheshimiwa Waziri, ameelezea jinsi mchakato wa uundwaji wa Baraza la Vijana utakavyokuwa, lakini bahati mbaya sana, hakutupa *timeframe* ya kwamba ni lini sasa Baraza la Vijana litakuwa tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nilikuwa nataka kujua nini hatma ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Chumvi Uvinza waliopunguzwa kazi?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Vijana kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ni kwamba, kilichokuwa kinacheleweshа ilikuwa ni ile sera ya sheria. Maadamu sasa imeshapitishwa na kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti kwamba, kwa mwaka huu wa fedha katika mambo ambayo tutayakamilisha ni pamoja na Kuundwa kwa Baraza la Vijana ili Vijana wapate chombo chao, ambacho kitasimamia mambo yao. Kwa hiyo, *timeframe* ni kwamba, ndani ya mwaka huu wa fedha, hiyo ni moja ya kazi ambayo tumejipangia kuifanya ya kuunda hilo Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafanyakazi wa Kiwanda cha Uvinza. Suala lake linafanana kama lile la *MUTEX*, nalo ni la siku nyingi kweli lipo *PSRC.* Kwa hiyo, ninataka tu kumwahidi kwamba, tutafuatilia tuone kwa nini hawajalipwa mafao yao na tutampa majibu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi wa eneo lile ambalo ninakusudia kuliuzia la fedha za kujenga uwezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, fedha za kujenga uwezo jihadhari, yameulizwa maswali mengi kama utauliza sawa sawa na wale hutapata majibu. Sasa uliza tukusikilize.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachotaka kueleza kwenye jedwali lililopo ukurasa wa 58 wa Kitabu cha Hotuba cha Mheshimiwa Waziri, zimeorodheshwa Wilaya ambazo zimepata fedha na kiasi ambacho wamegawiwa fedha hizo. Katika ukurasa wa 61 pale kwenye Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Simanjiro haijatajwa, pamoja na kwamba ukweli wenyewe ni kwamba, Simanjiro hadi sasa haijapata hata senti tano katika fedha hizo. Wilaya ya Kiteto kwenye jedwali hilo imepelekwa katika Mkoa wa Arusha, najua hayo ni marekebisho madogo ambayo yanaweza kufanyika. Kateshi ni Makao Makuu ya Wilaya ya Hanang, lakini katika jedwali hili Kateshi imechukuliwa kama Wilaya na Hanang ikaandikwa kama Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho madogo haya, ambayo yanaweza yakarekebishwa bado hoja yangu ya msingi inabaki kwamba, Wilaya ya Simanjiro ina mazingira tofauti na maeneo mengi ya nchi yetu. Inapakana na Wilaya zenye Mabenki. Simanjiro yenyewe haina Benki yoyote, umbali kutoka kijiji kimoja hadi kingine ni zaidi kilomita 50, 60, 70. Kwa hiyo, hata hiyo benki itakapokuja kwenye Makao Makuu ya Wilaya kwenye mwaka unaokuja, ipo hatari kwamba, kama umbali ambao watu wa benki wanaweza kwenda si zaidi ya kilomita 30. Maana yake watahudumia hicho kijiji kimoja ambapo Benki itakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nipate ufafanuzi kwa Wilaya ambazo hazina benki kabisa, kama ilivyo Wilaya ya Simanjiro, ambapo wananchi wanakwenda Mwanga, Same, Moshi, Hai, Arusha na Babati, kutafuta huduma hiyo na hakuna hata mmoja aliyekopeshwa mpaka hivi sasa ninavyozungumza. Nataka Waziri aweke bayana, Wilaya hizo ambazo hazina benki kabisa, kama ilivyo Simanjiro, zitawekewa utaratibu gani mahususi, ambao utaweza kukidhi utekelezaji huo wa Ilani na ahadi yetu ya Ilani kwamba, Simanjiro haitakuwa kisiwa na kwamba ikifika mwaka 2010, tutaweza kuelezea kwamba na sisi ni sehemu ya Watanzania waliostahili kupata huduma hiyo. Nataka kupata ufafanuzi katika hilo ili tusifike mahali tena katika bajeti ya mwaka ujao na kutaka kuwaomba radhi Watanzania katika jambo hilo.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Wizara, niombe radhi ya uchapishaji kwamba, Kiteto imepelekwa Mkoa wa Arusha na Kateshi ikaonekana kama Wilaya. Ni makosa tu ya uchapishaji, tunaomba radhi kwa hilo. Safari ijayo tutakuwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yake kubwa ni Simanjiro kwamba, haimo katika orodha na ni kweli. Orodha ile msingi wake ni zile Wilaya ambazo kuna mabenki.

Kwa hiyo, kwa zile Wilaya ambazo hazina mabenki kama Simanjiro, Namtumbo na nyingine za namna hiyo, hawamo katika lile jedwali kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza katika moja ya matatizo tuliyoyapata katika mwaka wa kwanza ni kuzifikia zile Wilaya ambazo hazina benki kama Simanjiro. Nataka nirudie tena kwamba, tutakapoanza mpango wa pili wa kutumia Asasi ndogo ndogo za fedha kukopesha, tutaanza katika zile Wilaya ambazo mwaka huu hazikuhudumiwa vizuri au hazikuhudumiwa kabisa kwa sababu hazina benki. Tutaanzia katika Wilaya hizo ili na wao wapate mikopo hiyo. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, nilisema nina matatizo mawili, pamoja na ombi moja. Nina tatizo Jimboni kwangu na Benki ya *CRDB. SACCOS* zote ambazo ziliomba mkopo, hakuna hata moja iliyopata. Mfano ipo *SACCOS* moja ya Bukwimba, ambayo ilituma maombi yake na kukamilisha taratibu. Afisa wa Benki alipoenda kule maana yake ni zaidi ya kilomita 100 kutoka Mwanza Mjini, alisema hatarudi tena huko kwa sababu ni mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka anieleze Mheshimiwa Waziri kwamba, je, safari hii baada ya kuwa wamemaliza mwaka mmoja, hao Bukwimba watapata mkopo? Maana wamekwisha kamilisha taratibu na ni wengi, lakini tatizo tu ni kwamba wanakaa mbali na hiyo Benki ya *CRDB* Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, *NMB* kuna wajasiriamali zaidi 50 wapo Busolwa, Nyang'hwale, Mwingiro na Kalumwa, wale ni wakulima wajasiriamali mmoja mmoja wa kilimo na mifugo. Mheshimiwa Waziri, amesema watapata wakati akimjibu Mheshimiwa Vita R. Kawawa, ni kweli Benki ya *NMB* mpaka sasa hivi wanapokaa meza moja na Serikali wanakubali, lakini wakitoka pale, *NMB* inaleta taratibu zake kwamba, hakuna mjasiriamali mmoja mmoja, mkulima na mfugaji atakayepata mikopo ya aina hiyo. Mimi kwangu wapo wenye *write-up* zao nzuri zipo na nyingine niliziandika mimi kuwasaidia, lakini wamekataliwa. Hebu Mheshimiwa Waziri, anieleze hapa kama watapata hiyo mikopo na nikienda huko niseme nini?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *CRDB* kule Geita na mimi ni Wilaya yangu vilevile, niliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya kule. Sasa kama *SACCOS* zote zimenyimwa kwa sababu tu kwamba, wapo mbali, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutazungumza na Mkuu wa Benki ya *CRDB*, Dr. Kimei, ili tuone namna ya kuwahudumia watu hao kwa sababu umbali si sababu ya wao kukosa mikopo, labda wangesema kuna *SACCOS* masharti fulani fulani walikuwa hawajayatimiza, hiyo ingeweza ikawa sababu, lakini umbali isiwe ni sababu. Kwa hiyo, tutazungumza na Dr. Kimei, tuone jinsi ya kuzifikia hizo *SACCOS* Mwanza mpaka Geita panafikika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NMB* kwamba, imesema wajasiriamali wakulima haiwakopeshi, kama nilivyotoa majibu mara ya kwanza kwamba, katika mpango huu wakulima na wafugaji wamo. Ni kwamba mwaka wa kwanza, *NMB* walikuwa na matatizo tu ya kuwafikia wakulima na wafugaji. Katika mwaka wa pili,

tutajitahidi kuweka utaratibu hao *NMB* na *CRDB* wawafikie huko, lakini utaratibu wa hakika zaidi ni zile Asasi ndogo ndogo ambazo mpaka Geita zitafika ili ziwafikie hao wakulima. Kwa hiyo, awape matumaini wasikate tamaa.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Ninaomba nianze na kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kueleza kwamba, suala la ajira kwa vijana ni suala mtambuka. Tunapozungumza inabidi tuziguse Wizara zote na ziweze kuona kwamba hilo ni muhimu sana kuhakikisha kwamba, tunawaangalia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa nimegusa Wizara mbili tu. Wizara ya Nishati na Madini, ina nafasi kubwa sana ya kuwaajiri vijana wetu. Kwa bahati mbaya kunatokea kwamba, kuna *contradiction*. Lakini Wizara ya Nishati na Madini, imeshaonesha kuwasaidia. Sasa kuna vijana wa Matabi wapatao karibu 10,000, walishaomba eneo la Matabi. Walishaleta maombi, nafahamu Waziri wa Nishati na Madini alishaandika barua kwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Maliasili na Utalii, alishatuma viongozi wake ili waweze kuwashughulikia vijana hao wapate eneo hilo kwa kufuata utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba tuwe kwenye Wizara hii, ukienda Wizara ya Nishati na Madini, ndiyo itabidi watujibu na Maliasili na Utalii itabidi wajibu. Hapa tupo kwenye vifungu vya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Naomba kabisa urudi hapo. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nazungumzia ajira binafsi, hao ni vijana ambao wanatarajia kujiajiri kwenye eneo la Nishati na Madini na nilikuwa nimemwomba Waziri, aweze kusaidia aone kwamba ni muhimu hao vijana kujiajiri, ndiyo hoja yangu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna suala lingine la ajira binafsi, tunao vijana wetu ambao kwa kweli sisi tunaotoka maeneo ya Kanda ya Ziwa, vijana wetu wamejiajiri binafsi kwa kutumia wengine pikipiki na baiskeli. Nafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu, alishazungumza kwamba, suala hili litakuja. Lakini hawa vijana wameweka *investment* kwenye kununua baiskeli na pikipiki, sasa sheria itakuja. Mwanzoni nilikuwa nimenyamaza, lakini baada ya kuona kwamba wanazuiliwa kufanya shughuli zao, suala linakuja anayewafukuza ni askari ambaye amempakia mwenzake kwenye pikipiki, anavunja sheria vilevile na yeye. Wakati mwingine unakuta askari akimfukuza mwenye baiskeli, naye amepanda baiskeli anamfukuza yule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge suala ni nini?

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ni kwamba, kuwazuia hao vijana kufanya shughuli hii, ningeomba lisitishwe kwa sababu kwa Wilaya ya Geita nikitoa mfano, ina barabara ambazo zinapitwa na magari. Nilikuwa nahesabu ni barabara tano, lakini barabara 21 zote zinatumia baiskeli. Sasa ukiwazuia manaa yake ni kwamba, hakuna shughuli itakayofanyika. Asante.

**NAIBUWAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba kama ifuatavyo: La kwanza, suala la vijana wake wa Matabi, tutashauriana naye binafsi kuona namna tunavyoweza kusaidiana katika kushauriana na Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, habari ya pikipiki na baiskeli, muda uliobaki sheria kufika Bungeni kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu si mrefu. Hivyo, avute subira, sheria itakuja na utekelezaji wa sheria ndiyo utaleta utulivu katika nchi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance na Accounts* … … … … … Sh.430,137,200
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … … … Sh. 412,998,100
Kif. 2001 - *Labour and Workers Participation Labour* Sh. 2,476,950,100
Kif. 2002 - *Employment Division* … … … … … … Sh.961,375,000
Kif. 5001 - *Youth Development* … … … … … … … Sh.1,006,290,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 65 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kif. 1001 - *Adiministration and General* … … … … Sh.496,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … … … … Sh.1,900,000,000

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nikiangalia katika hii *Sub-vote* 1003 na nikiangalia vifungu vyote hivi, yaani miradi ya *Support VETA* mpaka *Improve Labour Market*, naona kuanzia msimu wa *Financial Year*, 2005/2006, hakuna fedha zozote ambazo zimeshakuwa *located* katika hiyo miradi. Kwa bahati mbaya ni kwamba, katika *Financial Year* 2005/2006, fedha zote zilizowekwa hapo ni za nje na wala siyo fedha za ndani. Sasa nauliza Serikali inaweka umuhimu gani katika miradi hii; je, bila fedha za nje hatuwezi kuendesha mambo yetu wenyewe? Hilo la kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hili la kwanza, nikujibu kwamba, kama fedha hazipo maana yake hakuna shughuli, katika Vitabu vya Hazina kompyuta

inaonesha *zero.* Kwa hiyo, tusizungumzie *zero* kwa maana hakuna chochote. Ipo kwenye *Sub-item* tu lakini haina fedha. Sasa uliza swali la pili.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 5492, kuna fedha ambazo zimekuwa *allocated*, lakini hakuna mradi ambao umeoneshwa. Kwa hiyo, ninataka kujua ni mradi gani ambao umetengewa shilingi 100,000,000?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha ni kwa ajili ya kupambana na Ugonjwa wa UKIMWI.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kifungu hicho hicho, kifungu kidogo 6380 - *Rehabilitation of Labour Office and Youth Centres.* Nadhani ukarabati wa Ofisi za Kazi, pamoja na Kituo cha Vijana.

Sasa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, alipokuwa anajibu kama nilimsikia vizuri, alisema kwamba, zimetengwa shilingi milioni 50, kwa ajili ya uendelezaji wa Kituo cha Sasanda kule Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu niseme kwamba, Kituo hiki cha Sasanda kule Mbozi, kina ekari zaidi ya 800 na mimi wakati wote nimekuwa nikisema, kwa sababu sehemu hii ni kubwa haitumiki; je, isingekuwa vizuri pengine Wizara kama ina mkakati mzuri zaidi kwa ajili ya matumizi ya eneo hilo, kuliko wananchi waione kama vile imekaa bure bila matumizi?

Sasa Serikali kupitia Wizara hii, inawaeleza nini Wananchi wa Mbozi wasije wakaona kwamba, Serikali inawanyima eneo kubwa? Pengine Wizara ina mkakati mzuri zaidi, maana sioni kama hizi shilingi milioni 50 zinaweza zikafanya kazi kubwa zaidi ya kukarabati yale majengo machache, ambayo yapo mahali pale? Asante.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kama ifuatavyo: Kwanza, niseme kwa maana ya mpango mkubwa wa Kituo cha Vijana, ekari 800 ni ndogo sana hasa ukizingatia katika nchi sasa tuna vituo vitatu tu.

Kwa hiyo, mpango wa muda mrefu wa Serikali kwa kweli ingekuwa inawezekana tukangepanua zaidi eneo hilo, lakini hatuwezi kulipanua zaidi. Kwa hiyo, eneo hili tunahitaji, ila uchache wa fedha unatufanya tusitoe fedha nyingi kwa wakati mmoja. Lakini Serikali iko makini katika kuhakikisha eneo hili linatumika vizuri. Tunaomba ushirikiano wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kumhakikishia kwamba, kadri atakavyotupa ushirikiano, siku moja ataamini tunachokisema kwamba, nia yetu ni kuwa kituo kile kiwe na maslahi kwa Taifa zima, badala ya kuwa na maslahi kwa Mbozi peke yake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Labour* … … … … … … … … …        Sh.903,682,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Youth Development* … … … … … …    Sh. 823,308,000

**MHE. SUSAN A. S. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa naomba kupata ufafanuzi kuhusu kifungu 5492 kwamba, hizi fedha ni kwa ajili ya kile Kitengo cha Maendeleo Vijana pale Wizarani au kwa ajili ya masuala ya UKIMWI kwa vijana nchi nzima na kama hivyo ndivyo je, mgawanyo wake utakuwa namna gani na kwa nini fedha hizi zote zinatoka nje wakati tunajua tatizo la UKIMWI ni kubwa sana kwa vijana wetu? Je, fedha hizo zisipotoka nje vijana wetu watasaidiwa namna gani?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha za UKIMWI ni moja ya eneo ambalo Serikali yetu tuna wahisani wanatusaidia. Tatizo ni kubwa na ukipata mtu wa kukusaidia, huwezi ukakataa. Kwa hiyo, nafikiri ni busara tu kwamba, Serikali tumezipokea. Wizara yangu pamoja na kwamba na sisi tunapambana na UKIMWI, ndani ya Wizara na sisi wenyewe tupone kwenye UKIMWI.

Lakini vilevile ina jukumu la kuratibu shughuli kama hizi katika sehemu mbalimbali za kazi. Ku-*protect* wafanyakazi ambao ndiyo nguvu kazi isije ikamalizika kwa UKIMWI. Kwa hiyo, fedha hizi zitatumika ndani ya Wizara na nyingine zitatumika katika kuratibu mapambano ya UKIMWI katika maeneo mbalimbali ya kazi kote nchini.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha Makadirio ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana - Fungu 65, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote wameunga mkono, kwa hiyo, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, makadirio yake yamepitishwa na Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, sisi tunapenda wanaotusikiliza. Tunapopiga kura tena ya mdomo ni wakati wa kupitisha bajeti yote. Tunapokuja kwenye Wizara, tunahoji kama tulivyohoji. Mahali ambapo tunaweza kufanya maamuzi makubwa kabisa ni pale tunapopitisha kifungu kwa kifungu. Sasa wananchi wengine kwenye magazeti wanasema badala ya kusema ndiyo, mngekuwa mnapiga kura kila Wizara.

Kwa hiyo, tunaomba waelewe kwamba, sisi huu ndiyo utaratibu tunaoufanya na kama kuna wakati kazi inafanyika ni wakati wa Kamati ya Matumizi, ndiyo tunafanya kazi ya kifungu baada ya kifungu. Kwa hiyo, ni vizuri wakaelewa Bunge linavyofanya kazi. Wametoa zogo kubwa sana kwenye Kongamano, wanasema Waheshimiwa Wabunge wanapitisha tu mambo. Hapana, huu ni utaratibu wetu, tunafanya kazi kwa mujibu wa Kanuni. *(Makofi)*

Tangazo la pili, tunatangaza timu yetu sasa *VS – NSSF*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, amewaambia mnatakiwa kuwafunga magoli mengi *NSSF* pamoja na kuwasifia leo. Timu ya Bunge, hiyo nyingine sina, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Msolwa na *reserve* ni Ndugu Suleiman Makame, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Omar M. Nibuka. Akina mama vigelele siyo hapa, kule uwanjani. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao hawakutajwa wanaalikwa kesho kushangilia timu yetu na ni mategemeo yetu mtaturudishia kombe na sisi tutalipokea.

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyotangaza Mheshimiwa Spika, kesho pia kuna burudani kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida yetu, kwenye kiwanja chetu cha Utawala, pia wote mnakaribishwa nadhani kuanzia saa mbili usiku. Kwa hiyo, mnakaribishwa wote.

Baada ya kusema hivyo, naomba niahirishe Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.34 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 6 Agosti, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*